# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 4 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. ENG. SAMWELI X. HHAYUMA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu

ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 226

### Ujenzi wa Vituo vya Afya vya kimkakati Kata za Chikola na Makanda, Manyoni

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Chikola na Makanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deo Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu

swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokea vipaumbele vya ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za Sanza, Chikola na Makanda zilizopo katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Serikali ilipeleka Shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kimkakati cha Sanza ambapo ujenzi wa awamu ya kwanza kwa *OPD* na maabara umekamilika. Ujenzi wa awamu ya pili, unaohusisha wodi ya wazazi, chumba cha upasuaji na *laundry* upo kati hatua ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya kimkakati nchini ikiwa ni pamoja na kwenye Kata za Chikola na Makanda kadri fedha zitakavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Maweni, wananchi walijenga boma la kituo cha afya, miaka ya 2012, lakini mpaka sasaivi halijakamilishwa; je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba boma hilo linaenda kukamilishwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Serikali ilitoa shilingi milioni 50 kwa ajili ya kukamilisha Zahanati ya Mhalala, Sasajila, Igose, Magasai na Mahaka; bahati mbaya zile fedha hazijatosha: Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba zile zahanati zinakamilishwa ili ziweze kuanza kutoa huduma? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, la kwanza; kwenye Kata ya Maweni, ujenzi wa kituo cha afya ambapo boma limekamilika toka mwaka 2012, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma haya ambayo yamejengwa na wananchi kwenye vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge, ameleta orodha hii ya zahanati ambazo anazitaja, na alinikabidhi mimi mwenyewe juzi hapa. Tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ta umaliziaji wa zahanati hizi, lakini kwa sasa kuna tathmini ambayo inafanyika kwa ajili ya ramani zile ambazo zilipelekwa mwanzoni kwenye majimbo mbalimbali hapa nchini kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ili kuweza kujua ni kiasi gani sasa kinahitajika kwa ajili ya kumalizia.

**SPIKA:** Nataka kukuita Mheshimiwa Almasi Maige, lakini kabla hujauliza swali lako la nyongeza, hebu tusaidie neno *laundry* kwa Kiswahili linaitwa nini?

Washa kisemeo. *Laundry* ni nini kwa Kiswahili?

**MHE. ALMASI A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, ni nyumba ya kufulia au eneo la kufulia nguo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu yako yalipaswa kuandika hicho, kwa sababu mkianza kuchanganya ninyi majibu ya msingi Kiingereza na Kiswahili, kidogo itakuwa mtihani.

Mheshimiwa Almasi Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ALMASI A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nami niulize swali la nyongeza kwa swali

hili 226. Lini Serikali itaendeleza na kumalizia vituo viwili katika Kata za Usagali na Shitage? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya hivi ambavyo amevitaja Mheshimiwa Mbunge na kadiri pale bajeti itakavyoruhusu, basi tutakwenda kuvimalizia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kuuliza, ni lini Kituo cha Afya Mwaya, kilichopo Tarafa ya Mwaya, Wilayani Ulanga, kitafanyiwa ukarabati? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kipaumbele cha Serikali kufanya ukarabati kwenye vituo vya afya ambavyo ni vya muda mrefu na tutaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuweza kufanyiwa ukarabati kituo cha afya ambacho amekitaja Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni lini sasa Serikali itatekelea mapendekezo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ya ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za Mwabomba na Bugando?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeshatafuta fedha ya kuweza kuangalia ujenzi au kuanza ujenzi wa vituo vya afya katika maeneo ya kimkakati hapa nchini. Tutaangalia vilevile Kwimba imetengewa kiasi gani kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya hivi ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare, swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kata ya Idodyandole, Kata ya Gondi na Kata ya Ipande ni kata kubwa sana, na tulileta mapendekezo: Je, lini Serikali itatoa pesa kwa ajili ya kituo hiki cha afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, ni hivi karibuni tu Mheshimiwa Massare ameleta orodha hii ya kuomba vituo hivi vya afya na Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga kituo cha afya kipya katika maeneo ambayo ameyataja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Wananchi wa Kata ya Busangwa, Kijiji cha Mwanima, wameshaandaa eneo la ekari 15 kwa ajili ya ujenzi wa *health center* na tayari wameshaanza ufyatuaji: Nini mpango wa Serikali wa

kuhakikisha kwamba wana-*support* kwa ajili ya kukamilisha mradi huu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya afya kwenye maeneo ya kimkakati. Tayari kuna fedha ambayo imeshatengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivi vya afya kwenye maeneo kama anavyotaja Mheshimiwa Mbunge hapa. Kwa Busangwa, tutaangalia kama eneo hili pia limetengewa kwenye mwaka wa fedha huu ambao tunaenda kuuanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jengo la Tunduru Kusini, Kata ya Marumba, ni moja ya kata ya kimkakati kwa ajili ya kujenga kituo cha afya, ambayo ina umbali wa kilometa 80 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri: Je, ni lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya kujenga kituo cha afya katika Kata ya Marumba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilisema hapo awali, tayari Serikali imetafuta fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika maeneo mbalimbali nchini. Tutaangalia pia Kata ya Marumba kama ipo imetengewa bajeti kwenye mwaka wa fedha unaokuja, kama haijatengewa, basi tutaitengea fedha kwenye ule mwaka mwingine wa fedha wa 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 227

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Geterer na Masieda, Mbulu**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya Geterer na Masieda?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na umaliziaji wa maboma ya Vituo vya Afya kote nchini. Serikali itapeleka shilingi milioni 800 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Masieda na ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya kituo hicho. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Halmashauri hiyo imetengewa shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukamilishaji wa Kituo cha Afya Markad.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa Vituo vya Afya ikiwa ni pamoja na ukamilishaji wa Kituo cha Afya Geterer kwa kadri fedha inavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mbulu Vijijini tumeshaanzisha *slogan* ya kuhamasisha ujenzi wa vituo vya afya mimi na *DC* Kheri James. Tuna vituo vya afya vya Hayderer, Geterer, Masqaroda, Dinamu, Ladha, Endamilay na Maghang. Je, uko tayari sasa kupeleka fedha hizo ili kuzihamasisha juhudi za wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Hospitali ya Halmashauri bado haijaisha na inahitaji Shilingi milioni 500 na Kituo cha Hydom hakina jengo la upasuaji: Je, ni lini utapeleka fedha hizo ambazo maombi yetu unayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la kwanza la nyongeza la lini Serikali itapeleka fedha kuunga mkono juhudi za wananchi za kujenga vituo vya afya; kwanza, nampongeza Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, tumeona jitihada kubwa wanayoifanya katika kujenga vituo hivi vya afya. Serikali itajitahidi kadiri ya upatikanaji wa fedha kuweza kutenga bajeti kwa ajili ya kwenda kuongeza nguvu pale ambapo wananchi watakuwa wameishia.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, tayari Hospitali ya Wilaya imeshawekwa kwenye bajeti hii tunayoenda kuitekeleza ya 2023/2024, shilingi milioni 500. Fedha hizi zitakwenda kwa ajili ya ukamilishaji wa hospitali hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ujenzi wa Kituo cha Afya Kitaya umeshakamilika: Ni lini dawa na vifaa tiba vitapelekwa ili kianze kutoa huduma kwa wananchi wa Kitaya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeanza kupeleka vifaa tiba kwenye vituo vya afya mbalimbali hapa nchini na Waheshimiwa Wabunge wengine watakuwa ni mashahidi, vifaa tiba vinavyoenda ni vile vya kisasa kabisa ambapo zamani vilikuwa vinapatikana kwenye Hospitali za Rufaa. Hii ni juhudi kubwa sana ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika kituo hiki cha afya ambacho amekitaja Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha vifaa tiba vya kisasa kabisa vinaenda pale kuweza kupeleka huduma karibu, kwa Watanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini kwenye Kata ya Kwala, tulipokea pesa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya; je, ni lini Serikali itamalizia fedha zilizobaki kwa ajili ya kukamilisha na kuanza kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inafanya tathmini ya

vituo vya afya vyote vilivyopelekewa pesa na ambavyo havikukamilika. Pale tathmini itakapokamilika, basi tutatenga fedha kwa ajili ya kuweza kumalizia vituo hivi vya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 228

**Ujenzi wa mabweni kwa shule za watoto wa kike wanaosoma masomo ya sayansi**

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabweni kwenye shule za wasichana wanaosoma masomo ya sayansi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika ujenzi wa mabweni ya wanafunzi katika shule za bweni. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 Serikali imetoa Shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa shule 10 maalumu za sekondari za wasichana za masomo ya sayansi kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha sita. Ujenzi huu ni

awamu ya kwanza ya ujenzi wa shule 26 ambazo kila Mkoa utajengewa shule moja kupitia mradi wa *SEQUIP*.

Mheshimiwa Spika, mradi huo unahusisha ujenzi wa mabweni tisa katika kila shule na kila bweni litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 120. Aidha, kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Sekta ya Elimu, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati mabweni ili kuongeza nafasi zaidi za wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka kipaumbele cha ujenzi wa mabweni kwa shule za kidato cha tano na sita na kwa wanafunzi wote wa kike na wakiume, kwa kuwa wanafunzi wote wana changamoto.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Ni nini mkakati wa Serikali wa kujenga mabweni ya wasichana katika shule za sekondari za kata nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, katika shule hizo kumi ambazo mnajenga, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha shule hizo zinafunguliwa ifikapo Julai, mwaka 2023? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema kwenye

majibu yangu ya msingi, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni kujenga shule maalum hizi za bweni za wasichana katika kila mkoa katika nchi yetu hii. Hii itaenda kusaidia kupunguza *dropout* na mimba za utotoni, kwa sababu watoto wote katika mkoa ule wataenda kwenye shule hizi maalum.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, baadhi ya shule hizi ambazo zimejengwa, shilingi bilioni 30 imekwenda katika mikoa kumi kwa maana ya shilingi bilioni tatu kila Mkoa. Tayari baadhi ya shule hizi zimesajiliwa na ifikapo Julai mwaka huu 2023 shule hizi zote kumi zitaanza kupokea wanafunzi wa kike ili kuanza masomo yao ya sayansi katika maeneo hayo ambayo fedha imeshaenda.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shaban Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Bweni la Sekondari ya Mlongwema ni dogo sana na halikidhi mahitaji kwa wanafunzi wale; je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bweni kubwa ambalo linaweza kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa Mlongwema? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kipaumbele cha Serikali kujenga mabweni katika shule zote za *A-Level*. Tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuweza kuona shule hii ambayo ameitaja mahitaji hasa ni yapi ili tuweze kutafuta fedha ya kwenda kumalizia au kujenga mabweni mapya katika shule hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Wananchi wa Jimbo la Kwela wamejitahidi kuanza kujenga mabweni katika Sekondari za Mpui, Mzindakaya, Milenia na Vuma. Je, ni lini Serikali mtaunga mkono jitihada hizi kwa kuwapelekea fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali itapeleka fedha kuunga mkono juhudi za wananchi wa Kwela kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Ni kipaumbele kuhakikisha kwamba tunajenga mabweni katika shule hizi ambazo hasa ni za *A-Level* katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wananchi wa Kata ya Lumuli ambayo iko Jimbo la Kalenga, Mkoa wa Iringa, walijenga maboma kwa ajili ya mabweni ya watoto wa kike, kwa miaka 13 sasa hayajamaliziwa. Ni lini Serikali itamalizia mabweni haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokuwa nimeshasema hapo awali, Serikali itamalizia mabweni haya, hata hili la Lumuli kule Kalenga, kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Na tutaangalia katika mwaka huu wa fedha ambao tunakwenda kuuanza wa 2023/24 kama shule hii imetengewa fedha ili mabweni haya yaweze kukamilishwa na Serikali kuunga mkono juhudi za wananchi katika eneo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake liataulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa George Mwenisongole.

Na. 229

**Ujenzi wa barabara ya lami kilometa 10 – Mjini Tunduma**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Km 10 kwa kiwango cha lami Mjini Tunduma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka 2020 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliahidi ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilometa 10 kwenye Mji wa Tunduma.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ahadi hiyo umeanza ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya kilometa 2.8 zilijengwa kwa kiwango cha lami na shilingi bilioni 1.39 zilitumika. Aidha, mwaka wa fedha wa 2022/2023 shilingi bilioni 2.3 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 3.7 kwa kiwango cha lami ambapo shilingi bilioni 1.64 zimepokelewa na ujenzi umefikia asilimia 45.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kukamilisha ahadi hiyo kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo yanatia moyo, kuna barabara nyingine ndani ya Mkoa wetu wa Songwe ambazo zimekwama, kwa mfano barabara ya kutoka Mlowo – Itaka – Kamsamba na Barabara ya Mbalizi – Utengule mpaka Mkwajuni kule kwa Mheshimiwa Mulugo, zote hizo zina ahadi nyingi na ninaomba Serikali itilie mkazo zipate kutekelezwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga barabara hizi, hasa hizi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Katika mwaka huu wa fedha tunaokwenda wa 2023/2024, Bunge lako tukufu limeiidhinishia *TARURA* zaidi ya shilingi bilioni 772 kwa ajili ya kutengeneza

barabara mbalimbali hapa nchini, na ninaamini katika hizi barabara za Mlowo ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge nazo zitawekwa katika kipaumbele cha mwaka huu wa fedha tunaokwenda kuutekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati barabara ambazo zimeathirika na mvua katika Jimbo la Mbagala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni mkakati wa Serikali kutengeneza barabara hizi na ndiyo maana *TARURA* walikuwa na *emergency fund* ya shilingi bilioni 11 na sasa wameomba tena nyongeza iweze kufika shilingi bilioni 46 kwa ajili ya kutengeneza barabara hizi za Mbagala na za maeneo mengine ya Waheshimiwa Wabunge ambayo yameathiriwa na mvua ambazo zimeendelea kunyesha hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 230

**Kuwapeleka Maafisa wa Usalama Barabarani kujifunza nje ya nchi**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kupeleka Maofisa Usalama Barabarani Falme za Kiarabu na Vietnam ili kujifunza jinsi ya kudhibiti ajali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inao utaratibu wa kutoa mafunzo mbalimbali kwa maofisa wa polisi wa usalama barabarani ndani ya nchi na pia kuwapeleka nje ya nchi kujifunza namna bora ya kusimamia na kudhibiti ajali za barabarani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2023 Serikali imeshawapeleka maofisa wa usalama barabarani 30 kwenye nchi 15 ambazo ni Marekani, Ujerumani, Japan, China, India, Vietnam, Australia, Switzerland, Falme za Kiarabu, Israel, Tunisia, Misri, Ghana, Rwanda na Afrika Kusini ili kujifunza masuala ya usalama

barabarani. Mashirika ya kimataifa na wadau kama *JICA, UKAID, WFP, WHO, LATRA, TIRA, TRA, NIT* na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani wanaendelea kufadhili na kutoa mafunzo juu ya udhibiti na usimamizi wa taratibu za usalama barabarani ili kupunguza ajali nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa nafasi za mafunzo ndani na nje ya nchi kwa maofisa wa usalama barabarani ili kupata ujuzi juu ya usimamizi na udhibiti wa ajali kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Massaburi, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wenzetu wa nchi hizo wamekuwa wakitumia sheria kali ambazo kila dereva anatii sheria na kunusuru maisha ya wananchi wao; je, ni lini Serikali itatunga sheria kali ambazo zitaweza kutusaidia kunusuru maisha ya Watanzania yanayopotea kutokana na ajali za barabarani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali imeshindwa kuwadhibiti madereva wa bodaboda ambao hupita kwenye makutano bila kuzingatia taa za barabarani na hatimaye kusababisha ajali na kusababisha watu kufariki na kuleta walemavu wengi katika nchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Janeth Maurice Massaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja, juu ya sheria ya usalama barabarani iliyo kali zaidi; naamini Mheshimiwa Mbunge atakuwa anafahamu kwamba tulishawasilisha hapa sheria ikasomwa kwa mara ya kwanza na kwa busara ya Bunge lako Tukufu ilitakiwa irudishwe kwa ajili ya kuboresha maeneo ambayo yalikuwa na changamoto. Napenda kumhakikishia kwamba uboreshaji uko hatua za mwisho, katika Mabunge yajayo tunatarajia iletwe hapa ili Bunge likiridhia tuwe tumemaliza eneo hilo la sheria kali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kushindwa kuwadhibiti bodaboda; hatujashindwa. Tulichojifunza ni kwamba hawa vijana namna wanavyoingia kwenye uendeshaji ni kwamba wengine hawajapata kabisa mafunzo. Jeshi la Polisi, hususan Kitengo cha Usalama Barabarani, wameanza na hatua za kuwafundisha.

Mheshimiwa Spika, na bahati nzuri sasa hivi wamewekwa kwenye makundi katika maeneo mbalimbali wanayopangwa katika vikundi. Katika makundi yao yale wanapata mafunzo, *traffic police* na wenye vyuo vya udereva wanakwenda wanawasomesha ili wajue taratibu za usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, wale wanaokiuka hatua zinachukuliwa. Ndiyo maana tukienda maeneo ya polisi mtakuta pikipiki nyingi ziko kule za wale waliokiuka sheria. Tutaendelea kujenga uwezo wao na kuchukua hatua kwa wale wanaokiuka. Kupitia Bunge lako, nielekeze *traffic police* wasiwe na muhali na vijana hawa ambao wanakaidi sheria makusudi, hasa wanaopita kwenye taa za barabarani wakati zimezuia, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 Serikali iliondoa madereva wenye uzoefu na ujuzi wa udereva kwa kuwa walikosa kigezo cha kuwa na cheti cha *form four.* Na kwa kuwa ajali zimekuwa nyingi katika nchi hii ambazo zinaleta ulemavu au walemavu wengi nchini: -

Je, Serikali haioni sasa sababu ya kuwarudisha madereva hao kazini kwa sababu cheti cha *form four* hakina uhusiano na ujuzi au utaalamu wa udereva? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuwaondoa watumishi waliokuwa hawana vyeti vya *form four* wakiwemo madereva ilikuwa ni Sera ya Menejimenti ya Utumishi ambao tumeridhia wote kama nchi, kwamba tuna vijana waliokwisha soma mpaka kidato cha nne na kuendelea, ni vizuri utumishi wa umma uwazingatie hao na kuruhusu wale ambao walikuwa kwenye utumishi wa Umma wajiendeleze. Serikali bahati nzuri ilitoa muda maalum wa watu wale kujiendeleza, na walioshindwa kujiendeleza ndio waliondolewa.

Mheshimiwa Spika, wale wa darasa la saba waliojiendeleza wengi walibaki kwenye utumishi wa Umma. Nadhani bado hakuna hoja ya msingi ya kurejea darasa la saba wakati tunaowahitaji kwa mujibu wa sera yetu ni baada ya kidato cha nne, na vyuo vya udereva vipo ambapo hawazuii kuingia kupata mafunzo. Kwa hivyo tunalichukulia *positively* kwa maana kwamba wataendelea kujielimisha na wanaokiuka wanachukuliwa hatua, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, madereva wengi wa bodaboda hawana leseni kwa sababu ya gharama kubwa zinazotakiwa kwa ajili ya kupata leseni, na ndiyo maana wanaendesha pasipo kuwa na leseni. Sasa swali; kwa nini tusiweke utaratibu mzuri wa kuwafundisha pamoja kwa gharama nafuu ili waweze kufanya kazi hiyo kwa uzuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi Mathayo, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba katika baadhi ya maeneo ikiwemo kwenye jimbo lake, ameanzisha huo utaratibu, na sisi upande wa usalama wa raia tunaupokea.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwahamasisha maeneo mengine pia watumie utaratibu kama huu unaopendekezwa na Mbunge, kwamba wanapokuwa wengi katika chumba kimoja wakafundisha kwa gharama za chini, wakawekewa utaratibu nafuu wa kupata leseni zao ili kuepuka hao wanaokwepa kukata leseni kwa sababu ya gharama kubwa. Na bahati nzuri maeneo mengine wameruhusu kulipa leseni kidogo kidogo, kwa hiyo likifanyika hilo nadhani hakutakuwa na matatizo yoyote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge; ahsante sana.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

Na. 231

**Jeshi la Uhifadhi kuwa na Kamishna Jenerali**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza: -

Je, lini Jeshi la Uhifadhi litapata Kamishna Jenerali na kuleta muunganiko katika divisheni za *NCAA, TANAPA, TAWA* na *TFS?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu *(The Wildlife and Forest Conservation Service)* lilianzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Sura ya 283.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa taasisi zinazounda Jeshi hilo upo chini ya Kamishna wa Uhifadhi wa kila taasisi nao watakuwa ndio makamanda wa taasisi zao. Muundo wa Jeshi la Uhifadhi unaotumika kwa sasa unafanya kazi vizuri. Endapo kutabainika kuwa na changamoto katika kutekeleza mfumo huo, Serikali itafanya marejeo ya Sheria ya

Wanyamapori ili kuwezesha kuwa na Kamishna Jenerali wa Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Antipas Mgungusi, swali la nyongeza.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Ni *standard* ya kawaida kwa taasisi zote za Serikali, lakini hasa majeshi, kuwa na kiongozi mkuu wa taasisi husika kwa ajili ya *chain of command,* lakini Jeshi la Uhifadhi halina kiongozi mkuu kwa maana ya divisheni zile *TFS, TAWA, TANAPA,* kila mtu ana-*operate* mwenyewe anavyoona inafaa. Sasa ikitokea viongozi wakuu wa nchi wanataka kuongea na majeshi wao Jeshi la Uhifadhi wanampeleka nani kuwawakilisha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwamba wakiona changamoto wataanzisha mchakato wa kubadilisha sheria ili kupata kamishna. Anataka aone changamoto gani ilia one sasa kuna uhitaji wa kuwa na *Commissioner General* wa Jeshi la Uhifadhi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi ni kwamba taasisi hizi zina majukumu tofauti. Ukiangalia utekelezaji wa majukumu yao unaendana sambamba na namna ambavyo majeshi haya yameundwa. Kwa mfano kwenye Taasisi za *TANAPA* na Ngorongoro, taasisi hizi zina baadhi ya vitu ambavyo vinaruhusiwa kutumika lakini kuna baadhi ya taasisi ambazo zinazuia kama *TAWA* na *TFS*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye upande wa *TAWA* na *TFS* tunaruhusu masuala ya uvunaji na uwindaji wa kitalii. Kwa hiyo, utaona yale majukumu yenyewe ya taasisi yanatofautiana. Kwa hiyo, kila kamishna wa uhifadhi anatekeleza majukumu kulingana na muundo wa taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa sasa hivi tunaona bado wanafanya kazi vizuri na wote wanaripoti kwa Katibu Mkuu, kwa hiyo mkuu wa nchi anapotaka kuzungumza na majeshi haya anazungumza na Katibu Mkuu ambaye ndio msemaji wa Wizara kwa upande wa utendaji.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa maoni yake, tunayapokea na pale ambapo tutaona kwamba kuna uhitaji sasa wa kuunda jeshi ambalo litakuwa na mwakilishi ambaye ni Kamishna Jenerali, basi tutafanya hivyo na tutapitia kanuni zetu ili tuendane sambamba na majeshi yaliyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, sasa aulize swali lake.

Na. 232

**Ukarabati wa Kituo cha Posta – Kengeja**

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Posta kilichopo Kengeja kitafanyiwa ukarabati na kutumika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania linaendelea kufanya ukarabati wa majengo yake nchi nzima kwa kutumia fedha zake za ndani kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 – 2025/2026. Kutokana na mpango huu, ofisi ya Kengeja imepangwa kufanyiwa ukarabati kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumuuliza maswali mawili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ni lini ulikwenda kukikagua kituo hiki cha Kengeja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa imepangiwa mwaka 2024/2025, je, kwa nini tusiachane na ukarabati na badala yake tukakijenga upya kutokana na hali ya kituo hiki ilivyo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nimempata katika swali la kwanza, swali la pili naomba alirejee upya.

**SPIKA:** Swali la pili anasema kama mna mpango wa kuweka kwenye bajeti ya 2024/2025, kwa nini msikijenge upya kwa sababu kituo kina hali mbaya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bahati Khamis Kombo, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza, kwamba ni lini nitaenda kukagua. Ukaguzi unafanyika kila mara, naa tuna vituo nchi nzima na tunakwenda hatua kwa hatua. Tulifanya ukaguzi Shangani, Chakechake, na tayari tumeshafanya ukarabati katika maeneo hayo na fedha zitakapopatikana tutatenga muda wa kwenda kukagua ili tuweze kukarabati kutokana na mpango wa ndani unavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, vilevile swali la pili, badala ya kujenga tunaanza na utaratibu wa kukarabati kwanza maeneo ambayo tunayo kwa sababu tayari mahali palipo ni kwamba ndiyo maeneo ambayo yanamilikiwa na Shirika la Posta Tanzania. Baada ya kuona kwamba sasa uhitaji utabadilika na mahitaji ya watu yakawa mengi tofauti na eneo lililopo, basi tutaangalia uwezekano wa kutafuta eneo lingine ili tuhakikishe kwamba tunakidhi mahitaji ya utoaji wa huduma za posta, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Posta cha Dodoma ni kituo ambacho kimejengwa muda mrefu sana na hakiendani na hadhi ya makao makuu, nini mkakati wa Serikali wa kujenga kituo kipya cha posta cha kisasa ili kiendane na hadhi ya makao makuu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA NA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tumefanya ukarabati nchi nzima na kituo cha posta kikiwaki moja wapo. Pamoja na hivyo, tunaendelea na kutafuta maeneo ya kujenga vituo vingine vipya kulingana na Serikali kuingia makubaliano na Posta ya Oman. Tunaamini kabisa kwamba katika mradi huo ambao takribani milioni 100 USD zinaenda kutumika kujenga zile *logistic park*. Naamini kwamba kwa sababu Dodoma ndiyo makao makuu ya nchi tutaitazama na kuhakikisha kwamba inakuwa na posta ya kisasa na yenye kutoa huduma ambazo zinaendana na mahitaji ya Watanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Assenga Mbunge wa Kilombero na sasa aulize swali lake.

Na.233

**Ujenzi wa Chuo cha *VETA*- Kilombero**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Wilayani Kilombero baada ya wanachi kutenga eneo la hekari 30?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Kipanga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Ni azma ya Serikali kujenga chuo cha ufundi stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2203, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo. Tayari Serikali imeshakamilisha kuandaa michoro na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilombero eneo lililotengwa kujengwa chuo cha ufundi stadi ni katika Kijiji cha Nakaguru Kata ya Mchombe. Aidha, tayari kiasi cha shilingi million 45 kimetolewa mwezi Machi, 2023 kwa ajili ya shughuli za awali za ujenzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali walau Wilaya ya Kilombero sasa inapata chou cha *VETA*. Swali la kwanza, mtalifanyia nini eneo Kata ya Kisawasawa mlilopewa na wananchi na Mkurugenzi wa

Halmashauri ya Mji wa Ifakara, maana wataalam wameshaenda na wameshalichukua hilo eneo?

Swali la pili, kule shamba Nakaguru Mchombe ambako mnakwenda kujenga hicho chuo cha *VETA* hakuna hata barabara, na fedha milioni 45 ni ndogo sana. Je, ni lini fedha zingine zitaongezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asenga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu ya swali la msingi, wajibu wa kutambua au kuamua ni eneo gani chuo kiende kujengwa ni mamlaka za wilaya pamoja na mikoa. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi kwanza Mheshimmiwa Asenga na Bunge lako Tukufu, kwamba eneo hili la Kisawasawa alilolitaja ambalo labda lilitengwa awali na mamlaka za wilaya au na mkoa na kukabidhiwa Wizara ya Elimu nimwondoe shaka na wasiwasi, Serikali bado ina mipango mingi na mikubwa eneo hili bado tuna uhitaji nalo na tutapanga utaratibu mwingine na miradi mingine ya kimaendeleo inaweza kupelekwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, kwamba fedha iliyopelekwa ni ndogo ni kweli, tumepeleka fedha milioni 45 kwa ajili ya kazi zile za awali ambayo ilikuwa ni masuala ya *geotechnical survey, topographical survey* pamoja na *environmental and social impact assessment*. Hivi sasa tayari fedha kwa ajili ya kazi zile za *substructure* pamoja na *superstructure* ela zake tayari tumeshazipata. Nadhani ndani ya wiki hii au wiki ijayo fedha hizo zitakwenda kule kwa ajili ya kuanza rasmi ujenzi huo wa majengo yale tisa kama tulivyoweka kwenye mpango wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itakikarabati Chuo cha Ufundi *Music* ambacho kiko Korogwe ambacho ni kikongwe na kimechakaa sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava Mbunge wa Korogwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tunafahamu uwepo wa chuo hiki cha *FDC* pale Korogwe, na katika nchi yetu tuna vyuo 54 vya *FDC* ambavyo vingi sana ni vya muda mrefu. Tumeanza kufanya ukarabati tangu mwaka 2020/2021 katika bajeti ile na tumeweza kuvikia vyuo 35 kufanya ukarabati pamoja na upanuzi. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, katika bajeti yetu hii ya 2023/2024 tunakwenda kuvifikia vyuo 21 vilivyobaki kikiwemo na hiki cha Korogwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Chuo cha *VETA* Nyasa kina course mojawapo ambayo ni ya udereva lakini chuo hicho hakina gari kabisa ikiwemo ya utawala.

Je, nini mpango wa Serikali kukisaidia chuo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Manyanya Mbunge wa Nyasa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ya mwaka huu 2023 tuliweka azma ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia pamoja na samani kwa ajili ya vile vyuo 25 vya Wilaya vipya pamoja na vyuo vine vya mikoa. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Manyanya, katika bajeti yetu ijayo ya 2023/2024 tutaendelea kuweka bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa ikiwemo na magari ya kufundishia pamoja na vifaa mbalimbali vya kujifunzia kwa ajili ya vyuo vyetu vile vya zamani lakini pamoja na hivi vipya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Jimbo la Kilwa kusini halina chuo cha *VETA* na hakuna mpango wowowte wa Serikali kujenga chuo hicho isipokuwa tuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi pale Kilwa Masoko ambapo miundo mbinu yake ni ya muda mrefu na imechakaa. Sasa hivi kipaumbele chetu ni kujenga bwalo na tulishaomba.

Je, lini Serikali italeta fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa bwalo pale chuo cha wananchi Kilwamasoko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge Mbunge wa Kilwa Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kama nilivyokwisha eleza kwamba mpango wa Serikali ni ujenzi wa vyuo 64 katika wilaya

ambazo hazina, miongoni mwa Wilaya hizo ni pamoja na Wilaya ya Kilwa. Sasa utaratibu gani wa eneo gani linakwenda kujengwa, aidha ni Kilwa Kusini au ni Kilwa Kaskazini ni maamuzi ya Wilaya au Mkoa wa Lindi kuamua chuo hicho kinakwenda kujengwa wapi. Tunatambua uwepo wa Chuo cha *FDC* pale kulwa Kusini na mimi nakifahamu chuo hiki na tunajua kwamba tunauhitaji wa bwalo pamoja na baadhi ya mabweni. Kama nilivyosema kwa upande wa Korogwe katika mwaka ujao wa fedha tutatenga fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa vyuo vile, kuongeza miundombinu ya mabweni pamoja na mabwalo, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi katika bajeti ijayo mambo mazuri yanakuja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Je, ni lini Serikali itajenga karakana ngumu na mabweni katika Chuo cha *VETA* kilichopo Kitangali ili kuwezesha vija wengi kupata mafunzo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo Mbunge wa Viti Maalumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli na mimi nilishawahi kufika pale Kitangali, majengo yale yaliyokuwepo ni machache. Nakumbuka tuliweka kwenye bajeti yetu ya mwaka huu kwamba tuongeze majengo, madarasa na karakana katika Chuo kile cha Kitangali. Namwomba Mheshimiwa Hokororo mara tu baada ya kipindi hiki cha maswali tuweze kuonana

tuweze kuangalia kwa nini fedha zile zaidi ya milioni 200 ambazo tulizitenga katika bajeti yetu ya mwaka huu kwa ajili ya kwenda kuongeza miundombinu katika chuo kile cha Kitangali kama hazijakwenda tuweze kuzipeleka kwa haraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa swali la nyongeza. Chuo cha *VETA* Ulyankulu kimechaka sana na hakina majengo ya kutosha, lakini 2020/2022 kilitengewa bajeti ya shilingi milioni 638; fedha zile zilichukuliwa zikarudishwa Wizarani.

Je, Serikali iko tayari sasa kuzirudisha zile milioni 638 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa chuo changu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama unao ufahamu wa hizo fedha kama hauna ufahamu nazo nijulishe ili alete swali la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, sina taarifa kamili ya fedha hizi labda baada ya kipindi hiki tuweze kuonana na Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Sawa, aidha muonane au ulete kama swali la msingi Mheshimiwa Rehema Juma Migilla. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mimi ningependa nimuulize swali dogo la nyongeza Mheshimiwa Waziri. *Campus* ya *Marine Science* ambayo iko Zanzibar nayo imekuwa na uhaba wa madarasa;

Je, nayo imo katika mpango wa vile vyuo 21 vitakavyopata matengenezo makubwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chimboni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, vyuo 64 tunavyo vizungumza hapa ni kwa upande wa Tanzania bara. Kwa upande wa Tanzania Zanzibar tuna utaratibu maalum ambao tunautumia tukishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Kwa hiyo kwa upande wa ukarabati wakule bajeti itatengwa kwenye Wizara ile ili kuhakikisha maeneo yale ambayo yanahusika na vyuo vya ufundi kwa upande wa Zanzibar yanakwenda kushughurikiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Pamoja na kuishukuru Serikali kwa kutuanzishia *VETA* wilayani Irambo, je, ni lini Serikali itatuongezea majengo ili tupate mafunzo ambayo hatuyapati kutokana na uhaba wa majengo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi vya zamani viko zaidi ya vyuo 44, na ni kweli kabisa vina uhitaji mkubwa wa majengo, vifaa vya kufundishia pamoja na rasilimali watu. Nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kama nilivyokwisha kujibu maswali yaliyotangulia. Kwa upande wa pale Urambo tunajua kwamba chuo kile kina majengo machache ikiwemo na uhaba wa karakana pamoja na mabweni. Katika bajeti yetu ijayo tutahakikisha kwamba tunatenga fedha ili kuongeza miundombinu hiyo ya maabara, karakana pamoja na mabweni kwa ajili ya Chuo chetu cha Urambo. Kwa hiyo tuwasilinae tu Mheshimiwa Sitta ili tuliweke vizuri hili, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Miongoni mwa Wilaya ambazo hatuna chuo kipya cha *VETA* ni pamoja na Wilaya ya Bunda;

Je, ni lini sasa Serikali mtatujengea Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Bunda ili vijana wetu waweze kupata ujuzi na kujiajiri wenyewe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Bulaya Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha eleza kwenye majibu ya swali la msingi, katika mwaka wa fedha 2022/2023, yaani huu tunao endelea nao, tunawilaya 64 na mkoa mmoja ambao hauna chuo cha *VETA* Mkoa huo ni wa Songwe. Wilaya hizi 64 miongoni mwa Wilaya ya Bunda. Kwa hiyo nikuondoe wasiwasi, katika Mkoa wa Mara tuna wilaya

nne ambazo ni Serengeti, Bunda, Tarime, ndizo wilaya ambazo hazina vyuo vya *VETA*. Katika mwaka huu tayari tumeshapeleka fedha zile za awali na sasa tuna peleka fedha awamu ya pili kwa ajili ya kuanza ujenzi rasmi ikiwemo na chuo hiki cha Wilaya ya Bunda. Kwa hiyo nenda kawaambie wananchi Serikali ya Mama Samia iko kazini inawatendea haki wana Bunda.

**SPIKA:**Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani sasa aulize swali lake.

Na. 234

**Kuwajengea nyumba watumishi wa Serikali ya Muungano Zanzibar**

**MHE. JUMA USONGE HAMAD** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani kupitia *TBA* kuwajengea nyumba watumishi wa Serikali ya Muungano kwa upande wa Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Chaani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* umeanzishwa chini ya Sheria ya Wakala, Sura 245 ikisomwa pamoja na Agizo la Uanzishwaji wa Wakala *GN*. Na. 24 la

tarehe 14 Februari, 2003. Moja ya jukumu la msingi la *TBA* ni kujenga na kukarabati nyumba na majengo ya Serikali kwa ajili ya makazi kwa watumishi wa umma Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Jukumu la ujenzi wa nyumba kwa watumishi wa Umma kwa upande wa Zanzibar liko chini ya Wakala wa Majengo Zanzibar *(ZBA)*. Hata hivyo, *TBA* na *ZBA* wanashirikiana na kushauriana kwenye mambo mbalimbali ya kitaalam na kujengeana uwezo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Usonge Juma Hamadi swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ukweli uliokuwepo, Shirika la Nyumba la Bara halitumi fedha kupitia Shirika la Nyumba la Zanzibar hadi muda huu.

a) Je, kuna ushirikiano gani sasa ya kuliwezesha shirika la Nyumba la Zanzibar kwa kulipatia fedha kwa ajili ya kuwajengea watumishi wa bara?

b) Je, kuna mkakati gani wa ushirikiano kati ya *ZBA* pamoja na *TBA*? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyo kwisha kusema, ni kwamba nyumba za Zanzibar kwa watumishi wa umma zinajengwa chini ya Wakala wa Majengo wa Zanzibar lakini wana ushirikiano wa karibu sana kati ya *ZBA* pmoja na wakala wa majengo Tanzania Bara. Ushirikiano huo ni pamoja na kwamba Wakala wa Majengo Zanzibar

wamekuja mara kadhaa huku Bara kujifunza namna ambavyo *TBA* wameweza kuendesha miradi mbalimbali happa nchini ikwemo miradi ya Dar es Salaam Magomeni *quarter* hapa Dodoma pamoja na mji wa kiserikali.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa swali lake la pili ni kwa kiwango gani *TBA* iipatie fedha *ZBA*. *ZBA* fedha zake zinatengwa kwenye Wizara ya Ardhi, Maendeleo na Makazi kule Zanzaibar. Na kwa mwaka wa fedha ujao, kwa maelezo ya *ZBA* ni kwamba wametenga takribani kiasi cha shilingi bilioni 56 ili kujenga nyumba takriban 400 zitakazo jengwa kwa Zanzibar nzima kwa maana ya Unguja na Pemba, na walau kila Wilaya watagusa kupitia mradi huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa nyumba kadhaa zilizo chini ya mamlaka ya *TBA* hasa hapa Dodoma ni chakavu, miundombinu ya maji taka imechoka, maji ya karo na vyoo yanafurika hovyo na hivyo kuwa tishio kwa afya.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuisimamia mamlaka hii ya *TBA* ili kuhakikisha nyumba hizi ziko katika hali ya usalama na si tishio kwa wakazi, na hasa kwa vile wanalipwa kodi na hawakai bure?

**SPIKA:** Mheshimiwa ametaja hoja ya kukaa bure, Wabunge wengi mnadaiwa kodi na *TBA*. Wabunge mnao daiwa kodi na *TBA* muilipe *TBA* ili iweze kufanya majukumu yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa nasema hivyo kwa sababu nina barua zenu utakapofika muda wa kufukuzwa huko kwenye nyumba msinifuate mimi, nendeni mkalipe ili *TBA* ifanye kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Asha kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli badhi ya nyumba za *TBA* hapa Dodoma ni chakavu, na nikushukuru Mheshimiwa Spika, kwamba baadhi ya watumishi wa Serikali wanadaiwa. Na kwa kuwa wanadaiwa wanakila sababu ya kulipa ili tukarabati nyumba hizi ambazo ni chakavu, ukizingatia kwamba *TBA* fedha zake zinakata kutoka ruzuku za Serikali lakini pia na kodi za mpangaji, inapokusanywa ndipo inapokarabati nyumba hizi za *TBA*, ahsante.

**SPIKA**: Mheshimiwa Dorothy Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Uko ujenzi unaoendelea na *TBA* kule Temeke, tunaita Temeke *quarter*.

Je, Serikali mna mkakati gani wa kuwapatia nyumba wale ambao walikuwa wakiishi pale kabla ya ujenzi huu unao endelea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy Kilave kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli pale Temeke Mwisho na Temeke *quarter* kuna mradi unaendelea na mradi huu tutajenga majengo takribani saba ya ghorofa yatakayo kuwa na uwezo wa kubeba familia 1,008 na kwa maana hiyo sasa wale wote ambao watakuwa ni waathirika wa maeneo

hayo pia *TBA* tutaona ni namna gani ya kuwafanya hawa waishi katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka Serikalini. Wabunge mnaotembea mketi na wale mnaozungumza nimesimama, kwa hiyo tusikilizane. Mheshimiwa Shigongo tusikilizane. Ahsante sana.

Tutaanza na tangazo la wageni walioko hapa Bungeni; tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambao ni viongozi kutoka Wizara hiyo. Tutaanza na Dkt. Hashil Abdallah ambaye ni Katibu Mkuu; yupo pia Ndugu Neema Maregeli ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Mhandisi Bashir Juma Mlindoko, Mwenyekiti wa Bodi *TILDO;* Mhandisi Musa Nyamsigwa, Mwenyekiti wa Bodi SIDO; Profesa Ulingeta Mbamba, Mwenyekiti wa Bodi *TANTRADE;* Profesa Aurelia Kamuzora, Mwenyekiti wa Bodi *NEEC;* Profesa Othman Othman, Mwenyekiti wa Bodi *TBS;* Ndugu Nina Nchimbi, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi *CAMARTEC;* Profesa Wineaster Anderson, Mwenyekiti wa Bodi *CBE;* Dkt. Aggrey Mlimka, Mwenyekiti wa Bodi *FCC;* na Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mwenyekiti wa Bodi *TIC,* karibuni sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana. Wabunge mnazungumza. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, tusikilizane.

Wapo pia Dkt. Consolatha Ishebabi, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi *TEMDO;* Ndugu Judith Kadege, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi *BRELA;* Ndugu Raphael Maganga, Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania *(TPSF);*

Ndugu Leodiger Tenga, Mkurugenzi Mtendaji Shirika la Viwanda Tanzania; Ndugu Frank Nyabundege ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo (*TADB)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Waziri ana wageni wengine ambao ni Watendaji Wakuu kutoka Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Wasimame wote kwa pamoja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo vilevile wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri, hawa ni Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kondoa na waalikwa wa Kudumu wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Dkt. Khamis Mkanachi, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mwenyekiti CCM Wilaya ya Kondoa Ndugu Hija Bakari Suru. Mwenyekiti huyu wa Wilaya ameambatana na viongozi wengine wa CCM wa Wilaya ya Kondoa kwa maana ya Kamati ya Siasa ya Wilaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Makatibu Kata wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Kondoa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia watumishi kutoka Ofisi ya Mbunge, Jimbo la Kondoa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Exaud Kigahe, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambao ni familia yake na huyu ni Ndugu Rehema Henry Mponzi, mke wake, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni watano wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni wadau wa masumbwi kutoka Jijini Dar es Salaam na hawa wameambatana na Ndugu Karim Khalid Said maarufu kama Mandonga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wadau wa masumbwi kutoka Jijini Dar es Salaam, lakini sasa hebu Mandonga asimame, karibu sana Bungeni umezitangaza vizuri sana ngumi (masumbwi). Kwa hiyo, tunakupongeza sana, lakini pia umeitangaza vizuri nchi yetu, tunakupongeza sana, unaweza kuketi. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali; tunao wageni nane wa Mheshimiwa Mhandisi Andrea Kundo, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni Waheshimiwa Madiwani na Maafisa kutoka Jimboni Bariadi Mkoa wa Simiyu, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Uzini, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 22 wa Mheshimiwa Almasi Maige ambao ni Wenyeviti wa UVCCM Kata ya Uyui, Jimbo la Tabora Kaskazini. *(Makofi)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, ambao ni wachezaji na viongozi wa timu ya mpira ya wanawake ya *Bunda Queens* na ni washindi wa Ligi Daraja la Kwanza na wamefuzu kucheza ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara 2023/2024 kutoka Bunda Mkoani Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Changamoto tu iliyopo ni kwamba Mheshimiwa Ester Bulaya ameacha kucheza *netball* siku hizi hapa Bungeni, ahsanteni sana. *(Kicheko)*

Wapo pia wageni 23 wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambao ni washiriki wa Shindano la Urembo Kanda ya Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Furaha Matondo ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Hawa Mchafu ambao ni Wajumbe wa Baraza la Wazazi kutoka Kibaha Mkoa wa Pwani; hawa ni Ndugu Abubakari Nombo na Ndugu Luli Nyororo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Anastazia Wambura ambaye ni Meneja wa *SIDO* kutoka Jijini Dodoma; huyu ni Ndugu Twaha Sued, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Mwita Getere ambao ni Madiwani kutoka Bunda Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Chato Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, ambao ni Madiwani Ndugu Doa Limbu, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu na Ndugu Kulwa Shoto, Diwani wa Kata ya Bukomela, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Ussi Pondeza, ambao ni Viongozi kutoka Jimboni kwake Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 60 wa vyuo vikuu nchini kutoka Mkoa wa Simiyu, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Madiwani 116 wa Chama cha Mapinduzi Tanzania, karibuni sana Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo ya wageni.

Ninayo maelezo ya Spika kuhusu jambo ambalo tulikwishafanya hapa; Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Godwin Mollel na unayezungumza naye tusikilizane. Tatizo mkiwa mnaongea huku mbele hamsikii kinachosemwa na wakati mwingine kinawahusu ninyi.

Maelezo ya Spika kuhusu Shukurani za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Bunge kufuatia Bunge kupitisha Azimio la Kumpongeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kuwa mnamo tarehe 4 Aprili 2023, katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge, Bunge lilipitisha Azimio la Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuimarisha demokrasia nchini na kukuza diplomasia ya uchumi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia Azimio hilo, napenda kuwajulisha kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan analishukuru Bunge kwa pongezi hizo kwake na imani iliyooneshwa na Bunge hili kwa Serikali anayoiongoza. Aidha, Mheshimiwa Rais anaahidi na kusisitiza kuwa Serikali yake itaendelea kutekeleza vema mambo yote yaliyopo kwenye

Mipango ya Maendeleo na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Rais, anaomba ushirikiano wa Bunge ili Serikali iweze kutekeleza kwa ufanisi mkubwa yale yote yaliyoainishwa kwenye Mipango ya Serikali na Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni tangazo la Wafanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2023.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba siku ya Jumatatu tarehe 1 Mei, 2023 ilikuwa ni Siku ya Wafanyakazi Duniani ambapo Kitaifa ilifanyika Mkoani Morogoro na Mgeni Rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kwa kuwa wakati wa sherehe hiyo Wafanyakazi Bora wanatambuliwa na kupongezwa leo hii nimewaleta wafanyakazi bora wa Ofsisi ya Bunge ili tuwatambue na kuwapongeza. *(Makofi)*

Wa kwanza ni Ndugu Prosper Maingu ambaye ni Dereva Mwanadamizi na ndiye Mfanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge kwa ujumla, naomba asimame na ahsante sana. *(Makofi)*

Vilevile wapo wafanyakazi bora wengine kutoka Idara na Vitengo vingine kutoka Ofisi ya Bunge nao ni kama ifuatavyo:-

Kuna Ndugu Ashura Waijaa ambaye ni Msaidizi wa Mtendaji Mkuu II ambaye anafanya kazi Ofisi Binafsi ya Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Theresia Jacob ambaye ni Msaidizi wa Ofisi Mkuu na huyu yuko Ofisi Binafsi ya Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Mbegeya Malendemla ambaye ni Msaidizi wa Afya Mkuu, yuko Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko Ndugu Prudence Rweyomgeza, Afisa Sheria Mkuu I ambaye anatoka Idara ya Huduma za Sheria, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Maimuna Makoa ambaye ni Msaidizi wa Ofisi Mwandamizi, Idara ya Shughuli za Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Catherine Kitutu ambaye ni Mhudumu wa Jikoni na Mhudumu ndani ya Ukumbi wa Bunge anatoka Idara ya Kamati za Bunge, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yuko pia Ndugu Wilfred Magova, Afisa Hesabu Mwanadamizi, Idara ya Bajeti, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Mwajuma Ramadhani, Afisa Utafiti Mwandamizi, Idara ya Maktaba na Utafiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Gaitana Chima ambaye ni Msaidizi wa Ofisi Mwandamizi, Kitengo cha Fedha na Uhasibu, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Anselm Godfrey, Afisa Mkaguzi wa Ndani Mkuu II, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Ramadhani Shaban, Afisa Ugavi Mwandamizi, Kitengo cha Ununuzi na Ugavi, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko Pia Ndugu Naziel Mbaga, Katibu Mahsusi I, Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko Ndugu Christopher Kannonyele, Mwandishi wa Taarifa Rasmi za Bunge Mwandamizi, Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko pia Ndugu Fatuma Kiroga, Msaidizi wa Mtendaji Mkuu II, Kitengo cha TEHAMA, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Pia Ndugu Peter Magati, Katibu Msaidizi wa Bunge Mkuu II na Msaidizi wa *Serjeant-At-Arms* hapa Bungeni, Kitengo cha Ulinzi na Usalama, ahsante sana. *(Makofi)*

Wa mwisho ni Sherehe Mmanga ambaye ni Msaidizi wa Kumbukumbu I, Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar, ahsante sana. *(Makofi)*

Naona Mheshimiwa Ravia amepiga sana makofi atakuwa anatoka kwenye jimbo lake huyu, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nitumie fursa hii kuwapongeza sana watumishi wetu hawa ambao wametambuliwa mwaka huu 2023 kama wafanyakazi bora wa Bunge, lakini pia nimpongeze sana mshindi wa hawa wote anayewaongoza, dereva wetu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya pongezi hizo niwatakie kila la heri. Mwaka 2022 wale walioshinda sina hakika kama sura zao ziko hapo, lakini tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yenu na Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia pengine mtashinda tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**SPIKA:** Waheshimiwa wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Ashatu Kijaji, aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tarehe 21 hadi 22 Machi, 2023, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/2023. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia yaliyo mema na yenye kutupa baraka na siha njema na hatimaye kumudu kuyatekeleza yale tuliyokasimiwa na Mamlaka na

Umma wa Watanzania wote kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake na utayari wake wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini na kuifanya Tanzania kuwa eneo lenye mvuto kwa uwekezaji mpya na kupanua uwekezaji wa mitaji kwa miradi iliyopo Nchini tayari.

Mheshimiwa Spika, falsafa ya uchumi inasema uwekezaji endelevu hujengwa katika misingi ya imani. Ni katika misingi ya utawala bora na mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara yaliyojengwa chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mwanadiplomasia mahiri, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sasa tumeiona imani na hamu kubwa ya wawekezaji wa nje na ndani kuhitaji kuwekeza nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa dhati ya moyo wangu ninawiwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa, kwa kushirikiana na Naibu Waziri wangu, Viongozi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake tutaendelea kuacha milango yetu wazi wakati wote ili kusikiliza na kupokea maoni ya wawekezaji na wafanyabiashara juu ya namna ya kufanya maboresho zaidi katika Sheria, Sera na Miongozo yetu ili kupunguza vikwazo na kuendelea kuweka mazingira wezeshi na yanayotabirika kwa uwekezaji na ufanyaji biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa

Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa miongozo stahiki katika kukuza Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara nchini. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya Bajeti iliyowasilishwa kwenye Bunge lako tukufu tarehe 5 Aprili, 2023. Hotuba hiyo imetoa dira ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa mwaka 2023/2024 ambayo Wizara yangu itakuwa mstari wa mbele kuipokea na kuitafsiri kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar; na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa kuwa vinara wa kujenga mshikamano na kuchochea ushirikiano katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii ambazo ni chemchem ya maendeleo halisi ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Mudrick Ramadhan Soraga, Waziri wa Ofisi ya Rais Uwekezaji waSerikali ya mapinduzi Zanzibar kwa utayari wao na kunipa ushirikiano katika kutekeleza masuala ya Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza viongozi wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kushika nyadhifa mbalimbali. Kipekee, ninawapongeza Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki, Mbunge wa Kuteuliwa na Rais, na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa George Boniface

Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga na Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma, Mbunge wa Muheza kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu Tukufu. Mwenyezi Mungu akulinde na kukusimamia katika kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kuweza kusimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Viti Maalum na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na umakini wao wakati wa kujadili Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2023/2024. Ushauri na mwongozo wao umekuwa msingi muhimu katika kuandaa hotuba hii ninayoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa Baraza la Taifa la Biashara pamoja na sekta binafsi hususan Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania, Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania, Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake Tanzania na Baraza la Kilimo Tanzania kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Uwekezaji, Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda na Biashara Ndogo. Tutaendelea kuwategemea kama nguzo na mihimili muhimu ya kushirikiana katika kutekeleza kwa vitendo sera na mipango ya kisekta katika

kuendeleza viwanda na biashara na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wamiliki na waandishi wa vyombo vya habari kwa mchango wao mkubwa katika kuelimisha Umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji wa Wizara, taasisi na uendelezaji wa Sekta zake, kuvutia wawekezaji na kuhimiza uzalishaji viwandani. Nawaomba tuendeleze ari hiyo kwa lengo la kukuza uelewa kwa Umma ili washiriki kikamilifu katika kutekeleza masuala ya kuendeleza sekta hii na kutia chachu zaidi katika mafanikio tuliyoyapata.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza na kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Kondoa kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo. Nawapongeza kwa namna wanavyoshiriki shughuli za kiuchumi ili kujiletea maendeleo. Aidha, ninawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yenu hapa Bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kushamiri na kuleta matokeo ya mtu mmoja mmoja, Jimbo letu na hatimaye kuongeza mchango kwenye uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kwa ushauri na namna anavyosaidiana nami katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Naamini tutaendelea kushirikiana ili kuweza kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa pamoja na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo, ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Dkt. Hashil T. Abdallah, Katibu Mkuu Viwanda na Biashara; Dkt. Tausi M. Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Uwekezaji; Wakurugenzi, Wakuu wa

Vitengo na Taasisi; na Wafanyakazi wote wa Wizara. Napenda kuwashukuru sana na kuwapongeza sana kwa kazi yenu njema.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wanajimbo la amani, pamoja na Watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na viongozi wenzangu kutoa pole kwa Watanzania wote waliokumbwa na kadhia ya kuondokewa na wapendwa wao. Aidha, nawapa pole wananchi mbalimbali waliopata ajali katika mwaka huu na kusababisha majeruhi, ulemavu na uharibifu mkubwa wa mali. Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa ahueni waathirika wote ili warejee katika hali njema na hivyo kuendelea kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu yangu ambayo muda mwingi nipo nje ya nyumbani kwangu usingekuwa rahisi bila maombi na dua njema kutoka kwa watu wema. Nawashukuru sana Wazazi wangu; baba, Alhaji Abdallah Kijaji na mama yangu, Hajat Aziza Selemani; kwa mume wangu mpenzi, Dkt. Muhajir Kachwamba; na watoto wangu, Samirah na Aboubakar; ahsanteni sana kwa upendo, uvumilivu na utayari wenu unaonipa nguvu ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo, uzalendo na weledi wangu wote.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, viongozi wangu wa dini, ndugu, jamaa na marafiki wote, ahsanteni sana kwa kuendelea kunikabidhi kwa Mwenyezi Mungu ili niendelee

kutoa huduma njema kwa Taifa letu. Napenda kuwaahidi nyote na Watanzania kwa ujumla kwamba sitawaangusha na muda wote nitatenda majukumu yangu kwa kutanguliza maslahi ya Taifa letu mbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 na malengo ya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini. Juhudi hizo ni pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuuza fursa hizo kupitia makongamano ya ndani na nje ya nchi na kwenye ziara mbalimbali zinazofanywa na viongozi wetu wakuu wa nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara imesajili jumla ya miradi mipya 240 inayotarajiwa kuwekeza jumla ya Dola za Marekani milioni 4,387.17 na kutengeneza ajira kwa Watanzania 39,245, sawa na ongezeko la16.5% ikilinganishwa na miradi 206 iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kati ya miradi 240 iliyosajiliwa, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, miradi 187 sawa na asilimia 77.9 imeanza utekelezaji wake. Kwenye sekta za kilimo, miradi 18; majengo ya biashara, miradi10; miundombinu, miradi miwili; rasilimali watu, miradi mitano; viwanda, miradi101; huduma, miradi mitano; mawasiliano, mradi mmoja; utalii, miradi tisa; na usafirishaji, miradi 36.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda imeendelea kukua na kumilikiwa kwa sehemu kubwa na Sekta Binafsi. Kwa mujibu wa zoezi la utafiti wa utambuzi wa fursa za uwekezaji, viwanda na rasilimali lililofanyika nchini mwaka 2021 lilionesha kuwa viwanda vimesambaa nchi nzima na sehemu kubwa ya

viwanda hivyo ni vidogo sana ambavyo ni 62,400, sawa na asilimia 77; vidogo ni 17,274, sawa na asilimia 21; vya kati ni 684, sawa na asilimia 0.84; na vikubwa ni 618, sawa na asilimia 0.76.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi nchini zinazalishwa ndani ya nchi yetu, Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi na upanuzi wa viwanda vya kuzalisha sukari, kuzalisha mafuta ya kula, mbolea, nondo na mabati. Uhamasishaji huo umewezesha upatikanaji wa bidhaa hizi ndani ya nchi, kukuza mauzo ya nje na kuzalisha ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kufuatia uhamasishaji huo, viwanda mbalimbali vimeendelea kujengwa na kufanyiwa upanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji sukari nchini hufanywa na viwanda sita. Kati ya hivyo, viwanda vikubwa ni vinne ambavyo ni kiwanda cha sukari Kagera, Kiwanda cha Sukari Kilombero, Kiwanda cha Sukari Mtibwa, na Kiwanda cha Sukari *TPC* Moshi. Aidha, kuna kiwanda kimoja cha kati ambacho ni Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo, na Kiwanda Kidogo cha Sukari cha Manyara.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo kimeanza uzalishaji wa sukari mwezi Julai, 2022 na kinazalisha kwa kusaga kiasi cha miwa tani 1,500 hadi 1,800 kwa siku na kuzalisha sukari tani 30,000 kwa mwaka. Aidha, kiwanda kimeajiri wafanyakazi 600, ambapo kati ya wafanyakazi hao, wafanyakazi 250 ni wa kudumu na wafanyakazi 350 ni wa muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Sukari Kilombero kinamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia Msajili wa Hazina kwa asilimia 25, na Kampuni ya Illovo ambayo ina asilimia 75. Kiwanda hiki kipo katika hatua ya upanuzi ambao unalenga

kuongeza uzalishaji wa Sukari kufikia tani 271,000 kwa mwaka kutoka uzalishaji wa sasa wa tani 133,358 kwa mwaka. Upanuzi unaendelea vizuri na umefikia asilimia 46 kwa sasa. Kutokana na uzalishaji huo na upanuzi unaofanyika kiwanda hiki kinaajiri ajira za moja kwa moja 2,996 na zisizo ajira zisizo za moja kwa moja ni 50,000.

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha Sukari Kagera kilizalisha tani 123,190 katika mwaka 2022/2023 kutoka tani 82,400 zilizozalishwa mwaka 2021/2022. Mafanikio hayo yametokana na uwekezaji kwenye miundombinu ya barabara hasa Daraja la Kitengule ambalo lilikuwa ni kero kubwa huko nyuma na sasa limekamilika. Kiwanda kina uwezo wa kusafirisha miwa yake kwa gharama ndogo na muda mfupi. Pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha daraja hili linakamilika na tunarahisisha mazingira ya uwekezaji kwa wawekezaji wetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiwanda hiki kimefanya pia upanuzi kwa kuongeza vinu viwili vya kuchakata miwa na kufikia jumla ya vinu sita na upanuzi wa mashine nyingine za uzalishaji wa sukari. Kiwanda hiki kimetoa ajira za moja kwa moja, 436 na 10,667 za muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda hivi kumesababishwa na uwepo wa sera zinazotabirika na uboreshaji wa mazingira ya uzalishaji wa sukari nchini uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Uzalishaji sukari unaongezeka kutoka tani 379,191 msimu wa mwaka 2021/2022 hadi tani 460,000 msimu wa mwaka 2022/2023 ongezeko hili la uzalishaji sukari la zaidi ya tani 80,000 katika kipindi cha msimu mmoja tu ni kiwango cha juu kuwahi kutokea katika uzalishaji wa sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2023 Tanzania ina jumla ya viwanda 771 vya kuzalisha mafuta ya kula. Kati ya hivyo, viwanda 21 ni viwanda vikubwa na vya kati, na

viwanda vidogo ni 750. Aidha, viwanda hivyo vinazalisha tani 205,000 za mafuta ambapo tani 180,000 ni mafuta ya alizeti na tani 25,000 ni mafuta ya mawese na pamba. Viwanda vidogo vinatumia asilimia 20 tu ya uwezo uliosimikwa wa kusindika mbegu, wakati viwanda vikubwa na vya kati vinatumia asilimia 25 tu ya uwezo uliosimikwa.

Mheshimiwa Spika, viwanda hivi vinazalisha chini ya uwezo wake kutokana na ukosefu wa malighafi (mbegu za mafuta) ambazo hupatikana kwa takribani miezi minne tu. Aidha, mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takribani tani 570,000, hivyo tunaagiza tani 365,000 ili kutosheleza mahitaji ya mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022 matumizi ya bidhaa za chuma Nchini yameongezeka kutoka tani 226,000 hadi kufikia tani 1,000,000 kwa mwaka sawa na ongezeko la asilimia 303.54. Hadi Machi 2023 Nchi yetu ilikuwa na viwanda 25 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. Viwanda hivyo vipo katika makundi mbalimbali yanayojumisha bidhaa zikiwemo nondo, mambomba, misumari na seng'enge. Kati ya hivyo, viwanda vya kuzalisha nondo ni 16 vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,082,700 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 750,000 kwa mwaka, sawa na asilimia 69 ya uwezo uliosimikwa. Mahitaji ya nondo Nchini kwa mwaka ni tani 550,336 hivyo uzalishaji huo wa ndani hutosheleza mahitaji yote ya ndani na ziada kiasi cha tani 199,664 huuzwa nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, hadi mwezi Machi mwaka 2023 Tanzania ina viwanda viwili vikubwa vinavyozalisha mabati kuanzia hatua ya awali ambavyo ni *ALAF* na *MMI Steel* vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha jumla ya tani 158,000 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 58,189 kwa mwaka sawa na asilimia 37 ya uwezo uliosimikwa. Sambamba na viwanda hivyo vikubwa, viwanda vidogo zaidi ya 50 vya kukunja mabati hununua malighafi ya mabati yaliyokwisha

kupakwa rangi na kuyakunja migongo. Kwa ujumla viwanda hivyo vinavyozalisha bidhaa za chuma vimeajiri jumla ya wafanyakazi 23,588 ambapo wafanyakazi 3,588 ni ajira za kudumu na 20,000 ni ajira za muda.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2023 Tanzania ina viwanda vya saruji vipatavyo 14 ambapo viwanda vikubwa ni saba na vilivyobakia vinazalisha saruji kutokana na malighafi inayozalishwa na viwanda hivyo saba. Kutokana na takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2022, inaonesha kuwa viwanda vya saruji nchini vinazalisha tani 10,850,000 za saruji kwa mwaka. Ambapo mahitaji ya ndani ya nchi ni tani 7,100,000 kwa mwaka. Hivyo, kuna ziada ya tani 3,750,000 ambayo huuzwa katika soko la nje hususan katika nchi za *DRC* Congo, Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwezi wa Saba, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanikiwa kupata soko la jumla ya tani 9,765 za zabibu. Kati ya hizo, tani 9,265 zilinunuliwa na viwanda 18 vilivyopo Dodoma kwa ajili ya kuzalisha mchuzi na kutengenezea mvinyo na tani 500 zilinunuliwa na Kiwanda cha Jambo kwa ajili ya kuzalisha juisi. Aidha, kilo moja ya zabibu iliuzwa kwa wastani wa shilingi 1,200 na kufanya mauzo ya zabibu kuwa shilingi bilioni 11.7.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu 2023 tunataraji Kiwanda cha Jambo kitanunua tani 3,000 za zabibu kwa ajili ya kutengeneza juisi na hiyo ni baada ya Serikali kuweka mazingira mazuri ili tuondokane na matumizi ya zabibu za mvinyo pekee na sasa tutengeneze na juisi za zabibu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nguo ina jumla ya viwanda 10 vinavyofanya kazi. Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 15,300 na zisizo za moja kwa moja 45,000. Viwanda hivyo, kwa mwaka vina uwezo wa wastani wa kusokota nyuzi tani 36,742. Kusokota vitambaa milioni 145, kufuma vitambaa

tani 7,920 na uwezo wa kutengeneza mavazi zaidi ya nguo tofauti tofauti milioni 43.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya viwanda vya nguo ni ukosefu wa mitaji ya kuviwezesha viwanda hivyo kununua pamba inayokidhi mahitaji ya uzalishaji kwa mwaka. Ili kutatua changamoto hii, Serikali imeendelea kufanya majadiliano na umoja wa wenye viwanda vya nguo, kuona namna bora ya kuwezesha viwanda hivyi kupata mitaji kwa ajili ya kununua pamba yote inayozalishwa nchini na kuichakata hapa hapa Nchini. Aidha, Serikali imeondoa ushuru wa kuagiza malighafi ambazo hazipatikani ndani ya Nchi kwa lengo la kuhakikisha viwanda hivyo vinapata malighafi hizo kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2022, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika Soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ilikuwa ni Dola za Marekani milioni 1,802.2 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1,303.4 mwaka 2021 ambayo ni sawa na ongezeko asilimia 38.2. Kwa mwaka 2022, Tanzania iliagiza bidhaa kutoka Nchi za *SADC* zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 551.3 ukilinganishwa na Dola za Marekani milioni 653.9 kwa mwaka 2021 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 15.7. Ongezeko la mauzo ya Tanzania kwenye Soko la *SADC* ilitokana na kuongezeka kwa wauzaji wa bidhaa mbalimbali katika soko hilo. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na madini, pamba, chai, parachichi, kahawa, vigae, vyandarua, saruji, sabuni pamoja na mafuta ya kupaka.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2022, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia hususani kwa Nchi za China, India, Japan na Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 64.4 hadi kufikia dola za Marekani milioni 4,276.4, kutoka Dola za Marekani milioni 2,601.5 mwaka 2021. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na dhahabu, pamba, mbaazi, makaa ya mawe, shaba na tumbaku.

Aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia uliongezeka kwa asilimia 55.2 hadi kufikia dola za Marekani milioni 9,110.9 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 5,110.8 mwaka 2021. Ongezeko hili limetokana na uagizaji wa bidhaa ambazo hazizalishwi kwa wingi Nchini kama vile dawa baridi za binadamu, sukari ya kiwandani, nguo, magari na simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajatei ya Wizara kwa mwaka 2022/2023; katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 99,105,506,000. Kati ya Fedha hizo, shilingi 68,308,687,000 ziliidhinishwa kwa matumizi ya kawaida na shilingi 30,796,819,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 64,287,885,973.46, sawa na asilimia 53.67 ya Bajeti iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mipango; Wizara imeendelea kuhamasisha na kuvutia uwekezaji Nchini kwa kuandaa makongamano ya uwekezaji ikishirikiana na wadau mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imeandaa na kushiriki makongamano kumi likiwemo Kongamano la Tanzania na Umoja wa Ulaya. Hati za Makubaliano sita zenye thamani ya *Euro* Bilioni moja zilisainiwa baina ya Tanzania na Kampuni mbalimbali kutoka Umoja wa Ulaya. Hati hizo zilihusu Sekta za Usafirishaji na Uchukuzi, Nishati na Fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Hati za Makubaliano zilizosainiwa wakati wa ziara mbalimbali za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizofanya katika nchi za Ufaransa, Ubelgiji, Misri, Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu, Marekani na Oman. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Hati za Makubaliano 44 kati ya 50

zilizosainiwa ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji na Hati sita za Makubaliano zinaendelea kufuatiliwa. Wizara itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Hati hizi za Makubaliano hizo ili kuhakikisha malengo yanayotarajiwa kufikiwa kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa Watanzania yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa Mfumo wa Dirisha Moja la Kutoa Huduma kwa Wawekezaji kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huo unatarajiwa kuunganisha pamoja Taasisi 12 zinazohusika na uwezeshaji uwekezaji. Kukamilika kwa ujenzi wa mfumo huo utamuwezesha mwekezaji kupata vibali vya uwekezaji ndani ya siku tatu tu.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kisekta ilifanya uchambuzi na kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria 19. Kati ya hizo sheria 12 zenye lengo la kupunguza mwingiliano kati ya taasisi za udhibiti zilipitishwa na Bunge na kuanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai 2022. Mabadiliko hayo yaliwezesha kurekebishwa kwa ada na tozo 39 ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wawekezaji wetu pamoja na wafanyabiashara ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuendelea kuvutia uwekezaji Nchini, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa kongani za viwanda na maeneo maalum ya kiuchumi zikiwemo Kongani ya Viwanda ya Kwala, Eneo Maalum la Kiuchumi Mkulazi Morogoro, Eneo Maalum la Kiuchumi Nala Dodoma na Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai 2022 hadi Machi utekelezaji wa Kongani ya Viwanda ya Kwala Mkoani Pwani yenye eneo la ukubwa wa ekari 2,500 umefikia asilimia 30. Ambapo mwekezaji amekamilisha kazi ya kusafisha eneo la mradi, kuanza ujenzi wa geti kuu la kuingia, ujenzi wa jengo la

huduma kwa pamoja, ujenzi wa kituo cha polisi pamoja na kuweka miundombinu ya barabara za ndani. Mradi huo wa Kwala unatarajiwa kuvutia mtaji wa Dola za Marekani bilioni tatu pamoja na kuvutia viwanda 200. Pia, mradi utakapokamilika unatarajiwa kutoa ajira za ajira za moja kwa moja 100,000 na zisizo za moja kwa moja 300,000.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha uthamini wa eneo la viwanda la Nala lenye ukubwa wa ekari 1,500 lililopo katika Jiji la Dodoma. Taratibu za utwaaji wa eneo hilo kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwenda *EPZA* unaendelea. Eneo hili Maalum la Kiuchumi limepangwa kwa ajili ya viwanda vya mazao ya kilimo hususan mazao ya alizeti, zabibu na karanga, vifungashio, kuchakata madini, kuchakata malighafi za wanyama, vifaa vya ujenzi, nguo na kurahisisha biashara na kutunza bidhaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha mapitio mpango kabambe na upembuzi yakinifu wa uendelezaji wa mradi wa Bagamoyo. Kazi hii imezingatia mgawanyo wa uwekezaji wenye kuhusisha wawekezaji wa ndani na wale wa nje katika nyanja za uzalishaji wa viwanda vya kuongeza thamani, teknolojia na uwepo wa mji unaofungamanisha bandari, viwanda, huduma na makazi. Kukamilika kwa mpango mpango kabambe huo kunatoa fursa ya kulitangaza upya eneo hilo la Bagamoyo *SEZ* kiuwekezaji kwa wakezaji wa ndani, nje na wale wawekezaji wakubwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *TARURA* imeendelea na ujenzi wa awali wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita tatu katika eneo la Viwanda Zinga – Bagamoyo ambayo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 713.8 kwa wajasiriamali 2,203,838. Kati yao wanawake ni

1,234,149 sawa na asilimia 56 na wanaume 969,689 sawa na asilimia 44. Aidha, uchambuzi wa mikopo hiyo unaonesha jumla ya ajira 3,122,104 zilizalishwa. Kati ya ajira hizo, wanawake ni 1,623,494 sawa na asilimia 52 na wanaume ni 1,498,610 sawa na asilimia 48. Mikopo hiyo imetolewa katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa asilimia 31.07, ikifuatiwa na Sekta ya Viwanda na Biashara kwa asilimia 20.39.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo Kiwanda cha Viuadudu; Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma; Mradi wa Chuma Liganga ; Mradi wa Makaa ya Mawe wa Katewaka; na Mradi wa Magadi Soda – Engaruka.

Mheshimiwa Spika, wizara imefanya uhakiki wa mali za wananchi wanaopisha Mradi wa Makaa ya Mawe, Mchuchuma, kuanzia Mwezi Oktoba hadi Desemba mwaka 2022. Zoezi hili lilifanyika katika Vitongoji vya Nkomang'ombe, Idusi, Kilomos, Ntiule na Mhambalasi. Kati ya wananchi 651 waliotakiwa kuhakiki taarifa zao, wananchi 580 walijitokeza, sawa na asilimia 87. Vile vile Wizara imefanya uhakiki katika Eneo la Liganga vitongoji vya Mnyusi, Ilongi na Myorua katika Kijiji cha Mundindi na Kitongoji cha Luhaha katika Kijiji cha Amani kuanzia mwezi Oktoba – Desemba, 2022. Kati ya waathirika 494 waliotakiwa kuhakiki taarifa zao, walijitokeza 481 sawa na asilimia 98.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Aprili, 2023 Wizara imepokea fedha kiasi cha shilingi bilioni 15.4 sawa na asilimia 100 ya fedha, kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Miradi ya Liganga na Mchuchuma. Zoezi la ulipaji wa fidia linatarajiwa kukamilika Mwezi huu wa Tano na tayari timu ya Wizara ipo Mkoani Njombe kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkoa wa Njombe na hatimaye kuanza zoezi la ulipaji wa fidia ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia na kutoa fedha zote za fidia kwa wananchi wanaopisha mradi huu muhimu kama alivyahidi kwenye ziara yake aliyoifanya Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kiwanda cha viuadudu kilichopo *TAMCO* - Mkoa wa Pwani kilifanikiwa kuzalisha viuadudu lita 44,206 zenye thamani ya shilingi 642,737,524. Mauzo hayo yanajumuisha mauzo ya viuadudu lita 11,606 zilizouzwa Nchini, lita 11,500 ziliuzwa Kenya na lita 21,100 ziliuzwa kwa Kampuni ya *Swiss Tropical* na *Public Health.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kiwanda kimeweza kufanya matengenezo ya mitambo yake ambapo kwa sasa kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 2.5 kwa mwaka. Aidha, katika kipindi hicho Wizara imetafuta na kupata soko la kuuza bidhaa hiyo katika Nchi za Kenya, lita 28,000 Nchi ya Chad lita 80,000, Angola lita 25,000 na Niger lita 500,000. Ambapo jumla ya mahitaji ya nchi hizo ni lita 633,000. Hivyo ni wazi kuwa juhudi hizi zitaongeza uzalishaji wa kiwanda hadi kufikia lita 1,050,000 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu pia Mkutano wa Kamati ya Kitaifa ya Uondoaji wa vikwazo vya biashara visivyo vya kikodi uliofanyika mwezi Septemba 2022 Jijini Da es Saalam.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo jumla ya vikwazo 30 vilijadiliwa ambapo 10 vilitatuliwa na vitano vilifutwa kwa kukosa vielelezo vya kujitosheleza. Kwa upande wa Tanzania na Kenya vimebaki vikwazo 15 ambavyo vyote vipo katika ngazi ya wataalamu kwa majadiliano ili vyote

viweze kufutwa na wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara bila vikwazo vyovyote.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na ofisi za Balozi zetu zilizopo katika maeneo mbalimbali duniani katika kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ya mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini. Hii ni pamoja na kuainisha taarifa kuhusu kiasi na ubora wa bidhaa zinazohitajika na taratibu za kuyafikia masoko hayo na kuzifikisha taarifa hizo kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa ndani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na jitihada hizo, Wizara imefanikiwa kupata fursa ya soko la bidhaa mbalimbali nchini China. Bidhaa hizo ni kama vile maharage ya soya, korosho, mihogo na parachichi. Nchini Qatar tumepata soko la kuuza nyama, nchini Kenya tumepata soko la kuuza mchele na mahindi, nchini Uturuki tumepata soko la kuuza karanga, nchini India tumepata soko la kuuza mbaazi, soya na parachichi na Umoja wa Falme za Kiarabu tumepata soko la kuuza nyama pamoja na pilipili. Nchini Denmark tumepata soko la kuuza asali na pilipili kavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuendelea na majadiliano ya utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika, Wizara inaendelea na zoezi la kuhamasisha na kuhimiza wafanyabiashara kuchangamkia fursa za soko la *CFTA*. Wizara imefanya mikutano na warsha mbalimbali na sekta binafsi kuhusu matumizi ya fursa hizo. Mikutano ya hivi karibuni imefanyika tarehe 24 Januari, 2023 na tarehe 11 hadi 17 Aprili, 2023. Kupitia jitihada hizo, baadhi ya bidhaa zetu ikiwemo kahawa, viuadudu, matunda na mboga mboga, korosho na mchele zitaanza kuuzwa katika Soko la Eneo Huru la Biashara Afrika ifikapo Julai Mosi, mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei za vifaa vya ujenzi kwa mwaka 2022/2023 umeendelea kushuka na

kuonesha uhimilivu. Hali hii imesababishwa na kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa hizo sambamba na usimamizi madhubuti wa mwenendo wa soko la bidhaa hizo uliofanywa na Wizara pamoja na taasisi zake. Wastani wa bei ya nondo moja ya milimita 12 imeshuka kutoka shilingi 26,865 kipindi cha mwezi Februari 2022 hadi shilingi 24,417 mwezi Februari 2023 sawa na upungufu wa asilimia 9.1.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai mwaka 2022 hadi Machi 2023 Wizara ilikagua jumla ya magari 38,785 yaliyotumika nje ya nchi, sawa na asilimia 77.6 ya lengo la kukagua magari 50,000 kwa mwaka. Vile vile katika kipindi hicho, jumla ya vyeti vya ubora 80,055 vimetolewa kwa shehena ya bidhaa zitokazo nje ya nchi. Hii ni sawa na asilimia 80.1 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 100,000 kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Wizara imefanya uchunguzi wa mashauri manane yanayohusu mienendo inayoashiria kula njama ya kupanga bei kati ya washindani ambayo yako katika hatua mbalimbali za kiuchunguzi. Kati ya mashauri hayo, shauri moja la soko la uzalishaji na usambazaji wa nondo limetolewa maamuzi ya awali na mashauri mawili ya soko la sukari na soko la mafuta ya kula yamefungwa. Shauri moja la ununuzi wa korosho lipo katika hatua ya ukusanyaji wa taarifa, mashauri mawili ya soko la uagizaji na usambazaji wa magari mapya yapo katika hatua ya makubaliano na mashauri mawili yapo katika hatua ya utoaji wa maamuzi ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya kaguzi za kila siku katika Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilifanya kaguzi zote 249 ambazo ilipanga kufanya. Katika kaguzi hizo, jumla ya makasha 7,918 yalikaguliwa. Kati ya hayo, makasha 206 yalikutwa na bidhaa zilizokiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 zenye thamani ya shilingi

15,942,897,718. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na bidhaa za matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, vipuri vya piki piki na magari, vifaa vya kuandikia pamoja na zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inafanya kaguzi za kushtukiza 19 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Manyara, Iringa, Mbeya na Njombe. Katika kaguzi hizo bidhaa bandia zenye thamani ya shilingi 1,130,172,365 zilikamatwa. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na simu za mikononi, miswaki, vitasa vya milango, bidhaa za ujenzi pamoja na majani ya chai.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya bajeti mwaka 2023/2024. Katika mwaka 2023/2024 vipaumbele vikuu vya Wizara ni pamoja na kutekeleza miradi ya kielelezo, uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi na kongani za viwanda, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, kuratibu majadiliano ya biashara baina ya nchi na nchi na kuimarisha huduma za biashara na masoko.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2023/2024. Katika mwaka 2023/2024 Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya shilingi 119,017,998,000 katika Fungu 44. Kati ya fedha hizo, shilingi 75,451,494,000 ni matumizi ya kawaida ambapo shilingi 63,086,267,000 ni mishahara na shilingi 12,365,227,000 ni matumizi mengineyo. Aidha shilingi 43,506, 504,000 zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo shilingi 30,346,819,000 ni fedha za ndani na shilingi 13,219,685,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa maneno yafuatayo. Nichukue fursa hii kuwashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kutuunga mkono katika jitihada za kuendeleza sekta ya wwekezaji, viwanda na biashara. Tutaendeleza jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda

kama ilivyobainishwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kwa wafanyabiashara wetu fursa za ndani na nje ya nchi yetu zimefunguliwa na Mwanadiplomasia namba moja wa Taifa letu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni jukumu letu kuzienzi na kuzilinda jitihada hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uadilifu wetu ni muhimu sana ili kuhakikisha tunayashikilia masoko haya na kuyahudumia kwa manufaa yetu sote na uchumi wa Taifa letu. Ikumbukwe kwamba mfanyabiashara mmoja asiyemuadilifu anaweza kuharibu jina la nchi nzima na kuharibu fursa za masoko yetu yanayotafutwa kwa nguvu kubwa nje ya Taifa letuhii haikubaliki na itatafsiriwa kama uhujumu wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa wenye viwanda tuendelee kuzalisha bidhaa kulingana na uhitaji wa soko na kwa viwango vya kimataifa ili tunufaike na masoko yote ya kikanda na dunia kwa ujumla. Kwa wawekezaji wetu kwa ujumla. Mazingira ya uwekezaji ni salama sana chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ongezeni mitaji kwenye miradi mliyowekeza nasi na leteni miradi mingine mipya ili tuihudumie Afrika na dunia kwa ujumla kutoka Tanzania. Tupo tayari na wakati ni sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa watumishi wenzangu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tutaendelea kuacha milango yetu wazi wakati wote ili kusikiliza na kupokea maoni ya wawekezaji na wafanyabiashara juu ya namna ya kufanya maboresho zaidi katika sheria, sera na miongozo yetu ili kupunguza vikwazo na kuendelea kuweka mazingira wezeshi na yanayotabirika kwa uwekezaji na ufanyaji biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. ASHATU K. KIJAJI (MB.), WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tarehe 21 – 22 Machi, 2023, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/2023. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2023/2024.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa kutujalia yaliyo mema na yenye kutupa baraka na siha njema na kumudu kuyatekeleza yale tuliyokasimiwa na Mamlaka na umma wa Watanzania wote.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda nitumie fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umakini na umahiri wake katika kuliongoza Taifa letu kwa misingi ya uzalendo na mapenzi makubwa kwa Watanzania wote. Mwenyezi Mungu amzidishie moyo huo na kuendelea kumjalia afya njema,

hekima na busara ili matamanio ya Watanzania kuwa katika nchi ya neema, amani na inayotoa fursa za maendeleo kwa watu wake yaendelee. Aidha, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa, kwa kushirikiana na Naibu Waziri wangu, Viongozi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake nitaendelea kuyatekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa miongozo stahiki katika kukuza Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara nchini. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya Bajeti iliyowasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 5 Aprili, 2023. Hotuba hiyo imetoa dira ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Mwaka 2023/2024 ambayo Wizara yangu itakuwa mstari wa mbele kuipokea na kuitafsiri kwa vitendo.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar; na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa kuwa vinara wa kujenga mshikamano na kuchochea ushirikiano katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii ambazo ni chemchemi ya maendeleo halisi ya wananchi wake. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (SMZ) na Mheshimiwa Mudrick Soraga, Waziri wa Uwekezaji (SMZ) kwa utayari wao na kunipa ushirikiano katika kutekeleza masuala ya Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na

Biashara.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninawapongeza viongozi wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kushika nyadhifa mbalimbali. Kipekee, ninawapongeza Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu; Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki Mbunge wa Viti Maalum na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa George Boniface Simbachawene Mbunge wa Kibakwe na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega Mbunge wa Mkuranga na Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Hamis Mohamed Mwinjuma Mbunge wa Muheza kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Mwenyezi Mungu akulinde na kukusimamia katika kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kuweza kusimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Viti Maalum na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na umakini wao wakati wa kujadili Mpango na Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2023/2024. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa msingi muhimu katika kuandaa Hotuba hii ninayoiwasilisha leo.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa Baraza la Taifa la Biashara (Tanzania National Business Council – TNBC) pamoja na sekta binafsi: hususan Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (Tanzania Private Sector Foundation – TPSF); Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (Confederation of Tanzania Industries – CTI); Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (Tanzania Chambers of Commerce, Industry and Agriculture – TCCIA); na Baraza la Kilimo Tanzania (Agriculture Council of Tanzania – ACT) kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Uwekezaji, Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Tutaendelea kuwategemea kama nguzo na mihimili muhimu ya kushirikiana katika kutekeleza kwa vitendo sera na mipango ya kisekta katika kuendeleza viwanda na biashara na kuchochea ukuaji wa uchumi wetu kwa ujumla.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Nawashukuru wamiliki na waandishi wa vyombo vya habari kwa mchango wao mkubwa katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji wa Wizara, taasisi na uendelezaji wa Sekta zake, kuvutia wawekezaji na kuhimiza uzalishaji viwandani. Nawaomba tuendeleze ari hiyo kwa lengo la kukuza uelewa kwa umma ili washiriki kikamilifu katika kutekeleza masuala ya kuendeleza sekta hii na kutia chachu zaidi katika mafanikio tuliyoyapata.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kondoa kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo. Nawapongeza kwa namna wanavyoshiriki shughuli za kiuchumi ili kujiletea maendeleo. Aidha, ninawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yenu hapa Bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kushamiri na kuleta matokeo ya mtu mmoja mmoja, Jimbo na hatimaye kuongeza mchango kwenye Uchumi wa Taifa letu.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile, napenda kumpongeza Mheshimiwa Exaud S. Kigahe - Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Mbunge wa Mufindi Kaskazini; kwa ushauri na namna anavyosaidiana nami katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Naamini tutaendelea kushirikiana ili kuweza kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile, napenda kumpongeza Dkt. Tausi M. Kida – Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Uwekezaji kwa ushirikiano anaonipatia katika kuendeleza Sekta ya Uwekezaji nchini. Tutaendeleza ushirikiano huo kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu na watu wake.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa Viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Dkt. Hashil T. Abdallah, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara. Napenda kuwapongeza sana.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inafanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu na wadau mbalimbali katika kuendeleza Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Hivyo, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote wakiwemo Washirika wetu wa Maendeleo wa nje na ndani ya Nchi yetu.

16. ***Mheshimiwa Spika***, Natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar. Aidha, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wanajimbo la amani, pamoja na watanzania wote kwa kuondokewa na mpendwa wetu.

Mwenyezi ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Ninapenda kuungana na Viongozi wenzangu kutoa pole kwa Watanzania wote waliokumbwa na kadhia ya kuondokewa na wapendwa wao. Aidha, nawapa pole wananchi mbalimbali waliopata ajali nchini katika Mwaka huu na kusababisha majeruhi, ulemavu na uharibifu mkubwa wa mali. Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa ahueni waathirika wote ili warejee katika hali njema na hivyo kuendelea kulijenga Taifa letu.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kipindi cha Mwaka 2022/2023 na Malengo ya Mwaka 2023/2024.

## 2. HALI NA MWENENDO WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

### 2.1. Uwekezaji

19. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara imesajili jumla ya miradi mipya **240** (Wazawa - **89**, Wageni - **94** na Ubia - **57**) inayotarajiwa kuwekeza jumla ya dola za Marekani milioni **4,387.17** na kutengeneza ajira **39,245**, sawa na ongezeko la miradi **34** (16.5%) ikilinganishwa na miradi **206** (Wazawa - **63**, Wageni - **79** na Ubia - **64**) iliyosajiliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Kati ya miradi **240** iliyosajiliwa, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, miradi **187** sawa na asilimia **77.9** imeanza utekelezaji kwenye sekta za Kilimo (18), Majengo ya Biashara (10), Miundombinu (2), Rasilimali watu (5), Viwanda (101), Huduma (5), Mawasiliano (1), Utalii (9) na Usafirishaji (36).

20. ***Mheshimiwa Spika***, Tathmini inaonesha kuwa idadi ya

miradi iliyosajiliwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ipo katika Sekta za: Uzalishaji viwandani - miradi 104 (43.33%), Usafirishaji - miradi 56 (23.3%), Kilimo - miradi 18 (7.50%), Ujenzi wa majengo ya biashara - miradi 22 (9.2%), Utalii miradi 21 (8.8%), Huduma miradi 13 (5.4%), Miundombinu miradi 3 (1.3%) na Rasilimali watu miradi 3 (1.3%).

*21.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika miradi iliyosajiliwa kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Sekta ya Uzalishaji Viwandani inaongoza kwa kuwa na mtaji mkubwa wa dola za Marekani **bilioni 2.80** sawa na asilimia 65.40 ikifuatiwa na Sekta ya Usafirishaji yenye mtaji wa dola za Marekani **milioni 861.95** sawa na asilimia 19.65 na Sekta ya Ujenzi wa majengo ya biashara yenye mtaji wa dola za Marekani **milioni 382.45** sawa na asilimia 8.69. Aidha, sehemu kubwa ya miradi iliyosajiliwa katika kipindi hicho inatarajiwa kuwekezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam miradi **111** na Pwani miradi **33** ikifuatiwa na mikoa ya Mwanza miradi **12** na Arusha miradi **12** na Dodoma miradi **11**. Hali hiyo imechangiwa na uwepo wa masoko na miundombinu wezeshi kama vile umeme, maji, barabara, bandari na viwanja vya ndege katika mikoa hiyo.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023 Wizara imesajili miradi mitano (5) katika Maeneo Maalum kwa Mauzo Nje yenye thamani ya dola za Marekani **milioni 15.6.** Miradi hiyo inatarajiwa kuchangia mauzo ya nje yenye thamani ya dola za Marekani **milioni 12.46** na kutoa ajira kwa watu 1,247. Miradi hiyo imeanza uzalishaji katika sekta za kilimo (1), misitu (3) na bidhaa za viwandani (1).

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Miradi hiyo imewekeza kiasi cha dola za Marekani **milioni 11.99** na imeshafanya mauzo ya dola za Marekani **milioni 17.15** na imetoa ajira kwa watu 523 ambao kati yao wanaume ni 342 na wanawake ni 181. Aidha, masoko ya bidhaa zinazozalishwa ni pamoja na nchi za Ulaya, Marekani, Asia, Canada, Afrika ya Kusini, Jamhuri

ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan ya Kusini, China, Ukraine, Vietnam, Zambia, Misri, India, Dubai na Pakistani.

## 2.2. Viwanda

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Viwanda imeendelea kukua na kumilikiwa kwa sehemu kubwa na Sekta Binafsi. Kwa mujibu wa zoezi la utafiti wa mezani wa utambuzi wa fursa za uwekezaji, viwanda na rasilimali lililofanyika nchini mwaka 2021 lilionesha kuwa viwanda vimesambaa nchi nzima na sehemu kubwa ya viwanda hivyo ni vidogo sana ambavyo ni 62,400 sawa na asilimia 77, vidogo ni 17,274 sawa na asilimia 21, vya kati ni 684 sawa na asilimia 0.84 na vikubwa ni 618 sawa na asilimia 0.76.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo na viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi nchini ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa ndani ya nchi, kukuza mauzo ya nje na kuzalisha ajira. Kufuatia uhamasishaji huo, viwanda mbalimbali vimeendelea kujengwa na kufanyiwa upanuzi kama ifuatavyo:

### Viwanda vya Sukari

### i. Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo

26. ***Mheshimiwa Spika***, Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo kinachomilikiwa na Kampuni ya *Bakhresa Group* kimewekeza jumla ya dola za Marekani milioni 110 na kina eneo la ukubwa wa Hekta 10,000, ambapo hekta 500 ni eneo la kiwanda na hekta 2000 ni eneo la shamba lililolimwa hadi kufikia Machi, 2023. Kiwanda hicho kimeanza uzalishaji wa sukari mwezi Julai, 2022 na kinazalisha kwa kusaga kiasi cha miwa tani 1,500 hadi 1,800 kwa siku na kuzalisha sukari tani 30,000 kwa mwaka. Aidha, kiwanda kina jumla ya wafanyakazi 600, ambapo kati ya wafanyakazi hao,

wafanyakazi 250 ni wa kudumu na wafanyakazi 350 ni wa muda mfupi. Kiwanda kinatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025 na kitazalisha sukari tani 70,000 na kutoa ajira takriban 1,000**.** Kwa sasa, mahitaji ya sukari Nchini kwa Mwaka ni tani 482,000. Vile vile, uzalishaji wa sukari kwa mwaka 2021/2022 ulikuwa tani 379,280.83 na mwaka 2022/2023 tani 456,019.73. Kiwanda cha sukari cha Bagamoyo kikikamilika kinatarajiwa kupunguza pengo la uzalishaji wa sukari na utegemezi wa uagizaji sukari kutoka nje ya nchi.

**ii. Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi II (Mbigiri)**

27. ***Mheshimiwa Spika***, Ujenzi wa kiwanda cha Sukari cha Mkulazi II katika shamba la Mbigiri unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2023 na uzalishaji kuanza Julai, 2023. Kiwanda kitakapokamilika kinatarajiwa kuzalisha sukari tani 50,000 kwa mwaka. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, Kiwanda kimetoa ajira kwa watu 968, ambapo wafanyakazi 218 wapo kwenye ajira za kudumu, wafanyakazi 400 wameajiriwa kwa ajira zisizo za kudumu katika mashamba ya miwa, na wafanyakazi 350 wameajiriwa na mkandarasi anayejenga Kiwanda hicho.

**iii. Kiwanda cha Sukari cha Kilombero**

28. ***Mheshimiwa Spika*,** Kiwanda cha Kilombero Sugar Co. Ltd (KSCL) kinamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali (kupitia Msajili wa Hazina) kwa asilimia 25 na Kampuni ya Illovo Sugar Africa kwa asilimia 75. Kiwanda hicho kipo katika hatua ya upanuzi ambao unalenga kuongeza uzalishaji wa Sukari kufikia tani 271,000 kwa mwaka kutoka uzalishaji wa sasa wa tani 133,358 kwa mwaka ambapo upanuzi huo umefikia asilimia 46. Kutokana na uzalishaji huo, kiwanda kimezalisha ajira za moja kwa moja 2,996 na kikikamilisha upanuzi kitaongeza ajira mpya 1,504, na kufikia jumla ya ajira 4,500. Aidha, ajira zisizo za moja kwa moja ni 50,000 na unatarajia kuongeza ajira mpya 15,000 na kufikia jumla ya ajira zisizo za moja kwa moja 65,000.

**iv. Kiwanda cha Sukari cha Kagera**

29. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika msimu wa mwaka 2022/23 kiwanda cha Kagera Sugar kilizalisha tani 123,190 ikilinganishwa na tani 84,000 zilizozalishwa mwaka 2021/2022. Mafanikio hayo yametokana na Uwekezaji kwenye Kilimo, Upanuzi wa Shamba na Mitambo mipya ya kumwagilia. Aidha, kiwanda kimefanya upanuzi kwa kuongeza vinu viwili (2) vya kuchakata miwa na kufikia jumla ya vinu sita (6) na upanuzi wa mashine nyingine za uzalishaji wa sukari. Kiwanda hicho kimetoa ajira 436 za moja kwa moja na 10,667 za muda mfupi.

**v. Viwanda vya Mafuta ya Kula**

30. ***Mheshimiwa Spika***, Hadi kufikia Machi, 2023 Tanzania ina jumla ya viwanda 771 vya kuzalisha mafuta ya kula, kati ya hivyo, 21 ni viwanda vikubwa na vya kati; na viwanda 750 ni vidogo. Aidha, viwanda hivyo vinazalisha tani 205,000 za mafuta ambapo tani 180,000 ni mafuta ya alizeti na tani 25,000 ni mafuta ya mawese na pamba. Viwanda vidogo vinatumia asilimia 20 ya uwezo wa kusindika mbegu, wakati viwanda vikubwa na vya kati vinatumia asilimia 25 hadi 40 ya uwezo uliosimikwa. Viwanda hivi vinazalisha chini ya uwezo wake kutokana na ukosefu wa malighafi (mbegu za mafuta) ambazo hupatikana kwa takribani miezi minne (4) tu. Aidha, mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takribani tani 570,000, hivyo tunaagiza tani 365,000 ili kutosheleza mahitaji ya mafuta nchini.

**vi. Kiwanda cha Bia cha Serengeti Breweries - Moshi**

31. ***Mheshimiwa Spika*,** Kiwanda kipya cha *Serengeti Breweries* ni kiwanda kipya na cha kisasa kilichopo katika Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro. Kiwanda hicho kimewekeza jumla ya **shillingi bilioni 185.** Kiwanda hicho kimedhamiria kutumia malighafi zake kutoka kwa wakulima kwa **asilimia 70**. Kiwanda kitaongeza ajira kwa wakulima,

kukuza uchumi wa nchi na kuongeza Pato la Taifa. Uwekezaji huo umeenda sambamba na usimikwaji wa mitambo ya matanki 10 ya kuchachulia pombe, mstari mpya wa kufungashia vinywaji na mitambo ya kuzalishia pombe kali aina ya *sminorff ice* nyekundu na nyeusi.

**vii. Uongezaji Thamani Zao la Zabibu**

32. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kuhakikisha zao la zabibu linaongezwa thamani na wakulima wanapata hamasa ya kuongeza uzalishaji wa zao hilo, katika mwaka 2022/2023, Wizara iliwaunganisha wakulima na wasindikaji wadogo wa zabibu na viwanda vikubwa vya kutengeneza bidhaa zitokanazo na zabibu katika mkoa wa Dodoma. Hatua hiyo imewezesha wakulima kupata soko la uhakika ambalo limesaidia kuepusha kuharibika kwa zabibu zikiwa shambani kama ilivyokuwa siku za nyuma.

33. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanikiwa kupata soko la jumla ya tani 9,765 za zabibu. Kati ya hizo, tani 9,265 zilinunuliwa na viwanda 18 vilivyopo Dodoma kwa ajili ya kuzalisha mchuzi wa kutengenezea mvinyo na tani 500 zilinunuliwa na kiwanda cha Jambo kwa ajili ya kuzalisha juisi. Aidha, kilo moja ya zabibu iliuzwa kwa wastani wa shilingi **1,200** na kufanya mauzo ya zabibu kuwa **shilingi bilioni 11.7**. Wakulima walionufaika ni wa Vijiji vya Mpunguzi, Nkulabi, Matumbulu, Hombolo, Chibelela, Makang'wa, Mvumi na Veyula.

**viii. Viwanda vya Nguo na Mavazi**

34. ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ndogo ya nguo na mavazi ina jumla ya viwanda 10 vinavyofanya kazi. Viwanda hivyo na mahali vilipo ni: *JOC Ltd* (Shinyanga), *21 Century Textile Mills Ltd* (Morogoro), *Sunflag Textiles Ltd* (Arusha), *Mwatex* (2001) *Ltd* (Mwanza), *Namera Textiles Mills* (DSM), *NIDA Textiles Mills Ltd (DSM), A to Z Textile Mills Ltd (Arusha), Manzava Fabrics &*

*Production Ltd (Morogoro),* na *Tanzania Touku Garments* (DSM). Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 15,300 na zisizo za moja kwa moja 45,000. Viwanda hivyo, kwa mwaka vina uwezo wa wastani wa kusokota nyuzi (*spinning*) tani 36,742, kuseketa vitambaa (*weaving*) mita milioni 145, kufuma vitambaa (*knitting*) tani 7,920, na uwezo wa kutengeneza mavazi (*garments*) zaidi ya nguo tofauti tofauti milioni 43. Kwa takwimu za miaka mitatu ya hivi karibuni, uzalishaji katika viwanda vya nguo na mavazi umekuwa ukiongezeka. Kwa mfano, viwanda vya nguo na mavazi vilizalisha wastani wa mita za mraba milioni 45,415 mwaka 2019, mita za mraba milioni 53,067 mwaka 2020, na mita za mraba milioni 65,365 mwaka 2021. Changamoto kubwa inayovikabili viwanda vya nguo ni ukosefu wa mitaji ya kuviwezesha viwanda hivyo kununua pamba inayokidhi mahitaji ya uzalishaji kwa mwaka. Ili kutatua changamoto hii, Serikali imeendelea kufanya majadiliano na wenye viwanda kuona namna bora ya kuwezesha kupatikana malighafi ya kutosha. Aidha, Serikali imeondoa ushuru wa kuagiza malighafi ambazo hazipatikani ndani ya nchi.

**ix. Viwanda vya Mbolea**

35. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inaondokana na utegemezi wa kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi, Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya mbolea ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2023, Tanzania ina jumla ya viwanda 17 vya kuzalisha mbolea vikiwemo vikubwa viwili (2), kimoja (1) cha kati na 14 ni viwanda vidogo. Viwanda vikubwa ni Minjingu na *Intracom Fertilizer Limited*.

36. ***Mheshimiwa Spika***, Kiwanda cha Mbolea cha *Intracom Fertilizer Limited* kilichopo Dodoma eneo la Nala, ni kiwanda kikubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kiwanda hicho kinatarajia kuwekeza mtaji wenye thamani ya dola za Marekani milioni **180** na kitakapokamilika kitakuwa na uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mbolea tani **200,000** kwa mwaka na

kutoa ajira za kudumu **3,000** na ajira zisizo za kudumu zaidi ya **8,000**. Kwa sasa kiwanda kinazalisha tani **250** hadi tani **300** na kimetoa ajira **800** za kudumu. Aidha, kiwanda hicho kimepanga kuongeza *line* mbili 2 zaidi za uzalishaji ambazo zitafanya kuwa na *line* tatu zitakazokuwa na uwezo wa kuzalisha tani 600,000 ifikapo mwaka 2024.

37. ***Mheshimiwa Spika***, Kiwanda cha mbolea cha Minjingu kimewekeza shilingi bilioni **50** na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani **120,000** za mbolea kwa mwaka. Kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha tani **100,000** za mbolea aina ya *Phosphate* kwa mwaka ambazo ni sawa na asilimia 83 za uwezo uliosimikwa. Kiwanda hiki kimetoa ajira **200** za kudumu. Aidha, kiwanda hicho kimepanga kuongeza uzalishaji wa mbolea kutoka tani 120,000 hadi kufikia tani 300,000 kwa mwaka. Kwa sasa kiwanda kimesafisha eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo na imeagiza mitambo ya uzalishaji.

38. ***Mheshimiwa Spika***, Kwa ujumla Ongezeko hili la uzalishaji katika viwanda vyote vya mbolea litawezesha nchi kuweza kuzalisha tani 900,000 kwa mwaka ambazo ni asilimia 95 ya mbolea inayohitajika nchini kwa sasa. Pamoja na mipango mizuri ya viwanda hivyo, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi yanayovutia uwekezaji katika sekta hii ndogo ya mbolea.

**x. Viwanda vya saruji**

39. ***Mheshimiwa Spika***, Hadi Machi, 2023, Tanzania ina viwanda vya saruji vipatavyo 14 ambapo viwanda vikubwa (intergrated plant) ni saba (7) na vilivyobakia vinazalisha saruji kutokana na *clinker* iliyozalishwa na viwanda hivyo saba. Kutokana na takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2022, inaonesha kuwa viwanda vya saruji nchini vinazalisha tani 10,850,000 za saruji kwa mwaka ambapo mahitaji ya ndani ya nchi ni tani 7,100,000 kwa mwaka. Hivyo, kuna ziada ya tani 3,750,000 ambayo huuzwa katika soko la nje hususan katika nchi za Congo, Rwanda, Uganda, Malawi,

Zambia na Msumbiji. Changamoto za miundombinu zinazoikabili sekta hii zinatatuliwa na Serikali kupitia jitihada zinazoendelea katika uimarishaji na ujenzi wa reli, kuimarisha miundombinu ya umeme na ujenzi wa mitambo mipya ya kuzalisha umeme.

**xi. Viwanda vya kuzalisha bidhaa za chuma.**

40. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022, matumizi ya bidhaa za chuma nchini yameongezeka kutoka tani 226,000 hadi kufikia tani 1,000,000 kwa mwaka, sawa na ongezeko la asilimia 303.54. Hadi Machi, 2023, nchi yetu ilikuwa na viwanda 25 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. Viwanda hivyo vipo katika makundi mbalimbali yanayojumuisha bidhaa zikiwemo nondo, mabomba, misumari na seng'enge. Kati ya hivyo, Viwanda vya kuzalisha nondo ni 16 vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,082,700 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 750,000 kwa mwaka sawa na asilimia 69 ya uwezo uliosimikwa. Mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 550,336. Hivyo, uzalishaji huo wa ndani hutosheleza mahitaji yote ya ndani na ziada kiasi cha tani 199,664 huuzwa nje ya nchi.

**xii. Viwanda vya Mabati**

41. ***Mheshimiwa Spika***, Hadi machi, 2023 Tanzania ina viwanda viwili vikubwa vinavyozalisha mabati kuanzia hatua ya awali (intergrated) ambavyo ni ALAF na MMI Steel vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha jumla ya tani 158,000 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 58,189 kwa mwaka sawa na asilimia 37 ya uwezo uliosimikwa. Sambamba na viwanda hivyo vikubwa viwanda vidogo zaidi ya 50 vya kukunja mabati hununua malighafi ya mabati yaliyokwisha kupakwa rangi na kuyakunja migongo. Kwa ujumla viwanda hivyo vinavyozalisha bidhaa za chuma vimeajiri jumla ya wafanyakazi 23,588 ambapo wafanyakazi 3,588 ni ajira ya moja kwa moja na 20,000 ni ajira za muda.

**xiii. Viwanda vya Marumaru**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi Machi, 2023, Tanzania ina jumla ya viwanda viwili (2) vya marumaru ambavyo ni KEDA (T) Ceramics Co. Ltd kilichopo Chalinze na Goodwill (T) Ceramic Co Ltd kilichopo Mkuranga. Kiwanda cha Goodwill Co. Ltd kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mita za mraba milioni 18 za marumaru kwa mwaka ambapo uzalishaji halisi ni mita za mraba milioni 14.4 kwa mwaka. Aidha, Kiwanda cha KEDA (T) Ceramics Co. Ltd kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mita za mraba milioni 28.8 za marumaru kwa mwaka ambapo uzalishaji halisi ni mita za mraba milioni 18 kwa mwaka. Viwanda hivyo vimeajiri wafanyakazi 1,843 wa kudumu na 5,000 wa muda.

### 2.3. Biashara

43. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kushiriki majadiliano ya biashara baina ya Nchi na Nchi (*Bilateral*), Kikanda (*Regional*) na Kimataifa (*Multilateral*) kwa lengo la kupanua wigo wa fursa za masoko yenye masharti nafuu ya bidhaa na huduma na kuvutia biashara na uwekezaji. Katika mwaka 2022/2023 mwenendo wa biashara ulikuwa kama ifuatavyo:

### i. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022, Tanzania iliendelea kuboresha mahusiano ya kibiashara na nchi mbalimbali duniani. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa zilizouzwa kwenye soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ilikuwa dola za Marekani **milioni 1,414.9** ikilinganishwa na dola za Marekani **milioni 1,161.2** mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 17.93. Hali hiyo ilichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za kilimo, hususan chai, mahindi, ngano, alizeti, mchele, mbogamboga, pamoja na bidhaa za viwandani hususan, karatasi, vigae, saruji na chuma.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani **milioni 578.0** ziliagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika

Mashariki katika mwaka 2022 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani **milioni 562.8** mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Ongezeko hilo ni kutokana na uagizaji wa bidhaa ambazo zinahitajika viwandani kama vile Naitrojen, Tindikali ya Salfuriki na zinc oxide na bidhaa nyingine zinazohitajika sokoni kama vile *Blue Band* na Sabuni ya kufulia ya OMO. **(Jedwali Na. 1)**.

### ii. Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2022, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ilikuwa ni dola za Marekani **milioni 1,802.2** ikilinganishwa na dola za Marekani **milioni 1,303.4** mwaka 2021 ambayo ni sawa na ongezeko asilimia 38.2. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uuzaji wa bidhaa mbalimbali katika soko hilo. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na madini, pamba, chai, parachichi, kahawa, vigae, vyandarua, saruji, sabuni na mafuta ya kupaka.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2022, bidhaa zilizoagizwa kutoka soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zilikuwa na thamani ya dola za Marekani **milioni 551.3** ikilinganishwa na dola za Marekani **milioni 653.9** mwaka 2021, sawa na upungufu wa asilimia 15.7. Upungufu huo ulitokana na kuimarika kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na kuongezeka kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nchi wanachama zikiwemo juisi mchanganyiko, mabati na bidhaa za chuma. **(Jedwali Na. 2)**.

### iii. Soko la Ulaya

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2022 thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda soko la Ulaya ilipungua hadi dola za Marekani milioni 955.6 kutoka dola za Marekani **milioni 1,346.1** mwaka 2021, sawa na upungufu wa asilimia 29.1. Kupungua huko kulisababishwa na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 na Vita kati ya Urusi na Ukraine. Aidha, uagizaji wa

bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya umeongezeka kwa asilimia 12.4 na kufikia dola za Marekani **milioni 1,720.4** mwaka 2022 ikilinganishwa na dola za Marekani **milioni 1,530.3** mwaka 2021. Bidhaa zilizoagizwa na Tanzania kutoka Ulaya ni pamoja na Madawa baridi ya binadamu, Pembejeo za kilimo kama mbolea (urea), Vifaa vya kutengeneza reli, Lami ya *petrol*, Kloridi ya potasiam na *Reagent* ya maabara **(Jedwali Na. 3)**.

**iv. Bara la Asia**

49. ***Mheshimiwa Spika*,** Mwaka 2022, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia hususani kwa nchi za China, India, Japan na Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 64.4 hadi kufikia dola za Marekani **milioni 4,276.4** kutoka dola za Marekani **milioni 2,601.5** mwaka 2021. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na dhahabu, pamba, mbaazi, makaa ya mawe, shaba na tumbaku. Aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia uliongezeka kwa asilimia 55.2 hadi kufikia dola za Marekani **milioni 9,110.9** ikilinganishwa na dola za Marekani **milioni 5,110.8** mwaka 2021. Ongezeko hilo limetokana na uagizaji wa bidhaa ambazo hazizalishwi kwa wingi nchini kama vile dawa baridi za binadamu, sukari ya kiwandani, nguo, magari na simu za mkononi.

**v. Soko la Marekani Kupitia Mpango wa AGOA**

50. ***Mheshimiwa Spika*,** Mwaka 2022, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia Mpango wa AGOA yalikuwa jumla ya dola za Marekani **milioni 74.77** ikilinganishwa na dola za Marekani **milioni 33.04** kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 126.3. Ongezeko hilo limesababishwa na kuondolewa kwa amri ya kujifungia ndani (Lockdown) nchini Marekani kulikotokana na kujilinda na ugonjwa wa UVIKO-*19*. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi katika soko hilo ni nguo na mavazi na bidhaa za mazao ya kilimo. **(Jedwali Na. 4)**.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na uwepo wa masoko ya upendeleo, bado Tanzania ina fursa kubwa ya kuongeza mauzo ya bidhaa hususani bidhaa za kilimo na viwandani. Changamoto kubwa imekuwa ni uzalishaji mdogo, usio endelevu na masuala ya ubora. Changamoto hizo zinaendelea kufanyiwa kazi na Serikali ili kuongeza uzalishaji wenye tija na kukidhi ubora unaotakiwa kwa kutoa elimu ya mara kwa mara kwa wafanyabiashara na wakulima wetu kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mashamba Darasa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo.

## 3. MAZINGIRA YA UWEKEZAJI NA BIASHARA NCHINI

### 3.1. Sera

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara nchini ili kuvutia mitaji kutoka ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya Sera mbalimbali zinazosimamia Uwekezaji, Viwanda na Biashara nchini. Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996, Sera ya Maendeleo ya Viwanda (1996-2020) na Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003). Sera hizo ziko katika hatua ya ukusanyaji wa maoni ya wadau. Aidha, Sera ya Taifa ya Biashara (2003) ipo katika ngazi ya maamuzi ya Serikali. Sera hizo zinafanyiwa mapitio ili ziendane na mazingira ya sasa ya uwekezaji na biashara ikiwa ni pamoja na kujumuisha vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka (2021/2022 – 2025/2026) na mabadiliko mbalimbali yakiwemo ya kiuchumi na kiteknolojia.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji. Lengo ni kuongeza ushiriki wa Watanzania kupitia ajira, uhawilishaji teknolojia, ununuzi wa

bidhaa na huduma za ndani na huduma kwa jamii. Katika kufanikisha kazi hiyo, Wizara inaendelea kufanya tathmini ya hali ya ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji nchini. Tathmini hiyo imefanywa kwa kukutana na wadau mbalimbali wanaotekeleza masuala ya ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji ikiwa ni pamoja na wizara, taasisi za Serikali, taasisi za sekta binafsi, wawekezaji, wajasiriamali wadogo na wa kati, taasisi za udhibiti na watoa huduma. Aidha, tathmini hiyo itasaidia kuandaa Sera ya Taifa ya Ushiriki wa Watanzania kwa kuzingatia mapendekezo yatakayobainishwa katika taarifa ya tathmini.

**3.2. Sheria**

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliandaa na kuwasilisha Bungeni Muswada wa kutunga Sheria Mpya ya Uwekezaji ya mwaka 2022. Sheria hiyo ilipitishwa na Bunge mwezi Novemba, 2022. Aidha, mwezi Februari, 2023 Sheria hiyo ilisainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutangazwa katika gazeti la Serikali. Wizara imeendelea na maandalizi ya Kanuni ili kuwezesha utekelezaji wa sheria hiyo.

55. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mapitio ya Sheria za Ukanda Maalum wa Kiuchumi (SEZ) na Eneo Maalum la Uzalishaji kwa Mauzo Nje (EPZ) kwa lengo la kutoa mapendekezo yatakayopelekea kupunguza kero za kiuwekezaji hususani eneo la forodha kwa baadhi ya uzalishaji bidhaa na uuzaji wa bidhaa ikiwemo bidhaa za mifugo unaohusu programu hizo mbili zenye vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje. Aidha, Wizara imeendelea kushiriki kikamilifu kwenye programu zinazoratibiwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika uboreshaji na uandaaji wa kanuni (EAC Regulations) itakayopelekea sheria ya Ukanda Maalum wa Kiuchumi kuhuishwa katika sheria za forodha za Afrika Mashariki (East African Custom Management Act) hivyo kuondoa kero ya muda mrefu kwa wawekezaji wa

programu ya Ukanda Maalum wa Kiuchumi.

56. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilikusanya maoni ya wadau kuhusu marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara (Sura 208). Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria hiyo yaliwasilishwa kwa wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambapo maoni yaliyokusanywa ni pamoja na kurazinisha (harmonization) shughuli za utoaji wa Leseni na Vibali vya Biashara na kupunguza viwango vya adhabu na faini ili kutoathiri mitaji na kuongeza gharama za kufanya biashara nchini.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu kikao cha kujadili changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda, Sura ya 46 ya mwaka 1967 kilichofanyika mwezi Desemba, 2022 na kujumuisha washiriki kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Wizara ilifanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kuongeza kasi ya Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda nchini. Pamoja na mapungufu yaliyobainika katika Sheria hiyo, pande zote mbili zilipendekeza kuendelea kuitumia Sheria hiyo wakati jitihada za kuifanyia marekebisho zikiendelea kuchukuliwa kwa kuwashirikisha wadau wote muhimu. Aidha, timu ya wataalam wa TEHAMA kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar wanaendelea kushirikiana na BRELA kufanya muunganiko wa mifumo ya utoaji na usajili wa leseni za Viwanda ili iweze kusomana.

### 3.3. Mikakati

#### A. Marejeo ya Mkakati wa Pamba, Nguo na Mavazi na Mkakati wa Kuvilinda, Kuvikuza na Kuviendeleza Viwanda vya Ndani

58. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na marejeo ya mikakati mbalimbali ya kuendeleza Sekta ya Viwanda nchini

ukiwemo Mkakati wa Nguo na Mavazi. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya mkakati huo na wadau mbalimbali wameshiriki kutoa maoni. Vile vile, Wizara inaendelea na zoezi la kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mkakati wa Kuvikuza, Kuviendeleza na Kuvilinda Viwanda wa Mwaka 2011. Utekelezaji wa Mkakati huo pamoja na masuala mengine unalenga kuendelea kuiwezesha sekta binafsi kutekeleza majukumu yake kama mhimili mkuu wa uchumi. Mkakati huo una lengo la kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa unakidhi mahitaji ya ubora ili kuongeza ushindani nje na ndani ya nchi na kuendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vinavyotumia malighafi za hapa nchini.

**B. Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje (National Export Strategy – NES). Rasimu ya Mkakati imeandaliwa na kupata maoni ya wadau (*validation workshop*) kutoka pande zote mbili za Muungano. Maboresho ya rasimu ya mkakati huo yanaendelea kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na wadau na pindi yatakapokamilika Mkakati huo utazinduliwa. Kukamilika kwa Mkakati huo kutahamasisha uongezaji wa uzalishaji wa bidhaa, kukuza mauzo ya nje, kuongeza Pato la Taifa na ajira nchini.

**3.4. Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Nchini**

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kisekta ilifanya uchambuzi na kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria 19, kati ya hizo sheria 12 zenye lengo la kupunguza mwingiliano katika taasisi za udhibiti zilipitishwa na Bunge na kuanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai 2022. Mabadiliko hayo yalisababisha kurekebishwa kwa ada na tozo 39. Aidha, Serikali imeanzisha Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zote 184 na Sehemu za Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwenye Sekretarieti ya Mikoa yote 26 hapa nchini ambapo utekelezaji wake ulianza rasmi tarehe 1 Julai, 2022.

Uanzishwaji wa Idara na Sehemu hizi ni chachu ya maboresho mbalimbali ya mazingira ya biashara katika mamlaka hizo ikiwa ni pamoja na: kuimarisha mfumo wa usimamizi wa masuala ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa sekta binafsi na kuharakisha utatuzi wa changamoto zao; na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) katika ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na maboresho hayo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu- Sera, Bunge na Uratibu, Sekta Binafsi na Umoja wa Ulaya ilifanya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) na kuandaa Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa MKUMBI (Blueprint Impact Assessment Report). Lengo lilikuwa kupata hali halisi ya utekelezaji wa MKUMBI kwa kipindi chote cha utekelezaji kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22. Tathmini ilionesha matokeo chanya katika maeneo muhimu. Maeneo hayo ni (a) wastani wa siku za kupata vibali kutoka mamlaka za uthibiti ulipungua kutoka wastani wa siku 14 hadi siku tatu (3) pekee baada ya maboresho; (b) kupungua kwa foleni au kutokuwa na foleni kabisa katika Ofisi za Mamlaka za Udhibiti kutokana na kuanzishwa kwa mifumo ya kielektroniki; na (c) kupungua kwa idadi ya siku zinazotumiwa na malori ya mizigo kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Mpaka wa Zambia (Tunduma) na Rwanda (Rusumo) kutoka wastani wa siku nne (4) na siku saba (7) hadi wastani wa siku mbili (2) na siku tatu (3), mtawalia.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Matokeo mengine chanya ni (d) kuondolewa kwa muingiliano wa mamlaka kati ya TFDA na TBS, kati ya Taasisi ya Udhibiti na Viatilifu katika Ukanda wa Kitropiki (TPRI) na Idara ya Mimea umeondolewa. Aidha, Serikali imefanya mapitio ya Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) Sura ya 415 iliyokuwa ikitoa haki ya upekee (excusive mandate) ya uondoaji na usafirishaji wa

shehena kwa njia ya maji (clearing and forwarding) kwa bidhaa mbalimbali zinazosafirishwa kwa njia ya maji zikiwepo mafuta ya kula, sukari, ngano, kemikali za viwandani, makinikia, wanyama hai kwa mujibu wa sheria ya wanyamapori, kemikali zinazotumika migodini, nyara za Serikali, silaha na vilipuzi. Sheria hiyo imerekebishwa na hivyo kwa sasa TASAC inatoa huduma hizo kwa bidhaa zifuatazo; makinikia, wanyama hai, kemikali zinazotumika migodini, nyara za Serikali, silaha na vilipuzi. Hatua hiyo imeongeza ushindani na ushiriki wa sekta binafsi katika biashara hiyo; na (e) mwitikio wa sekta binafsi katika ufuasi (compliance) wa sheria, kanuni na taratibu kwenye ufanyaji biashara umeongezeka na hatimaye umeongeza mapato kwa Mamlaka za Udhibiti na kupunguza gharama za kufanya biashara kwa sekta binafsi.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuongeza uwazi kwa wawekezaji na wafanyabiashara katika eneo la ada, tozo na faini wanazopaswa kulipa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na wadau mbalimbali inaendelea na zoezi la kuandaa mfumo/dirisha litakaloainisha ada, tozo na faini zinazotozwa kwa kila aina ya kibali au leseni zinazotolewa. Tayari ubunifu (design) wa mfumo/dirisha huo umekamilika na ujenzi wa mfumo/dirisha unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2023.

## 4. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA 2022/2023

### 4.1. Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2022/2023

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 99,105,506,000**. Kati ya Fedha hizo, **shilingi 68,308,687,000** ziliidhinishwa kwa matumizi ya kawaida na **shilingi 30,796,819,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai,

2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya **shilingi 64,287,885,973.46**, sawa na asilimia **53.67** ya Bajeti iliyopitishwa na Bunge. Aidha, fedha zilizopokelewa zinajumuisha kiasi cha **shilingi 882,128,048** kupitia uhamisho wa kati ya mafungu (Reallocation Between) kwa ajili ya taasisi ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani kuhamia Dodoma.

### 4.1.1. Matumizi ya Kawaida

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilitengewa jumla ya **shilingi 68,308,687,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 8,728,788,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **shilingi 59,579,899,000** kwa ajili ya Mishahara. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilipokea jumla ya s**hilingi 6,279,188,030.27** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na **asilimia 71.94** ya fedha zilizotengwa na **shilingi 41,595,200,672.15** kwa ajili ya Mishahara sawa na **asilimia 69.81** ya fedha iliyotengwa.

66. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilitengewa **shilingi 30,796,819,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 30,346,819,000** ni fedha za ndani na **shilingi 450,000,000** ni fedha za nje. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilipokea jumla ya **shilingi 16,413,497,271.04** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 53.30** ya fedha zilizotengwa.

## 4.2. Utekelezaji wa Mipango

### 4.2.1. Uwekezaji

### A. Kuvutia Uwekezaji Ndani na Nje ya Nchi

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini kwa kuandaa makongamano ya

uwekezaji ikishirikiana na wadau mbalimbali. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imeandaa na kushiriki makongamano kumi (10) ndani na nje ya nchi, ikiwemo: *The Africa Debate* lililofanyika Jijini London, Uingereza; Mkutano wa Uwekezaji wa Biashara ya Kilimo uliofanyika Jijini Dar es Salaam; Kongamano la Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA) lililofanyika Kigali, Rwanda; Kongamano la Kuvutia Uwekezaji kutoka Nje ya Afrika (MIGA Africa FDI) lililofanyika Jijini Dar es Salaam; Kongamano la Pili la Uwekezaji kati ya Uingereza na Tanzania; Kongamano la Uwekezaji wa Maendeleo Endelevu Tanzania (SDG Investors Map); na Kongamano la Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU). Katika Kongamano la Tanzania na Umoja wa Ulaya lililofanyika mwezi Februari, 2023, Hati za Makubaliano sita (6) zenye thamani ya Euro Bilioni moja zilisainiwa baina ya Tanzania na Kampuni mbalimbali kutoka Umoja wa Ulaya. Hati hizo zilihusu sekta za Usafirishaji na Uchukuzi, Nishati na Fedha. Hati hizo ni pamoja na: Hati ya Makubaliano kati ya Ufaransa na Tanzania katika sekta ya anga (Aviation); Hati ya Makubaliano kati ya Bandari ya Kimataifa ya *Antwerp* na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania; Hati ya Makubaliano ya Kujenga Kituo cha Kuzalisha Umeme wa Maji Kakono mkoani Kagera; Hati ya Makubaliano kati ya *European Investment Bank* na Benki za NMB, CRDB na KCB; na Hati mbili za Makubaliano kati ya *Netherland Bank* na NMB.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Hati za Makubaliano (MoUs) zilizosainiwa wakati wa ziara mbalimbali za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizofanya katika nchi za Ufaransa, Ubelgiji, Misri, Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE), Marekani na Oman. Katika ziara hizo, Mheshimiwa Rais ameweka kipaumbele suala la kuvutia uwekezaji kutoka nje kwa kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini na kueleza jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuweka mazingira

wezeshi ya biashara na uwekezaji nchini. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Hati za Makubaliano (MoUs) 44 kati ya 50 ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji, Hati za Makubaliano sita (6) zinaendelea kufuatiliwa. Wizara itaendelea kufuatilia utekelezaji wa Hati za Makubaliano hizo ili kuhakikisha malengo yanayotarajiwa kufikiwa kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa ajira kwa watanzania yanafikiwa.

**B. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji**

69. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa Mfumo wa Dirisha Moja la Kutoa Huduma kwa Wawekezaji kwa Njia ya Kielektroniki (Tanzania Electronic Investment Single Window - TeIW). Mfumo huo unatarajiwa kuunganisha pamoja Taasisi 12 zinazohusika na uwezeshaji uwekezaji. Ujenzi wa Mfumo awamu ya kwanza umekamilika na umeunganisha mifumo ya taasisi saba (7) ambazo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); Idara ya Uhamiaji, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC). Aidha, ujenzi wa mfumo kwa awamu ya pili utahusisha uunganishaji wa taasisi tano (5) ambazo ni: Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), na unatarajia kuanza kutekelezwa kuanzia mwezi Mei, 2023 baada ya uzinduzi wa mfumo kwa awamu ya kwanza.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Kukamilika kwa ujenzi wa Mfumo huo, kutakuwa na manufaa kwa wawekezaji na taifa kiujumla ikiwemo: mwekezaji kuweza kusajili mradi popote ndani na nje ya nchi bila kuonana na watoa huduma wa taasisi husika; mwekezaji kupata kipaumbele cha kuhudumiwa kwa haraka katika taasisi zinazotoa huduma;

mwekezaji kuweza kuingiza taarifa zake mara moja kwenye mfumo wa TeIW; na mwekezaji kupata vibali vya uwekezaji ndani ya siku tatu (3).

**C. Kuratibu Uanzishwaji na Uendelezaji wa Miradi Mikubwa ya Uwekezaji yenye Manufaa Mapana kwa Taifa**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika jitihada za kuendelea kuvutia uwekezaji nchini, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa Kongani za Viwanda na Maeneo Maalum ya Kiuchumi kama ifuatavyo:-

**Kongani ya Viwanda ya Kwala - Pwani**

72. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu uendelezaji wa Kongani ya Viwanda ya Kwala mkoani Pwani yenye eneo la ukubwa wa ekari 2,500 inayotarajiwa kuvutia mtaji wa dola za Marekani bilioni 3. Aidha, kukamilika kwa mradi huo utawezesha uvutiaji wa viwanda 200 na ajira za moja kwa moja 100,000, ajira zisizo za moja kwa moja 300,000 na kuzalisha bidhaa za takriban dola za Marekani **bilioni 6** kwa mwaka.

73. ***Mheshimiwa Spika***, Utekelezaji wa Mradi umefikia asilimia 30 ambapo Mwekezaji (SINO TAN) ametekeleza yafuatayo katika eneo la mradi:- kusafisha, kuanza ujenzi wa geti kuu la kuingia, ujenzi wa jengo la huduma kwa pamoja, ujenzi wa kituo cha polisi, pamoja na kuweka miundombinu ya barabara za ndani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI inaendelea kuhakikisha ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme, gesi na barabara inakamilika kwa wakati. Vile vile, maombi ya hadhi ya Mwekezaji Mahiri Maalum yamejadiliwa na Kamati ya Taifa ya Uwekezaji Rasilimali mwezi Oktoba, 2022 kwa ajili ya kupatiwa vivutio maalum vya ziada vya uwekezaji.

**Eneo Maalum la Kiuchumi Mkulazi SEZ - Morogoro**

74. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutafuta

mwekezaji wa kuendeleza eneo Maalum la Kiuchumi Mkulazi SEZ - Morogoro kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari na mazao mengine yanayofaa kupitia mradi wa shamba la Mkulazi lenye ukubwa wa hekta 60,103. Kupitia jitihada hizo, Wizara imepokea maombi kutoka kwa kampuni ya *Eagles Hills Properties LLC* (Kampuni dada ya Symphony Invest. Ltd iliyokuwa imesaini Hati ya Makubaliano wakati wa maonesho ya Dubai Expo) ikiomba kupatiwa shamba hilo kwa ajili ya uwezekaji katika mradi wa sukari. Wizara inaendelea kufanya uchambuzi wa maombi hayo.

**Eneo Maalum la Kiuchumi Nala - Dodoma**

75. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaratibu uendelezaji wa eneo la viwanda la Nala lenye ukubwa wa ekari 1,500 katika Jiji la Dodoma. Aidha, Mpango Kabambe wa uendelezaji wa eneo hilo ulioandaliwa na Jiji la Dodoma utahuishwa ili kuendana na programu ya SEZ. Eneo hili Maalum la Kiuchumi (SEZ) limepangwa kwa ajili ya viwanda vya mazao ya kilimo hususan mazao ya alizeti, zabibu na karanga. Pamoja na viwanda vya vifungashio, kuchakata madini, kuchakata malighafi za wanyama, vifaa vya ujenzi, nguo na vituo vya kuwezesha biashara usafirishaji na kutunza bidhaa (trade logistics and commercial centers). Uthamini wa eneo umekamilika na taratibu za utwaaji wa eneo kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwenda EPZA unaendelea.

**Mradi wa Eneo Maalum la Kiuchumi Bagamoyo**

76. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya mapitio ya Mpango Kabambe na upembuzi yakinifu kwa Uendelezaji wa Bagamoyo SEZ na mpango huo umekamilika mwezi Aprili, 2023. Kazi hiyo imetekelezwa na taasisi ya ushauri ya ABECC inayomilikiwa na Chuo Kikuu cha Ardhi na imekamilika kwa asilimia 90. Kazi hii imezingatia mgawanyo wa uwekezaji wenye kuhusisha wawekezaji wa ndani na wale wa nje katika nyanja za uzalishaji wa viwanda vya kuongeza thamani, teknolojia na uwepo wa mji unaofungamanisha bandari,

viwanda, huduma na makazi. Kukamilika kwa mpango huo kunatoa fursa ya kulitangaza upya eneo hilo la Bagamoyo SEZ kwa wawekezaji wa ndani, nje na wale wawekezaji wakubwa (Strategic Investors) katika sekta ya uendelezaji wa kongani za viwanda na kuvutia uzalishaji. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TARURA imempata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa awali wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 3 katika eneo la viwanda Zinga - Bagamoyo. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, ujenzi huo umefikia asilimia 15. Ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2023.

### 4.2.2. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi

### A. Kuimarisha Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

77. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kuimarisha mifumo ya Majadiliano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (Public Private Dialogue - PPD) kupitia Mabaraza ya Biashara ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa kwa lengo la kutatua vikwazo na changamoto zinazokwamisha biashara na uwekezaji. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya mikutano 10 imefanyika katika ngazi ya mikoa. Matokeo ya vikao hivyo ni kuendeleza juhudi za makusudi za kuchochea ushiriki wa Sekta Binafsi katika kufanya maboresho muhimu ya Sera, Sheria, Miongozo na Kanuni mbalimbali zinazosimamia Sekta Binafsi.

78. ***Mheshimiwa Spika***, Maboresho hayo yanalenga kujenga mazingira rafiki na wezeshi ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji kwani Sekta Binafsi inapoimarika na kuwa shindani inatarajiwa kuchochea maendeleo ya Nchi kupitia makusanyo ya kodi mbalimbali na kuzalisha fursa za ajira. Aidha, maboresho haya ni muhimu kwa lengo kujenga uwezo kwa wananchi kutekeleza Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA). Vie vile, mikutano hii inatoa

fursa kwa Sekta Binafsi kuelewa kuhusu mwelekeo wa Serikali na majukumu ya msingi yanayotekelezwa kwa lengo la kuaminiana miongoni mwa wadau na hivyo kuifanya Sekta Binafsi kuwa endelevu. Maboresho hayo yamewezesha kutatua changamoto zinazokabili sekta binafsi nchini ikiwa ni pamoja na kupunguza kodi na tozo 39 katika mwaka 2022/2023.

**B. Kuandaa Kanzidata ya Sekta Binafsi Nchini**

79. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya utambuzi wa muundo wa Sekta Binafsi nchini. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imebaini jumla ya Kampuni 488 zenye Ukomo wa Ahadi (Limited by Guarantee) za Sekta Binafsi ambazo zimesajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Jumuiya za Biashara 22 zimesajiliwa na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya nchini. Katika zoezi hilo, Kampuni za Sekta Binafsi na jumuiya za biashara zilizotambuliwa zinajihusisha na masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kilimo, viwanda, mazingira, biashara na utalii. Utambuzi huo, utawezesha Wizara katika kuimarisha uratibu na kuongeza ushirikiano na Sekta Binafsi pamoja na kuandaa daftari lenye taarifa za Sekta Binafsi nchini ambalo litakuwa likihuishwa mara kwa mara.

80. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kuwatambua wamachinga kama kundi maalum linalohitaji kupewa kipaumbele katika kukuza uchumi wa nchi na kuzalisha ajira kwa wingi. Aidha, Serikali kupitia Halmashauri imekuwa ikiweka mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo rafiki kwa ajili ya machinga kufanya biashara. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya Halmashauri 114 kati ya 184 zimesajili wafanyabiashara ndogondogo maarufu kama machinga 329,662. Kati yao wamachinga 110,452 wamepangiwa maeneo rasmi yenye ukubwa wa mita za mraba 4,729,229 za biashara. Vile vile, Serikali imeboresha jumla ya masoko 367 ambayo yanaweza kumudu wajasiriamali 136,041.

**C. Kukuza Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji Nchini**

81. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 miradi ya kimkakati na uwekezaji imezalisha ajira 101,353 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja ikilinganishwa na ajira 72,395 zilizozalishwa kwa mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia 28.6. Kati ya hizo, ajira zilizozalishwa kwa wanawake ni 27,588 na wanaume 73,765. Aidha, ajira 81,082 zilikuwa ni kwa vijana kati ya umri wa miaka 18 – 35 ambapo zaidi ya asilimia 78 wanafanya shughuli zenye ujuzi wa chini na asilimia 14 ni za ujuzi wa kati na asilimia 8 ujuzi wa juu. Vile vile, miradi ilitoa fursa kwa watu wenye ulemavu 237 katika ajira za ujuzi wa kati na juu.

82. ***Mheshimiwa Spika***, Ongezeko la ajira katika miradi ya kimkakati na uwekezaji inayotekelezwa hapa nchini imetokana na uwepo wa mazingira wezeshi ya utekelezaji Kanuni, taratibu na Miongozo kuhusu ushiriki wa watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mikataba inayosainiwa inazingatia suala la ushiriki wa watanzania katika ajira na utoaji wa huduma.

**D. Kusimamia Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji**

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuongeza ushiriki wa watanzania katika miradi ya Kimkakati na Uwekezaji, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya kampuni 2,827 za watanzania ziliingia mikataba kwa ajili ya kutoa huduma za ukandarasi ambapo kampuni 848 ni za ukandarasi, kampuni 83 ni za ushauri elekezi na kampuni 1,896 ni za huduma ya chakula, ulinzi, usafiri, bima na bidhaa za ujenzi kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na kampuni 2,019 zilizonufaika mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 28.6. Jumla ya kampuni tano (5) za kitanzania ziliweza kuingia ubia wa kuungana na kufanya kazi katika utoaji wa huduma

katika miradi ya kimkakati. Aidha, kwa upande wa ununuzi, jumla ya shilingi **trilioni 6.49** zilitumika katika utoaji wa huduma na manunuzi ya bidhaa katika miradi ya kimkakati na uwekezaji ambapo kiasi cha shilingi **trilioni 6.27** kilitumika katika ununuzi wa bidhaa na huduma za ndani. Miongoni mwa bidhaa na huduma zilizozalishwa na viwanda na kampuni za ndani ni saruji, nondo na kokoto na malighafi za ujenzi kama vile mchanga, vifusi na changarawe (*earth works materials)*, vifaa vya afya na ulinzi, huduma za mawasiliano, bima, huduma za ulinzi, kukodisha magari, ushauri elekezi, huduma za chakula na huduma za kisheria. Vile vile, Wizara imetoa mafunzo kwa watanzania ili kuongeza ushiriki wao katika miradi ya kimkakati na uwekezaji nchini. Jumla ya watanzania 10,100 ikihusisha wafanyakazi 8,940 wenye ujuzi wa juu, 336 wenye ujuzi wa kati na 824 wasio na ujuzi walishiriki mafunzo hayo.

**E. Kukuza Ushiriki wa Wananchi kwenye Shughuli za Kiuchumi**

84. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zimetoa mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 713.8** kwa wajasiriamali 2,203,838 kati yao wanawake ni 1,234,149 sawa na asilimia 56 na wanaume 969,689 sawa na asilimia 44. Aidha, uchambuzi wa mikopo hiyo unaonesha jumla ya ajira 3,122,104 zilizalishwa, kati ya ajira hizo, wanawake ni 1,623,494 sawa na asilimia 52 na wanaume ni 1,498,610 sawa na asilimia 48. Mikopo hiyo imetolewa katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi (31.07%), ikifuatiwa na sekta ya viwanda na biashara (20.39%).

85. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali Wananchi (NEDF) imetoa jumla ya mikopo 1,474 (wanawake 668 (45.3%) na wanaume 806 (54.7%) yenye thamani ya shilingi **bilioni 3.50**. Mikopo 516 (35%) yenye

thamani ya shilingi **bilioni 1.225** ilitolewa kwa miradi ya vijijini. Mikopo hiyo iliweza kuzalisha ajira 5,489 (wanawake 2,668 (48.6%) na wanaume 2,821 (51.4%). Aidha, Wizara imeweza kuwaungisha wajasiriamali kumi na tatu (13) ambao walipata mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 1.151** kupitia Benki za Azania na CRDB ambapo jumla ya ajira 259 zimezalishwa.

86. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanya tathmini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF). Tathmini hiyo ililenga kupima matokeo ya utendaji wa huo katika kupunguza mzunguko wa umaskini katika jamii. Matokeo yamebainisha masuala yafuatayo: Jumla ya kaya 1,965,743 zimetambuliwa kati ya kaya hizo, kaya 1,283,266 zilikidhi vigezo na kupatiwa ruzuku; Kuwezesha watu 1,236,945 kupata ajira za muda mfupi; Kuwezesha jumla ya watoto 1,280,779 kutoka katika kaya maskini kuhudhuria masomo; na kupunguza kiwango cha umaskini uliokithiri kwa asilimia 8 na kiwango cha umaskini wa kaya kumudu gharama za mahitaji ya msingi kwa asilimia 10.

## F. Mpango wa Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN Viwanda Scheme)

87. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Kuendeleza Viwanda Vidogo na vya Kati (SANVN Viwanda Scheme). Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Mpango umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 3.62** katika miradi 63. Mikopo hiyo ilitolewa katika mikoa 13 ambayo ni Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza, Shinyanga, Geita, Dar es Salaam, Tabora, Songwe, Simiyu, Iringa, Arusha, Njombe na Dodoma. Aidha, Mpango umetengeneza jumla ya ajira 3,384 ambapo ajira za moja kwa moja zilikuwa 697 na ajira zisizo za moja kwa moja zilikuwa 2,687 katika Sekta za Kilimo, Mifugo, Ujenzi, Viwanda, Misitu na Maliasili, na Ufundi wa Mitambo. Nitoe wito kwa wajasiriamali kuendelea kutumia fursa za mikopo kutoka

katika Mpango huo ili kutekeleza shughuli mbalimbali za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo.

**G. Kuhamasisha Ukuzaji, Ujuzi, Maarifa na Elimu ya Ujasiriamali**

88. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kukuza ujuzi, maarifa na elimu ya ujasiriamali, Wizara imetekeleza Programu ya Mashindano ya Kibiashara katika shule za Sekondari kwa ufadhili wa Shirika la Ujerumani la Probono kwa kushirikiana na taasisi ya TAMTF (Teach A Man to Fish). Programu hii ni ya majaribio ambapo katika hatua ya awali imetekelezwa katika shule 11 za sekondari katika mikoa ya Dar es Salaam (3), Arusha (4) na Kilimanjaro (4). Aidha, Programu hiyo imetoa mafunzo kwa wakufunzi 22 wa shule hizo ili kutekeleza programu ya mashindano ya kibiashara katika shule za Sekondari (*School Enterprise Challenge)*. Vile vile, imewezesha kuanzishwa kwa klabu za wanafunzi zijulikanazo kama *Probono Entrepreneurship Programme's Club* (PEP Club). Utekelezaji wa Programu hiyo, umewezesha wanafunzi wenye Miradi inayokopesheka kushindanishwa ili kuwajengea hamasa ya kujenga mitazamo chanya ya ujasiriamali.

89. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilitekeleza kwa majaribio Programu ya Vijana 2JIAJIRI (2JIAJIRI Youth Entrepreneurship Training Program) kwa kushirikiana na Benki ya KCB, Programu hiyo ilifanikiwa kuwafikia vijana waliohitimu Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi kwa ajili ya mafunzo ya ujasiriamali kwa lengo la kuendeleza biashara. Jumla ya vijana 303 wamenufaika ambapo vijana 172 ni wanawake na vijana 131 ni wanaume kutoka mikoa sita (6) ya Dar es Salaam, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza na mkoa mmoja (1) kutoka Zanzibar. Programu hiyo imemaliza muda wa utekelezaji mwaka 2022 na Wizara itaendelea kufuatilia wahitimu wa programu hiyo ili kutathmini maendeleo ya biashara wanazozifanya na matokeo ya programu hiyo. Wizara imetekeleza Programu ya majaribio ya kuendeleza wafanyabiashara wa mkoa wa Geita kuweza kunufaika na

fursa za ununuzi za Mgodi wa Dhahabu wa Geita. Matokeo ya mradi huo ni kuanzishwa kwa kituo cha uwezeshaji na taarifa katika Mji wa Geita ili kuwajengea uwezo wafanyabiashara wa Mkoa wa Geita ikiwemo kurasimisha biashara, kuwaunganisha wafanyabiashara na fursa za migodi, pamoja na makampuni yaliyo na mikataba na mgodi.

90. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu uanzishaji wa vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi katika mikoa mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma za uwezeshaji kwa wananchi. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya vituo vya uwezeshaji vitatu (3) vya Ushetu, Kibaha Mji na Morogoro Manispaa vimeanzishwa na kufikia vituo vya uwezeshaji 20. Katika kipindi hicho, vituo vya uwezeshaji vilitoa huduma kwa wananchi 34,441 (wanaume 21,646 na wanawake 12,795). Vituo vya uwezeshaji viliwezesha upatikanaji wa mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 9.4** kwa wajasiriamali 4,017 kutoka katika taasisi mbalimbali za fedha na mifuko ya uwezeshaji.

91. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya tathmini ya utendaji wa Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika mikoa ya Geita (Nyang'hwale), Shinyanga (Kahama), Ruvuma (Mbinga) na Dodoma (Chamwino, Mpwapwa, Kongwa, Kondoa, Chemba, Bahi na Dodoma Jiji). Zoezi hilo lililenga kupima utendaji wa vituo hivyo katika mikoa mbalimbali na kuangalia hatua zilizochukuliwa na Halmashauri husika katika kuendeleza vituo hivyo. Tathmini hiyo imebaini uwepo wa changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Uhaba wa miundombinu ya majengo na kutokuwepo kwa majengo yenye kukidhi ubora na mahitaji katika kutoa huduma kwenye vituo na kusababisha utendaji hafifu wa vituo; na Uhaba wa miundombinu inayojitosheleza kwenye vituo kwa mfano baadhi ya vituo kutokuwa na mtandao, kompyuta na samani. Aidha, Wizara inaendelea

kufanya mapitio ya Mwongozo wa Uanzishaji na Usimamizi wa Vituo vya Uwezeshaji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na sekta binafsi ili kuimarisha huduma za uwezeshaji kwa lengo la kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi.

**4.2.3. Maendeleo ya Viwanda**

**A. Miradi ya Kimkakati**

**Kiwanda cha Viuadudu (TBPL)**

92. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo Kiwanda cha Viuadudu (TBPL); Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma; Mradi wa Chuma Liganga ; Mradi wa Makaa ya Mawe wa Katewaka; na Mradi wa Magadi Soda – Engaruka. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

93. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kiwanda cha viuadudu kilichopo TAMCO - Mkoa wa Pwani kilifanikiwa kuzalisha na kuuza viuadudu lita 44,206 zenye thamani ya shilingi **642,737,524**. Kati ya lita hizo, lita 11,606 ziliuzwa nchini, lita 11,500 ziliuzwa Kenya, na lita 21,100 ziliuzwa kwa Kampuni ya *Swiss Tropical and Public Health*. Aidha, kiwanda kiliweza kufanya majaribio ya viuatilifu awamu ya pili na kukarabati baadhi ya mitambo. Zoezi hili linaendelea kwa mitambo ya *Production Chiller na Office Chiller; Industrial Softener, Fermenters; na Cooling Tower Pump* na linatarajiwa kukamilika Mwezi Juni, 2023.

**Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya uhakiki wa mali za wananchi wanaopisha Mradi wa Makaa ya mawe Mchuchuma kuanzia mwezi Oktoba – Desemba, 2022. Zoezi lilifanyika katika vitongoji vya Nkomang'ombe, Idusi, Kilomos, Ntiule na Mhambalasi. Kati ya wananchi 651 waliotakiwa

kuhakiki taarifa zao, wananchi 580 walijitokeza, sawa na asilimia 87. Baadhi ya wananchi hawakujitokeza wakati wa zoezi la uhakiki kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo na hivyo kutowakilishwa na wasimamizi wa mirathi. Wizara inaendelea kuwafuatilia wale ambao hawakujitokeza ili kupata taarifa zao.

**Mradi wa Chuma wa Liganga**

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya uhakiki katika eneo la Liganga vitongoji vya Mnyusi, Ilongi na Myorua katika Kijiji cha Mundindi na Kitongoji cha Luhaha katika Kijiji cha Amani kuanzia mwezi Oktoba – Desemba, 2022. Kati ya waathirika 494 waliotakiwa kuhakiki taarifa zao, 481 walijitokeza sawa na asilimia 98. Baadhi ya wananchi hawakujitokeza wakati wa zoezi la uhakiki kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo vifo na hivyo kutowakilishwa na wasimamizi wa mirathi. Wizara inaendelea kuwafuatilia wale ambao hawakujitokeza ili kupata taarifa zao.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwezi Aprili, 2023 Wizara imepokea fedha kiasi cha shilingi **bilioni 15.4** kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha miradi ya Liganga na Mchuchuma. Aidha, Wizara imeanza maandalizi ya ulipaji wa fidia kwa kushirikiana na Mkoa wa Njombe na Halmashauri ya Ludewa ambapo wataalam wako katika eneo la mradi wakiendelea maandalizi ya ulipaji wa fidia. Zoezi la ulipaji wa fidia linatarajia kukamilika Mei, 2023 na litaambatana na kujenga uelewa wa matumizi bora ya fedha watakazopata na manufaa ya mradi.

**Mradi wa Makaa ya Mawe wa Katewaka**

97. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya uthaminishaji wa mali za waathirika 689 wa Mradi wa makaa ya mawe Katewaka katika Kijiji cha Nkomang'ombe katika Kitongoji cha Nyambalapi na Mhumbi kuanzia mwezi Novemba – Desemba, 2022. Mwezi Januari, 2023 Vitabu vya uthaminishaji viliwasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya

mapitio na uhakiki wa fidia. Aidha, Mwekezaji yuko tayari kulipa fidia baada ya kupata kiasi halisi cha fidia na kukamilisha majadiliano.

**Mradi wa Magadi Soda Engaruka**
98. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imekamilisha uthamini wa mradi wa Magadi Soda Engaruka kuanzia mwezi Januari – Februari, 2023. Vitabu vya uthamini wa fidia vimewasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali na gharama ya fidia iliyohakikiwa ni shilingi **billioni 14.5**. Aidha, Wizara inaendelea kutafuta mwekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na jumla ya wawekezaji 14 wameonesha nia ya kuwekeza kwenye mradi huo. Zabuni itatangazwa mara baada ulipaji fidia inayotarajiwa kulipwa katika mwaka 2023/2024.

**B. Mikopo Katika Viwanda vya Uchakataji/Uongezaji Thamani Mazao ya Kilimo**
99. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilitoa mikopo ya **Shilingi bilioni 47.042** ili kuwezesha uwekezaji katika viwanda vya uchakataji na uongezaji thamani wa mazao mbalimbali nchini. Mikopo iliyotolewa imefanikisha uwekezaji katika viwanda vipya 5 na viwanda 9 vilivyokuwepo kupitia mikopo ya uendeshaji *(working capital)* na ununuzi wa mashine za kisasa *(asset financing)*.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile, Mikopo iliyotolewa kwa viwanda vipya inajumuisha viwanda vifuatavyo:- kiwanda kikubwa cha uzalishaji wa Sukari kilichopo Bagamoyo ambacho kimeanza uzalishaji kwa kusaga tani 1,500 za miwa kwa siku; Kiwanda cha kukoboa mpunga na utengenezaji wa chakula cha mifugo chenye uwezo wa kukoboa tani 192 za mpunga kwa siku pamoja na kutengeneza tani 240 za chakula cha mifugo kwa siku kilichopo Kahama; Kiwanda cha uzalishaji wa mafuta ya kupikia ya mawese kilichopo Kigoma chenye uwezo wa kuzalisha tani 1 ya mafuta ghafi kwa saa na lita 2,000 za mafuta yaliyosafishwa (refined) kwa

siku. Kiwanda hiki kipo Kigoma.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile, Viwanda viwili vya usindikaji wa maziwa vilivyopo Tanga na Kagera vyenye uwezo wa kusindika lita 120,000 na lita 10,000 za maziwa mtawalia; na Kiwanda cha uzalishaji wa mchuzi wa zabibu kilichopo Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 3 za mchuzi kwa mwaka vilinufaika na mikopo. Jumla ya **shilingi bilioni 8.725** zilitolewa kusaidia viwanda vidogo vidogo vya uchakataji wa mazao ya alizeti, mawese, usagaji wa unga wa mahindi, ukoboaji wa mpunga vilivyopo katika maeneo mbalimbali nchini.

**C. Kueneza Dhana ya KAIZEN Nchini**

102. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanikiwa kuingia Mkataba wa Awamu ya III ya ufadhili wa JICA katika kutekeleza falsafa ya KAIZEN. Aidha, Wizara kupitia Maonesho ya Viwanda vya ndani yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Desemba, 2022, imefanikiwa kueneza falsafa ya KAIZEN na kuwezesha washiriki wa maonesho wakiwemo wenye viwanda kushiriki mashindano ya KAIZEN Afrika. Vile vile, Wizara imehamasisha utumiaji wa falsafa ya KAIZEN kwa wenye viwanda **190** katika Mikoa ya Iringa na Kigoma kwa lengo la kuongeza ufanisi, tija na ubora katika uzalishaji.

**D. Kuendelea na Ukarabati wa Kiwanda cha KMTC Katika Mkoa wa Kilimanjaro**

103. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na ukarabati wa Kiwanda cha KMTC ambapo usimikaji wa mashine ya *overhead crane* na ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kwa ajili ya tanuru ikiwemo *Induction furnace* umekamilika. Usimikaji wa kinu cha kuyeyushia chuma (induction furnace) umefikia asilimia 98, ambapo ujenzi wa msingi kwa ajili ya kusimika chuma umekamilika. Majaribio na mafunzo ya namna ya kutumia kinu cha kuyeyushia chuma yamefanyika kwa awamu ya kwanza mwezi Januari 2023. Aidha, ukarabati wa

mfumo wa umeme umekamilika kwa asilimia 99. Mikataba ya ununuzi wa malighafi kwa ajili ya uzalishaji imekamilika na mafunzo ya awamu ya pili ya utumiaji wa mitambo yameanza mwezi Aprili, 2023 na yatakamilika mwezi Mei 2023 tayari kuanza uzalishaji.

**E. Kuendelea na Ujenzi wa Miundombinu ya Msingi katika Kongani ya Viwanda – TAMCO na Kufanya Ukarabati wa Majengo ya Kiwanda cha Nyanza**

104. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na ukamilishaji wa miundombinu katika Kongani ya Viwanda - TAMCO na Nyanza. Kwa upande wa kongani ya viwanda TAMCO, ujenzi wa barabara ya ndani (Viuatilifu Road) yenye urefu wa Mita 230 kufikia mwezi Machi, 2023 umefikia asilimia 85 na usimikaji wa bango la kutangaza eneo umekamilka. Maandalizi ya mkataba wa ujenzi wa barabara ya *China Boarder* yenye urefu wa Mita 320 yamekamilika na mkataba umepelekwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya upekuzi. Aidha, Wizara inaendelea na mazungumzo na wawekezaji ambao wameonesha nia ya kuwekeza katika eneo la kongani ya TAMCO. Vile vile, katika kongani ya Nyanza, Mkataba kwa ajili ya kupata Mkandarasi ulisainiwa mwezi Desemba, 2022. Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ukarabati wa ghala namba 1 na ukarabati ghala namba 2 umefikia asilimia 10.

**F. Kufanya Utafiti katika Kanda Saba (7) Nchini ili Kubaini Fursa za Uwekezaji na Maeneo yenye Viwanda na Rasilimali zilizopo (IndustrialMapping)**

105. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imekamilisha zoezi la ukusanyaji wa taarifa katika mikoa ya Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam, Pwani na Morogoro) lililofanyika kuanzia Agosti, 2020 hadi Julai, 2022. Zoezi hilo limebaini uwepo wa viwanda vidogo sana 8,539, viwanda vidogo 3,779, viwanda vya kati 184 na viwanda vikubwa 235 katika Mikoa hiyo. Katika mkoa wa Dar - es - salaam, zoezi limebaini uwepo wa viwanda 7,723 ambapo, viwanda vidogo sana ni 5,050,

viwanda vidogo ni 2,433, viwanda vya kati ni 122 na viwanda vikubwa ni 118. Aidha, katika Mkoa wa Morogoro kuna jumla ya Viwanda 2,762 ambapo, viwanda vidogo sana ni 1,588, viwanda vidogo ni 1,137, viwanda vya kati ni 16 na viwanda vikubwa ni 21. Vile vile, katika Mkoa wa Pwani kuna jumla ya viwanda 2,252 ambapo, viwanda vidogo sana ni 1,901, viwanda vidogo ni 209, viwanda vya kati ni 46 na viwanda vikubwa ni 96. Aidha, zoezi limebaini kuwa, viwanda vingi vinashughulika na uongezaji thamani mazao ya kilimo kwa kutumia malighafi za ndani. Wizara itaendelea na zoezi hilo kwa Kanda sita (6) zilizobaki kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**G. Utoaji wa Huduma za Kitaalam Viwandani**

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya zoezi la upimaji wa uharibifu na kutoa ushauri wa utunzwaji wa mazingira unaotokana na uzalishaji viwandani na mazingira kwa ujumla. Zoezi hilo limehusisha ukaguzi wa kimazingira katika kampuni ya *Serengeti Breweries* Dar es Salaam, *Tanzania National Electric Supply Company Limited* (TANESCO) na *Tanzania Cigarette Company* (TCC). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na STAMICO imeweza kusimika mtambo wa kuzalisha mkaa mbadala wa makaa ya mawe (coal briquette) ili kulinda uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi ya kuni. Vile vile, Wizara imefanya tafiti na kufanikiwa kutoa teknolojia ya kuchakata ngozi kwa njia ya asili isiyochafua na kuharibu mazingira. Teknolojia hiyo imeonesha mafanikio mazuri.

107. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanikiwa kupima jumla ya **sampuli 90** katika Maabara za: Chakula na Bioteknolojia; Kemia; Nishati; Makaa ya Mawe; na Mazingira. Aidha, Wizara imesaidia Kiwanda cha Bia cha Serengeti, Kiwanda cha Mabati cha Alaf na Kiwanda cha Sigara kupima sampuli za maji taka zipatazo **14** ili kuona kama zinakidhi viwango vya kuachiwa bila kuwa na athari kwenye mazingira kwa lengo la kuthibiti uharibifu wa mazingira.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Maabara ya Makaa ya Mawe imefanya uhakiki wa ubora wa bidhaa kwa kuweza kuhakiki sampuli zipatazo **54** za mkaa wa vumbi la makaa ya mawe na mkaa wa vifuu vya nazi kwa makampuni mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje ya nchi. Vile vile, kupitia Maabara ya Nishati, Wizara imeweza kuhakiki majiko ya kupikia yapatayo **60** kwa kuangalia ubora wake wa kutunza nishati wakati wa matumizi. Uhakiki huo una lengo la kujenga mazingira safi na sahihi ya ufanyaji biashara na kuendelea kuvilinda viwanda vyetu kwa kuvisaidia kufuata viwango vya ubora vilivyowekwa ili kuwa na ushindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

**H. Kufanya Utafiti na Kutoa Mafunzo kwa Wadau wa Sekta ya Ngozi, Nguo na Mavazi**

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT) Kampasi ya Mwanza imeandaa na kuendesha mafunzo ya uchakataji wa ngozi. Mafunzo hayo yalilenga kuwafundisha wadau kutoka taasisi za umma ili wakawafundishe wadau walio chini yao. Taasisi zilizoshiriki mafunzo hayo ni TBS, SIDO, UDSM, DUCE, Kiwanda cha Ngozi cha *Kilimanjaro International Leather Industries Ltd*, pamoja na Umoja wa Wazalishaji wa Ngozi Tanzania (Leather Association of Tanzania – LAT).

110. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na mradi wa kuandaa wasifu na kanzidata ya Taifa katika Sekta ya Nguo, Ngozi na Mkonge unaofadhiliwa na Shirika la Utafiti la REPOA. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanikiwa kutembelea viwanda **103** vilivyo katika sekta hizo kwa ajili ya kupata taarifa. Wizara inaendelea na hatua ya uchakataji wa taarifa hizo kwa ajili ya kuandaa wasifu wa Taifa uitwao *National Profile and Database for Textile, Leather and Sisal Sectors in Tanzania*.

**I. Kuendeleza Utafiti na Uendelezaji wa Teknolojia za Kilimo**

111. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda Darasa cha kubangua Korosho katika Wilaya ya Manyoni, Mkoani Singida chenye jumla ya mashine na vifaa **129** ambacho kitakuwa na uwezo wa kubangua zaidi ya tani 3 za korosho ghafi kwa siku na kutoa ajira kwa vijana zaidi ya **70** kwa mwaka. Utekelezaji wa Mradi umefikia asilimia **80** na unatarajia kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Mei, 2023. Mradi huo umeanza baada ya kukamilika kwa majaribio ya awali (piloting) kwa kushirikiana na Kampuni ya Korosho (Cashew Nut (2005) Company Limited) ya Mkoani Mtwara na baadae kuanzisha Kiwanda cha mfano kupitia Kikundi cha *Brotherhood* cha Manyoni, Mkoani Singida.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni hiyo imeanza kubangua korosho, kufungasha na kuuza, ambapo, kwa kutumia mashine **8** za mkono za kubangua korosho, kikundi kina uwezo wa kubangua kilo **320** za korosho ghafi kwa siku, sawa na kilo **80** za korosho zilizobanguliwa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, kikundi cha *Brotherhood* cha Manyoni kimeanza kubangua korosho, kufungasha na kuuza, ambapo, ajira **22** za vijana zimezalishwa. Vile vile, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Kitovu cha Teknolojia za Kihandisi (Engineering Technology Hub - ETH) Wilayani Karatu katika Mkoa wa Arusha. Kituo hicho kinalenga kusogeza karibu na kutoa huduma za teknolojia za Kihandisi kwa wakulima wadogo na wa kati kwa gharama nafuu, kwa kuunda na kununua jumla ya mashine **49** za kuchakata mazao mbalimbali yatokanayo na kilimo. Utelekezaji wa Mradi huo umefikia asilimia **80.**

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, imefanya utafiti kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini wa kubaini mahitaji na kiwango cha matumizi ya zana za kilimo na teknolojia za

vijijini katika mikoa ya Songwe (Wilaya ya Momba); Arusha (Wilaya ya Karatu) na Dodoma (Wilaya ya Chemba). Utafiti huo ulihusisha wakulima **352** kutoka katika Wilaya hizo. Utafiti ulibaini kuwepo kwa upungufu wa mashine za kulima, kupanda, kupalilia, kunyunyiza dawa, kuvuna, kupura na kuchakata malisho ya mifugo. Mapendekezo ya utafiti huo ni kuanzisha vituo vya teknolojia katika maeneo hayo kwa ajili ya kusogeza zana hizo muhimu za kilimo.

114. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Sukari Tanzania imekamilisha usanifu wa Mtambo wa kutengeneza sukari kwa kiwango cha mjasiriamali wa kati (*sugar mini-plant, Capacity 200TCD*)**.** Uundaji wa mitambo mbalimbali itakayounganishwa kukamilisha mtambo mmoja upo kwenye hatua mbalimbali (*clarifier machine 90%, hot water cane seed treatment plant 98%, vacuum pan evaporators 85%, mini-boiler 75%, fabrication of vacuum pan evaporator frame 80% and crystallizers 80%)*. Mtambo huo umekamilika kwa asilimia 65 na utakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 20 za sukari kwa siku.

115. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imekamilisha usanifu wa teknolojia ya kisasa ya kuhifadhi mazao ya matunda na mboga mboga kwa kiwango cha mkulima mdogo. Maandalizi ya awali ya uundaji wa chasili cha mtambo yanaendelea. Mtambo huo utasaidia kuhifadhi mazao ya matunda na mboga mboga kwa muda mrefu na pasipo kuharibika na hivyo kusaidia mazao hayo kufikia masoko ya mbali.

116. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imekamilisha usanifu na utengenezaji wa mtambo wa kukausha mhogo wilayani Handeni. Mtambo huo una uwezo wa kukausha tani 12 za muhogo mbichi kwa saa kumi (10) na kutoa tani tatu (3) za unga wa muhogo. Mtambo huo umenunuliwa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (CPB), na umefungwa kijiji cha Kwachaga Wilaya ya Handeni

kwa ajili ya majaribio na kukabidhi vikundi vya wakulima wa muhogo.

**J. Ukaguzi wa Zana za Kilimo na Teknolojia za Vijijini kwenye Maeneo ya Mipakani**

117. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanya majaribio ya zana za kilimo na kuthibitisha aina 11 za modeli ya zana hizo kwa matumizi nchini. Vile vile, Wizara imeendelea kudhibiti zana dhaifu za kilimo na teknolojia za vijijini kutoka nje ya nchi ili kuwalinda watumiaji. Vile vile, Wizara imeanza ukaguzi wa zana za kilimo zisizothibitishwa kwenye maeneo matano ya mipakani. Maeneo hayo ni Namanga mkoani Arusha; Tunduma mkoani Songwe; Sirali Mkoani Mara; Holili mkoani Kilimanjaro na Kasumulu mpakani na Malawi.

**K. Kusanifu na Kuendeleza Utengenezaji wa Vifaa Tiba vya Hospitali**

118. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha usanifu na inazalisha vifaa tiba vya hospitali vikiwemo *wheel chairs, 6-body Mortuary cabinets, stretchers na theatre trolleys.* Aidha, Wizara inaendelea na utengenezaji wa chasili cha jokofu la ngazi sita (6) (*six-bodies mortuary carbinet*).

**L. Uatamizi wa Wabunifu**

119. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imeatamia wabunifu watano (5) ikilinganishwa na wabunifu 27 walioatamiwa mwaka 2021/2022. Kati ya wabunifu walioatamiwa mwaka 2021/22, watatu (3) walipata kazi hivyo wakaondoka katika atamizi, wane (4) waliweza kusajili makampuni chini ya uangalizi wa atamizi. Aidha, wabunifu wanaoatamiwa na Wizara wako katika makundi manne (4) ambayo ni: Bunifu za Kimifumo zinazolenga kutatua changamoto katika utendaji maeneo mbalimbali mfano; Urahisi wa Ukataji bima na utoaji wa huduma za bima ya afya, mfumo wa kuwezesha na kurahisisha makampuni yanayokubali malipo kidogokidogo,

mfumo wa kuwezesha wanafunzi kuomba udahili vyuoni na kufanya usajili; Bunifu za uundaji wa vifaa vya kielectroniki (smart electronic products); Bunifu za upande wa Nishati mfano; kuwezesha upatikanaji wa umeme maeneo yasiyo na umeme (power booster na umeme dumu) pamoja na bunifu za uzalishaji wa umeme mfano wa jenereta (powerwall); Bunifu za upande wa Mekanikia (Mechanical) mfano; uzalishaji wa bushi za bajaji na pikipiki na uundwaji wa machine ya kusafisha fukwe; na Bunifu upande wa *Geotextile*; Utengenezaji wa material bora (woven fibers) kutoka kwenye maganda ya nazi.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Kabla ya kuruhusu bidhaa zilizobuniwa kuzalishwa na kuwekwa sokoni, bidhaa hizo hukaguliwa na kufanyiwa majaribio kitaalamu ili kujiridhisha na utendaji kazi wake. Aidha, Wizara itaendelea kuhakikisha bunifu zote zinakidhi viwango vya ubora. Vile vile, Faida wanazopata wabunifu ni kama vile: Kuanzisha viwanda vidogo (production plants) ambavyo vitaweza kutoa ajira kwa vijana wengine; Kupata wawekezaji wakubwa ambao huchukua bunifu na kuzalisha kwa wingi na kuongeza ajira; Kufungua kampuni ambazo zinatoa huduma mbalimbali hivyo kuwezesha upatikanaji wa ajira; Kuzalisha bidhaa na huduma ambazo zimelenga kuleta ufanisi na kuondoa changamoto mbalimbali katika jamii mfano upatikanaji wa umeme unaoweza kuwasha taa za nyumba na kuchaji simu sehemu zisizo na umeme; na Ukuzaji ujuzi kwa vijana wenye mawazo ya kibunifu hivyo kuwaepusha na vitendo visivyofaa.

### 4.2.4. Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

### A. Kuhamasisha Urasimishaji wa Shughuli za Wajasiriamali Wadogo na wa Kati

121. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuhamasisha na kuelimisha wajasiriamali wadogo na wa kati kurasimisha

biashara zao na kufanya shughuli zao katika maeneo rasmi ili kuwawezesha kutambulika na Serikali na taasisi mbalimbali zikiwemo taasisi za kifedha. Katika kurahisisha upatikanaji wa kanuni na taratibu mbalimbali za urasimishaji biashara na huduma mbalimbali, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa urasimishaji biashara nchini. Jumla ya taasisi 78 zinazohusika na usajili, utoaji wa leseni na vibali mbalimbali vya kuanzisha na kuendesha biashara nchini zimehusishwa katika Mwongozo huo. Aidha, kukamilika kwa Mwongozo huo kutasaidia kupunguza muda na gharama kwa wajasiriamali wadogo na wa kati pindi watakapohitaji kujua kanuni na taratibu mbalimbali za kurasimisha biashara.

**B. Kuhawilisha Teknolojia kwa Kuimarisha Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCS) na Vituo vya Mafunzo na Uzalishaji (TPC)**

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara kwa kutumia mashine/mitambo iliyopo katika vituo saba (7) vya kuendeleza teknolojia (TDCs) vilivyopo katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga iliweza kuzalisha mashine 463 na vipuri 3,136 ambavyo viliuzwa kwa wajasiriamali. Vituo hivyo vinajihusisha na uendelezaji wa teknolojia na kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali Wadogo na wa Kati waliopo mjini na vijijini kwa kuzingatia "Mkakati wa Wilaya Moja, Bidhaa Moja" na fursa zinazojitokeza.

**C. Kutoa Mafunzo na Huduma za Ushauri wa Kibiashara na Ufundi**

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 12,091, wanaume 5,082 (42%) na wanawake 7,009 (58%) kupitia kozi 519 katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji. Vile vile, huduma za ushauri wa kibiashara na ufundi kwa wajasiriamali 17,113, wanaume 8,215 (48%) na

wanawake 8,898 (52%) zimetolewa katika nyanja za ufundi, uchumi, uongozi, masoko, ubora wa bidhaa, teknolojia, kubuni, kusanifu na kutayarisha uchambuzi yakinifu wa miradi ya viwanda na biashara. Mafunzo na ushauri ulitolewa kwa wajasiriamali na vikundi/vyama vya wajasiriamali yakilenga kuviimarisha na kuviwezesha kujenga msingi wa kujitegemea katika Sekta ya Viwanda na Biashara Ndogo.

### 4.2.5. Mtangamano wa Biashara

#### A. Kuendeleza Majadiliano ya Kibiashara Kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya Kupanua Fursa za Masoko na Kuvutia Uwekezaji Nchini

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutafuta fursa za uwekezaji na biashara kati ya nchi na nchi, ambapo Wizara ilishiriki kwenye Mkutano wa 15 wa Tume ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji uliofanyika mwezi Agosti 2022, Jijini Dar es Salaam. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kujadili utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa 14 wa Tume ya Kudumu ya Ushirikiano uliofanyika mwaka 2006 na kupendekeza maeneo mapya ya ushirikiano katika sekta za Ulinzi, Nishati, Madini, Ujenzi, Usafirishaji, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Elimu, Sayansi na Teknolojia, Maji, Afya, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Makubaliano yaliyofikiwa katika Mkutano huo ni pamoja na:- Kushirikiana katika kuondoa Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru (Non Tariff Barriers - NTBs); Kushirikiana katika maeneo ya Uwekezaji kati ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Kituo cha Uwekezaji cha Msumbiji (APIEX); Kushiriki katika maonesho ya biashara yanayoandaliwa na kila nchi ili kukuza biashara na kufanya marejeo ya Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Chama cha

Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) na Chemba ya Biashara ya Msumbiji iliyosainiwa mwaka 2019 ili kuhakikisha malengo tarajiwa yanafikiwa kama yalivyopangwa ikiwa ni pamoja na MoU hiyo kuzingatia mahitaji halisi ya wakati wa sasa.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki Mkutano wa Tano (5) wa Tume ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Malawi uliofanyika mwezi Oktoba, 2022 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulipitia utekelezaji wa maazimio ya Mkutano wa 4 wa Tume hiyo uliofanyika mwezi Februari, 2017 Lilongwe, Malawi ikiwa ni pamoja na kubainisha maeneo mapya ya ushirikiano. Maeneo yaliyoazimiwa ambayo tayari yameshaanza kushughulikiwa ni pamoja na:- Matumizi ya Mfumo Rahisi wa Kufanya Biashara (Simplified Trade Regime - STR) kwa wajasiriamali wa kati na wadogo wanapovuka mpaka wa nchi hizi mbili; Utatuzi wa Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Kiushuru (Non-Tariff Barriers - NTBs); na Uimarishaji Ushirikiano wa Sekta Binafsi na Umma ili kurahisisha Biashara baina ya nchi hizo.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia majadiliano baina ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa nchi imenufaika kwa kupatikana kwa fursa nafuu za biashara kwa bidhaa na huduma zaidi ya **8,000** kuuzwa kwenye masoko ya kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Katika ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoifanya nchini China mwezi Novemba 2022, nchi ya China imetoa upendeleo wa asilimia 98 wa bidhaa za Tanzania kuingia katika soko lake bila kutozwa ushuru wa forodha. Mpango huo ulianza mwezi Desemba 2022 na kwa sasa Wizara inaendelea kuhamasisha na kuhimiza Sekta Binafsi kuchangamkia fursa hiyo. Masoko mengine ya aina hiyo ni pamoja na India, Urusi na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

128. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (Joint Commission for Cooperation - JCC) kati ya Tanzania na Oman uliofanyika tarehe 07 – 11 Desemba 2022 Jijini Muscat, Oman ikiwa ni miaka tisa (9) baada ya mkutano wa kwanza (1) uliofanyika tarehe 24 - 25 Februari 2013 jijini Dar es Salaam, Tanzania. Kupitia mkutano huo maeneo ya ushirikiano yaliyokubalika ni pamoja na: Kuimarisha na kukuza Uwekezaji na Biashara, kuanzisha Jukwaa la Biashara (Business Forum) baina ya Tanzania na Oman pamoja na Kikundi cha Watalaam (Technical Working Group) kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji na biashara na kufuatilia utekelezaji wa masuala yaliyokubalika.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** Masuala mengine yaliyojadiliwa na kukubalika katika mkutano huo ni pamoja na: Uanzishwaji wa Mkataba wa Biashara baina ya Tanzania na Oman, Uanzishwaji wa Mfuko wa Uwekezaji (Oman - Tanzania Investment Vehicle), Matumizi ya Bandari ya Salalah Oman kwa mizigo inayotoka au kwenda sehemu mbalimbali duniani na ushirikiano katika usafirishaji wa pamoja wa mizigo baharini (Joint Cargo Shipping). Aidha, kwa kuwa masuala yaliyojadiliwa na kukubalika katika mkutano huo yanahitaji muda katika utekelezaji wake, Wizara imeendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala husika kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na taasisi husika.

**B. Kuendelea na Majadiliano ya utekelezaji wa Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Bara la Afrika (African Continental Free Trade Area – AfCFTA)**

130. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika jitihada za kuendelea na majadiliano na utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (AfCFTA), Wizara ilifanya maandalizi na kushiriki Mkutano wa Tisa (9) wa Baraza la Mawaziri wa

Biashara la AfCFTA uliofanyika mwezi Julai, 2022, Accra, Ghana. Katika mkutano huo, Tanzania ilifanikiwa kutetea msimamo wake kwenye suala la Uasili wa Bidhaa zinazozalishwa katika Maeneo Maalum ya Uzalishaji. Aidha, Tanzania iliweza kusimamia suala la Uasili wa Bidhaa ya Tumbaku ambapo kigezo kilichopitishwa kitakuwa na manufaa makubwa kwa kuwalinda wazalishaji wa ndani wa zao la Tumbaku dhidi ya ushindani kutoka nchi nyingine.

131. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliandaa na kushiriki Kongamano la kwanza la Wanawake na Vijana katika Biashara kwenye Eneo Huru la Biashara la Afrika lililofanyika mwezi Septemba, 2022 Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo limefanikiwa kutangaza fursa za biashara na utalii zilizopo nchini. Kongamano hilo liliweza kutoa maoni na mapendekezo ambayo yatatumika katika mchakato wa kuanzishwa Itifaki ya Wanawake na Vijana katika biashara chini ya AfCFTA ili kuimarisha ushiriki na mchango wao katika maendeleo ya Bara la Afrika. Kongamano hilo lilifanyika chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mhamasishaji wa Wanawake na Vijana katika biashara Barani Afrika chini ya Mkataba wa AfCFTA.

132. ***Mheshimiwa Spika***, Kupitia Kongamano hilo, tulifanikiwa kutangaza fursa za utalii na uwekezaji zilizopo nchini, ambapo jumla ya washiriki 116 walitembelea banda la Bodi ya Utalii na Kamisheni ya Utalii Zanzibar pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Novemba 2022, Niamey, Niger. Mkutano huo ulihusu Maendeleo ya Viwanda Barani Afrika na Uanuai wa Uchumi na AfCFTA. Mkutano huo ulijikita katika masuala ya kisera na mikakati ya kuimarisha maendeleo ya viwanda barani Afrika pamoja na matumizi ya fursa za mkataba wa AfCFTA katika

kukuza biashara miongoni mwa nchi za Afrika. Katika mkutano huo, Tanzania ilizihimiza nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya biashara barani Afrika ili kuondokana na changamoto ya matumizi ya lugha tofauti baina ya nchi za Afrika ambayo kwa kiasi kikubwa yanarudisha nyuma jitihada za ufanyaji wa biashara kati ya nchi za Afrika.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa sasa nguvu kubwa tumewekeza kwenye utekelezaji wa Mkataba wa AfCFTA ambapo Wizara inaendelea na zoezi la kuhamasisha na kuhimiza wafanyabiashara kuchangamkia fursa za soko la AfCFTA na baadhi ya wafanyabiashara wako tayari kuuza bidhaa zao kwenye soko hilo. Wizara imefanya Mikutano na Warsha mbalimbali na Sekta Binafsi kuhusu matumizi ya fursa za AfCFTA na mikutano ya hivi karibuni imefanyika tarehe 24 Januari 2023 na tarehe 11 - 17 Aprili, 2023 na wafanyabiashara pamoja na Wataalam kutoka Sekretarieti ya AfCFTA ambapo uelewa uliendelea kutolewa juu ya taratibu za kufuata wakati wa kuuza bidhaa katika soko la AfCFTA. Kupitia jitihada hizo na zingine zinazoendelea kutolewa na Wizara, bidhaa zetu zitaanza kuuzwa katika soko la AfCFTA na nchi kuanza kunufaika na Mkataba huo.

**C. Kukamilisha Majadiliano ya Biashara ya Huduma kwa Sekta Sita (6) za Kipaumbele katika Nchi Wanachama wa SADC**

135. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya SADC iliandaa warsha ya wadau wa Sekta za Umma na Binafsi wanaohusika na Biashara ya Huduma kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa sekta sita (6) za Biashara ya Huduma zilizofunguliwa katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) iliyofanyika tarehe 12 - 14 Septemba 2022, Dodoma. Aidha, huduma zilizofunguliwa ni Mawasiliano, Fedha, Uchukuzi, Utalii, Nishati na Ujenzi. Lengo jingine la warsha hiyo lilikuwa ni kujipanga kwa ajili ya

maandalizi ya majadiliano ya awamu ya pili ya kufunguliana sekta ndogo za Biashara za Huduma zilizobakia ambazo ni Biashara, Elimu, Afya, Usambazaji, Mazingira na Utamaduni na Michezo. Kupitia warsha hiyo na majadiliano yaliyofanyika na uelewa uliopatikana, Wizara inaendelea na maandalizi ya rasimu ya maeneo ambayo nchi inaona yatafaa kufunguliwa katika sekta hizo kwa kuzingatia maslahi ya nchi katika maeneo husika.

**D. Kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye masuala ya Biashara ya Bidhaa na Huduma**

136. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishiriki kwenye mkutano wa Mawaziri wa Baraza la Kisekta la Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji (SCTIFI) uliofanyika tarehe 28 Novemba hadi 2 Desemba, 2022, jijini Arusha. Kupitia mkutano huo, masuala mbalimbali yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na suala la Tanzania kuridhia Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Utatu (COMESA-EAC - SADC Tripartite) na taarifa ya uchambuzi wa wataalam kuhusu Mkataba wa Ubia wa Uchumi baina ya Uingereza na Kenya (Kenya-UK EPA). Katika mkutano huo ilibainika kuwa, Mkataba huo umekiuka masharti ya Ibara ya 37 ya Itifaki ya Umoja wa Forodha ya EAC. Ibara hiyo inazitaka nchi wanachama kufanya majadiliano ya pamoja na nchi za nje hasa zinazoomba ushirikiano wa kiuchumi au endapo nchi moja itafanya majadiliano na nchi nyingine nje ya EAC inapaswa kutoa taarifa kwa Sekretarieti ya EAC, ili kuzitaarifu nchi nyingine wanachama na hatimaye ipate ridhaa ya nchi hizo na Kenya haikufuata utaratibu huo. Majadiliano ya suala hili bado yanaendelea ndani ya Jumuiya yetu ya EAC.

**E. Kuimarisha Kamati za Kitaifa za Kusimamia Urahisishaji wa Biashara Nchini**

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu Mkutano wa Kumi

(10) wa Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia masuala ya afya ya Wanyama, Mimea na Usalama wa Chakula uliofanyika mwezi Agosti, 2022 Mkoani, Morogoro. Mkutano huo pamoja na mambo mengine ulijadili utekelezaji wa masuala yaliyokubalika katika Mkutano wa Tisa (9) wa Kamati ya Kitaifa ya kushughulikia masuala ya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula katika biashara uliofanyika mwezi Februari 2022 Mkoani, Morogoro pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Mradi wa *Quality Infrastructure and SPS* unaofadhiliwa na Taasisi ya TMEA.

138. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara iliratibu mkutano wa Kamati ya Kitaifa (National Monitoring Committee - NMC) ya Uondoaji wa vikwazo vya Biashara visivyo vya Kiushuru (NTBs) uliofanyika mwezi Septemba, 2022 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo ulipokea na kujadili taarifa ya mikutano ya kikanda ya uondoaji wa NTBs iliyofanyika kwa kipindi cha mwezi Septemba 2021 hadi Septemba 2022. Katika mkutano huo jumla ya vikwazo 30 vilijadiliwa ambapo 10 vilitatuliwa na 5 vilifutwa kwa kukosa vielelzo vya kujitosheleza. Kwa upande Tanzania na Kenya vimebaki vikwazo 15, ambapo dhidi ya Tanzania vimebaki vikwazo 7 na dhidi ya Kenya vimebaki vikwazo 8. Kamati iliazimia kufuatilia kwa karibu uondoaji wa vikwazo vilivyobakia kwa ajili ya kuwezesha biashara baina ya Tanzania na nchi jirani kuendelea kufanyika bila vikwazo na usumbufu kwa wafanyabiashara.

#### 4.2.6. Maendeleo ya Biashara

#### A. Kuhamasisha Jumuiya ya Wafanyabiashara Kuhusu Fursa za Masoko

139. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi za Balozi zetu zilizopo katika maeneo mbalimbali duniani katika kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya uhakika ya mazao na bidhaa zinazozalishwa nchini. Hii ni pamoja na kuainisha taarifa kuhusu kiasi na ubora wa bidhaa zinazohitajika na taratibu za kuyafikia masoko hayo na

kuzifikisha taarifa hizo kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa ndani. Kutokana na jitihada hizo, Wizara imefanikiwa kupata fursa ya soko la bidhaa mbalimbali nchini China (maharage ya soya, korosho, muhogo na parachichi); Qatar (Nyama); Kenya (Mchele); Uturuki (Karanga); India (Soya na parachichi); Umoja wa Falme za Kiarabu (pilipili mbuzi na nyama); na Denmark (asali na pilipili kavu). Aidha nchi ya India imeruhusu Tanzania kuingiza kiasi cha tani 200,000 za mbaazi kwa kipindi cha kuanzia Februari 2022 hadi Machi 2023. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo inaendelea kuhamasisha uzalishaji wa ndani ili kufikia viwango vya ubora na kiasi kinachohitajika na kuendelea kuwasiliana na Balozi zetu kwa lengo la kuwaunganisha wazalishaji wa ndani na soko hilo.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeweza kushawishi viwanda vidogo vya ubanguaji korosho kuingia makubaliano ya kuuza korosho kwa kampuni ya *Ward Holdings International LLC* ya Marekani yenye tawi nchini Tanzania (Ward Holdings Tanzania). Kampuni hiyo imefanikiwa kuanza kuuza Korosho tani nane (8) kwa rajamu ya *TanzaNuts* katika Soko la Marekani. Aidha, taratibu zinaendelea kuwezesha jumla ya viwanda vidogo vipatavyo 102 vinavyobangua korosho katika Mikoa ya Pwani, Lindi, Ruvuma na Mtwara kunufaika na fursa hiyo.

*141.* ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imewezesha Wafanyabiashara wa Tanzania wapatao 859 kupata fursa ya kutangaza bidhaa zao kupitia maonesho, misafara ya kibiashara na makongamano ya kibiashara yaliyoratibiwa na TanTrade. Wafanyabiashara hao walitangaza bidhaa kwa wanunuzi kutoka nchi za China, Saudi Arabia, Kuwait, Qatar, Kenya, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo, Comoro, Oman na Marekani. Bidhaa zilizotangazwa ni pamoja na vito, madini, nyama, matunda, mbogamboga, nafaka (mahindi, mchele, maharage) muhogo, mbao, asali, pilipili, karanga, alizeti, viungo, vanila na soya.

## B. Uratibu wa Majukumu ya Watalaam wa Biashara Nchini

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inashirikiana na OR - TAMISEMI katika kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya biashara nchini. Lengo ni kuhakikisha majukumu yanayotekelezwa na Wataalam wa Biashara walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) yanawezesha biashara na kuweka mazingira rafiki kwa Wawekezaji na Wafanyabiashara. Wizara imeendelea kupokea taarifa mbalimbali za masoko na bei za bidhaa zinazowasilishwa na Maafisa Biashara katika maeneo wanayosimamia kupitia Idara mpya ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iliyoanzishwa kwenye Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inashirikiana na OR - TAMISEMI katika kutoa mafunzo kuhusu Sheria ya Leseni za Biashara (Sura 208) kwa Wataalam wa Biashara. Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023, mafunzo yalifanyika katika Mikoa ya Kanda ya Magharibi; Kanda ya Pwani na Kanda ya Kaskazini. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo na uelewa Wataalam wa Biashara walioko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwawezesha kutekeleza na kusimamia Sheria ya Leseni za Biashara kwa ufanisi na hivyo kuboresha mazingira ya uanzishaji na uendeshaji wa biashara kwenye maeneo yao. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Majukumu ya Wataalam wa Biashara ambao utaisaidia kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## C. Mwenendo wa Bei za Bidhaa Muhimu Nchini

144. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya tathmini na kutoa taarifa kwa wananchi kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu na bei za mazao ya chakula nchini. Taarifa

hizi ni muhimu kwa ajili ya kuwawezesha wadau ikiwa ni pamoja na wazalishaji wa mazao na bidhaa mbalimbali, watumiaji wa bidhaa hizo, wenye viwanda na wafanyabiashara kupata taarifa ili kufanya maamuzi yatakayochangia kukuza uchumi na kipato katika ngazi ya mtu mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** Mwenendo wa bei za vifaa vya ujenzi kwa mwaka 2022/2023 umeendelea kushuka na kuonesha uhimilivu hasa kwa upande wa nondo. Hali hii imesababishwa na kuimarika kwa uzalishaji wa ndani wa bidhaa hizo sambamba na usimamizi madhubuti wa mwenendo wa soko la bidhaa hizo uliofanywa na Wizara pamoja na taasisi zake. Wastani wa bei ya Nondo moja ya mm 12 imeshuka kutoka shilingi **26,865** kipindi cha mwezi Februari, 2022 hadi shilingi **24,417** mwezi Februari, 2023 sawa na upungufu wa asilimia 9.1; Nondo moja ya mm 16 imeshuka kutoka shilingi **46,097** hadi shilingi **45,587** sawa na upungufu wa asilimia 1.1; Nondo moja ya mm10 imeshuka kutoka shilingi **19,450** hadi shilingi **18,629** sawa na upungufu wa asilimia 4.2. Vile vile, bei ya Nondo moja ya mm 8 imeshuka kutoka shilingi **15,250** hadi shilingi **15,083** sawa na upungufu wa asilimia 1.1. Aidha, wastani wa bei ya saruji imeonesha uhimilivu ambapo mfuko mmoja (1) wa saruji wa Kg 50 ulikuwa shilingi 17,606 mwezi Februari 2022 na shilingi **17,688** mwezi Februari, 2023. Vile vile, bei ya bati imeongezeka kwa asilimia 6.4 kutoka shilingi **23,091** kwa kipindi cha mwezi Februari 2022 hadi shilingi **24,563** mwezi Februarui, 2023 mtawalia.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na kuondolewa kwa vikwazo vya biashara kwa baadhi ya nchi zinazozalisha na kusambaza kwa wingi mafuta ya kupikia katika soko la Dunia, bei ya mafuta ya kupikia imeshuka. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, wastani wa bei ya mafuta ya alizeti imeshuka kutoka dola za Marekani **1,491.30** kwa tani moja kwa kipindi cha mwezi Machi, 2022 hadi dola za Marekani

**1,088.10** sawa na upungufu asilimia 27.03. Vile vile, bei ya mafuta asili ya mawese imeshuka kutoka dola za Marekani **1,776.96** kwa tani moja kwa kipindi cha mwezi Machi, 2022 hadi kufikia dola za Marekani **975.63** kwa kipindi cha mwezi Machi 2023 sawa na upungufu wa asilimia 45.09.

147. ***Mheshimiwa Spika***, Kumekuwa na ongezeko la bei za mazao ya chakula nchini. Wastani wa bei ya Maharage imepanda kutoka shilingi 215,193 kwa gunia la kilo 100 mwezi Februari, 2022 hadi kufikia shilingi 301,297 mwezi Februari, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 40. Aidha, wastani wa bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 imeongezeka kutoka shilingi 90,330 mwezi Februari, 2022 hadi kufikia shilingi 115,141 mwezi Februari, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 27.5. Vile vile, wastani wa bei ya mchele kwa gunia la kilo 100 imeongezeka kutoka shilingi 216,738 mwezi Februari, 2022 hadi shilingi 291,819 mwezi Februari, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 34.6.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake kwenye kiasi cha mavuno ya mazao muhimu ya chakula kama vile mchele, mahindi, maharage na viazi mviringo, mahitaji ya bidhaa hizo kwenye nchi jirani yamekuwa makubwa kuliko uzalishaji hivyo, kuchangia kupanda kwa bei za bidhaa za vyakula nchini na nchi jirani. Aidha, kwa ujumla bei za vyakula katika nchi nyingi duniani zimepanda. Hata hivyo, mfumuko wa bei nchini Tanzania ni wa kiwango cha chini zaidi ikilinganishwa na nchi jirani ambapo kwa Tanzania kiwango cha mfumuko wa bei ni asilimia 4.9 kwa mwezi Januari 2023 ikilinganishwa na asilimia 9.1 nchini Kenya, asilimia 10.4 nchini Uganda na asilimia 21.7 nchini Rwanda kwa mwezi Januari, 2023. Aidha, katika mwaka 2022 mfumuko wa bei ulikuwa kwa wastani wa asilimia 4.3.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa taarifa za uhakika za bei za bidhaa na

masoko, kufanya uchambuzi na kusambaza kwa wadau. Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI kupitia Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji iliyoanzishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini ili kupata taarifa za kuaminika na kwa wakati kutoka maeneo yote nchini. Nawahimiza Maafisa Biashara kote nchini kwa kushirikiana na Maafisa Ugani waliopo katika maeneo yao kuhakikisha wanafuatilia kwa karibu uzalishaji wa bidhaa hasa za kilimo pamoja na mwenendo wa bei katika maeneo wanayosimamia ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa za bei na kuziwasilisha kwa wakati Wizarani.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kufuatilia na kufanya tathmini ya bei za bidhaa muhimu ili kulinda maslahi ya wadau wote ikiwa ni pamoja na wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa husika. Aidha, nitoe rai kwa Wafanyabiashara kote nchini kuendelea kuzingatia misingi ya ushindani wa haki katika kufanya biashara ili kuunga mkono jitihada za Serikali za kukuza uchumi kwa manufaa ya Wananchi wote. Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ushindani Namba 8 ya mwaka 2003 na Kanuni za Ushindani za mwaka 2018 kwa lengo la kumlinda mlaji na kushajihisha ushindani. Vile vile, Serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa muhimu na mazao ya chakula ili kudhibiti mfumuko wa bei nchini.

**D. Kuhamasisha na Kuwezesha Utangazaji wa Bidhaa na Huduma za Tanzania kwenye Masoko ya Ndani na Nje**

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu Maonesho ya Biashara ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwawezesha wazalishaji wa mazao, bidhaa na huduma mbalimbali nchini kujitangaza na kunufaika na fursa za masoko hayo. Maonesho hayo ni pamoja na Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika kuanzia mwezi Juni hadi Julai, 2022. Kupitia maonesho hayo, jumla ya

Wafanyabiashara 3,200 wa Kitanzania na wafanyabiashara 225 kutoka nchi 23 za Afrika, Asia, Ulaya na Marekani ya Kusini walishiriki. Jumla ya watu 315,000 walitembelea maonesho hayo na jumla ya ajira za muda 11,650 zilipatikana.

152. ***Mheshimiwa Spika*,** Kupitia uratibu wa Maonesho ya 46 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), jumla ya Mikataba 10 ya Makubaliano (MoU) yenye thamani ya shilingi **billioni 176.65** ilisainiwa. Mikataba hiyo ilihusu utoaji wa huduma na bidhaa mbalimbali kama vile huduma za Matengenezo ya Mashine na Mitambo ya uokoaji, Huduma ya mafunzo ya uendeshaji mitambo, Maguta yenye Injini, Koili za mfumo wa vyombo vya ubaridi, na bidhaa za Mahindi Meupe, Maharage ya Soya, Mchele,Katuni za mbao kwa ajili ya Urembo wa Sakafu na Kuta za nyumba, Mashine za kukoboa na kusaga nafaka.

153. ***Mheshimiwa Spika*,** Kati ya mikabata hiyo, mikataba mitano imetekelezwa ambayo ilihusisha:- Shirika la Viwanda vidogo vidogo (SIDO) na Chama cha Waokaji Tanzania (TBA) yenye thamani ya shilingi 41, 000,000 ya kutoa huduma ya mafunzo ya uendeshaji mitambo kwa wanachama 15,000. Hadi sasa, TBA kwa kushirikiana na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) wametoa mafunzo ya usimamiaji wa biashara (Business Management) kwa wajasiriamali 70 na mafunzo ya uendeshaji mitambo kwa wajasiriamali 140 wa tasnia ya Uokoaji yaliyofanyika mwezi Novemba, 2022.

154. ***Mheshimiwa Spika*,** Makubaliano yenye thamani ya dola za Marekani 515,700 yalisainiwa kati ya Kampuni ya *East Africa Commercial and Logistics Ltd ya Dar es Salaam* na kampuni ya EFL Company ya Dar es Salaam kuuza kontena 20 za mbao kwa ajili ya urembo wa sakafu na kuta za nyumba. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, kontena 7 zenye thamani ya dola za Marekani **195,966** zimeuzwa kupitia makubaliano hayo.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** Makubaliano yenye thamani ya dola za Marekani **579,000** yalisainiwa kati ya Kampuni ya *Shandong Sishui Haiyon Food Processing Machine Co. Ltd* ya China na Kampuni ya *Halce Group Ltd* ya China kuuziana Seti 100 za machine ya kukoboa na kusaga. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, mashine 46 kati ya mashine 1 zenye thamani ya dola za Marekani **266,340** ikiwa ni sawa na thamani ya shilingi **621,903,900** zimeuzwa. Vile vile, makubaliano yenye thamani ya dola za Marekani **364,500** yalisainiwa kati ya *Shandong Jin Hua Iron &Steel Co. Ltd* ya China kuiuzia Kampuni ya *GSB Mat Doors Ltd* ya Tanzania tani 27 za koili za mfumo wa vyombo vya ubaridi. Katika kipidi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, tani 12 zenye thamani ya dola za Marekani **167,670** zimeuzwa.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Makubaliano yenye thamani ya dola za Marekani **1,130,000** yamesainiwa kati ya *Shandong Wuzhen Group Co.Ltd* kuiuzia Kampuni ya Chico Co.Ltd ya Tanzania maguta yenye injini. Hadi Machi, 2023, maguta 200 yenye thamani ya dola za Marekani **339,000** yameuzwa.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu Maonesho ya saba (7) ya Bidhaa za Viwanda mwezi Desemba, 2022 ambayo yalikwenda sambamba na sherehe za Maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Taifa letu. Jumla ya Viwanda Vidogo, Vya Kati na Vikubwa **502**, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi Tanzania Bara na Zanzibar zilishiriki. Maonesho hayo yalitoa fursa ya kutangaza bidhaa ikiwemo Bidhaa za Maziwa yaliyosindikwa Viwandani; bidhaa za batiki; na kutambulisha kazi za ubunifu, sanaa, utamaduni na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

## E. Utayarishaji wa Viwango vya Kitaifa katika Sekta Mbalimbali

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022

hadi Machi, 2023, Wizara imeweza kuandaa viwango muhimu katika sekta ya kilimo, chakula, uhandisi na viwango vya vifungashio mbalimbali. Jumla ya viwango **191** sawa na asilimia **30.3** ya lengo la kutayarisha viwango 630 kwa mwaka vimeandaliwa, asilimia **70** ya viwango ambavyo havijaandaliwa viko katika hatua za mwisho za utayarishaji ambapo vinatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2023. Aidha, kati ya viwango **191** vilivyokamilika, viwango **35** katika nyanja ya kemikali, **2** katika nyanja ya uhandisi umeme, **14** katika nyanja ya mazingira, **1** katika nyanja ya ujenzi, **84** katika sekta ya kilimo na chakula, **35** katika nyanja ya nguo na ngozi, **6** katika nyanja ya uhandisi mitambo, **9** katika nyanja ya migodi na madini na **5** katika sekta mtambuka.

**F. Kutoa Leseni ya Ubora kwa Bidhaa za Wajasiriamali Wadogo**

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imetoa jumla ya leseni **666** za nembo ya ubora ya TBS sawa na asilimia **102.5** ya lengo la kutoa leseni **650** kwa mwaka 2022/2023. Miongoni mwa leseni hizo, leseni **315** zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha mafuta ya kupaka, chaki, mchele, korosho, unga wa mahindi, sabuni za aina mbalimbali, viungo, mafuta ya nazi, keki, juisi, pombe za nafaka, mkate, pombe isiyotokana na nafaka, pombe kali, mvinyo, nyama za kuku, na nyama za kusindika. Aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali katika dhana nzima ya kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

**G. Kusajili Bidhaa na Majengo, Maeneo ya Uzalishaji, Uuzaji na Usambazaji wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi**

160. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imesajili jumla ya bidhaa za chakula na vipodozi **1,323** sawa na asilimia **49.0** ya matarajio ya kusajili

bidhaa za chakula na vipodozi **2,700** kwa mwaka 2022/2023, idadi ya bidhaa zilizobaki ziko katika hatua za mwisho za usajili. Aidha, jumla ya majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi **6,904** sawa na asilimia **69.0** ya matarajio ya kusajili na kutoa vibali **10,000** kwa mwaka 2022/2023 yamesajiliwa. Vile vile, Wizara inaendelea na utekelezaji wa lengo hilo kwa kuandaa mifumo na taratibu za udhibiti wa usalama wa vipodozi ikiwa ni pamoja na kuendelea kuijengea maabara uwezo wa kupima viambata sumu katika vipodozi.

**H. Kupima Sampuli za Bidhaa na Kufanya Ugezi kwa Vifaa/Mashine**

161. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilipima jumla ya sampuli 22,533 katika maabara za TBS ikilinganishwa na lengo la kupima sampuli 40,000 sawa na asilimia 56.3. Idadi hii ya sampuli ilisababishwa na ongezeko dogo la sampuli kutoka nje ya nchi kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 na vita vya Urusi na Ukraine. Aidha, Wizara ilifanyia ugezi jumla ya vifaa 7,291 sawa na asilimia 60.8 ya lengo la kufanyia ugezi vifaa 12,000 kwa kipindi cha mwaka 2022/2023.

**I. Udhibiti wa Bidhaa Zinazotoka Nje ya Nchi**

162. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ilikagua jumla ya magari 38,785 yaliyotumika nje ya nchi sawa na asilimia 77.6 ya lengo la kukagua magari 50,000 kwa mwaka. Vile vile, katika kipindi hicho jumla ya vyeti vya ubora 80,055 vimetolewa kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi; hii ni sawa na asilimia 80.1 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 100,000 kwa mwaka 2022/2023.

**J. Kuelimisha Umma Juu ya Umuhimu wa Kufanya Sajili Mbalimbali za Kibiashara**

163. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanya kaguzi elimishi tano (5) za Viwanda na Ukaguzi wa Leseni za Biashara katika mikoa ya Songwe, Pwani, Mara, Geita na Njombe ambapo elimu juu ya Sheria ya Taifa ya Viwanda (Leseni na Usajili) Sura 46 na namna ya kutuma maombi ya Leseni za Viwanda kwa njia ya mtandao ilitolewa. Katika kaguzi hizo, jumla ya biashara 879 za Kundi A zilikaguliwa ambapo biashara 363 zilibainika kufanyika bila kuwa na Leseni za Biashara, biashara 97 zilibainika kuwa na leseni zilizoisha muda wake na biashara 419 zilikuwa na leseni zilizo hai. Aidha, wafanyabiashara ambao walikutwa hawana leseni walielimishwa na waliandikiwa barua za kuwataka kukata Leseni. Baadhi ya wafanyabiashara waliokaguliwa, kuelimishwa na kuandikiwa barua za kuwataka kukata leseni, tayari wamekata leseni za biashara. Hatua za ufuatiliaji zinaendelea kuchukuliwa na Wizara kuhakikisha wafanyabiashara wanakuwa na leseni halali.

**K. Kuboresha na Kuimarisha Mifumo ya kurahisisha ufanyaji Biashara Nchini**

164. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha na kuboresha Mifumo ya Sajili (Online Registration System – ORS) na Dirisha la Taifa la Biashara (Tanzania National Business Portal-TNBP) ili kurahisisha utoaji wa huduma. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kazi ya kufanya maboresho kwenye mfumo wa ORS imekamilika katika Moduli ya Makampuni na Majina ya Biashara. Aidha, maboresho katika moduli za Alama za biashara na Huduma na Hataza yapo katika hatua ya majaribio kwa watumiaji wa ndani (User Acceptance Test - UAT).

165. ***Mheshimiwa Spika***, Kupitia maboresho hayo, Wizara imefanikiwa kutoa huduma zake kama ifuatavyo: Kusajili jumla ya Makampuni 10,918 kati ya 13,000 yaliyokusudiwa

sawa na asilimia 84, Kusajili Majina ya Biashara 19,954 kati ya 25,100 yaliyopangwa, sawa na asilimia 79, Kusajili Alama za Biashara na Huduma 2,944 kati ya 4,120 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 71. Vile vile, Wizara imefanikiwa kutoa Hataza 15 kati ya 35 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 43, leseni za Viwanda 138 kati ya 200 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 69; na imetoa Leseni za Biashara kundi "A'' 11,978 kati ya 13,750 zilizokuwa zimepangwa sawa na asilimia 87.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imekamilisha uunganishaji wa mifumo ya Maombi ya Leseni, Mfumo wa Usimamizi wa Ghala (WRRB MIS) na Mfumo wa Ghala la Kimtandao (e-Warehouse). Aidha, mifumo hiyo inafanyiwa majaribio na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kabla ya kuanza kutumika rasmi.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imesanifu mfumo wa Taarifa za Biashara kwa lengo la kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa taarifa mbalimbali za fursa za biashara nchini. Vile vile, Wizara imeboresha mfumo wa Taarifa za Taratibu za Ufanyaji Biashara nchini (Tanzania Trade Portal) kwa kuongeza taratibu za usafirishaji wa mazao ya nyuki kwenda nje ya nchi (Export Procedures). Wizara imeanza kurahisisha taratibu za usajili, leseni na vibali kwa kuoanisha mifumo ya ATMIS ili kuruhusu kupata taarifa za makampuni/biashara kwa kutumia Leseni ya Biashara au nambari za utambulisho wa mlipa kodi (TIN) na Cheti cha Hali ya Ulipaji Kodi (Tax clearance).

168. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imekamilisha maandalizi ya ujenzi wa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za FCC utakaojulikana kama *FCC Management Information System (FCC – MIS).* Aidha, Wizara imekamilisha mfumo wa kupokea na kuchambua miungano ya kampuni na umewasilishwa Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa ajili ya kukaguliwa. Vile

vile, mfumo wa kupokea maombi ya kuidhinishiwa Mikataba inayoandaliwa na upande mmoja (Standard Form Consumer Contracts – SFCCs) umeanza kujengwa.

**L. Kusimamia Utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala**

169. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ambapo, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, kaguzi 165 zimefanyika kabla na baada ya kutoa leseni. Jumla ya leseni 54 zilitolewa kwa kampuni 35 za waendesha ghala na nne (4) za Meneja Dhamana kwenye mazao ya Maharage, Mhogo Mkavu, Korosho, Mahindi, Mpunga, Mchele, Mtama, kahawa, Kakao, Karanga, Mbaazi, Soya, Ufuta na Iriki. Aidha, jumla ya tani 297,550.120 za mazao tajwa zilikusanywa na kuhifadhiwa katika ghala kuu na kuuzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Mwongozo mmoja (1) wa zao la Korosho na Iriki umeandaliwa na kukamilika. Aidha, rasimu ya miongozo kwa mazao ya Asali na Pamba zimeandaliwa na zipo katika hatua za kupata maoni ya wadau kwa ajili ya maboresho kabla ya utekelezaji wake.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Viwanda vitatu (3) vya kahawa viliunganishwa na Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mikoa ya Kagera (1), Mbeya (1) na Ruvuma (1). Aidha, Kiwanda kimoja cha Iriki Mkoani Morogoro kinatarajiwa kuunganishwa na mfumo wa stakabadhi za ghala na kiwanda kimoja (1) cha asali kilichopo katika Mkoa wa Tabora kipo katika hatua za mwisho za kuingizwa kwenye mfumo huo. Vile vile, katika maeneo yote yanayoendelea kutekeleza Mfumo wa Stakabadhi za ghala nchini, Wizara imeendelea kuongeza wigo wa mazao yanayotumia mfumo.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mapitio ya utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa lengo la kuboresha utendaji na ufanisi. Katika kipindi cha Julai, 2022

hadi Machi 2023, Wizara imefanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Lindi na Pwani kwenye mazao ya Kahawa, Korosho na Ufuta. Matokeo ya tathmini hiyo yamebaini uhitaji mkubwa wa matumizi ya mizani za kidijitali katika kupima mazao.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi mwezi Machi 2023, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imekamilisha uundaji wa mfumo wa Maombi ya Leseni kwa njia ya mtandao. Hii imeondoa adha waliyokuwa wakiipata waendesha ghala kulazimika kufika katika ofisi za bodi kwa ajili ya kuwasilisha maombi ya leseni. Aidha, Mfumo wa Usimamizi wa Ghala (WRRB MIS) na Mfumo wa Ghala la Kimtandao (e-Warehouse) imehuishwa na kufanyiwa majaribio (User Acceptace Test) tayari kuanza kutumika mwezi Julai, 2023.

**M. Kuendelea Kupanua Wigo na Kuimarisha Utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Maeneo Mapya na yale Yanayotumia Mfumo kwa sasa**

173. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeongeza wigo katika mazao ya kahawa na kokoa na kuongeza idadi ya mazao yanayotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, kutoka 12 (mwaka 2022) hadi kufikia 17 (mwaka 2023). Mazao yaliyoongezeka ni pamoja na Mhogo Mkavu, Karanga, Mtama, Mchele na Iriki.

174. ***Mheshimiwa Spika,*** Vile vile, ghala la kuhifadhi zao la asali katika Mkoa wa Tabora limeainishwa na kutambuliwa kwenye mfumo. Taratibu za ununuzi zinakamilishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, na Mfumo utaanza kufanya kazi mwezi Juni, 2023 katika kipindi cha msimu wa Asali. Aidha, zao la Pamba katika Mikoa ya Mwanza, Simiyu na Shinyanga limeingizwa katika mfumo ambapo taratibu za

mwongozo wake ziko katika hatua za mwisho ili kuliwezesha zao hili kutumia mfumo. Katika kupanua wigo na kuimarisha utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, Wizara imeweza kutoa leseni saba (7) za Meneja Dhamana kwa Kampuni za *Tanzania Traders and Merchant's Ltd, Ace Global Depository (T) Limited, City Coffee Ltd, Dan and Associates Enterprises Ltd, Mbinga Coffee Curing Company Limited, Microfinance Support Service Company Limited, Vission Control and Supperintendence Ltd* Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023.

**N. Kutengeneza Mkakati Mahsusi kwa ajili ya Kutangaza Mfumo wa Stakabadhi za Ghala**

175. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imetekeleza Mkakati wa Uhamasishaji wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika Mikoa ya Rukwa kwa mazao ya Mpunga na Mahindi; Njombe kwa mazao ya Parachichi (ambapo mashamba yenye parachichi yatatumika kama ghala, na hivyo kupunguza hasara itokanayo na parachichi zilizovunwa na kushindwa kuuzwa) na Mahindi. Aidha, kwa upande wa Manyara mazao ya Mbaazi, Dengu, Ufuta na Vitunguu Swaumu yataingizwa kwenye mfumo. Lengo kuu la Mkakati huo ni kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika ngazi ya Mikoa, Halmashauri za Wilaya na Wakulima Vijijini kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS).

**O. Kuimarisha Ushindani wa Kibiashara Nchini**

176. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara iliratibu programu 10 za mafunzo kwa wafanyabiashara ili kuimarisha uwezo wao, kuweza kujiendesha kiushindani na kutumia ipasavyo fursa za masoko zinazopatikana. Kupitia programu hizo wafanyabiashara 509 walipewa mafunzo ya usimamizi wa biashara na wafanyabiashara 22 waliunganishwa na taasisi saidizi za kibiashara ili kupata huduma mbalimbali.

## P. Kuratibu Uendeshaji wa Kliniki ya Biashara

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu utoaji wa huduma ya Kliniki ya Biashara katika Maonesho manne (4) yaliyofanyika Dar es Salaam (2), Geita (1) na Zanzibar (1). Katika maonesho hayo, jumla ya wafanyabiashara 549 walihudumiwa na Taasisi wezeshi zipatazo 22 zilipatiwa ushauri, usaidizi na ufumbuzi wa mahitaji yao. Vile vile, jumla ya changamoto 513 zilipokelewa ambapo kati ya hizo, changamoto 181 zilipata ufumbuzi na changamoto 332 zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi na taasisi husika.

## Q. Kuandaa Mwongozo wa Fursa za Biashara na Uwekezaji

178. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Biashara ya Marekani iliratibu uandaaji wa Mwongozo wa fursa za Biashara na Uwekezaji baina ya Tanzania na Marekani kwa lengo la kutangaza fursa za uwekezaji na Biashara nchini Marekani. Mwongozo huo ulisambazwa kwa Wakuu wa nchi za Afrika zaidi ya 40 walioshiriki Mkutano wa Wanachama wa Chemba ya Biashara ya Marekani na Viongozi na Wadau wa Biashara kutoka Tanzania na Wanachama Milioni tatu wa Chemba ya Biashara ya Marekani uliofanyika mwezi Desemba, 2022.

## *R.* Kusimamia, Kuhakiki na Kukagua Vipimo Vitumikavyo na Viingiavyo

179. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imekagua na kuhakiki vipimo 975,367 sawa na asilimia 103 ya lengo la kukagua vipimo 944,359. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa, vipimo 30,883 vilirekebishwa na vipimo 1,281 vilikataliwa. Aidha, Wizara iliendelea kufanya kaguzi za kawaida na kaguzi za kushtukiza ambapo jumla ya kaguzi 4,157 kati ya kaguzi 3,500

sawa na asilimia 118.7 ya kaguzi zilizopangwa kufanyika zilifanyika, ambapo vipimo mbalimbali vitumikavyo kwenye biashara, afya, usalama na mazingira vilikaguliwa. Vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni mizani, pampu za kuuzia mafuta, dira za maji, malori ya kubebea mchanga/kokoto na magari ya kubebea mafuta. Uhakiki na ukaguzi huo wa kushtukiza ulifanyika maeneo mbalimbali yakiwemo: - Masoko ya nafaka, viwandani, vituo vya mafuta, maduka ya nyama na ya kawaida.

**S. Ukaguzi wa Bidhaa Zilizofungashwa kwenye Maeneo ya Mipakani, Bandarini na Viwandani**

180. ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanya na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa (prepacked goods) kutoka nje ya nchi na zile zinazozalishwa hapa nchini. Bidhaa hizo zilikaguliwa kupitia vituo vilivyoko katika mipaka ya Sirari (Mara), Mtukula (Kagera), Namanga (Arusha), Holili (Kilimanjaro),Tunduma (Songwe), Tarakea (Kilimanjaro), Horohoro (Tanga), Kasumulu (Mbeya) na Kasesya (Rukwa). Aidha, vituo vipya vitatu (3) vya ukaguzi katika maeneo ya Manyovu (Kigoma), Mbweni (Dar es Salaam) na Bagamoyo (Pwani) vimefunguliwa. Vile vile, Wizara imeendelea kukagua bidhaa zinazozalishwa na zilizofungashwa na viwanda vya ndani ili kuhakiki usahihi wa kiasi kilichobainishwa. Baadhi ya bidhaa zilizokaguliwa ni vyakula, vilainishi, saruji, rangi, mitumba, mabati na nondo.

**T. Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Matumizi Sahihi ya Vipimo**

181. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imeshiriki katika maonesho mbalimbali ikiwemo maonesho ya TCCIA - Mwanza, Maonesho ya Nane nane Mbeya, Maonesho ya Madini Geita, Maonesho ya Wanawake Wajasiriamali (TWCC), maonesho ya bidhaa za Viwanda vya Tanzania, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa

Sabasaba Dar es Salaam. Kupitia maonesho hayo, Wizara ilitoa elimu kwa Wafanyabiashara na Wakulima wa viazi mviringo na parachichi katika Wilaya za Njombe Mjini, Makete, Wanging'ombe na Baraza la Madiwani Mpwapwa, Dodoma. Wizara ilitoa elimu kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi kwa watu wenye uhitaji maalum Ikwiriri katika Wilaya ya Rufiji. Vile vile, Wizara imeandaa *infographics* 70 kwa ajili ya kutangaza matukio mbalimbali ikiwa ni pamoja na taarifa zilizotolewa kwenye vyombo vya habari.

**U. Kuboresha Hali ya Ushindani katika Soko**

182. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanya uchunguzi wa mashauri nane (8) yanayohusu mienendo inayoashiria kula njama ya kupanga bei kati ya washindani (price fixing) ambayo yako katika hatua mbalimbali za kiuchunguzi. Kati ya mashauri hayo, shauri moja (1) la soko la uzalishaji na usambazaji wa nondo limetolewa Maamuzi ya Awali (Provisional Findings); na Mashauri mawili (2) ya soko la sukari na soko la mafuta ya kula yamefungwa; shauri moja (1) la ununuzi wa korosho lipo katika hatua ya ukusanyaji wa taarifa; mashauri mawili (2) ya soko la uagizaji na usambazaji wa magari mapya (GPSA Complaint) yapo katika hatua ya makubaliano (settlement); na Mashauri mawili (2) yapo katika hatua ya utoaji wa Maamuzi ya Mwisho (Final Findings).

183. ***Mheshimiwa Spika***, Mashauri matatu (3) yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko (Abuse of dominance) yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Mashauri hayo ni shauri la soko la majani ya chai, shauri la soko la maziwa mabichi na shauri la soko la vifaranga.

184. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara hufanya uchambuzi na kuidhinisha miungano ya kampuni kwa lengo la kuziwezesha kampuni husika kukuza mitaji, kuongeza ufanisi na kuongeza uzalishaji. Katika kipindi husika, Wizara imechambua maombi 54 ya miungano ya kampuni kutoka katika sekta za misitu,

kilimo, uzalishaji, nishati, madini, fedha, bima, uzalishaji na biashara.

185. ***Mheshimiwa Spika***, Kati ya maombi hayo, maombi ya miungano ya kampuni 42 sawa na asilimia 77.8, yalitolewa maamuzi ambapo maombi 39 yaliidhinishwa bila masharti yakilenga kukuza mitaji katika sekta za madini, misitu, kilimo na fedha, kufikisha umeme vijijini na kufanya utafiti (exploration) wa uwepo wa madini ya "uranium" nchini. Aidha, maombi matatu (3) yaliidhinishwa kwa masharti yenye lengo la kulinda ushindani, kukuza uchumi pamoja na kulinda maslahi ya umma katika soko husika. Maombi 12 yaliyobaki yanaendelea kushughulikiwa. Miungano ya Kampuni imeendelea kukuza uwekezaji katika sekta mbalimbali ambapo shilingi bilioni **347** zimewekezwa katika Sekta Ndogo ya Mbao, jumla ya dola za Marekeni **1,500,000** ziliwekezwa katika Sekta ya Madini.

*186.* ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilishughulikia mashauri tisa (9) ya miungano ya kampuni ambayo hayakuidhinishwa na FCC (unnotified mergers). Kati ya mashauri hayo, shauri moja (1) la soko la usafirishaji wa mizigo limetolewa maamuzi ya awali na wahusika wamejulishwa; Mashauri matano (5) yanayohusu soko la uingizaji na usambazaji wa madawa na vifaa tiba yako katika hatua ya ukamilishaji wa uchunguzi. Mashauri mawili (2) yapo katika hatua ya makubaliano (settlement) ambayo yanahusu uzalishaji wa gesi asilia na madawa; na shauri moja (1) lipo katika hatua za utoaji wa maamuzi ya mwisho.

## V. Kumlinda Mtumiaji Kutokana na Vitendo Hadaifu na Kandamizi katika Soko

187. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilishughulikia malalamiko 35 ya walaji. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 21 yaliyohusu Mikataba ya

huduma kwa wateja ambapo malalamiko 11 yalipatiwa ufumbuzi na 10 yanaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, malalamiko tisa (9) yaliyohusu taarifa za kupotosha kuhusu huduma, mawili (2) yalipatiwa ufumbuzi na saba (7) yanaendelea kupatiwa ufumbuzi. Vile vile, malalamiko matatu (3) yaliyohusu usalama wa bidhaa (*Product safety*) wahusika walishauriwa kuyawasilisha TBS; na Malalamiko mawili (2) yaliyohusu huduma za bima yanaendela kufanyiwa kazi.

**W. Mapambano Dhidi ya Bidhaa Bandia**

188. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kufanya kaguzi za kila siku katika Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu (ICDs). Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023 Wizara ilifanya kaguzi zote 249 ambazo ilipanga kufanya. Katika kaguzi hizo, jumla ya Makasha (containers) 7,918 yalikaguliwa. Kati ya hayo, makasha 206 yalikutwa na bidhaa zilizokiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963 zenye thamani ya shilingi **15,942,897,718.** Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na bidhaa za matumizi ya nyumbani, vifaa vya ujenzi, vipuri vya pikipiki na magari, vifaa vya kuandikia (*stationeries*) pamoja na zana za kilimo.

189. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya kaguzi za kushtukiza (*raids*) **19** katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Manyara, Iringa, Mbeya na Njombe. Katika kaguzi hizo, bidhaa bandia zenye thamani ya **shilingi 1,130,172,365** zilikamatwa. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na simu za mkononi, miswaki, vitasa vya milango, wino wa kompyuta, miswaki, bidhaa ya ujenzi mifuniko, majani ya chai na plagi za magari na pombe kali.

190. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara ilishiriki katika zoezi la ukamataji wa bidhaa bandia ya sukari yenye nembo ya "Bwana Sukari". Zoezi hilo lilisimamiwa na Bodi ya Sukari Tanzania kwa kushirikiana na TRA, TBS na Jeshi la Polisi Mkoa

wa Songwe ambapo watu wanne (4) walikamatwa kwa kujihusisha na kuuza bidhaa hizo bandia na mmoja kwa kuzalisha na kuuza bidhaa bandia. Vile vile, imeharibu bidhaa bandia zilizokamatwa Mkoa wa Mbeya (wino wa printa katoni 246) na Mkoani Ruvuma (wino wa printa katoni 186) na Mkoani Iringa (Kilogramu 1,302 za vifungashio).

191. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya kaguzi za masoko (Market Surveillance) mbili (2) kati ya nne (4) ilizopanga kufanya. Kaguzi hizo zilifanyika katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Ruvuma pamoja na mikoa ya Lindi na Mtwara. Kaguzi hizo zililenga kubaini aina ya bidhaa zilizopo sokoni na namna zinavyofuata Sheria ya Alama za Bidhaa ya mwaka 1963 na kuandaa mpango madhubuti wa kudhibiti bidhaa zinazokinzana na sheria hiyo. Ukaguzi huo ulibaini uwepo wa bidhaa bandia katika maduka mbalimbali yaliyokaguliwa. Bidhaa hizo ni pamoja na sabuni, wembe, dawa ya meno, simu na vipuri.

## X. Kushughulikia Mashauri ya Rufaa na Haki katika Ushindani wa Soko

192. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imepokea mashauri 56. Kati ya hayo mashauri 27 yametolewa maamuzi, na mashauri 29 yanaendelea kusikilizwa.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na hatua za uboreshaji wa Mfumo wa uendeshaji wa mashauri yanayowasilishwa katika Baraza. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, ujenzi wa mfumo huo umefikia asilimia 85. Mfumo huo pamoja na mambo mengine utapokea na kusajili kesi kwa njia ya mtandao.

## 5. VIPAUMBELE VYA BAJETI

194. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika Mwaka 2023/2024,

Vipaumbele vikuu vya Wizara ni pamoja na: -

i. Kutekeleza Miradi ya Kielelezo ya Magadi Soda Engaruka, Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga;
ii. Uwekezaji katika maeneo maalum ya kiuchumi (SEZ) na kongani za viwanda ikiwa ni pamoja na Nala SEZ, Kwala SEZ, Mkulazi SEZ, Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo;
iii. Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma;
iv. Kuboresha Mazingira ya Biashara;
v. Kukuza Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
vi. Kukuza Sekta Binafsi;
vii. Kuratibu majadiliano ya biashara baina ya nchi na nchi, Kikanda na Kimataifa na;
viii. Kuimarisha Huduma za Biashara na Masoko.

## 6. MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024

### 6.1. Uwekezaji

195. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuendeleza Uwekezaji: -

i. Kukamilisha maandalizi ya Sera mpya na Mkakati wake kuhusu Uwekezaji na kuanza utekelezaji wake;
ii. Kuratibu uanzishaji na uendelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji yenye manufaa mapana kwa Taifa;
iii. Kuendelea kuratibu programu za uhamasishaji wa uwekezaji ndani na nje ya nchi;
iv. Kuratibu programu za kuimarisha mifumo ya udhibiti wa uwekezaji inayolenga katika kupunguza gharama za uwekezaji nchini;
v. Kuratibu ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya uwekezaji;
vi. Kuendelea kuratibu utatuzi wa migogoro na changamoto za uwekezaji nchini;
vii. Kuendelea kuratibu uanzishwaji wa maeneo maalum ya kiuchumi (Special Economic Zones);

viii. Uendelezaji wa miradi ya kitaifa ya Kielelezo (National Flagship Projects) (Bagamoyo SEZ na Tanga SEZ);
ix. Kukamilisha malipo ya fidia katika maeneo ya SEZ (Bagamoyo, Tanga, Manyoni, Nala na Ruvuma;
x. Kuhamasisha uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi kupitia Soko la Mitaji (Capital Markets);
xi. Kufanya ukarabati wa miundombinu ya ndani katika Eneo Maalum la Uwekezaji la Banjamin William Mkapa (BMW SEZ);
xii. Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika maeneo 7 ya viwanda vilivyokabidhiwa kwa Mamlaka ya EPZ;
xiii. Uendelezaji katika maeneo ya SEZ (Mpango Kabambe - Master Plan na Upembuzi Yakinifu - Feasibility Study);
xiv. Kuhamasisha Sekta binafsi, Serikali za Mikoa na taasisi wadau kuwekeza katika kuendeleza Maeneo Maalum ya Uwekezaji (SEZ);
xv. Kufanya tafiti, ufatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa na Mamlaka ya EPZ;
xvi. Kuendelea kuboresha mifumo ya kusajili ili kuongeza idadi ya Miradi ya uwekezaji inayosajiliwa na Kituo;
xvii. Kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma zitolewazo kwa wawekezaji katika Kituo cha Huduma za mahali pamoja;
xviii. Kuendelea kutafuta ardhi kwa ajili ya uwekezaji;
xix. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya masuala mbalimbali ya uwekezaji nchini;
xx. Kufanya tafiti mbalimbali za uwekezaji ili kuibua fursa za uwekezaji nchini na kuboresha mazingira ya uwekezaji;
xxi. Kuendelea kushirikiana na Balozi za Tanzania katika kuitangaza Tanzania ili kuvutia uwekezaji
xxii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania; na

Kuunganisha taarifa za vivutio vya uwekezaji vinavyotolewa na taasisi mbalimbali za umma nchini.

**6.2. Uwezeshaji Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi**

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuendeleza wananchi kiuchumi na maendeleo ya sekta binafsi: -

i. Kuratibu sekta binafsi ili iweze kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za maendeleo;
ii. Kukuza ushiriki wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi;
iii. Kuratibu uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo na za kati;
iv. Kuongeza ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji;
v. Kutekeleza Mkakati wa Kisekta wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NMSFEE)na Mwongozo wake;
vi. Kuratibu Mpango wa Uwezeshaji wa Uanzishaji wa Viwanda vya Kuchakata Mazao ya Kilimo kwa kushirikisha taasisi za umma;
vii. Kuhamasisha Wananchi kuanzisha na kujiunga na vikundi vya uzalishaji mali, vyama vya kuweka akiba na kukopa (SACCOS), benki za jamiii vijijini (VICOBA) na vikundi vingine vya kiuchumi;
viii. Kutoa elimu kwa wananchi kufahamu fursa zilizopo katika mifuko na program za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
ix. Kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananachi Kiuchumi yamwaka 2004;
x. Kuratibu upatikanaji wa elimu ya Biashara na ujasiriamali kwa vijana, vyama vya ushirika na vikundi vya kiuchumi;
xi. Kuratibu mipango ya ujengaji wa uwezo miongoni mwa watanzania ili kuwaongezea ujuzi na maarifa ya kibiashara na uzalishaji;
xii. Kuimarisha Mifumo ya t aasisi na uwezo wa kuratibu na kufuatilia shughuli zote za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
xiii. Kuendeleza Mitaa ya Viwanda ya SIDO kwa kujenga majengo mapya ya viwanda katika Mikoa ya Kigoma,

Dodoma na Simiyu na Kukarabati majengo na miundombinu

xiv. Kukamilisha Mfumo Unganishi wa TEHAMA wa shirika la SIDO katika mikoa ya Pwani, Simiyu, Katavi, Songwe na Manyara;

xv. Kuhawilisha teknolojia kwa kuimarisha vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) vya SIDO;

xvi. Kutunisha Mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi (NEDF);

xvii. Kutangaza Shirika na Bidhaa za viwanda vidogo;

xviii. Kuongeza wigo wa huduma za SIDO kwa Wajasiriamali kwa kutoa mafunzo ya biashara na ufundi pamoja na ushauri kwa kutumia Tehama; na

xix. Kuimarisha utendaji kazi wa Shirika kwa kuongeza vitendea kazi hususan magari, kompyuta, vifaa vya mafunzo na samani.

**6.3. Maendeleo ya Viwanda**

197. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka wa 2023/2024 Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuendeleza Viwanda: -

i. Kukamilisha Sera, Mikakati na Miongozo ya kuendeleza sekta ya Viwanda;

ii. Kuboresha na kuongeza ustawi na tija ya viwanda nchini;

iii. Kuwa na takwimu, tathmini na taarifa zitakazowezesha kuendeleza sekta ya Viwanda;

iv. Kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vipya na kongani za viwanda;

v. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati na kielelezo;

vi. Kufanya majadiliano na mwekezaji ili kusaini Mkataba wa ubia Pamoja na kulipa leseni za uchimbaji wa Makaa ya Mawe Katewaka;

vii. Kufanya utafiti wa kina wa kijiolojia (Geological study) na Kulipia leseni za uchimbaji katika Mradi wa Makaa ya Mawe Muhukuru;
viii. Kuendeleza kiwanda cha KMTC katika Mkoa wa Kilimanjaro;
ix. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya msingi katika Kongani ya Viwanda – TAMCO;
x. Kuendeleza Kiwanda cha TBPL na kuendelea kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa;
xi. Kukamilisha majadiliano na mwekezaji na kusaini mkataba wa ubia (JVA Agreement) na kulipia leseni za uchimbaji - Maganga Matitu;
xii. Kutafuta mwekezaji na Kufanya ukarabati wa majengo katika kiwanda cha Mang’ula;
xiii. Kufanya maandalizi ya awali kwa mradi wa mafuta ya kula (preliminary preparation for establishment of edible oil);
xiv. Kuendelea kufanya ukarabati wa majengo ya Nyanza Glass ili kuvutia wawekezaji wa viwanda;
xv. Kuendelea kuimarisha Idara ya Uhandisi ya TIRDO kwa kuongeza wataalam na vifaa;
xvi. Kuendelea na ukamilishaji wa maabara ya ngozi;
xvii. Kuendelea kufanya utafiti katika kanda saba (7) nchini ili kubaini fursa za uwekezaji na maeneo yenye viwanda na rasilimali zilizopo (Industrial Mapping);
xviii. Kuendelea na ukamilishaji wa Jengo la Utawala la Shirika la TIRDO;
xix. Kuendelea na kukamilisha mchakato wa ithibati (Accreditation) na kuboresha Maabara ya mazingira, kemia, makaa ya mawe, mafuta na gesi;
xx. Kuendelea kufanya tafiti na kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora;
xxi. Kufanya mapitio ya Sheria ya TIRDO Na. 5 ya mwaka 1979;
xxii. Kuendeleza Utafiti na Uendelezaji wa Teknolojia;
xxiii. Kuendeleza Mafunzo na Kuhawilisha zana za kilimo;

xxiv. Kutengeneza mashine za kubangua korosho zitakazopelekwa wilayani Mtwara;

xxv. Kujenga uwezo wa Rasilimali Watu kwenye Kada ya utafiti na wafanyakazi wengine wasio watafiti;

xxvi. Kujenga ufahamu kwa wadau kuhusu shughuli za CAMARTEC;

xxvii. Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na kufanya Ukaguzi wa Miradi;

xxviii. Kubuni na kuunda chasili cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo (Korosho) ili kuongeza thamani na kuendeleza teknolojia ya mtambo wa kuchakata chikichi ili kuongeza thamani;

xxix. Kubuni na kuunda teknolojia ya kuhifadhi maziwa wakati wa kukusanya na kusafirisha ili yasiharibike mapema (kwa kiwango cha mjasiriamali mdogo, wa kati na mkubwa) katika kukuza Sekta ya viwanda na kuongeza ujuzi na ajira;

xxx. Kuendeleza na kuhawilisha teknonolojia ya mitambo ya kuzalisha mafuta ya alizeti na mtambo mdogo wa kuzalisha sukari (mini-sugar plants) kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo;

xxxi. Kubuni na kuunda teknolojia ya kutengeneza matofali ya kuzuia joto kali (refractory bricks) kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa;

xxxii. Kubuni na kuunda mtambo wa kuteketeza taka ngumu za hospitali mahususi kwa kuchomea damu isiyofaa na dawa zilizoharibika na kupitwa na muda (incinerating carcass from livestock/cattle abattoir, biomedical waste blood and expired drugs) katika sekta ya afya.

xxxiii. Kusanifu na kuendeleza utengenezaji wa vifaa tiba vya hospitali kwa awamu ya III (*Autoclave and Laundry machines*);

xxxiv. Kutembelea, kukagua na kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo (M&E);

xxxv. Kujitangaza ili kujenga uelewa kwa umma kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi ya TEMDO kwa kushiriki kwenye maonesho ya teknolojia/biashara pamoja na

kufanya ziara za kihandisi kwenye viwanda hapa Nchini ili kubaini na kutatua changamoto zao;

xxxvi. Kuendelea na uboreshaji wa miundombinu ya karakana, ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi ya TEMDO ;

xxxvii. Kuboresha Karakana kwa kusimika mashine na vifaa vya kisasa (*Heavy duty 6-axes CNC Machines*) ili kuzalisha teknolojia zenye ubora;

xxxviii. Ujenzi wa karakana ya kisasa ya kutengeneza vifaa tiba pamoja na ghala la kuhifadhia vifaa tiba; na

xxxix. Kujenga uwezo wa Taasisi ya TEMDO kwa kuwapatia wafanyakazi mafunzo mbalimbali kuhusu teknolojia mpya.

**6.4. Mtangamano wa Biashara**

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuendeleza Mtangamano wa Biashara: -

i. Kuendelea kuratibu majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na kuvutia uwekezaji nchini;

ii. Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika kwa Nchi za Bara la Afrika (African Continental Free Trade Area – AfCFTA);

iii. Kuratibu uanzishaji wa Eneo Huru la Biashara la Utatu linalojumuisha Kanda za COMESA, EAC na SADC;

iv. Kukamilisha utungaji wa Sheria ya Ahueni ya Athari za Biashara; na

v. Kukamilisha Mapitio na Kuanza Utekelezaji wa Sera Mpya ya Taifa ya Biashara.

**6.5. Maendeleo ya Biashara**

199. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2023/2024,

Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuendeleza Biashara: -

i. Kusimamia, kuratibu na kuboresha mazingira wezeshi ya kufanya biashara nchini;
ii. Kuwaunganisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara na masoko ya ndani na nje ya nchi;
iii. Kuhamasisha na kurahisisha biashara mipakani;
iv. Kuimarisha na kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko;
v. Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu upatikanaji wa masoko ya mazao na bidhaa;
vi. Kupitia Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo ya mwaka 2008;
vii. Kutayarisha viwango 640 vya kitaifa katika sekta/nyanja mbalimbali;
viii. Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 800 kutoka katika sekta mbalimbali;
ix. Kusajili majengo 12,000 ya maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi (food and cosmetic premises);
x. Kusajili bidhaa 2,000 za chakula na vipodozi (food and cosmetic products);
xi. Kuendelea na na utafiti wa utengenezaji vinasaba ambavyo vitatumika kwenye mafuta ya petroli, diseli na mafuta ya taa;
xii. Kukagua na kutoa vibali 120,000 kwa bidhaa zitokazo nje ya nchi ambapo kati ya hizo, vibali 40,000 ni kwa bidhaa zitakazokaguliwa nje ya nchi (PVoC) na vibali 80,000 ni kwa bidhaa zitakazokaguliwa nchini (Destination Inspection);
xiii. Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 46,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;
xiv. Kutoa mafunzo na semina kuhusu viwango na udhibiti ubora kwa wadau 1,400;

xv. Kuthibisha kampuni 14 chini ya mifumo ya ubora na uongozi (management systems);
xvi. Kupima sampuli 38,000 za bidhaa mbalimbali;
xvii. Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 11,000;
xviii. Kuweka kinasaba katika lita 4,000,000,000 za mafuta ya petrol, dizeli na mafuta ya taa;
xix. Kuendelea na ujenzi wa Viwango House Dodoma;
xx. Ujenzi wa maabara na ofisi katika kanda ya Ziwa (Mwanza);
xxi. Kusajili Kampuni 15,000, Majina ya Biashara 28,000, Alama za Biashara na Huduma 4,200, Hataza 40 na vyeti vya Viwanda 44;
xxii. Kutoa leseni za Biashara kundi ‘A’ 14,000 na za Viwanda 210;
xxiii. Kuendelea kutoa Elimu kwa Umma juu ya umuhimu wa kufanya sajili mbalimbali za kibiashara zinazofanywa na Wakala;
xxiv. Kufanya kaguzi elimishi 18 za leseni za Biashara kundi ‘A’ na Viwanda;
xxv. Kuendelea kuboresha na kuimarisha mifumo na miundo mbinu ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma;
xxvi. Kukamilisha mapitio ya sheria za usajili na leseni;
xxvii. Kuboresha mazingira ya kazi ikiwa ni pamoja kuongeza idadi ya Watumishi, kutoa Mafunzo kwa Watumishi na kuongeza vitendea kazi;
xxviii. Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa stakabadhi za ghala kwa wadau;
xxix. Kutoa elimu na kuhamasisha Matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za ghala kwa wadau;
xxx. Kuthaminisha stakabadhi (Monetization of Warehouse Receipt) za ghala;
xxxi. Kuainisha waongeza thamani wa mazao na kuwaunganisha na matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za ghala;

xxxii. Kuainisha na kusajili Mameneja Dhamana kwa kushirikiana na taasisi za fedha nchini;
xxxiii. Kuthaminisha ghala zilizosajiliwa na Bodi ya Usimamizi wa stakabadhi za ghala (International Certification) katika ithibati mbalimbali;
xxxiv. Kuendelea na utambuzi wa ghala pamoja na usajili wake kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA);
xxxv. Kutangaza Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kupitia maonesho ya Nanenane, Wiki ya Ushirika na Siku ya Stakabadhi za Ghala (Ghala Day) pamoja na mikutano mbalimbali ya wadau;
xxxvi. Kusimamia na kuimarisha mifumo ya ufanyaji Biashara;
xxxvii. Kuimarisha uwezo wa Taasisi kujiendesha kiufanisi;
xxxviii. Kusimamia, kuhakiki na kukagua vipimo vyote vitumikavyo na viingiavyo nchini;
xxxix. Kufanya ukaguzi wa bidhaa kwenye maeneo ya mipakani, bandarini na viwandani;
xl. Kununua vitendea kazi vya taasisi ya WMA ikiwemo vitendea kazi vya kitaalam na magari Matatu (3);
xli. Kuongeza idadi ya watumishi ikiwemo Maafisa Vipimo 20, Maafisa Vipimo wasaidizi 10;
xlii. Kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi sahihi ya vipimo;
xliii. Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu ya Wakala wa Vipimo Mkoa wa Dodoma;
xliv. Kuboresha hali ya ushindani katika soko;
xlv. Kumlinda mlaji kutokana na vitendo hadaifu na kandamizi katika soko;
xlvi. Kuongeza mapambano dhidi ya bidhaa bandia katika soko;
xlvii. Kuongeza ufanisi katika kutoa huduma;
xlviii. Kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri ya rufaa 70 yanayowasilishwa katika Baraza;
xlix. Kuimarisha uwezo wa kutekeleza majukumu ya Baraza;
l. Kufanya utafiti wa kisheria na kiuchumi kuhusu ushindani; na

li. Kuongeza uelewa kwa Wadau na Jamii kuhusu shughuli za Baraza na haki katika ushindani wa Soko.

### 6.6. Maboresho ya Mazingira ya Biashara

200. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2023/2024, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo katika kuboresha Mazingira ya Biashara:-

i. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara nchini;
ii. Kuanzisha muundo wa ufuatiliaji na tathmini wenye ufanisi katika kukuza biashara;
iii. Kuhamasisha na kuratibu majadiliano ya kisekta yanayopelekea maboresho ya mazingira ya biashara; na
iv. Kuhakikisha majukumu ya mamlaka za udhibiti yanayoingiliana yanaondolewa na yanayofanana yanaunganishwa.

## 7. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024

### 7.1. Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2023/2024

201. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/2024, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaomba kutengewa jumla ya **shilingi 119,017,998,000** katika Fungu 44. Kati ya fedha hizo, **shilingi 75,451,494,000** ni matumizi ya kawaida, ambapo **shilingi 63,086,267,000** ni mishahara na **shilingi 12,365,227,000** ni matumizi mengineyo. Aidha, **shilingi 43,566,504,000** zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambapo **shilingi 30,346,819,000** ni fedha za ndani na **shilingi 13,219,685,000** ni fedha za nje.

## 8. HITIMISHO

202. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru tena Watanzania wote kwa kuendelea

kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza Sekta ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Tutaendeleza jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Tunahitaji kila Mtanzania popote alipo kutimiza wajibu wake, kujituma, kubadilisha mtizamo na kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea jitihada na kuendeleza uwekezaji, viwanda na biashara. Inawezekana, tutimize wajibu wetu.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana katika Tovuti ya Wizara www.mit.go.tz.

204. ***Mheshimiwa Spika,*** Naomba kutoa hoja.

## VIAMBATISHO

***Jedwali Na. 1**: **Biashara ya Bidhaa kati ya Tanzania na Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2013-2022 (Dola za Marekani "000,000")***

| Mwaka | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa zilizouzwa | 419.1 | 598.1 | 1,062.4 | 437.7 | 349.6 | 444.3 | 674.4 | 807.9 | 1,161.2 |
| Bidhaa zilizoagizwa | 394.7 | 706.4 | 322.8 | 298.9 | 220.4 | 302.8 | 329.2 | 324.3 | 562.8 |
| **Jumla** | **813.8** | **1,304.5** | **1,385.2** | **736.6** | **570** | **747.1** | **1003.6** | **1132.2** | **1684.6** |

***Chanzo:*** *Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*

***Jedwali Na.2: Biashara kati ya Tanzania na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kwa Mwaka 2013-2022 (Dola za Marekani "000,000")***

| Mwaka | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa zilizouzwa | 1,243.55 | 1,235.9 | 1,357.7 | 1,017.9 | 877.8 | 993.6 | 1,350.9 | 1,458.3 | 1,303.4 | 1,802.2 |
| Bidhaa zilizoagizwa | 835.9 | 773 | 771.2 | 612.4 | 1,7781.4 | 604.2 | 594.0 | 492.4 | 653.9 | 551.3 |
| **Jumla** | **2079.45** | **2008.9** | **2128.9** | **1630.3** | **18659.2** | **1,597.8** | **1,944.9** | **1,950.7** | **1,544** | **2,353.5** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

*Jedwali Na. 3: Biashara kati ya Tanzania na Jumuiya ya Ulaya kwa Mwaka 2013-2022 (Dola za Marekani "000,000")*

| Mwaka | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa zilizouzwa | 898.4 | 791.7 | 708.7 | 236.5 | 441.4 | 657.3 | 725.9 | 1,475.9 | 1,346.1 | 955.6 |
| Bidhaa zilizoagizwa | 2,759.4 | 2,895 | 1,159.8 | 557.7 | 936.1 | 982.4 | 1,069.9 | 1,072.0 | 1,530.4 | 1,720.4 |
| **Jumla** | **3,657.8** | **3,686.7** | **1,868.5** | **794.2** | **1,377.5** | **1,639.70** | **1,795.80** | **2,547.90** | **1,860.80** | **2,676** |

**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**Jedwali Na. 4**: *Mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia Mpango wa AGOA (AGOA/GSP) kwa Dola za Kimarekani Milioni*

| Mwaka | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2021/22 Badiliko % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa zilizouzwa** | 18.28 | 28.6 | 37.48 | 40.85 | 42.83 | 55.32 | 40.3 | 33.04 | 74.77 | 126.3 |

Chanzo: US Department of Commerce (https://agoa.info/profiles/tanzania.html)




**Eneo la Uwekezaji wa Kongani ya Viwanda Kwala Kibaha Mkoa wa Pwani**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iafikiwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsante sana. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri aje awasilishe Taarifa ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Mheshimiwa Mariam.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji

wa majukumu ya Wizara pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 44 kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6(1)(a) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inatambua uchambuzi huo.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi masharti ya Kanuni 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, taarifa inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini. Sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na hoja ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Masuala yanayochambuliwa ni taarifa za utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida na upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayoitaka Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuanzia tarehe 17 hadi 18 Machi, 2023. Ziara hii ililenga kukagua Miradi iliyotengewa fedha chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Maeneo na Miradi iliyokaguliwa. Katika ziara hii Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo:-

a) Mradi wa Jengo la Utawala la *TIRDO* ulioko Dar es Salaam ambao unalenga kuwezesha uanzishaji wa Kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashari wa Teknolojia na Viatamizi;

b) Mradi wa Kuimarisha Idara ya Uhandisi *TIRDO* ambao unalenga kununua vifaa vya upimaji ubora bila kuharibu *(non-ddestructive testing)* wa mabomba ya mafuta na gesi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa; na

c) Mradi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu Kibaha *(Bio avicides Products)* ambao umelenga kupambana na malaria nchini.

Mheshimiwa Spika, yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi. Uchambuzi wa Kamati katika Miradi tajwa ulibaini mambo ya msingi kuhusu mafanikio, changamoto pamoja na hatua za kuchukuliwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo. Mradi wa kwanza, Mradi wa *TIRDO* ulitengewa shilingi bilioni 1.9 ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2023, shilingi milioni 406 sawa na asilimia 21 zilipokelewa kutoka Hazina. Kiasi hiki ni kidogo na kulingana na muda uliobaki, ni vigumu kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vilevile, athari zinazoweza kuambatana na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Hazina, ni kuongezeka kwa gharama za mradi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ucheleweshwaji wa fedha za miradi ya maendeleo, Kamati pia imebaini mapungufu ya kandarasi ambapo mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Jengo la Utawala la *TIRDO*, ameshindwa kutekeleza mradi kwa wakati bila kutoa maelekezo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yoyote duniani yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa taasisi imara za utafiti. Hivyo, ni muhimu Serikali kulipa kipaumbele Shirika la Utafiti kwa kutenga fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati ili jengo hili liweze kukamilika na kuwezesha kazi ya utafiti kufanyika kikamilifu na kuhamasisha maendeleo ya viwanda vyetu. Aidha, Serikali ihakikishe inatumia wakandarasi ambao wanaendana na kasi ya utekelezaji wa miradi ili kuepusha ucheleweshaji wa miradi ambao unaongeza gharama.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Viuadudu Kibaha ulitengewa shilingi milioni 350, lakini hadi kufikia mwezi Februari, 2023 hakukuwa na fedha yoyote iliyotolewa kutoka Hazina kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo usioridhisha, unakwamisha utekelezaji wa mradi huu kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutopatiwa fedha za kutosha na kwa wakati, Kamati imebaini kuwa kiwanda hiki hakijapewa umuhimu wa kutosha kwani bidhaa zinazozalishwa ambazo kimsingi zinalenga kutokomeza ugonjwa hatari wa malaria nchini hazina soko la uhakika, ambapo hali hii imefanya kiwanda kujiendesha kwa hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali ikisaidie kiwanda kupata soko la uhakika la bidhaa zake ili kufikia lengo la kuanzishwa kwake. Vilevile Serikali iielekeze TAMISEMI kupitia halmashari zote pamoja na Wizara ya Afya kutenga fedha za kununua dawa hizi badala ya kununua kwenye taasisi nyingine. Aidha, tafiti za kutosha zinazohusu mpango wa kupanua wigo wa kiwanda kwa kuzalisha dawa za kilimo zitakazosaidia kutokomeza wadudu wanaoathiri mazao na kuwasaidia wakulima kupata

mavuno chanya, zifanyike ili kuepuka hasara zinazoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Watumishi. Serikali haijaweka uzito katika kuendeleza wataalamu wake na hivyo kukosa mwendelezo. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri na kuhakikisha mpango wa urithishaji wa ujuzi/utaalam *(Succession Plan*) unaimarishwa ili kuepuka kupoteza aina za ujuzi/utaalam pindi wataalam wanapomaliza muda wa utumishi.

Mheshimiwa Spika, viwanda kukosa ithibati. Ithibati ni mojawapo ya njia za kusaidia bidhaa kutambulika, kuaminika na kuingiza fedha za kigeni nchini. Katika ukaguzi, Kamati imebaini kuwa, Kiwanda cha Viuadudu Kibaha hakina ithibati na hivyo kusababisha bidhaa zinazozalishwa kutouzika nje ya nchi licha ya kuwa zina ubora. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha viwanda vyote vinavyozalisha na ambavyo bidhaa zake zimethibitika kuwa na ubora unaofaa vinapata ithibati ili viweze kutambulika Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliidhinishiwa shilingi bilioni 99.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 68.3 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 30.8 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 53.2 sawa na asilimia 53.7. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 42.5 ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na 62.2%, na shilingi bilioni 10.7 ni fedha za matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 35.2. Mchanganuo huu wa Fungu 44 ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba moja.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji na Bajeti kwa Mwaka 2022/2023. Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa Fedha ikilinganisha bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kipindi cha utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa mtiririko wa fedha kutoka Hazina haukuwa wa kuridhisha kwa sababu hadi kufikia Mwezi Februari, 2023, Wizara ilipokea asilimia 53.7 tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Wizara ilipokea asilimia 35.2 tu ya bajeti yote iliyoidhinishwa. Kutopatikana bajeti kwa wakati kunachangia baadhi ya shughuli kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaliomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha kwa Wizara kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuweza kukamilisha shughuli zilizopangwa kabla ya mwaka wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Spika, fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 30.8 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 30.3 ni fedha za ndani na shilingi milioni 450, ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 10.7 ya Fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 35.2 ya Fedha zilizotengwa. Hadi wakati Kamati inakamilisha uchambuzi, Wizara ilikuwa haijapokea fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo:-

(i) Kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Februari kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni asilimia 35.2 tu ya fedha zilizotengwa. Kiasi hiki ni chini ya asilimia 66.6 ambayo ilitakiwa kuwa imepatikana kwa kipindi hicho; na

(ii) Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha hauridhishi na hautoi mwelekeo mzuri wa ukamilishaji wa miradi iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, Wizara hii iongezewe fedha za Miradi ya Maendeleo za ndani ili iweze kutekeleza shughuli zake na kuhakikisha kuwa mchango wa sekta ya biashara kwenye pato la Taifa unaendelea kuimarika na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi na wananchi kwa ujumla. Aidha, ili kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni muhimu kwa Serikali kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kubuni mikakati zaidi ili kujenga uchumi wa viwanda jumuishi, fungamanishi, shindani na vinavyotumia malighafi za ndani, teknolojia ya kisasa na vinavyokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati; Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Fungu 44 wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara hii ilipewa maagizo 10 ambapo Taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri. Aidha, yapo maagizo ambayo utekelezaji wake bado

unaendelea. Mfano mmojawapo ni suala la ulipaji fidia kwa wananchi katika maeneo ya Miradi ya Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, taarifa za utekelezaji zilionesha kuwa, Serikali imetenga shilingi bilioni 15.4 kwa ajili ya kuwalipa wananchi 1,143 na kwamba kiasi hicho cha fedha kinatarajiwa kulipwa mwezi Aprili, 2023. Kamati inaishauri Serikali kulipa suala hili kipaumbele ili wananchi walipwe fidia mapema kuepuka nyongeza ya gharama za fidia itokanayo na kuchelewesha malipo hayo. Aidha, wananchi waelimishwe kuhusu malipo haya ili watumie pesa zao vizuri pindi watakapolipwa.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara – Fungu 44, inaomba kutengewa jumla ya shilingi bilioni 117.8. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 74.3 sawa na asilimia 63 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 43.6 sawa na asilimia 37 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika fedha za maendeleo, shilingi bilioni 30.3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 13.2 ni fedha za nje. Ulinganisho wa bajeti kwa mwaka 2022/2023 na 2023/2024 unafafanuliwa katika kielelezo namba nne.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, makadirio ya bajeti yameongezeka kwa shilingi bilioni 18.7 sawa na asilimia 19 ukilinganisha na Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Ongezeko katika fedha za matumizi ya kawaida la shilingi bilioni 5.9 sawa na asilimia tisa ya bajeti iliyotengwa limetokana na ajira mpya pamoja na kupanda madaraja kwa watumishi. Fedha za maendeleo za nje zimeongezeka shilingi bilioni 12.7 sawa na asilimia 2.83 kutokana na kuongezeka kwa shughuli ambazo hazikuwepo katika mpango kazi kwa mwaka 2022/2023. Aidha, pamoja na ongezeko hili kuwa kubwa, bado

Kamati inaona utekelezaji wake utakuwa mgumu hasa kwa uzoefu wa mwaka unaoisha ambao fedha zilizotengwa hazikutoka kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya viwanda yatapatikana endapo utafiti wa mazao, masoko na uwekezaji vitafanyika kwa ufasaha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuongeza ufanisi na kupata tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(a) Upatikanaji wa Fedha na Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara; pamoja na Serikali kuendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda bado Kamati inaona kuwa kiasi hiki ni kidogo kuweza kutekeleza shughuli zake kikamilifu. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Wizara hii na kuhakikisha kuwa inapelekwa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

(b) Ulipaji wa Fidia kwa Wananchi Wanaopisha Miradi ya Kimkakati Liganga na Mchuchuma; zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma limechukua muda mrefu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuanza kutenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi hao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) kuhakikisha wananchi wote ambao maeneo yao yanatwaliwa wanalipwa fidia haraka kulingana na thamani ya ardhi yao;

(ii) Elimu itolewe kwa wananchi wote kuhusu matumizi sahihi ya fedha watakazolipwa;

(iii) Ulipaji wa fidia kwa wananchi uende sambamba na mpango mkakati wa kuanza utekelezaji wa Miradi hii ili kufikia lengo lililokusudiwa; na

(iv) Serikali ihakikishe kuwa mwekezaji katika mradi huu anarudisha fedha za fidia zinazolipwa na Serikali wakati wa kuanza utekelezaji wa mradi kama mkataba wa makubaliano unavyosema.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Magadi Soda – Engaruka; Mradi huu umeainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026. Muda uliokadiriwa kukamilika mradi huu ni mwaka 2026 ambao unaelekea ukingoni lakini bado Serikali ipo katika hatua ya kutafuta mwekezaji, jambo ambalo linaweza kuchelewesha ukamilikaji wa mradi huu kwa wakati. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ilipe fidia kwa wananchi 599 waliofanyiwa uhakiki ambao maeneo yao yanatwaliwa;

(ii) Zoezi la kutafuta mwekezaji atakayeshirikiana na Serikali lifanyike kwa haraka ili mgodi huu uanze kazi ya kuzalisha magadi soda yatakayotumika kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwemo karatasi, vioo, sabuni na kadhalika ili kukuza uchumi wa nchi; na

(iii) Serikali iongeze wigo wa wateja wa bidhaa hizo kwa kutafuta masoko zaidi ndani na nje ya nchi.

(c) Utekelezaji wa Uchumi wa Bluu; ipo changamoto ya kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa bluu ambapo Tanzania haijaweka mkazo katika kukuza mazao yanayotokana na bahari, mito, maziwa na mabwawa. Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:

(i) Kujenga viwanda vikubwa vya kuchakata samaki na vya uzalishaji wa chakula cha samaki hapa nchini; na

(ii) Kuweka mikakati madhubuti ya kuuza samaki nje ya nchi na kudhibiti samaki kutoka nje ambao wanapatikana nchini wasiingie nchini kwetu.

(d) Upatikanaji wa Masoko kwa Bidhaa Zinazozalishwa Nchini; ipo changamoto ya bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda vyetu vya ndani kukosa soko la uhakika na hivyo kujiendesha kwa hasara. Mfano, Kiwanda cha Viuadudu Kibaha ambacho kinazalisha dawa za kuua viluilui vya mazalia ya mbu. Hali hii imeshusha tija ya uzalishaji na kuingiza hasara kwa kuwa viwanda vimeshindwa kujiendesha na kuitwisha Serikali mzigo wa kuviendesha. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) itafute muafaka wa kiwanda hiki kwa kuhakikisha kinapatiwa soko la uhakika la bidhaa zake ili kutokomeza kabisa mazalia ya mbu yanayoleta ugonjwa hatari wa malaria;

(ii) Kwa kushirikiana na *TANTRADE* ihakikishe inatafuta masoko ya uhakika kwa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na viwanda vyetu nchini;

(iii) Serikali iweke mkakati wa kuwatumia Mabalozi wetu katika nchi mbalimbali kutangaza na kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini; na

(iv) Serikali itafute soko la uhakika kwa mazao ya kimkakati nje ya nchi ili kuinua uchumi wa wakulima na kuongeza fedha za kigeni.

(e) Mheshimiwa Spika, leseni za biashara; uwepo wa changamoto ya wafanyabiashara kutakiwa kulipa kodi ya mauzo kabla ya kuanza biashara badala ya kulipa kodi hiyo miezi sita baada ya kuanza biashara, kumeleta usumbufu kwa walipa kodi hao na kuwakatisha tamaa hata wengine kuanzisha biashara. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) kuhakikisha vyombo husika vinatoza kodi kwa mujibu wa sheria;

(ii) Kupunguza urasimu katika mchakato wa kuanzinisha biashara ili kuvutia wafanyabiashara wengi zaidi;

(iii) Elimu ya mlipakodi itolewe mara kwa mara kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima; na

(iv) Wizara ijiwekee mikakati ya kukutana na wafanyabiashara kwa madaraja yao ili kusikiliza changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi.

(f) Ufufuaji wa viwanda vilivyobinafsishwa; viwanda ambavyo vilibinafsishwa lakini mpaka sasa havifanyi kazi iliyokusudiwa, vinakiuka lengo la ubinafsishwaji wake na hivyo kulitia Taifa hasara. Kamati inaishauri Serikali kuvirudisha viwanda vyote vilivyobinafsishwa ambavyo havijaendelezwa na

kuvitangaza upya kwa wamiliki wengine ili viweze kuzalisha na kuongeza tija, ajira na mapato.

(g) Sera, Sheria na Kanuni Zilizopitwa na Wakati; uwepo wa sera, sheria na kanuni ambazo zimepitwa na wakati, unaweza kupunguza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. Mfano wa sera hizo ni Sera ya Taifa ya Uhamasishaji Uwekezaji ya Mwaka 1996, Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya Mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003 na nyinginezo ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kufanya mapitio ya Sera, mikakati na sheria za kisekta ili ziweze kuendana na mahitaji ya sasa katika kuchochea kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. Aidha, uandaaji wa Sera mpya katika masuala mbalimbali yahusuyo sekta hii uwekewe mkazo ili kufikia malengo.

(h) Uingizaji wa Bidhaa za Chakula Nchini; suala la uingizaji wa bidhaa za chakula nchini limepata sura tofauti kutokana na hali ilivyo duniani ambapo baadhi ya wafanyabiashara wamekosa uaminifu na kutengeneza vyakula visivyo salama. Mfano, tumeona kwenye mitandao mchele usio salama (wa *plastic*) ukitengenezwa na kuonekana kama mchele halisi. Hali hii inatishia usalama wa wananchi wetu. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) *TBS* iongezewe uwezo kifedha, rasilimali watu na vitendea kazi ili idhibiti bidhaa zisizo na ubora zinazoingia nchini kwa wingi na kuleta athari kwa watumiaji;

(ii) Kuziwezesha sekta za uzalishaji wa bidhaa za viwandani na mazao yatokanayo na kilimo nchini kuzalisha kwa wingi ili kujitosheleza kwa chakula na kupunguza uingizaji bidhaa hizo; na

(iii) Kuhakikisha bidhaa zote za chakula zinazoingizwa nchini zina ubora stahiki na usalama kwa walaji.

(i) Changamoto ya Rumbesa; upakiaji wa mazao na bidhaa kupita ujazo au uzito uliowekwa kisheria katika magunia (rumbesa), umeleta changamoto nyingi ikiwemo kumnyonya mzalishaji na mkulima pamoja na kuikosesha Serikali mapato. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

(i) Iweke mkakati wa kusimamia utekelezaji wa sheria hii ili kuondoa tofauti zilizopo kati ya wakulima na wafanyabiashara ili kila upande uweze kunufaika; na

(ii) Itoe elimu kwa wakulima na wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi vinavyokubalika kisheria sambamba na kusimamia marufuku hiyo ili kuondoa usumbufu.

(j) Mfumo wa Stakabadhi Ghalani; ipo changamoto ya wakulima kulalamika malipo kuchelewa kulipwa na vilevile mazao kushuka thamani. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha malipo yanafanyika kwa haraka. Wakulima wapewe elimu kuhusu umuhimu wa kuweka mazao yao kwenye madaraja mazuri ili wapate bei nzuri. Maghala yatumike kuhifadhi mazao vizuri ili yasinyauke na kupunguza gharama. Aidha, Serikali iendelee kuboresha mfumo huu na kuhakikisha maghala yanakatiwa bima ya kuwalinda wakulima.

(k) Uimarishaji wa Taasisi za Utafiti. Hatuwezi kufikia lengo la kuwa na uchumi wa viwanda ikiwa hatutawekeza kwenye kufanya tafiti zitakazoleta tija katika viwanda vyetu nchini. Kamati inaishauri Serikali kulipa kipaumbele Shirika la utafiti na Maendeleo ya Viwanda *(TIRDO)* kwa kuitengea fedha za kutosha ili kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala na Wenyeviti wote wa Bunge kwa weledi na umahiri wao katika kukusaidia kuongoza vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia kwa kipekee kabisa tumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati Mheshimiwa Kihenzile na pia Bunge limemwamini zaidi na kuwa Mwenyekiti wa Bunge na unashirikiana nao kwenye kuongoza Bunge.

Mheshimiwa Spika, orodha yao ya Wajumbe ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kumshukuru mwanamke shupavu, jasiri na mchapakazi wa kweli, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge wa Kondoa na Waziri wa Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe,

Naibu Waziri; Daktari Hashil T. Abdallah, Katibu Mkuu; Neema Magereli, Naibu Katibu Mkuu; na Watumishi wote pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Joyce Mwihambi, *(ndc),* Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Michael Chikokoto *(ndc)* pamoja na watendaji wote wa Bunge kwa msaada wanaotoa kwa Kamati zetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Makatibu wa Kamati, Ndugu Elieka Saanya, Ndugu Thuwaiba Jumbe, Ndugu Asia Msangi pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hoja; baada ya maelezo hayo, sasa naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fungu 44 - Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA (FUNGU 44) KWA MWAKA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU 44 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 Maelezo ya Jumla

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Fungu 44, naomba kutoa taarifa ya Kamati inayofafanua masuala **manne** yafuatayo: -

a) Sehemu ya **Kwanza** inayotoa maelezo ya jumla kuonesha msingi, muundo wa Taarifa pamoja na namna kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya **Pili** inayoripoti matokeo ya uchambuzi na tathmini kwa kuchanganua utekelezaji wa Miradi ya

Maendeleo, Utekelezaji wa Malengo ya Mpango wa Wizara hii, Upatikanaji wa Fedha, Makadirio ya Mapato na Matumizi na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

c) Sehemu ya **Tatu** inayoripoti Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na Uchambuzi; na

d) Sehemu ya **Nne** na ya mwisho ni hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6 (1)(a) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inatambua uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii.

### *1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa*

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inahusu Fungu 44.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyochambuliwa, inagusa maeneo makuu yafuatayo: -

i) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

ii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara hadi kufikia mwezi Februari, 2023;

iii) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yaliyobainishwa hapo juu yanajitokeza katika Taarifa hii. Kwa muktadha huo, naliomba Bunge lako Tukufu lifuatilie kwa kina mtiririko wa Taarifa hii ili kupata msingi wa ushauri unaotolewa na Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 Matokeo ya Uchambuzi na Tathmini

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara baada ya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.

Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na ukusanyaji wa Maduhuli, upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida na upatikanaji wa Fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

#### 2.2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayoitaka Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa

fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuanzia tarehe 17 hadi 18 Machi, 2023. Ziara hii ililenga kukagua Miradi iliyotengewa fedha chini ya Wizara hii.

### 2.2.2 Maeneo na Miradi iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hii Kamati ilitembelea na kukagua Miradi ifuatayo:-

a) Mradi wa Jengo la Utawala la TIRDO ulioko Dar es Salaam ambao unalenga kuwezesha uanzishaji wa Kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashari wa Teknolojia na Viatamizi;

b) Mradi wa Kuimarisha Idara ya Uhandisi TIRDO ambao unalenga kununua vifaa vya upimaji ubora bila kuharibu *(Non Destructive Testing)* wa mabomba ya mafuta na gesi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa; na

c) Mradi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu Kibaha *(Biolavicides Products)* ambao umelenga kupambana na malaria nchini.

### 2.2.3 Malengo ya Ziara katika maeneo yaliyotembelewa

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kutekeleza ratiba ya ziara, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za vituo ilivyovitembelea ambapo ilipata fursa ya kuona shughuli mbalimbali zinazotekelezwa katika Mradi wa Jengo la Utawala TIRDO na Mradi wa Kuimarisha Idara ya Uhandisi TIRDO lililopo Dar es Salaam na Kiwanda cha Viuadudu kilichopo Kibaha Pwani.

**Mheshimiwa Spika,** ziara ililenga kubaini yafuatayo: -

a) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi ya TIRDO na Kiwanda cha Viuadudu Kibaha;

b) Thamani halisi ya fedha zilizotengwa na endapo utekelezaji wa Miradi una tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla;

c) Nini kifanyike kuhakikisha Miradi hii iliyotengewa fedha na Bunge inakamilika kwa muda uliokusudiwa; na

d) Mafanikio na changamoto zilizopo wakati wa kutekeleza Miradi hii.

### 2.2.4 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Miradi tajwa ulibaini mambo ya msingi kuhusu mafanikio, changamoto pamoja na hatua za kuchukuliwa kama ifuatavyo: -

a) **Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo**

i) Mradi wa TIRDO ulitengewa **Shilingi 1,900,000,000** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2023, **Shilingi 406,134,115** sawa na **asilimia 21** zilipokelewa kutoka Hazina. Kiasi hiki ni kidogo na kulingana na muda uliobaki, ni vigumu kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vilevile, athari zinazoweza kuambatana na ucheleweshwaji wa fedha kutoka Hazina, ni kuongezeka kwa gharama za Mradi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ucheleweshaji wa fedha za miradi ya maendeleo, Kamati pia imebaini upungufu katika kandarasi ambapo mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Jengo la Utawala

la TIRDO, ameshindwa kutekeleza mradi kwa wakati bila kutoa maelezo ya kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** maendeleo ya nchi yoyote duniani yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa taasisi imara za utafiti, hivyo, ni muhimu Serikali kulipa kipaumbele Shirika la Utafiti kwa kutenga fedha za kutosha na kuzitoa kwa wakati ili jengo hili liweze kukamilika na kuwezesha kazi ya utafiti kufanyika kikamilifu na kuhamasisha maendeleo ya viwanda vyetu. Aidha, Serikali ihakikishe inatumia wakandarasi ambao wanaendana na kasi ya utekelezaji wa Miradi ili kuepusha ucheleweshaji wa Miradi ambao unaongeza gharama.

ii) Mradi wa Viuadudu Kibaha ulitengewa **shilingi 350,000,000** lakini hadi kufikia mwezi Februari, 2023 hakukuwa na fedha yoyote iliyotolewa kutoka Hazina kwa ajili ya kutekeleza Mradi huu. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo usioridhisha, unakwamisha utekelezaji wa Mradi huu kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kutopatiwa fedha za kutosha na kwa wakati, Kamati imebaini kuwa, Kiwanda hiki hakijapewa umuhimu wa kutosha kwani bidhaa zinazozalishwa ambazo kimsingi zinalenga kutokomeza ugonjwa hatari wa malaria nchini hazina soko la uhakika ambapo hali hii imefanya kiwanda kujiendesha kwa hasara kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali ikisaidie kiwanda kupata soko la uhakika la bidhaa zake ili kufikia lengo la kuanzishwa kwake. Vilevile Serikali iielekeze TAMISEMI kupitia Halmashari zote pamoja na Wizara ya Afya kutenga fedha za kununua dawa hizi badala ya kununua kwenye taasisi nyingine. Aidha, tafiti za kutosha zinazohusu mpango wa kupanua wigo wa

kiwanda kwa kuzalisha dawa za kilimo (*bio-pesticides*) zitakazosaidia kutokomeza wadudu wanaoathiri mazao na kuwasaidia wakulima kupata mavuno chanya, zifanyike ili kuepuka hasara zinazoweza kutokea.

**b) Upungufu wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali haijaweka uzito katika kuendeleza wataalam wake na hivyo kukosa mwendelezo. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuhakikisha mpango wa urithishaji wa ujuzi/utaalam (*Succession Plan*) unaimarishwa ili kuepuka kupoteza aina za ujuzi/utaalam pindi wataalam wanapomaliza muda wa utumishi.

**c) Viwanda kukosa ithibati**

**Mheshimiwa Spika,** ithibati ni mojawapo ya njia za kusaidia bidhaa kutambulika, kuaminika na kuingiza fedha za kigeni nchini. Katika ukaguzi, Kamati imebaini kuwa, Kiwanda cha Viuadudu Kibaha hakina ithibati na hivyo kusababisha bidhaa zinazozalishwa kutouzika nje ya nchi licha ya kuwa zina ubora. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha viwanda vyote vinavyozalisha na ambavyo bidhaa zake zimethibitika kuwa na ubora unaofaa vinapata ithibati ili viweze kutambulika Kitaifa na Kimataifa.

**2.2.5 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara - **Fungu 44** iliidhinishiwa **Shilingi 99,105,506,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 68,308,687,000.00** ni matumizi ya kawaida na **Shilingi 30,796,819,000.00** ni matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 53,185,836,547.87** sawa na **asilimia 53.7**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 42,495,329,297.86** ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na **asilimia 62.2,** na **Shilingi 10,690,507,250.01** ni fedha za matumizi ya maendeleo, sawa na **asilimia 35.2.**


**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo kuhusu Fungu 44 ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo Namba 1.**

**Kielelezo Namba 1: Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa 2022/2023 na kiasi cha fedha zilizopatikana kufikia Mwezi Februari, 2023 na kiasi cha fedha zilizopatikana hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 - Fungu 44**

| **Upatikanaji wa Fedha Fungu 44 Mwaka wa Fedha 2022/2023** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Kiasi Kilichoidhinishwa** | **Kiasi Kilichopokewa Hadi Februari, 2023** | **Asilimia** |
| Mishahara | 59,579,899,000.00 | 36,876,337,146.73 | 61.89 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 8,728,788,000.00 | 5,618,992,151.13 | 64.37 |
| Maendeleo (Ndani) | 30,346,819,000.00 | 10,690,507,250.01 | 35.23 |
| Maendeleo (Nje) | 450,000,000.00 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **99,105,506,000.00** | **53,185,836,547.87** | **53.67** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara*

**Kielelezo Namba 2: Ufafanuzi kuhusu upatikanaji wa fedha kwa asilimia - Fungu 44**




**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara*

**2.2.6 Matokeo ya Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa Fedha ikilinganisha bajeti iliyoidhinishwa na Bunge pamoja na kipindi cha utekelezaji wa bajeti.

Kamati ilibaini kuwa mtiririko wa fedha kutoka Hazina haukuwa wa kuridhisha kwa sababu hadi kufikia Mwezi Februari, 2023 Wizara ilipokea **asilimia 53.7** tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Wizara ilipokea **asilimia 35.2** tu ya Bajeti yote iliyoidhinishwa. Kutopatikana bajeti kwa wakati kunachangia baadhi ya shughuli kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaliomba Bunge kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha kwa Wizara kama

zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kabla mwaka wa fedha kumalizika.

### 2.2.7 Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ilitengewa jumla ya **shilingi 30,796,819,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 30,346,819,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 450,000,000** ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Februari, 2023, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 10,690,507,250.01** ya Fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, sawa na **asilimia 35.2** ya Fedha zilizotengwa. Hadi wakati Kamati inakamilisha uchambuzi, Wizara ilikuwa haijapokea Fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini yafuatayo: -

i) Kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Februari kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni **asilimia 35.2** tu ya fedha zilizotengwa. Kiasi hiki ni chini ya **asilimia 66.6** ambayo ilitakiwa kuwa imepatikana kwa kipindi hicho; na

ii) Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha hauridhishi na hautoi mwelekeo mzuri wa ukamilishaji wa miradi iliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** ni maoni ya Kamati kuwa, Wizara hii iongezewe fedha za Miradi ya Maendeleo za ndani ili iweze kutekeleza shughuli zake na kuhakikisha kuwa mchango wa sekta ya biashara kwenye Pato la Taifa unaendelea kuimarika na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi na wananchi

kwa ujumla. Aidha, ili kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ni muhimu kwa Serikali kuendeleza mafanikio yaliyopatikana na kubuni mikakati zaidi ili kujenga uchumi wa viwanda jumuishi, fungamanishi, shindani na vinavyotumia malighafi za ndani, teknolojia ya kisasa na vinavyokidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

### 2.2.8 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Fungu 44 wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara hii ilipewa maagizo 10 ambapo Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri. Aidha, yapo maagizo ambayo utekelezaji wake bado unaendelea. Mfano mmojawapo ni suala la ulipaji fidia kwa wananchi katika maeneo ya Miradi ya Liganga na Mchuchuma.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji zilionesha kuwa, Serikali imetenga **Shilingi 15,424,364,900** kwa ajili ya kuwalipa wananchi 1,143; na kwamba kiasi hicho cha fedha kinatarajiwa kulipwa mwezi Aprili, 2023. Kamati inaishauri Serikali kulipa suala hili kipaumbele ili wananchi walipwe fidia mapema kuepuka nyongeza ya gharama za fidia itokanayo na kuchelewesha malipo hayo. Aidha, wananchi waelimishwe kuhusu malipo haya ili watumie pesa zao vizuri pindi watakapolipwa.

## 2.3 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.3.1 Uchambuzi wa Malengo/Mpango

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara –Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi pamoja na mambo mengine ulilenga kujihakikishia iwapo Mpango na Makadirio haya umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

### 2.3.2 Mpango wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara - **Fungu 44** inaomba kutengewa jumla ya **Shilingi 117,817,998,000**. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 74,251,494,000** sawa na **asilimia 63** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 43,566,504,000** sawa na **asilimia 37** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Katika fedha za maendeleo, **Shilingi 30,346,819,000** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 13,219,685,000** ni Fedha za Nje.

**Kielelezo Namba 3: Asilimia ya Fedha zilizotengwa 2023/2024**




***Chanzo**: Randama ya Wizara Fungu - 44*

2.4 **Ulinganisho wa Fedha Zilizoombwa kwa Mwaka 2022/2023 na Fedha Zinazooombwa 2023/2024**

**Kielelezo Namba 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

| ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 44 KWA MWAKA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **2022/2023** | **2023/2024** | **ONGEZEKO/ PUNGUFU** | **ONGEZEKO/ PUNGUFU %** |
| Mishahara | 59,579,899,000 | 63,086,267,000 | 3,506,368,000 | 5 |
| OC | 8,728,788,000 | 11,165,227,000 | 2,436,439,000 | 21.4 |
| **Jumla ndogo 1** | **68,308,687,000** | **74,251,494,000** | **5,942,807,000** | **8.7** |
| Maendeleo ndani | 30,346,819,000 | 30,346,819,000 | 0 | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Maendeleo nje | 450,000,000 | 13,219,685,000 | 12,769,685,000 | 2,837.7 |
| **Jumla ndogo 2** | **30,796,819,000** | **43,566,504,000** | **12,769,685,000** | **41.6** |
| **Jumla ya ulinganifu** | **99,105,506,000** | **117,817,998,000** | **18,712,492,000** | **18.9** |

***CHANZO: Randama ya Wizara - Fungu 44***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa: -

**i)** Makadirio ya bajeti yameongezeka kwa **Shilingi 18,712,492,000** sawa na **asilimia 19** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023;

**ii)** Ongezeko katika fedha za matumizi ya kawaida la **shilingi 5,942,807,000** sawa na **asilimia 9** ya bajeti iliyotengwa limetokana na ajira mpya pamoja na kupanda madaraja kwa watumishi;

**iii)** Fedha za maendeleo za ndani hazikuongezeka na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutokana na kukosekana kwa fedha za ndani;

**iv)** Fedha za maendeleo za nje zimeongezeka **Shilingi 12,769,685,000** sawa na **asilimia 2,837.7** kutokana na kuongezeka kwa shughuli ambazo hazikuwepo katika Mpango Kazi kwa Mwaka 2022/2023. Aidha, pamoja na ongezeko hili kuwa kubwa, bado Kamati inaona utekelezaji wake utakuwa mgumu hasa kwa uzoefu wa mwaka unaoisha ambao fedha zilizotengwa hazikutoka kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** maendeleo ya viwanda yatapatikana endapo utafiti wa mazao, masoko na uwekezaji vitafanyika kwa

ufasaha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ili kuongeza ufanisi na kupata tija iliyokusudiwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati inatoa Maoni na Ushauri ufuataao kwa Serikali: -

### a) Upatikanaji wa Fedha na Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

Pamoja na Serikali kuendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda bado Kamati inaona kuwa kiasi hiki ni kidogo kuweza kutekeleza shughuli zake kikamilifu. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza Bajeti ya Wizara hii na kuhakikisha kuwa inapelekwa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### b) Ulipaji wa fidia kwa Wananchi wanaopisha Miradi ya Kimkakati

### i) Liganga na Mchuchuma

Zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma limechukua muda mrefu. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ya kuanza kutenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi hao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

- Kuhakikisha wananchi wote ambao maeneo yao yanatwaliwa wanalipwa fidia haraka kulingana na thamani ya ardhi yao;

- Elimu itolewe kwa wananchi wote kuhusu matumizi sahihi ya fedha watakazolipwa;

- Ulipaji wa fidia kwa wananchi uende sambamba na mpango mkakati wa kuanza utekelezaji wa Miradi hii ili kufikia lengo lililokusudiwa; na

- Serikali ihakikishe kuwa mwekezaji katika mradi huu anarudisha fedha za fidia zinazolipwa na Serikali wakati wa kuanza utekelezaji wa mradi kama mkataba wa makubaliano unavyosema.

**ii) Mradi wa Magadi Soda - Engaruka**

Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka umeainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano *(FYDPIII) 2021/2022 – 2025/2026))*. Muda uliokadiriwa kukamilika mradi huu ni mwaka 2026 ambao unaelekea ukingoni lakini bado Serikali ipo katika hatua ya kutafuta mwekezaji, jambo ambalo linaweza kuchelewesha ukamilikaji wa Mradi huu kwa wakati. Kamati inashauri yafuatayo: -

- Serikali ilipe fidia kwa wananchi 599 waliofanyiwa uhakiki ambao maeneo yao yanatwaliwa;

- Zoezi la kutafuta mwekezaji atakayeshirikiana na Serikali lifanyike kwa haraka ili mgodi huu uanze kazi ya kuzalisha magadi soda yatakayotumika kutengenezea bidhaa

mbalimbali ikiwemo karatasi, vioo, sabuni na kadhalika ili kukuza uchumi wa nchi; na

- Serikali iongeze wigo wa wateja wa bidhaa hizo kwa kutafuta masoko zaidi ndani na nje ya nchi.

**c) Utekelezaji wa Uchumi wa Bluu**

Ipo changamoto ya kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa bluu ambapo Tanzania haijaweka mkazo katika kukuza mazao yanayotokana na bahari, mito, maziwa na mabwawa. Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(i) Kujenga viwanda vikubwa vya kuchakata samaki na vya uzalishaji wa chakula cha samaki hapa nchini; na

(ii) Kuweka mikakati madhubuti ya kuuza samaki nje ya nchi na kudhibiti samaki kutoka nje ambao wanapatikana nchini wasiingie nchini kwetu.

**d) Upatikanaji wa Masoko kwa Bidhaa Zinazozalishwa Nchini**

Ipo changamoto ya bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda vyetu vya ndani kukosa soko la uhakika na hivyo kujiendesha kwa hasara. Mfano, Kiwanda cha Viuadudu Kibaha ambacho kinazalisha dawa za kuua viluilui vya mazalia ya mbu. Hali hii imeshusha tija ya uzalishaji na kuingiza hasara kwa kuwa viwanda vimeshindwa kujiendesha na kuitwisha Serikali mzigo wa kuviendesha.

Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i) Itafute mwafaka wa kiwanda hiki kwa kuhakikisha kinapatiwa soko la uhakika la bidhaa zake ili kutokomeza

kabisa mazalia ya mbu yanayoleta ugonjwa hatari wa malaria;

ii) Kwa kushirikiana na TANTRADE ihakikishe inatafuta masoko ya uhakika kwa bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na viwanda vyetu nchini;

iii) Serikali iweke mkakati wa kuwatumia Mabalozi wetu katika nchi mbalimbali kutangza na kutafuta masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini; na

iv) Serikali itafute soko la uhakika kwa mazao ya kimkakati nje ya nchi ili kuinua uchumi wa wakulima na kuongeza fedha za kigeni.

**e) Leseni za Biashara**

Uwepo wa changamoto ya wafanyabiashara kutakiwa kulipa kodi ya mauzo kabla ya kuanza biashara badala ya kulipa kodi hiyo miezi sita baada ya kuanza biashara, kumeleta usumbufu kwa walipa kodi hao na kuwakatisha tamaa hata wengine kuanzisha biashara. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i) Kuhakikisha vyombo husika vinatoza kodi kwa mujibu wa sheria;

ii) Kupunguza urasimu katika mchakato wa kuanzinisha biashara ili kuvutia wafanyabiashara wengi zaidi;

iii) Elimu ya mlipa kodi itolewe mara kwa mara kuepuka usumbufu usiokuwa wa lazima; na

iv) Wizara ijiwekee mikakati ya kukutana na wafanyabiashara kwa madaraja yao ili kusikiliza changamoto zao na kuzipatia ufumbuzi.

**f) Ufufuaji wa Viwanda vilivyobinafsishwa**

Viwanda ambavyo vilibinafsishwa lakini mpaka sasa havifanyi kazi iliyokusudiwa, vinakiuka lengo la ubinafsishwaji wake na hivyo kulitia Taifa hasara. Kamati inaishauri Serikali kuvirudisha viwanda vyote vilivyobinafsishwa ambavyo havijaendelezwa na kuvitangaza upya kwa wamiliki wengine ili viweze kuzalisha na kuongeza tija, ajira na mapato.

**g) Sera, Sheria na Kanuni zilizopitwa na Wakati**

Uwepo wa Sera, Sheria na Kanuni ambazo zimepitwa na wakati, unaweza kupunguza kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. Mfano wa Sera hizo ni Sera ya Taifa ya Uhamasishaji Uwekezaji ya Mwaka 1996, Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya Mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003 na nyinginezo ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho.

Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kufanya mapitio ya Sera, Mikakati na Sheria za Kisekta ili ziweze kuendana na mahitaji ya sasa katika kuchochea kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini. Aidha, uandaaji wa Sera mpya katika masuala mbalimbali yahusuyo sekta hii uwekewe mkazo ili kufikia malengo;

**h) Uingizaji wa Bidhaa za Chakula Nchini**

Suala la uingizaji wa bidhaa za chakula nchini limepata sura tofauti kutokana na hali ilivyo duniani ambapo baadhi ya

wafanyabiashara wamekosa uaminifu na kutengeneza vyakula visivyo salama. Mfano, tumeona kwenye mitandao mchele usio salama (wa plastic) ukitengenezwa na kuonekana kama mchele halisi. Hali hii inatishia usalama wa wananchi wetu. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo: -

i) TBS iongezewe uwezo kifedha, rasilimali watu na vitendea kazi ili idhibiti bidhaa sizizo na ubora zinazoingia nchini kwa wingi na kuleta athari kwa watumiaji;

ii) Kuziwezesha sekta za uzalishaji wa bidhaa za viwandani na mazao yatokanayo na kilimo nchini kuzalisha kwa wingi ili kujitosheleza kwa chakula na kupunguza uingizaji bidhaa hizo; na

ii) Kuhakikisha bidhaa zote za chakula zinazoingizwa nchini zina ubora stahiki na usalama kwa walaji.

**i) Changamoto ya Rumbesa**

Upakiaji wa mazao na bidhaa kupita ujazo au uzito uliowekwa kisheria katika magunia (rumbesa), umeleta changamoto nyingi ikiwemo kumnyonya mzalishaji na mkulima pamoja na kuikosesha Serikali mapato. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri Serikali yafuatayo: -

i) Iweke mkakati wa kusimamia utekelezaji wa sheria hii ili kuondoa tofauti zilizopo kati ya wakulima na wafanyabiashara ili kila upande uweze kunufaika; na

ii) Itoe elimu kwa wakulima na wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi vinavyokubalika kisheria sambamba na kusimamia marufuku hiyo ili kuondoa usumbufu.

### j) Mfumo wa Stakabadhi Ghalani

Ipo changamoto ya wakulima kulalamikia malipo kuchelewa kulipwa na vilevile mazao kushuka thamani. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha malipo yanafanyika kwa haraka. Wakulima wapewe elimu kuhusu umuhimu wa kuweka mazao yao kwenye madaraja mazuri ili wapate bei nzuri. Maghala yatumike kuhifadhia mazao vizuri ili yasinyauke na kupunguza gharama. Aidha, Serikali iendelee kuboresha mfumo huu na kuhakikisha maghala yanakatiwa Bima ya kuwalinda wakulima.

### k) Uimarishaji wa Taasisi za Utafiti

Hatuwezi kufikia lengo la kuwa na uchumi wa Viwanda ikiwa hatutawekeza kwenye kufanya tafiti zitakazoleta tija katika viwanda vyetu nchini. Kamati inaishauri Serikali kuipa kipaumbele Shirika la utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) kwa kuitengea fedha za kutosha ili kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa viwanda.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika - Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wote wa Bunge kwa weledi na umahiri wao katika kukusaidia kuongoza Vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, Napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard);*

1. Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Yustino Job Ndugai, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Prof. Patrick Aloisi Ndakidemi, - Mjumbe
18. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma Xaday, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Yahya Ally Khamis, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Abdul Aziz Abood - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mb - Waziri wa Viwanda na Biashara,

Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe, Mb - Naibu Waziri, Dkt. Hashil T. Abdallah - Katibu Mkuu, Ndg. Ally S. Gugu - Naibu Katibu Mkuu Uwekezaji, pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc* na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati - Ndg. Michael Chikokoto, *ndc,* kwa kwa kuisaidia Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu iliyopangiwa kwa ufanisi. Aidha, Nawashukuru makatibu wa Kamati Ndg. Elieka Saanya, Ndg. Thuwaiba Jumbe na Ndg. Asia Msangi pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuratibu shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

## 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naomba kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya **Fungu 44 - Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara** kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

David Mwakiposa Kihenzile, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

4 Mei, 2023

**SPIKA:** Ahsante sana. Kabla hatujaendelea na ratiba yetu kama utaratibu wetu wako wageni ambao hawakupata nafasi ya kuingia kipindi tulipotangaza wageni, niwatangaze sasa halafu tuendelee na ratiba.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na wageni wangu ambao wapo Jukwaa la Spika.

Hawa ni watangazaji wa *Wasafi Media*; yupo Ndugu Nelson Kisanga ambaye ni Mkurugenzi wa vipindi *Wasafi FM*; Ndugu Spencer Lameck, Mkuu wa Idara ya Uhusiano *Wasafi Media Group;* Ndugu Maulid Kitenge, Mkuu wa Kipindi cha *Sports Arena* na *Good Morning*, Ndugu Gerald Hando, Mkuu wa Kipindi cha *Good Morning;* Ndugu Hillary Mtuta ambaye ni Mtangazaji Kipindi cha *Good Morning;* Ndugu Charles William ambaye ni Mchambuzi wa Masuala ya Siasa, *Wasafi Media* na ni Mtangazaji wa Kipindi cha *Good Morning;* Ndugu Salma Dakota ambaye ni Mtangazaji Kipindi cha *Good Morning;* na Ndugu Mussa Charles huyu ni mpiga picha, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni hawa wamepita hapa Dodoma, wako safarini wakielekea Mbeya kwa ajili ya kukimbia siku ya Jumamosi na wataungana na Ndugu Naseeb Abdul Juma *(Diamond Platnumz)* kwa ajili ya kazi hiyo, tunawakaribisha sana Mbeya.

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni pia wa Wabunge wengine; tunao wageni 53 wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi na hawa ni wanafunzi wa Chuo cha Mahakama Lushoto *(IJA)*, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 118 wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni Wajumbe wa Baraza la

Umoja wa Wanawake Tanzania – CCM, Wilaya ya Dodoma Mjini wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Ndugu Zabibu Mtoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni 170 wa Mheshimiwa Sylvia Sigula ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma. Haya nafikiri hawajapata nafasi ya kuingia, pengine wataingia baadaye kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la Moravian Manyoni. Mchungaji Michael Mgandila, karibu *sana*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndio wageni ambao hawakupata nafasi wakati tukitangaza wageni asubuhi, na tunawakaribisha sana wageni wetu Bungeni.

Sasa tunaendelea na uchangiaji. Ninayo majina hapa ya Wabunge ambao wameomba kuchangia hoja hii kwa siku ya leo. Tutaanza na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti muhimu sana hii kwa mustakabali wa nchi yetu. Kama muda utaniruhusu, ninayo mambo matatu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, tumeipongeza Serikali, inafanya kazi nzuri ya kuitangaza nchi yetu na kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza kwenye nchi yetu, lakini ni ukweli usiofichika kwamba hatujafanya kazi nzuri kwenye kufufua viwanda vilivyokufa. Hasa viwanda vilivyokuwa vikimilikiwa na Umma na

tukavibinafsisha na viwanda hivi vingi ni viwanda muhimu sana. Bahati mbaya sana kule Korogwe kuna Kiwanda cha *Tembo Chipboard,* ni kiwanda muhimu sana, na kimetelekezwa muda mrefu. Mheshimiwa Naibu Waziri aliniahidi humu ndani atakuja kukitembelea, mwaka umekwisha sijamwona. Naomba niishauri Wizara tuongeze nguvu kwa kushikana na Msajili wa Hazina na Wizara za Kisekta.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu *NDC,* Shirika letu la maendeleo. *NDC* lilikuwa ni shirika muhimu sana na nadhani bado ni shirika muhimu. Lilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 90 la mwaka 1969, na limeendelea kuwepo chini ya utaratibu wa Sheria ya Mashirika ya Umma. Hata hivyo kuendelea kuwepo kwa *NDC* leo, mkazo wake hasa ni maamuzi ya Baraza la Mawaziri, Waraka Na. 6 wa Baraza la Mawaziri wa Mwaka 1996.

Mheshimiwa Spika, waraka ule ulieleza kwamba Shirika liendelee kubaki Serikalini, limilikiwe asilimia mia moja na Serikali, liendelee kufanya miradi hii muhimu ya kimkakati ya kusaidia viwanda vingine. Ni ukweli kwamba, hali na utendaji wa *NDC* bado hauridhishi. Mheshimiwa Waziri baadaye atakapokuwa anafanya majumuisho kesho, nangetamani kujua, kwa sasa *NDC* in miradi mingapi? Ni mingapi ambayo inafanya kazi? Ninyi kama Wizara mtuambie, hivi kweli mnaridhika na namna *NDC* inavyofanya kazi zake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, moja ya njia nzuri ya kuvutia na kushawishi wawekezaji ni kuwahakikishia utulivu kwenye nchi yetu lakini kuwahakikishia kwamba nchi yetu inafuata utawala wa sheria. Hakuna mwekezaji anaweza kuja kuwekeza kwenye nchi ambaye ana wasiwasi na utawala wa sheria unavyotekelezwa kwenye nchi. Nchi yetu inafuata utawala wa sheria, lakini siku za karibuni kumekuwa na matukio ambayo

yanafanywa na baadhi ya Taasisi za Serikali yanayopelekea nijaribu kuamini kwamba pengine taasisi hizi zinakoelekea ni kutokutii utawala wa sheria kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, yapo mazingira ambayo ningeweza nikatoa mfano, lakini naomba nitoe mfano kwenye eneo moja tu. Jana wakati namaliza *research* yangu hii kwa ajili ya kuchangia leo, ndugu yangu Mheshimiwa Shabiby aliniambia, kama unachangia kesho na mimi nimo. Sasa nataka naye pia anisikilize vizuri.

Mheshimiwa Spika, hapa nataka nitolee mfano sakata linaloendelea la *Twiga Cement* na *Tanga Cement*. Hapa nataka nioneshe tu madhara ya kisheria ambayo yanaweza kuleta taswira mbaya kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, nitalisema kwa kirefu, naomba unisadie, maana muda hautoshi. Mwezi Oktoba, 2021 Kampuni ya Scancem *International* na Kampuni ya *AfriSam*. Scancem *International* ni *subsidiary company* ya kampuni yenye hisa nyingi kwenye Kiwanda cha *Twiga Cement;* na *AfriSam* ni Kampuni yenye hisa nyingi, asilimia 68 kwenye Kiwanda cha *Tanga Cement*.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, Mwaka 2021 walitoa *joint statement* kwamba wamemaliza *terms* na makubaliano ya kuhamisha hisa za *AfriSam* kwenda *Scancem*. Tarehe 2 Novemba, Scancem akaiandikia *FCC* kuomba *approval. FCC* wakapokea, wakachakata, na *FCC* wakaridhia kuhamisha hisa hizi kutoka kwa *AfriSam* kwenda kwa Scancem lakini walitoa masharti. Yapo kadhaa ambayo *FCC* waliyatoa, na nimeyasoma vizuri kwenye *major analysis report* ya *FCC* yenyewe.

Mheshimiwa Spika, wapo wadau ambao hawakuridhika. Wadau watatu wakaenda kufungua shauri kwenye Baraza la Biashara. Mdau wa kwanza ni *Scancem* yenyewe akifungia shauri kutokuridhishwa na masharti aliyowekewa na *FCC*. Mdau wa pili ni Kampuni ambayo inafanya biashara kwa jina la *Chalinze Cement* na mdau wa tatu ni *Tanzania Consumers Protection Associations.* Wakafungua shauri kwenye Baraza la Ushindani, shauri linasikilizwa. Mwezi Septemba tarehe 23 Mwaka 2022 Baraza la Washindani likatoa uamuzi kwamba baada ya kupima hoja za pande zote, na kwa kutumia *major analysis report* yenyewe ya *FCC,* Baraza la Ushindani likazuia kwamba *acquisition* hii ya *shares* za *AfriSam* kwenda kwa Scancem isimame.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, uamuzi wa Baraza ukishatolewa kuna namna mbili tu, aidha kuomba review warudishe kwenye Baraza lenyewe au kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa. Hayakufanyika. Mwezi Desemba, 2022 *Scancem* wanaandika tena *FCC* kuomba kupewa *approval* ya kufanya *acquisition* ya hizi *shares* za *AfriSam.* Tarehe 11 Februari, 2023 *FCC* anatoa *notice* watu wapeleke maoni.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza Baraza hili ni la kwetu, tumeliunda kwa sheria. Utaratibu wa ku-*challenge* uamuzi wa baraza hili upo. Kwanini utaratibu haukufuatwa? Wameacha, wanakuja ku-*file application* nyingine mpya.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo ambalo Baraza lilizingatia ni *measure analysis report* ya *FCC* ambayo ilionesha kwamba Scancem na *AfriSam* waki-*merge* watakuwa na 42.27 ya *market share* kwenye biashara ya *cement*, kitu ambacho ni hatari na ni kinyume na kifungu cha 11(1) cha Sheria ya

Ushindani. Pia hakuna aliyekata rufaa, mwisho wa siku watu wamekuja kivingine.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linatia mashaka sana. Kinachotia mashaka zaidi, mwezi Machi mwaka huu, Taasisi nyingine ya Wizara hii, *BRELA* ikai-*deregister* Chalinze *Cement* ambayo ndiyo *challenger* mkubwa wa hili jambo, wakitoa sababu kwamba haja-*file annual returns.*

Mheshimiwa Spika, mimi ni kiongozi, najua suala la *annual returns* ni suala la kisheria, siwezi kulikataa, lakini hivi ni kweli? Mtuambie, makampuni yote tunayo *BRELA* sasa hivi yamekidhi? Yana-*file annual returns* kwa wakati? Mheshimiwa Waziri ukija tunataka tujue, maana kunakuwa na harufu ya jambo ambalo siyo zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi huu, mimi binafsi sikatai *acquisition,* sikatai ku- *merge,* ni mchakato wa kawaida kwenye biashara kwa ajili ya kuyafanya makampuni yaendelee kufanya kazi vizuri, lakini kwenye jambo hili, kuna maswali lazima tujiulize, mbona kuna kulazimisha sana Twiga kuinunua Tanga *Cement?* Mbona jambo hili halikutangazwa na halikuwa wazi? Walikaa wakakubaliana; *Twiga Cement* amekuwa *registered* kwenye *stock exchange,* akatangaze, watu waje, kuwe na ushindani. Jambo la pili, wakiungana hawa, hii asilimia ambayo kisheria inakataza ya ku-*monopolize* biashara hii, ninyi mnalionaje kama Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, sisi watu wa Tanga ni wahanga wakubwa sana wa mambo ya namna hii; ni wahanga wa hizi *merge,* ni wahanga wa hizi *acquisition,* ni wahanga wa wabinafsishaji, ni wahanga wa uuzaji wa Mashirika na Makampuni, kwa namna ambayo inakuwa haijanyooka vizuri.

Mheshimiwa Spika, hofu yetu sisi tunaotoka Mkoa wa Tanga, Waziri anajua na Serikali inajua, kwamba eneo la Kiwanda cha *Tanga Cement* ndiyo kiwanda pekee kime-*deposit* vya kutosha *raw materials* za kuzalisha *cement* kuliko sehemu nyingine yoyote kwenye nchi yetu. Tanga ndiyo inaongoza kuwa na *deposit* kubwa ya *clinker* ambayo kwenye uzalishaji wa *cement* huwa kunainahitajika *content* yake, ni karibu asilimia 95. Huyu Twiga hana *deposit* ya namna hiyo. Tuna hofu, anapomchukua huyu, usalama utakuwepo? Biashara hii itaendelea? *Brand* ya *Tanga Cement* itaendelea kuwepo? Ndiyo hofu yetu. Tunasema haya, hofu hii siyo kufikirika, yametukuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Korogwe tulikuwa na Kiwanda cha Mrwazi Kamba, aka-*merge* na kiwanda kingine, aliishia kufungua mashine za Mrwazi Kamba, akaenda kufanya shughuli nyingine. Tanga tulikuwa na Kiwanda cha *Amboni Plastic,* kikanunuliwa na Kampuni nyingine ya Dar es Salaam mnaijua. Kilipoishia, iko wapi ambayo ni *plastic* yetu leo Tanga? Haipo, imekufa. Hii ndiyo hofu yetu. Lazima Serikali mjiridhishe ili mtutoe sisi wenzenu kwenye hii hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, nini kifanyike kwenye eneo hili? Moja, kama nchi tuiambie Jumuiya ya Kimataifa, tunaheshimu Mfumo wa Utawala wa Sheria. Uamuzi uliotolewa na Baraza la Ushindani, uheshimiwe. Tunaweza kufanya *merger* au kufanya *acquisition* kwenye viwanda hivi kwa kutumia taratibu ambazo zitatutoa kwenye eneo la kutokuheshimu uamuzi wa Mahakama zetu, tunaweza kutafuta watu wengine, tunaweza kuangalia mabadiriko kwenye *market shares,* tunaweza kuangalia mabadiliko kwenye *considerations* ya hiyo *transfer* inayotakiwa kufanyika. Tukifanya hivyo, tutakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ushauri wa pili kwenye eneo hili, kama *Tanga Cement* iko *registered* kwenye *stock exchange,* kuna *public individuals* wanayoiyona hisa mle, kuna shida gani kutangaza huu mchakato ukaenda vizuri? Utangazwe, tuondoe usiri na malalamiko ambayo yalikuwepo. Kwa sababu ukitangaza, faida zake, jambo litakuwa wazi, watu watashindana, tutapata mwekezaji anayeweza kutoa fedha nzuri itakayosaidia kuongeza kodi ya Serikali. Pia akitoa hela ya kutosha, ni rahisi kuwa *serious* na biashara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mauziano yaliyokuwa yamefanyika ambayo *FCC* iliyabariki na Baraza likayakataa, wanataka kuuza hisa moja kwa shilingi 3,100, jumla kwa hisa zote ni shilingi bilioni 137 na *point* kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, tunawaomba sana, vyombo vyetu vya Serikali na taasisi zetu za Serikali, zisitumike kama sehemu ya kuharibu utawala wa sheria kwenye nchi yetu. Kubwa, zingatieni maslahi ya Taifa, zingatieni maslahi ya walio wengi, zingatieni maslahi ya nchi yetu. Tunachohitaji hapa ni kazi hii iende. Sisi hatutaki kuona *Tanga Cement* inakuja kufikia mahali inafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles John Paul Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Bajeti ya Wizara hii

ambayo naipenda sana na ninaifahamu. Nina mambo machache ya kuzungumzia.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda niunge mkono hoja ya Bajeti hii. Takataaje kuiunga mkono? Watu wa Mtelakuza hawatanielewa, na nimemwona Profesa wangu hapo, Profesa Winnie-Esther hatanielewa, kwa sababu hii ndiyo *dissertation* yangu ya *Ph.D* iko hapa. Jambo la kwanza, nimekuwa nikizungumza kwamba shughuli zote za kiuzalishaji zitueleze mauzo ya nje. Nampongeza Waziri, ameonesha kwamba Dola bilioni 8.52 anauza nje, na kwa gazeti la *Citizens* na tarehe 20 Aprili, limeandika, Tanzania tunauza nje shilingi bilioni 12.383. Hiyo tumekubaliana.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kuhusu *blueprint*. *Blueprint* imefanikiwa, na mafanikio ya kwanza yalitokana na pale sisi wenyewe tulipokubali kujitathmini. *Blueprint* tuliiandika sisi wenyewe na ninapenda kusema, *architect* mkubwa alikuwa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda. Niwape changamoto nyingine, na hii siyo Wizara tu, ni Serikali, ni wadau wote, ni wananchi wote, tuendelee kujitathmini na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara kwa sababu ina tija kubwa.

Mheshimiwa Spika, namba tatu, kulinda tasnia au kulinda viwanda. Nimemsikia Mbunge wa Tanga anazungumzia viwanda kufa. Kufa kwa viwanda mimi nakujua vizuri sana. Vingine nilijitahidi kuvifufua, aah, nikashindwa.

Mheshimiwa Spika, nitachambua ulinzi wa viwanda na Profesa Winnie-Esther yuko hapo, ananisikia, kwenye *marks* zangu utaniongezea, nitatumia ngeli *Michaek Porter,* Profesa wa *Harvard Business University* kuchambua ni kutumia *industry*

*strategy* kuwaonesha namna ya kulinda viwanda vya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiacha viwanda kuna kitu kinaitwa tasnia nitawapa mfano rahisi, chukulia viwanda vya magurudumu ya magari, kama Michelin, *Bridge Stone*, *Ring Long*, *Fire Stone* na Safari, *assume* viwanda hivyo vingekuwa hapa nchini, unapoangalia *industry strategy,* unaangalia kitu cha kwanza, unaingiaje kwenye ile *industry structure?* Unaangalia ile *barrier of entry* na *barrier of exit,* lakini unajiuliza, unakwenda kumkuta nani mle ndani? *The competitions*, the *players,* lakini unaangalia nani mteja wako *(the consumer)?* Unaangalia nani *supplier* wako mle? Unajiuliza, ushindani ukoje? Ni ushindani wa kirafiki au wa kihasama? Au wa kukatana vimeo?

Mheshimiwa Spika, unapokuwa unaangalia mambo hayo kuna watu wana maslahi. Mojawapo ya watu wenye maslahi ni Watanzania kwa kesi ya viwanda hivi nilivyovitaja ambavyo siyo vya ukweli, kwa sababu hatuna viwanda vya magurudumu. Mojawapo, kwanini tunajenga viwanda? Tunajenga viwanda:-

(i) Kutengeneza ajira;

(ii) Kutengeneza bidhaa za kutumia na bidhaa za kuuza nje na yote yanakwenda pamoja. Naipongeza Wizara, inauza nje na inaonekana.

(iii) Kuchangamsha uchumi. Pale penye viwanda, uchumi unachangamka, na ndiyo maana nasikia kilio cha Tanga; na

(iv) Kukusanya mapato ya Serikali kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa unaangalia *ES structure* ya Michael Porter wakiwemo wadau watano au sita katika ile *structure,* angalia wanavyofanya kazi. Ndiyo maana unakuta yanaundwa makundi ya watu kutetea wateja wale watano, wale waendeshaji wa shughuli wanaweza kulumbana au wakaungana pamoja wakamuumiza *supplier.* Unaleta malighafi, wanakupa bei ndogo. Au wakaungana, wakamuumiza mlaji. Wanazalisha bidhaa, wanaziuza kwa bei kubwa. Ama wakashindana wao kwa wao, kwa ushindani unaoitwa ushindani wa kukata kimeo, unakuta wawili wanakufa katika wale watano, watatu wanaobaki sasa, wana *conspire*, wana-*collude* na kuongeza bei. Kwa hiyo, walaji mnaendelea kuumia. Au waka-*merge,* wakaungana mtu na dada yake, unadhani ni *players* wengi, kumbe ni wale wale, halafu ikatokea kuja kumuumiza mlaji.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kitu kingine. Kwanini tunatengeneza viwanda? Kutengeneza ajira. Unapo-*merge* hawa washindani wa matairi ninaozungumza, wanaweza kuungana watu, kwa mfano, ukitokea mtikisiko katika *industry* katika shughuli; hawa watano wa matairi wakapatwa na mtikisiko, *industry* ikafa yote, siyo kwamba mmoja akabaki, kafa. Kitatakachotokea ni nini? Ni kwamba itatokea *supply* itatoka nje. Mtaagiza bidhaa za matairi kutoka nje. Fikiria, mkiagiza kutoka nje, dola mtazipata wapi? Hiyo ndiyo hatari kubwa. Mnapozungumza *measure* na *acquisition,* kama *industry* ikitikisika na kupasuka, *you will end up importing. Now, you will end up using the rare dollars you have*. Yaani Dola kidogo mliozonazo mtaweza kuzitumia kwa kuagiza bidhaa. Kwa hiyo, nataka kuwaeleza katika *industry* unapomwangalia…

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, kuna taarifa kutoka kwa Godwin Kunambi.

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, namuunga mkono mzungumzaji. Nchi inaponunua sana nje na siyo kuuza, kwenye uchumi naye ataniunga mkono, kuna *terminology* inaitwa *cutoff right inflations*, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage unapokea taarifa hiyo?

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Chifu Kunambi. Unajua maprofesa wako juu hapa, watu wanatafuta kiki ya *dissertations* huko kwa maprofesa.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuzungumza ni kwamba, *industry* ina mambo matatu. Moja, *players* wachache wanaweza kufa, waliobaki wakaua soko, lakini *industry* yenyewe inaweza kufa mkaamua kuagiza kutoka nje. Kwa mfano, wa Tanga niwaeleze, *industry* ya *cement* ya Tanzania iliwahi kupata tatizo la *supply.* Anafahamu Profesa Muhongo. Mimi na Profesa Muhongo tulikwenda kuwahakikishia Watanzania *(Industrialist)* kwamba mkaa wa Tanzania ni bora duniani. Yule tajiri namba moja duniani alipotuona, *cv* yangu na ya Profesa Muhongo, akakubali kwamba mkaa wa mawe wa Tanzania ni mzuri. Nazungumza kuhusu hawa *suppliers*.

Mheshimiwa Spika, mimi na Profesa Muhongo tulikwenda kuwahakikishia watanzania, kuwahakikishia *industrialist* kwamba mkaa wa Tanzania ni bora duniani. Yule tajiri namba moja

duniani alipotuona *cv* yangu na ya Profesa Muhongo akakubali kwamba mkaa wa mawe wa Tanzania ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, nazungumza kuhusu hawa *supplier* matokeo yake ni nini? Hii *merge*, merge ya Twiga na Simba matokeo yake ni kwamba *industry* inaweza kufa tukaishia kununua bidhaa nje, kwa hiyo *merge* pamoja na kuangalia sheria huyo ni mwanasheria mimi sijasoma sheria lakini pamoja na kuangalia maslahi ya wananchi lazima tuangalie kwamba tunapoungana hakuna uwezekano wa *industry* nzima kufa? Ili baada ya kufa bidhaa itatoka nje na ukuzingatia kwamba Tanzania leo tunahitaji saruji kuliko maelezo.

Mheshimiwa Spika, nimeshiriki kwenye ma–*group* mengi na nimewashauri, niipongeze Serikali kwa kujenga reli sisi hapa tunajiandaa kwa *African Continental Free Trade*. Kwa hiyo, vigezo vya kuwa na *market share* vizingatiwe ili kwa kuwa na *market share* unazuia watu kukurudi, watu kupanga bei na wakawaumiza wale wadogo wanaoota, matabirio yetu sisi ni kutengeneza Tanzania *industry* ya *cement* yenye tani 25,000,000 twende mbele kama anavyosema Baba Askofu Gwajima kwamba tuangalie mbele na kuangalia mbele ni kuangalia ile *industry* isiweze kuyumba.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Shabiby atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga ajiandae.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nimekuwa mmoja wa wachangiaji lakini kwenye

mchango wangu sitokita sana kunukuu maprofesa au watu wengine. Nitakwenda sana kuongea kwenye lugha nyepesi ambayo watanzania au Wabunge wenzangu wataielewa. Leo michango yangu ni miwili tu. Mchango wa kujiunga kwa viwanda hivyo viwili pamoja na kiwanda cha pale kibaha cha kuunganisha magari.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitaanza na kile kiwanda cha kuunganisha magari *FAO* pale Kibaha. Nataka niwape maangalizo Mawaziri wetu na hasa Waziri wa Viwanda kwa sababu wewe ndio mhusika wa viwanda, lakini vilevile na Waziri wa Fedha kwa sababu katika nchi hii tunakusanya kodi mpaka kwa watu wa chini ndio maana kuna tozo kuna nini kuna nini kwa sababu hatuna mapato kwenye hii nchi ili tuajiri wafanyakazi tufanye nini yani lazima tupate mapato. Lakini unavyoona kuna kitu kinaanzishwa hakina msingi wa aina yoyote halafu tena kuna kodi inatolewa pale bila manufaa yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kile kiwanda cha kuunganisha magari cha *assembly* pale Kibaha. Kile sio kiwanda cha *assembly* kile kiwanda cha kuchukua gari ambalo limefunguliwa kutoka China pale wanakuja kuliunganisha yaani sawasawa na gari lako unalichukua hapa Dodoma unalifungua fungua unaliweka kwenye boksi halafu unalipeleka Dar es Salaam unalichukua *engine* unalibandika unachukua *cabin* unabandika mnasema *assembly*, hiyo sio *assembly*. Halafu baada ya hapo unamwambia kwamba yule atakaye mwenye magari mengine akileta kutoka China analipa *VAT* ila lile linaloungwa ungwa pale halipi *VAT* kwa hiyo, ni kuikosesha Serikali mapato bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana ya *assembly* za Mwalimu Nyerere mpaka zimekuja kwa kina Mwinyi mpaka wakina Mkapa

maana yake ni nini? Maana ya *assembly* gari inatengenezwa Tanzania kwa 21% ni malighafi kutoka Tanzania kwa mfano, wakati ule *TAMCO* imeanzishwa ilikuwa inaunganisha magari ya *Scania.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wale *Afro Cooling* kiwanda cha Tanzania nacho kimeajiri wafanyakazi wengi, kilikuwa kinatoa *rejetor* zote *made in* Tanzania. *AFRI cable* walikuwa wanatoa *wire* zote zinaunganishwa *wire* za Tanzania *Yuasa* zilikuwa betri za Tanzania. Kiwanda cha Tanzania mali yake inaunganisha pale, *Tasia* walikuwa wanatengeneza *spring* ndio wanaenda *spring* za Tanzania zinatumika, Mangula walikuwa wantengeneza letras zote zinakwenda pale zinatumika. Hawa *Coast sterio* walikuwa wanatengeneza ngazi na vitu vingine kwa hiyo ukiangalia 21%. *General Tyle* walikuwa wanatengeneza matairi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukichukua maana ya kuongeza ajira kwa ajili ya *assembly* unaunganisha na hivyo viwanda vyote. Leo kwenye magari haya hakuna mali yoyote ya Tanzania inayohusika pale. Halafu mnasema tunaongeza ajira Tanzania, wale wafanyakazi wako 100 tu pale, ajira ipi? lakini ukosefu tunayokosa kwenye *VAT* mabilioni ya pesa. Hii utapeli wa aina huu haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake na sisi wafanyabiashara wa mabasi tunataka na sisi, maana yake basi moja ushuru peke yake ukiuliza Tanzania ni 100,000,000 wakati lori ni 30,000,000 sasa wa mabsi nae akija kwa hiyo Serikali mtakusanya wapi pesa? Tuachane na hii Habari ya viwanda vya utapeli tapeli huu na Mheshimiwa nilishaongea nae hata kwa mdomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ni hiki kiwanda cha nilikuwa sitaki kuongea lakini nimeona ndugu yangu Mnzava amenitaja pale na mimi acha niseme. Hiki kiwanda kuungana kiwanda cha Twiga *Cement* na Tanga *Cement* sioni shida, hivi shida iko wapi? Mwenye mali mwenyewe wa Tanga *cement* ana 68.8% hawa mashirika yetu haya ya Mifuko ya Jamiii yana hisa 32.2% anayetaka kujitoa ni yule mwenye 68% anataka kuuza *share* yake mtu anataka kuuza *share* yake tatizo liko wapi? Hakuna shida, ukisema hivyo kwamba huyu mtaleta *competition* kuna viwanda 11 nchi hii na cha Tanga sasa hivi ni cha nne kwa uzalishaji wala sio cha pili kama mnavyosema, kuna viwanda 11 vya *cement*. Hivyo *TBL* ameshika soko la nchi hii asilimia ngapi? Yapombe, si Kashika Zaidi ya 90%, ukija Bakhresa asilimia ngapi za unga? Zaidi ya asilimia 80%, ukija Mtibwa *Sugar*, Mtibwa *Sugar* ndio mwenye kiwanda cha Kagera *Sugar* sio mtu mmoja? Kwa hiyo kama…

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mnzava.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji sekta ya saruji ni moja kati ya *non regulated sectors* kwenye nchi yetu, na kwa sababu hiyo kanuni za ushindani kusimamiwa ni jambo muhimu kuliko kitu kingine chochote kile, nakushukuru. (*Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili. Isipokuwa ninachozungumzia tusiwe tuna hiyo

mambo kama hayo, tunachotakiwa sisi kuangalia je, Tanga *Cement* ana *clinker* nyingi Zaidi ya kuvuna miaka 100 pale kwake? Twiga cement hana *clinker* nyingi. Kinachotakiwa ni kusimamia kwamba hiki kiwanda kitafanya kazi? Wafanyakazi wale hawatakosa ajira? Sasa ni kazi ya Serikali muwe na mikataba ya aina ile, kiwanda kifanye kazi na wasije Twiga wakanunua wakachukua ile *clinker* wakaihamisha. Hicho ndio cha msingi lakini cha msingi kusema *FCC*, f ni nini sasa imekuja kwenye hii *cement,* nataka niiulize hii Serikali kwamba haina mpango maalumu wa kupanga bei?

Mheshimiwa Spika, Lazima uwe na wataalamu, waangalie je uzalishaji wa Tanzania una *cost* bei gani? Niwapeni mfano nchi kama Oman au Kenya tu, nchi mbili tu, *cement* ya aina yoyote inayozalishwa kuna wataalamu wetu tuna Maprofesa tuna manini huko Vyuo Vikuu wako wasomi wataalamu wanaangalia ina-*cost* bei gani? wakiweka na kodi bei gani? Wanaweka na bei ya kuuza ni hii hasa kama hii nchi kila mtu akizalisha kitu anauza anavyotaka basi itakuwa ni balaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusiogope kwa hilo tusiseme eti mtu kwamba mimi hapa nina mali yangu nataka kuuza eti unaniambia eti peleka kwenye mashindano, mashindano yapi hayo? Kitu changu haya, kwa mfano nimeamua kuhujumu? Sipeleki lakini taarifa ya uzalishaji umepumzika. (*Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

## TAARIFA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa mzungumzaji mzuri tu, Mheshimiwa Shabiby rafiki yangu mkubwa kwamba kiwanda cha Tanga *Cement* ni moja ya viwanda vinavyothaminiwa katika Uhuru wa Tanzania na kiwanda kilichobinafsishwa mwaka 1966 ni kiwanda cha wananchi na ni kiwanda cha Serikali kwa masharti ya kubinafsisha sio cha mtu binafsi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, taarifa naiopokea lakini naona haelewi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika kwa sababu kama mnataka hivyo nyumba za Serikali zote zilikuwa nyumba za Uhuru ziko hapa? si zimeuzwa? Viwanda vyote vya Nyerere vilikuwepo hapa, si vimeuzwa? Sasa mkitaka, zimeuzwa nyumba mpaka kwenye makao ya Polisi, utakuta nyumba ya Polisi ipo kwenye eneo la Polisi kauziwa *RPC* sasa mkitaka namna hiyo hiyo msizungumze vitu hivi. Sisi twende tuzungumze kile kitu cha kweli, hizi ni biashara tunazungumzia mambo ya biashara hatuzungumzi Habari ya sijui ilikuwa hivo ilikuwa hivo, tuzungumzie biashara. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawasihi ndugu zangu tusijiingize huko kwenye mambo ambayo hatuyajui tuwachie wawekezaji wawe huru sisi tuwabane tuweke vitu vya *regulation* kwa ajili ya kuwabana kwenye bei na vitu vingine, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mheshimiwa Neema William Mgaya.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nichangie kwenye hoja iliyoko mbele yetu. Nataka nitumie fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayofanya kwenye Wizara hii, tuna imani naye tunachomuomba aendelee kuweka umakini katika kusimamia sekta zilizoko chini ya Wizara hii. Nataka nimpongeze sana ndugu yangu Mnzava ambaye ameeleza vizuri jambo hili kwa maslahi ya watu wa Mkoa wa Tanga na uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika sisi watu wa Tanga ni wahanga wa uwekezaji, siye tumegongwa na nyoka kwa hiyo, tukiona unyasi lazima tushtuke. Mwaka 2017 alijitokeza muwekezaji akiitwa Hengia akionesha nia ya kuwekeza kenye sekta ya saruji katika nchi hii na kiwanda kile alikuwa aje akijenge Mkinga. Mwaka 2019 *TIC* ilimpa leseni aje awekeze, mwaka 2020 akaanza kutoa fidia kwa ardhi aliyoitwaa kule Mkinga wananchi wakaachia maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, tangu wakati huo fidia stahiki haijatolewa, hivi ninavyozungumza wako wananchi 143 wa Mkinga kutoka Kwale na Mtimbwani wanadai Zaidi ya milioni mia tano na sabini na kitu hivi hazijalipwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilituma timu ikaja kukaa na uaongozi wa Mkoa na uongozi wa Wilaya na mwekezaji, wakakubaliana ifanyike kazi ya tathmini isiyo na shaka ili watu hawa walipwe, kazi imekamilika. Mwekezaji huyu wamepelekewa amegoma kulipa viwango stahiki vya kisheria.

Mheshimiwa Spika, hawa ni wananchi wamepoteza ardhi zao, hawana ruhsa ya kuingia kwenye maeneo yale mpaka leo hawalipwi. Kwa nini mwekezaji halipi? Ni kwa sababu ana

machungu nilisema hapa kwamba jamani uwekezaji huu wa Hengia ambao wakati ule kama ungefanyika mwekezaji alikuwa anakuja kujenga kiwanda chenye thamani ya trilioni 2.3 uzalishaji wa saruji alikuwa anaenda kuzalisha tani 7,000,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, nimesikia taarifa ya Wizara hapa inazungumzia kwamba leo viwanda 14 tunazalisha tani 10,000,000 tulikuwa na mwekezaji ambaye alikuwa tayari kuja kuwekeza mtaji wa trilioni 2 azalishe tani 7,000,000,000 tuka–*frustrate*, nilikuja kusema maneno haya hapa nikasema wapo watendaji wetu hawana nia njema wanam–*frustrate* mwekezaji, wapo watu ndani ya *industry* ya saruji hawataki mwekezaji huyo awepo kwa sababu ataleta ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunapozungumza tumepoteza uwekezaji ule, watu wa Tanga tuna machungu, tumegongwa na nyoka tukiona unyasi tunashtuka. Naiomba Serikali tathmini hii ilifanywa na timu ya Serikali Mheshimiwa Waziri nakuomba simamia ndugu zetu wale wa Mkinga 143 walipwe stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, Sasa kwa muktadha huo huo, linapokuja suala la uuzaji wa hisa za *Tanga Cement* sisi hatuna hatupingi, lakini tunasema taratibu zifuatwe, watu wa Tanga leo hii pale Tanga tuna viwanda nane, baada ya kubinafsishwa vimegeuka kuwa magodauni vimegeuka kuwa magofu havifanyi kazi. Hatutakuwa tayari kuona *Tanga Cement* inabinafsishwa inageuka kuwa godauni mtu anakuja kuchukua *raw materials* Tanga anakwenda kuzalisha Dar es Salaam hilo hatutaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Viwanda vile nane tumehangaika ndani ya Serikali ili wawekezaji wale waheshimu mikataba yao wakati wanauziwa viwanda vile Serikali mmeshindwa kulisukuma hili, hii ndio hofu yetu, watu wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali taratibu zifuatwe uwekezaji ufanyike tujenge *confidence* ya wawekezaji tunapata shida kwenye sekta ya madini kila mwekezaji anayetaka kuja akija anang'ang'aniza kwamba kukiwa na *disputy* twende tukaamuliwe mashauri hayo nje ya Tanzania, kwa nini? Kwa sababu wanasema mahakama zetu haziaminiki. Kama kuna jambo lililoamuliwa kisheria tusikiuke maamuzi yale yaliyoamuliwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kila muwekezaji kwenye sekta kule akija anaenda kujificha kwenye maeneo ambayo tuna mikataba ya kimataifa kwa hiyo anaenda kujisajili kampuni kwenye maeneo hayo ili mashauri yake yasiamuliwe Tanzania yaende kule. Tukiendelea kukiuka maamuzi ya vyombo vyetu vya kisheria tunaenda kupeleka ujumbe kwamba tusitumie mahakama zetu za ndani mashauri yote yakaamuliwe nje, hii haiwezi kuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ajiandae.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ambayo iko mezani na kwa kuanza ningependa nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kwamba sekta hii ya Uwekezaji Viwanda na Bashara inaleta tija katika Taifa letu, lakini kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo Wizara inafanya, lakini pia niwapongeze watendaji wakiongozwa na

Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo inafanyika schini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kipekee kwa sababu, wasilisho la Mheshimiwa Waziri limeonesha namna ambavyo Mheshimiwa Rais amefungua fursa za ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Waziri imetuambia kuanzia Julai, 2022 mpaka mwezi huu Machi, 2023 takribani ajira 81,8200 zimezalishwa katika sekta za miradi ya kimkakati na uwekezaji kwa kweli ni jambo ambalo linatia faraja sana kwa sababu wote tunafahamu changamoto ya ajira kwa vijana wetu. Kwa hiyo, kipekee sana nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo tumeahidi ajira kwa vijana ifikapo 2025 inatekelezwa kwa kasi na kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kujikita kuchangia kuhusiana na programu za ubunifu ambazo Mheshimiwa Waziri ameziongea kwanza niipongeze Wizara kwa hatua ambazo inafanya katika kuhakikisha kuwa ajira kwa vijana zinapatikana na Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa namna ambavyo Wizara inawekeza katika programu za ubunifu za vijana ikiwemo kuatamia wabunifu vijana. Ameeleza hapa katika mwaka wa fedha uliopita waliwatmia vijana wabunifu 27 na kufikia Machi mwaka huu wamewatamia vijana watano.

Mheshimiwa Spika, ameeleza hapa, kwamba katika mwaka wa fedha uliopita waliatamia vijana wabunifu 27 na kufikia Machi mwaka huu wameatamia vijana watano. Niipongeze Wizara, lakini nimshauri Mheshimiwa Waziri, jitihada hizi hazijitoshelezi kulingana na maendeleo ya teknolojia ambayo tunayo, lakini vilevile kutokana na fursa ambazo vijana wanazihitaji programu

hizi bado ni ndogo sana. Na sio kwamba, tunailaumu Wizara kwamba, haifanyi kwa kadiri ya ambavyo inatakiwa kufanya, mimi naamini Wizara hii ilitakiwa kufanya zaidi ya haya ambayo yanafanywa.

Mheshimiwa Spika, programu za ubunifu katika Taifa hili zinafanywa na kila Wizara, lakini hatuna uratibu ambao unaonesha ni programu ngapi zinafanya biashara na ambazo zimekuwa stahimilivu kwenye soko la biashara; na hii ndiyo Wizara ambayo ina jukumu la masuala yote ya kibiashara. Kwa hiyo mimi nilitegemea pamoja na kwamba Wizara inatuonesha *program* ambazo wao wanazifanya, walitakiwa kutuonesha uratibu wanaoufanya kwenye programu za ubunifu katika Wizara zote, na watuoneshe ni programu ngapi za vijana zinafanya biashara na zimechangia ajira kwa kiasi gani, ndiyo kazi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapoendelea mbele, mimi nafahamu kwa mfano *COSTECH* ambayo iko chini ya Wizara ya Elimu wameingia mkataba na CRDB hapa juzi kwa ajili ya kuwawezesha vijana kwenye programu za ubunifu. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pia inafanya programu hizo, Wizara ya Kilimo na Wizara nyingi sana, lakini Wizara hii itusaidie kufanya uratibu ili tuweze kujua programu gani za ubunifu zinastahimili kwenye soko la ajira na soko la kibiashara.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwa sababu, hapa tumesema ajira ambazo zinaratibiwa, ndizo hizi ambazo zimeripotiwa. Ajira hizi ambazo wanazalisha vija awenyewe ni muhimu sana kwa sababu tunakoelekea kila siku tunasema teknolojia ndiyo ambayo inaajiri vijana wengi zaidi. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atusaidie ili tuhakikishe kwamba vijana hawa ambao wanaweka jitihada kubwa sana katika programu zao za ubunifu Serikali inawa-*support* na wanaratibiwe vizuri. Pale

ambapo uratibu ukifanyika changamoto zikitokea ni rahisi sana kwa Wizara husika kuelekeza sekta inayohusika kuwasaidia vijana hawa ili wasiweze kudondoka katika soko la kibiashara.

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kidogo pia kuhusiana na suala ambalo limezungumziwa hapa awali. Sisi kama Taifa wote tunafahamu, kwamba shughuli zote zinazohusisha utawala wa Taifa letu lazima ziongozwe na Katiba, Sheria, taratibu na kanuni ambazo tumejiwekea sisi wenyewe. Ibara ya 97 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalipa Bunge hili jukumu la kutunga sheria, lakini Katiba hiyohiyo inaipa Mahakama jukumu la kusimamia haki; na Kikatiba ndio taasisi ya mwisho ambayo inasimamia haki katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane; katika kutekeleza miongozo na shughuli ambazo zinaleta tija ya maendeleo katika Taifa letu ni busara na weledi mkubwa kwamba, taratibu na kanuni ambazo tumejiwekea sisi wenyewe na sheria ambazo Bunge hili limezitunga ni lazima zizingatiwe. Sheria yetu ya Ushindani inasema wazi kabisa; nasema hivi kwa sababu, tukicheza tusifuate wenyewe sheria ambazo tumejiwekea tutakuwa hatuendi katika mwenendo ambao ni sahihi; sheria ya ushindani inasema wazi kabisa kwamba kwenye makubaliano yoyote ambayo yanachagiza kuathiri soko ama yanachagiza kuathiri soko kwa maana ya ushindani, makubaliano yote ambayo yanajikita kwenye kuharibu ushindani ni makubaliano ambayo hayakubaliki kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sheria ambayo tulitunga sisi wenyewe ya ushindani, kifungu cha nane kifungu pia cha 5 kinatuambia wazi namna ya makubaliano ambayo yanakubalika katika soko letu la ushindani. Kifungu hicho kinasema kwamba makubaliano ambayo yanakubalika ni yale ambayo, moja,

yanakuwa makubaliano ambayo hayazidi utawala wa soko kwa asilimia 35, lakini makubaliano haya ambayo sheria inatambua ni yale makubaliano ambayo yanalinda walaji dhidi ya soko la ushindani.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa *issue* ni kufuata sheria na taratibu. Hakuna mwekezaji yeyote anayekatazwa kununua hisa za kampuni yoyote, *issue* kubwa ni kwamba taratibu ambazo tumejiwekea ni lazima zifuatwe.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu sababu ya sheria kuweka taratibu hizi, moja, ni lazima tudhibiti soko dhidi ya ushindani, lakini pili, lazima tuhakikishe walaji wanapata bidhaa kwenye soko, na tatu, bidhaa lazima ziwe stahimilivu kwenye soko. Sasa tusipohakikisha kwamba taratibu hizi zinafuatwa inakuwa ni jambo ambalo kwa kweli linaleta maswali mengi sana. Lakini mategemeo yetu yalikuwa ni kwamba, taasisi ambazo tumezikasimu madaraka haya ya kusimamia taratibu hizi zinafanya mambo hayo kwa weledi mkubwa sana, ili kuepuka hii tafaruku ambayo tunayo sasahivi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme yafuatayo; wakati hii Kampuni ya *Scancem* inataka kununua hizi *shares* za *AfriSam Mauritius* ni jambo ambalo ni la heri, lakini mgogoro umeanzia kwenye kujiridhisha kama hawa wawili wakiwekwa kwa pamoja wanazidi utawala wa soko kwa asilimia 35. *FCC* wenyewe wamefanya tafiti na wana *data* za kuonesha kuwa hizi kampuni mbili zikiungana kwa pamoja zitasababisha utawala wa soko kwa zaidi ya asilimia 35.

Mheshimiwa Spika, na ningependa nitoe mfano; kigezo kikubwa ambacho Mahakama imetuongoza tukifuate ni kigezo cha utawala wa soko, kwamba ni nani anayeuza zaidi.

Ukiangalia takwimu za *FCC* ukiunganisha hizi kampuni mbili, *Twiga Cement* na *Tanga Cement,* kwa pamoja zitauza asilimia 52 katika soko. Lakini pia takwimu zinatuonesha, kwamba katika uuzaji, katika kanda tano kubwa, kanda nne zitatawaliwa na hizi kampuni mbili. Kwa mfano, Kaskazini watauza kwa asilimia 92, Kanda ya Ziwa asilimia 77, Pwani asilimia 60. Kanda ya Kati asilimia 49 ni Kanda ya Kusini tu pekee ambayo imeachwa kwa sababu, soko lake liko *dominated* na Dangote.

Mheshimiwa Spika, sasa kama sisi wenyewe, sheria tunazitunga wenyewe, takwimu tunafanya wenyewe na tunazo sisi wenyewe, ni kwa nini tunakwenda kinyume na taratibu ambazo sisi wenyewe tumejiwekea?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa hakuna mtu anayekatazwa kununua hisa, tunachoshauri, taratibu zifuatwe. Kama *Scancem* hisa zake zinaonekana zimezidi…

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, kuna Taarifa kutoka kwa mtoa hoja.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza mchangiaji anavyochangia. Naomba tu kumpa taarifa kwenye eneo la kwamba, kanda nyingi zitakuwa zinahudumiwa na kampuni hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, uuzaji wa saruji kwenye nchi hii hauuzwi kikanda. Ukienda Kagera utakutana na Dangote, ukienda Tanga

utakutana na Dangote, ukienda Mtwara utakutana na Dangote. Kwa hiyo, Tanzania nzima inauziwa saruji na kampuni zote 14. Kwa hiyo, hiyo hoja ya mwanzo ya *analysis* tutaijibu badaye, lakini nilitaka tu kumpa hiyo, soko la Tanzania halijagawanywa kikanda. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, siipokei kwa sababu Mheshimiwa Waziri hajanielewa. Hii sio ripoti yangu mimi, ni ripoti ya Tume ya Ushindani inayoeleza mauzo kwenye kila kanda; na ndiyo ripoti iliyotumika kuamua kama *Scancem* wanapewa hisa za *Tanga Cement* ama hapewi. Kwa hiyo, mimi nilichofanya hapa ni kudurufu kile ambacho *FCC* wenyewe wamesema. Na hii ripoti inaeleza tu kama hawa wawili watauzaje kwenye soko. Ndio kila kampuni inauza, lakini inategemea na *percent* ya kila kampuni kwenye kanda husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha, muda wangu umeisha. Tunachoshauri ni kwamba, taratibu zifuatwe, kama twiga anataka kununua wahakikishe manunuzi hayazidi ile *threshold* ambayo tumejiwekea, asilimia 35 mpaka 40 kwa vigezo maalum. Kwa sababu wao wenyewe, tunatambua, hata vigezo ambavyo amepewa na *FCC* vya kununua baadhi yake anavipinga. Sasa na sisi kama Watanzania lazima tuwe tuna maswali. Mama amefungua fursa, wawekezaji ni wengi, Serikali iweke mchakato vizuri, wawekezaji wengi wapo, mchakato uwe wa wazi, usilete maswali ili tuhakikishe kwamba, rasilimali za Watanzania zinalindwa na taratibu na sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe zinafuatwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema William Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya. Nianze kuchangia kwa kumpongeza Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ndani ya nchi yetu. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri, Dada yangu, Mheshimiwa Dkt. Ashatu kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Naibu Waziri wake na watendaji wote wa Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba, sera kubwa ya viwanda ni *agro processing*. Sisi Tanzania tunataka tuchakate malighafi zetu ili tuweze kusafirisha bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivi tutasaidia kuongeza thamani ya tunachokizalisha, lakini vilevile sambamba na kuongeza ajira ndani ya nchi yetu. Lakini tukisema tusafirishe mazao ina maana tutakuwa tunapoteza ajira na tunapoteza mapato. Na hii ajenda tumekuwa tukiizungumza takribani miaka mitano sasa, lakini hivi sasa kama inaenda kuwa kimya. Labda ningependa Mheshimiwa Waziri aweze kuniambia akija kufanya majumuisho, ile ajenda tuliyokuwa tukiimba ya Tanzania viwanda bado ipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulianza kutengeneza *industrial park* pale kurasini miaka miwili iliyopita, nafikiri kipindi kile Waziri wa Viwanda na Biashara alikuwa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, kama sijakosea. Tulikubaliana tuanzishe kiwanda cha chai,

kiwanda cha kahawa, kiwanda cha parachichi na viwanda vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tulikubaliana Tanzania tuwe na soko kubwa la chai kama lilivyokuwa kule Mombasa kwa majirani zetu. Hii ingeweza kusaidia wakulima wetu wa chai waache yale manung'uniko, ya kwamba tunakosa soko la chai, na hivi sasa mpaka wameamua hata kuacha uzalishaji wa chai na kung'oa baadhi ya mashamba ya chai kwa kukosa soko. Na ningependa kujua Mheshimiwa Waziri huu mchakato umefikia wapi? Ukija kuleta majumjuisho hapo utuambie kwamba, huu mchakato ambao tuliuanza pale Kurasini wa *industrial park* umeishia wapi?

Mheshimiwa Spika, sasa nipende kuzungumzia suala la zao la parachichi. Kama tunavyojua kwamba, Tanzania kwa *East Africa* ni moja ya nchi ambazo zinazalisha parachichi kwa wingi na Mkoa wa Njombe ndio unaoongoza. Paparachichi yetu tunazalisha kwa wingi na yenye ubora, lakini ni miaka mingi sana tumakuwa tukipigia kelele Wabunge wa Mkoa wa Njombe na wa Nyanda za Juu Kusini wa mikoa mingine kuhusiana na suala zima la uanzishwaji wa viwanda vya kuchakata zao la parachichi ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufike wakati sasa kama tutakuwa tunatoa ushauri haujapokelewa, basi Serikali ituambie kwamba, ushauri huu bwana, sisi hatujaupokea, ili tusiendelee kupiga makelele humu ndani ya Bunge. Maana sasa tunapiga makelele mpaka sasa tunataka kufanana na hayo maparachichi yenyewe.

Mheshimiwa Spika, katika biashara yoyote duniani kitu cha kwanza unachotakiwa kufanya katika uzalishaji wowote ni

kuhakikisha kwamba una uhakika wa soko la ndani. Ili kuwa na uhakika wa soko la ndani lazima tutengeneze miundombinu ya kuwa na viwanda vya kuzalisha hili zao la parachichi. Hii fursa tuliyoiona ya kusafirisha parachichi nje ya nchi, nchi nyingi zimeona hii fursa. Hebu tukae chini tutafakari, tujiulize, je, nchi nyingine zote zilizoona fursa hii zikiamua kuzalisha kwa wingi, vipi soko huko mbele? Vipi mustakabali wa wakulima wetu wa zao la parachichi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sisi Wabunge tunasisitiza kwamba, tuanzishe viwanda vya kuchakata zao hili, ili badaye *supply* ikiwa kubwa, *demand* ikishuka kule, huku sisi tuwe na uhakika wa soko letu ndani ya nchi. Na hii itasaidia kuwalinda wakulima wa zao la parachichi wawe na uhakika na wafurahie kile ambacho wanacho…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Nilikuwa sijamuita, ili umalizie sentensi yako maana naona umeishia, "kwa kuwa…". Sasa sijui ataanzia wapi kutoa Taarifa. Malizia sentensi uliyokuwa unasema, ili nimpe nafasi.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema hivi, ni kwamba, umuhimu wa zao hili la parachichi, ili liweze kuleta tija kwa wananchi ambao tunazalisha zao hili la parachichi ni kuhakikisha kwamba, tuna viwanda ambavyo vitakwenda kuchakata zao letu la parachichi, ili tuwe na uhakika wa soko la ndani endapo soko la nje likija kuharibika hapo badaye.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Neema Mgaya, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

## TAARIFA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa Taarifa Mheshimiwa; hotuba ya Waziri inaonesha kwamba, tunaagiza mafuta kutoka nje tani 365,000. Hoja ya Mheshimiwa Neema ni kwamba, tukiwa na viwanda vyetu vya kuchakata maana yake vilevile na mafuta yanayotokana na zao la parachichi tutaweza kutengeneza ndani. Maana yake sasa tutafidia hicho anachokisema, lakini vilevile kuzuia fedha za kigeni kwenda nje. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Neema Mgaya, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naipokea Taarifa ya Mheshimiwa Halima kwa mikono miwili kwa sababu, ina tija kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie suala la Liganga na Mchuchuma. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametueleza taarifa njema za kulipa fidia wananchi wetu wa Mkoa wa Njombe ili kuweza kuendelea na zoezi hili la Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, kulipa fidia tu haitoshi. Sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe na Watanzania kwa ujumla kwa unyeti wa mradi huu wa Liganga na Mchuchuma tunataka kujua, ni lini chuma kitaanza kuchimbwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nafikiria kwa kuwa, tumeshasema faida nyingi sana za mradi huu, na tumesema hasara za kucheleweshwa kwa mradi huu, ikiwa na kupitwa kwa wakati kwa makaa ya mawe, tumezungumza sana ndani ya

Bunge hili. Mimi nafikiri ni wakati sasa Bunge lako liunde Kamati Teule ya kuchunguza Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma; na mimi nitaleta hoja binafsi ya kuunda kamati teule ya kuchunguza suala la Liganga na Mchuchuma ili kusudi suala hili liende kufanyiwa kazi kwa uharaka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikileta hoja hiyo Mezani kwako unikubalie na uniunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Nipende kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri, najua, nimefanya naye kazi katika Wizara hii ya Viwanda, mimi nikiwa mjumbe wa Kamati yake. Ni Waziri mahiri sana, anajiweza katika vitu vingi. Namshukuru kwa kufanya kazi vizuri na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, lakini nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa mapambano yake haya ambayo anaendanayo katika viwanda. Nilikuwa naona katika shughuli hizi alizokuwa anazungumzia Mheshimiwa Mgaya hapa, juu ya Liganga na Mchuchuma. Sasa kutokana na hayo mimi nikaona nije na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, nianzenayo kabisa, Ukurasa wa 58; inasema, kuendeleza na kujenga viwanda mama ikiwemo viwanda vya chuma, Miradi ya Mchuchuma na Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, wazo limekuwepo tangu uhuru, ilani imeandikwa zaidi ya miaka 40. Sasa mimi nataka kujiuliza, Liganga na Mchuchuma sasa ni wimbo au ni mradi? Maana sasa tujue, Liganga na Mchuchuma ni wimbo au ni mradi? Maana tumesema Liganga na Mchuchuma hadi tumezeeka na tunaenda kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Liganga na Mchuchuma tunaenda kufa, Liganga na Mchuchuma tunaenda kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe hakuna jambo lisilowezekana duniani. Hakuna jambo…

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Katani.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naye ameanza mapema huyu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Aah, ngoja, samahani, sijamsikia. Umesemaje Mheshimiwa Getere?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ameanza mapema. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nadhani katika watoa taarifa humu ndani unaongoza kwa hiyo, uvumilie tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Katani katani.

## TAARIFA

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa Mheshimiwa Getere kwa alichokisema. Tangu mimi nakuwa Mbunge mwaka 2015 mpaka leo, habari ya Liganga na Mchuchuma imekuwa ni maandishi ya kwenye makaratasi. Kwa hiyo, naunga mkono hoja yake tuone jambo hili linakaaje.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nakuunga mkono kamanda. Na ninapokea Taarifa yako…

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere unasubiri uitwe kwanza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa yake kwa sababu, ana uchungu na huo mradi. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Subiri kwanza Mheshimiwa Getere, usiwe na haraka sana.

Mheshimiwa Getere, unapokea taarifa ya Mheshimiwa Katani?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naipokea.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumza kwamba hakuna jambo ambalo haliwezekani duniani. Tumekuwa na wazo la kuja Dodoma toka mwaka 1972, lakini limewezekana. Nami nilikuwa kwenye Kamati, naona juhudi za mama katika huu mradi inawezekana. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Rais kwamba hii jitihada aliyonayo ya Liganga na Mchuchuma iwezekane kwenye hii miaka inayokuja. Kwa hiyo ikifika 2030 wakati Rais anaanza labda anataka kuacha au kama anataka kuendelea, basi mradi utakuwa umekamilika. Nimwombe sana kwa jitihada yake hii, ili

Liganga na Mchuchuma sasa zisifutike kwenye mawazo ya Watanzania, uwe mradi ambao unatuletea faida.

Mheshimiwa Spika, nizungumze habari ya viwanda vilivyotaifishwa na viwanda vilivyobinafsishwa. Wamezungumza wengi hapa. Hii nataka nitoe mfano na Wabunge wengine msikilize humu ndani, maana yake kuna watu wengine wakizungumza kwenye mikoa mingine tunakuwa tunagunaguna, mikoa mingine mna-*support*.

Mheshimiwa Spika, wamezungumza jana hapa Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Rukwa habari ya Ziwa Tanganyika, Wabunge tumewa-*support* na Serikali imewasikia, imekwenda kuwasikiliza. Tulizungumza sisi wafugaji ambao tulikuwa watu wanaofuga ng'ombe kuhusu mambo ya hereni, tumezungumza sana, Serikali ikasikia ikasimamisha mradi. Hivyo, wanapozungumza watu wa Tanga kuhusu eneo la Kiwanda cha *Tanga Cement* tuwasikilize. Kwa nini tusiwasikilize? Kwa sababu mikoa yote tumewasikiliza. Tuwasikiliza tujue nia yao ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natazama haya maneno yaliyokuwa yanaendelea hapa, kilichokuwa kinazungumzwa. Ukiangalia kwenye mitandao yote hili jambo limeandikwa, ukiangalia kila mahali hili jambo limeandikwa na ukilitazama vizuri liko kisheria. Kuna mahakama, kuna taasisi zetu, Tume ya Biashara na kuna Tume ya Mahakama, wamezungumza vizuri, wametoa maamuzi yao yanafuatwa. Kwa nini Serikali haitaki kuchunguza haya maamuzi?

Mheshimiwa Spika, kingine, amezungumza Mheshimiwa Shabiby hapa, inawezekana kabisa na siyo kuwezekana, ndivyo ilivyo, Kiwanda cha Tanga ndicho kina *deposits* nyingi miaka

milioni karibu 30 na Kiwanda cha Twiga kina mitambo mizuri sana hapa Tanzania. Sasa hapo upime uone; je, kitu gani kitahama, kama *Twiga Cement* itachukua kile kiwanda itachukua *clinker* na malighafi kutoka Tanga kuja Dar es Salaam au itapeleka mitambo mizuri ya Dar es Salaam kwenda Tanga? Waliangalie hili sana, waliangalie.

Mheshimiwa Spika, walipozungumza Wabunge wa Tanga maana yake tuna imani kwamba inawezekana wakaweka maboksi pale kikawa ni *godown* pale. *Clinkers* zote zikaja Dar es Salaam, *cement* ikazalishwa biashara ikaendelea, lakini itakuwaje kwa wafanyakazi?

Mheshimiwa Spika, katika viwanda, tuna aina mbili ya viwanda; kuna *labour intensive* na *capital intensive*. Kiwanda cha Tanga ni *capital intensive,* kiwanda chenye mtaji wa kati ambapo wafanyakazi wengi ni Watanzania, ndiyo wanaweza kutengeneza thamani ya mnyororo. Sasa leo tunaona kuuza ni sahihi, *cement* inaweza kutengenezwa hata katika maeneo yote ya Tanzania, lakini kwa sababu tumetawanya kwenye mikoa mbalimbali kila mkoa tunataka upate faida yake.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali iangalie watu wa Tanga, wananung'unika nini. naomba hili jambo Mheshimiwa Waziri asilichukulie kama kawaida. Maana yake nasikia mtu anasema ni kiwanda cha mtu binafsi, anauza, anafanyaje, hapana, viwanda vyote vilivyobinafsishwa vya Serikali ni lazima tukae na kuviangalia vinafanyaje kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba, Mheshimiwa Waziri namwamini sana, utawasikiliza Watanzania wanaonung'unika na utafanya maamuzi ili kiwanda kile kifanye kazi. Ni kweli mtu anayemiliki kile kiwanda hana uwezo, lakini ni kweli kama kuna

wazawa wanataka kumiliki kile kiwanda tuwaruhusu wamiliki hicho kiwanda kama wana uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo naomba tuendelee kuangalia hili jambo linafanyikaje.

Mheshimiwa Spika, wakati niko kwenye Kamati ya Viwanda, mara nyingi sana wamesema tunajenga *industrial park* Bunda. Wilaya ya Bunda na Mkoa wa Mara kwa ujumla viwanda vya samaki vimekufa, viwanda vya pamba vimekufa, viwanda vya maziwa vimekufa, yaani ule mkoa sasa umebaki ni hewa tu. Tunaomba sasa Serikali iangalie Mkoa wa Mara kwa maana ya viwanda vya samaki, maziwa na pamba. Vinginevyo ule mkoa umebaki hewa, hakuna namna. Kwa hiyo naomba Waziri ufikirie jambo hili la kutufufulia viwanda ili watu wapate fedha katika Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, kama muda utasalia tutamalizia na Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri wanayoifanya, kweli inaonekana. Niwapongeze sana uongozi mzima wa Wizara pamoja na Mheshimiwa Rais ambaye anawasimamia.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme machache tu, mambo kama manne. La kwanza, kuna eneo zuri sana na la kimkakati la kuweza kuweka kongani au kuweka *export processing zone* kwenye Jimbo la Vunjo, eneo lile la mpakani na Nchi ya Kenya

ambalo linaitwa Lokolova. Ni eneo ambalo limekuwa na migogoro kidogo kwa sababu ya wafugaji na wakulima wanapigana kidogo pale, lakini kuna eneo la zaidi ya eka 2,500 na Serikali tayari ina eka 140 ambazo zinaweza zikachukuliwa na zikaanza kutumiwa kwa kujenga kongani hilo.

Mheshimiwa Spika, naamini hilo litakuwa jambo la msingi kwa sababu litakuwa limefungua nchi yetu na mpaka wa Kenya pamoja na *South Sudan,* Djibouti na kadhalika ambapo naamini sehemu ile ilikuwa tayari pale Himo palikuwa pameibuka Soko la Kimataifa la *Grain,* ikawa ni *reference point* ya bei za mahindi na nafaka nyingine kwa nchi zote za kaskazini pale. Kwa hiyo naamini kwa vile zimepakana kuna eneo la kutosha, naamini kwamba Wizara itafikiria kuona mkakati wa kujenga kongani au *export processing zone* kama itawafurahisha.

Mheshimiwa Spika, kuna suala tulikuwa tunaizungumza sana la *ETS*. *ETS* naizungumza kwa sababu baadaye nitazungumza kidogo kuhusiana na uwekezaji pamoja na *Business Competitiveness Index* ya Tanzania. *ETS* sijui imekuja kuishia wapi, hatujui, sisi kama Wabunge hatujapata ripoti ambayo inaweza ikaturidhisha kwamba suala hili limekamilika na kwamba wanaviwanda wale ambao wanalipa hela nyingi sana kwa kutumia *electronic tax stamps* ambapo kweli ni kitu kimoja ambacho naamini hao watu watakuja kufidia gharama kwa walaji kwa kutumia hizo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo mwenzangu, Mheshimiwa Mnzava, amelizungumzia kidogo, kuhusiana na idadi ya viwanda. Nilipoingia hapa Bungeni mwaka 2021 tulikuwa tunaambiwa kwamba viwanda vilivyotengenezwa katika mwaka ule vilikuwa ni 8,000 sijui, sasa hatujapata tena hiyo idadi. Sijui vimefika vingapi sasa hivi, lakini inaonekana kwamba pengine ile

dhana ya kutaka kwamba kila mkoa au wilaya iwe na *specialization* fulani ya kiwanda chake ambacho Serikali itasaidia kuhimiza wawekezaji waweze kwenda kule kufanya na kupewa *incentives* ili waweze kuendeleza viwanda vile, sijui ile sera imeishia wapi.

Mheshimiwa Spika, niseme pia suala nyingine kwa harakaharaka kwa sababu yale ya jumla nitayasema mwishoni hapa, suala la *SIDO, TEMDO* na kadhalika wamekuwa wanajaribu kubuni mashine na vitendea kazi mbalimbali ambavyo vitasaidia kwenye ujasiriamali wetu; kwenye kilimo na kwenye viwanda na kadhalika, lakini nafikiri kwamba kazi ya ubunifu imekuwa ni ndefu sana, kama vile unataka ku-*invent a wheel,* unataka kuvumbua gari ambayo tunaona linatembea ambayo hata hayatushangazi sana sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sasa wewe unataka kuvumbua kwa kujenga, kutengeneza mwenyewe. Nafikiri kwamba wangekita nguvu zao sana kwenye kwenda kwenye maonyesho ya bidhaa za viwanda kwenye nchi hizi ambazo wana maonyesho ya muda mrefu kama China au India wanakuwa nayo, waone vitu gani halafu tu-*expose* vijana wetu kwa teknolojia ambazo zipo rahisi, *very simple* ambazo pia zinazaa matunda kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale kwenye jimbo langu kwa mfano nikiwaambia kwamba kuna mashine ya shilingi 200,000 ya kuchakata ndizi na kuweza kuzigeuza zikawa ni chipsi wanashangaa kwa sababu ni *cheap,* lakini pia unaweza ukatumia kwenye *scales* mbalimbali, *scale* kubwa na ndogo, lakini ukweli ni kwamba ukisema unabuni, *innovation* lazima tujaribu ku-*leverage* na ku-*leapfrog* kwenye vile vitu ambavyo viko sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la *TIC;* ukienda kwenye *website* yao unashangaa. Mtu anasema je, kuna fursa gani ya uwekezaji Tanzania wanasema iko fursa kwenye sekta ya *mining,* kwenye kilimo. Lakini huwezi kujitangaza namna hiyo, kwa kusema njoo kwenye *industry* au kwenye *mining* au kilimo.

Mheshimiwa Spika, nilitarajia kwamba kwenye *website* ya *TIC* ukiingia utakuta *a package of areas and projects* ambazo tayari zimefanyiwa tathmini na upembuzi yakinifu, lakini hawatoi *information* yote wanatoa *little/scant information* kwamba tumefanyia uchambuzi na huu uchambuzi umefanyika na wabobezi, ma-*investment bankers* au wachambuzi wazuri ambao wana *business analytics* zao.

Mheshimiwa Spika, twende tu hata hii ya Liganga na Mchuchuma, kuna Mradi wa kimkakati wa Liganga na Mchuchuma na *parameters* zake ziko hivi na hivi, *payback period* yake itakuwa hivi, *investment* itakuwa hivi na faida itakuwa hivi. Kwa hiyo unakuwa ume-*package* hii miradi ya kimkakati kwa kuweka *information* ambayo wewe umeshaifanyia tathmini na upembuzi.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni hili; hakuna mtu yuko nje ya Tanzania anayeweza akaufanya tathmini mradi mkubwa bila kutumia hela nyingi sana. Kwa hiyo inawa-*put off,* lakini akikuta kwamba imeshafanyika kuna *basic information* ambayo inaweza ikam-*lead* yeye kupeleka pesa inakuwa rahisi kwake kusema, *okay,* najua hiki, hebu ngoja nipate hiyo *package,* nitanunua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo atakulipa wewe *TIC,* wewe Wizara uliyetengeneza hiyo *feasibility study* halafu atakulipa ili achukue ile *package* yeye mwenyewe akaiangalie, akafanye *stressing testing* zake halafu aseme anapeleka hela yake

Tanzania kwenye Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Hiki siyo kitu ambacho ni siri. Kama unajiuza useme unafanya siri, watu wanasema huu mchakato wa kupata wawekezaji wa Liganga na Mchuchuma inakuwa siri kabisa, huambiwi kuna nini *on the table, what is on the table.*

Mheshimiwa Spika, kwenye kila sekta kuna mradi wa kimkakati ambao ukifanyiwa uchambuzi halafu ukawekwa kwenye *package* yetu ya kujitangaza, siyo kusema hapana njoo tu kuna *tourism. Tourism is not enough,* sema ukija kule kuna eneo limekuwa *identified* unaweza uka-*invest* kwa kiasi hiki cha pesa na *return* yako itakuwa hivi. Kwa hiyo hiyo itakuwa ni rahisi sana kupata wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni kwamba huwezi kuwa tu na Mheshimiwa Rais anayekimbizana, anapata *pledges* za miradi, watu wanasema watakuja lakini unaona kwamba hawaji, kwa nini; kwa sababu mpaka wanze sasa kutafuta *information. From where?*

Mheshimiwa Spika, nilifikiri kwamba kila mahali anapokwenda Mheshimiwa Rais au viongozi wetu wa juu wa Serikali wakasema kama kuna *investors* wanataka kuja Tanzania basi iundwe timu ya *investment bankers* au *relationship managers* ambao watakuwa moja kwa moja wanafanya *direct communication* na wale walioonesha nia ili wale watu waone kwamba wana *contact person* ambaye akitaka kumwona Rais yule jamaa yupo, atanipeleka. Kwa hiyo itakuwa ni rahisi sana kupata hawa watu, lakini tukikaa tu kimya hivi, haitakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala la *blueprint. Blueprint* ni nzuri, tumeitengeneza yetu wenyewe, tunasema tufanye hivi tutapanda, lakini mpaka tutengeneze *blueprint actually*

tumeshuka kwenye *Business Competitiveness Index*. Ya mwisho ilikuwa 2019 kwa sababu baada ya UVIKO hawakufanya, lakini ukweli ni kwamba hii *Business Competitiveness Index* ya *World Bank* ina vigezo 98 lakini vinajikita kwenye maeneo 12.

Mheshimiwa Spika, tungejaribu kupitia hivyo vigezo vinavyotumika *internationally* ambavyo vimewekwa kama *standard,* tujaribu kupitia na tulinganishe na vile vyetu vya *blueprint* ili tuweze kukamilisha, kila mtu amepewa kazi yake, wewe fanya hivi, mwingine afanye hivi, tunamaliza tunaweza kuona kwamba nchi yetu ina-*move* kutoka 118 kwenye *index* ile, ije hata kwenye 70. Turudi kule, siyo tuendelee tu tunatengeneza *blueprint,* lakini tunaona kwamba bado hatujaweza ku-*improve* mazingira yetu ya biashara kwa maoni au kwa macho ya wawekezaji kutoka nje. Kwa hiyo naamini tukiweza kufanya hivyo tutaharakisha mambo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niseme hivi; kuna suala hili la masoko, sasa inakuwa ni vigumu kujua hata masoko yako wapi. Kwa mfano lile soko lililoanzishwa pale *Stock Exchange* linaitwa *Tanzania Mercantile Exchange,* linatoa fursa nzuri kwa wakulima wetu kujua bei gani wauze mazao yao kwa sababu vigezo viko pale, siyo hii ya kwenda mmoja mmoja kutafuta. Tujaribu kuingiza mengi kwenye *stock exchange,* lakini ninachosema ni hivi; mpaka sasa hivi hatujaelewa kama masoko yako kwenye Wizara hii ya Viwanda au yako kwenye Kilimo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kimei, sekunde 30.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoitoa Bungeni leo. Nina imani tunampongeza pia kwa kuwa ni Waziri ambaye anafanya kazi kwenye mazingira mazuri sana ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri afungue nafsi, tunamtegemea sana kukuza wafanyabiashara, hasa wazawa wa Tanzania, kwa kipindi hiki ambacho nadhani ana uhuru mkubwa sana wa kuwasikiliza watu na kuamua. Tatizo ni kwamba Wizara haimalizi matatizo ya wafanyabiashara, yaani imekuwa kama ni mahakama, nenda, rudi, njoo kesho au keshokutwa. Nimwombe Waziri asiyakimbie matatizo ya wafanyabiashara. Wafanyabiashara wana matatizo mengi sana, wanategemea busara ya Waziri na yeye ni daktari na madaktari huwa hatukimbii matatizo, unakabiliana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nizungumze kidogo Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hapa aniambie. Tuna kampuni inaitwa *SICPA*, anaifahamu, inafanya kazi ya kuweka stika kwa ajili ya kukusanya kodi ya *TRA;* wafanyabiashara wamemlalamikia sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri afikirie mkataba waliouweka miaka mitatu iliyopita, kila kizibo kimoja cha juisi inayotengenezwa Tanzania anakusanya shilingi nane na Serikali inapata shilingi sita. Mtu wa kuja na *briefcase* anachukua shilingi nane. Waziri anatambua mkataba wao umeshaisha miaka mitatu. Bado wameongeza muda na wazawa ndio wanafanya

hiyo kazi. Swali langu ni kama lilelile la jana, najiuliza hivi kweli wasomi wetu wa Tanzania waliosomea mambo ya *IT* wameshindwa ku-*copy* ule mfumo tukauendesha wenyewe? Kwa sababu na mkataba unasema ile mali imeshakuwa mali ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, najua wakati wanasaini mkataba walipunjwa kwa sababu labda kulikuwa na viwanda 19, leo tuna mia na kitu. Kiwanda kimoja tu nimefanya mfano wa Azam, anachukua karibu milioni 300 mpaka 400 kwa siku. Ukienda viwanda vilivyoongezeka mia mbili na kitu mwaka jana peke yake kaondoka na shilingi bilioni 100 na wazawa na makampuni mengine yako Tanzania yanakwambia tuko tayari kuendesha huu mfumo kwa shilingi moja, Waziri ameng'ang'ania nini kwenye shilingi nane? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu anayekuchaji wewe Tanzania shilingi nane…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, kampuni hiyo inayofanya kazi hiyo ya kuweka stempu inapewa leseni na Kampuni ya Serikali inayofilisika ya Posta. Posta wangeweza kufanya kazi hii na pesa zote zikaenda Serikalini. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naipokea. Darasa la saba huwa tuko *active* sana; nampongeza Mheshimiwa Hamis. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii kampuni inayochukua kazi hiyohiyo shilingi nane Tanzania, inafanya kazi Kenya kwa shilingi moja, inafanya kazi Uganda kwa chini ya shilingi moja. Sasa mtu huyu bado anaongezewa mkataba. Mkataba umekwisha, ongeza tena mwaka mmoja.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Tuamini kwamba Watanzania hatuna uwezo wa kuuendesha huu mfumo.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mfumo ni mali yetu, halafu tunaweka wakala tu katikati, mtu *briefcase,* anakusanya hela anapeleka Ulaya, halafu huku tunang'ang'ana kukamata mabegi ya watu huko Kariakoo wamebeba vijora viwili, vitatu. Hili… *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka nimpe msemaji taarifa kwamba kulingana na utafiti uliofanywa pamoja na kushirikisha *Federation* ya Wenye Viwanda Tanzania, kampuni hii Tanzania ndiyo nchi peke yake Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa kutoza fedha nyingi zinaoumiza

viwanda na Watanzania katika kugonga stempu za kielektroniki kwenye bidhaa. *Federation* ya Wafanyabiashara wameshapeleka *concerns* zao Serikalini, lakini ninachoshangaa kampuni hii bado imeendelea kukumbatiwa katika Taifa letu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naipokea.

Mheshimiwa Spika, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri; kweli hatupendi aondoke au kuharibu huu mfumo, lakini sasa hivi *margin* ni kubwa. Viwanda 19 kwa viwanda 200, halafu hela zote zinakwenda nje, Wizara inachukua shilingi sita, mtu kati shilingi nane, inahitaji kwenda shule kweli? Si bora muwe Madokta kama mimi wa wa heshima tu tumalizane huko? Jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wamekuja kwa Mheshimiwa Waziri, wameshakaa vikao zaidi ya kumi; ugumu uko wapi kuchukua maamuzi? Watuambie nani yuko nyuma ya mchezo huu, kwa sababu ni suala ambalo kwa mtu wa kawaida ukielezwa unajiuliza tu mara mbili, hata nikikataa kupunguza, wafanyabiashara wanasema tupunguze turudishe hata shilingi tatu wamemwambia, barua tunazo hapa, lakini Kiswahili, *come tomorrow,* wafanyabiashara mwisho wake labda wanasema kuna mtu nyuma yake. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwombe Waziri, asiyakimbie matatizo, yeye ni daktari wa akili, wa kisomo. Amalize matatizo ya Watanzania wafanyabiashara wafanye kazi kwa uhuru. Mheshimiwa Rais anafungua masoko, wafungue uwanja wa kusikiliza watu na wawe na tabia ya kumaliza matatizo. Hatuna sababu ya kuja kupigizana kelele humu ndani, wala hatuhitaji tutajane, Hapana. Kama kuna mtu yuko nyuma ya mchezo

amekula ametosha, watu wameshanawa, matongotongo yameisha, tuanze upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, maana hata Wabunge tu kwa hili somo la muda mchache la Dkt. Musukuma hapa, wameelewa mchezo unaendaje. Sasa unahitaji kutumia *degrees* mbili mpaka tatu kwenye hili? Haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, nazungumzia suala la wafanyabiashara kulalamika kuhusu *TRA*. Tunajua Mheshimiwa Rais akitamka watu wa viwanda na biashara wafanye kazi ya kukamilisha ndoto ya Mheshimiwa Rais. Alipokuwa Bukoba alisimama kwenye *mic* akawaambia *TRA* msisumbue watu madeni ya miaka mitatu au minne nyuma. Mpaka leo bado wanasumbuliwa, ukiwauliza *TRA* wanasema hatujapata maelekezo kutoka Serikalini. Sasa wanataka watu wakimwona Rais wetu anazungumza tuamini kwamba wao hamna uwezo wa kutekeleza? Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, afanyie kazi matatizo ya wafanyabiashara ili aweze kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nazungumza kwa uelewa wangu na sitaki taarifa kuhusiana na *Tanga Cement*. Unajua sheria mbovu ndiyo zinatufukuzia wawekezaji. Najua kila mtu ana wasiwasi, lakini lazima Wabunge tuwe na akili za kufikiria mara mbilimbili. Hili suala la *Tanga Cement* kuna mchezo tunachekechwa, ama humu ndani au huko nje, kuna mtu pia yuko nyuma.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia watu waliofungua kesi ya *Tanga Cement* kuna kampuni inaitwa *Chalinze Cement Limited*. Nataka waniambie hii kampuni iko wapi. Nataka waniambie Kiwanda cha *Cement* cha Chalinze kiko wapi. Tanzania hii mimi

ni mwenyeji, hiki kiwanda kiko wapi? Watu wana kiwanda mfukoni halafu wanakwambia kiko Chalinze. Nimetoka Chalinze juzi, nimezunguka Lugoba yote sijaona, na Mheshimiwa Ridhiwani yumo humu, nimemuuliza kiwanda kiko wapi, Mbunge hajui. Aasa huyo Chalinze ni nani anayetufungulia kesi? Maana yake tunachekechwa hapa, tusioneone aibu, tusitembeze dili humu ndani Waheshimiwa Wabunge. Chalinze na Chama cha Kutetea Walaji kiko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani tunatengeneza hofu, wanatengeneza utawala bora halafu wanajenga tabia mbaya. Mtu anawaambia mimi nimefilisika, nauza mali yangu, kama sheria ni mbovu, haya, akifunga tutauza skrepa? Wanampeleka wapi? Akiamua kufunga sasa mmezuia nisiuze. Nashauri, inawezekana hawa wenzetu wakati mwingine ni wajanja, wanatukwepa tusipate kodi ile ya zuio. Serikali isimamie mchakato, lakini hawa wacheza dili Waziri akija hapa najua anashughulika na hili suala, naomba atutangazie humu Bungeni hicho kiwanda cha Chalinze kiko wapi.

Mheshimiwa Spika, Wabunge ni wafanyabiashara; mimi ni Chalinze ninayefungua kiwanda cha *cement,* lazima nijue mkubwa ambaye nitashindana naye ni fulani, halafu anafilisika mimi nasema hapana, usifilisike, wakati mimi ndio nataka kufungua kiwanda. Jamani, hizi dili zitatumaliza Tanzania, lazima tutumie akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri akija hapa aje na majibu mazuri, tusije tukaharibu *image* ya nchi yetu kwa wahuni wanaotembea na *briefcase* kwenye kwapa, hatuwezi kuishi kwa madili. Mshindani wako unamwoneaje wivu kufilisika mpaka ukafungue kesi, ulishaona wapi hii? Kama sheria tulitunga mbovu tuacheni kutembea na madili kwapani jamani, tutetee Tanzania.

Rais anataka wawekezaji tumwache aoneshe ndoto zake, tutaulizana baadaye, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kikao chetu cha leo. Nitaje baadhi ya Wabunge ambao tutaanza nao mchana.

Waheshimiwa Wabunge, sitachoka kuwakumbusha, nimejitolea kwa hilo, wala sina wasiwasi. Waheshimiwa Naibu Mawaziri hapo nawaona, tusikilizane.

Nitatangaza majina ya baadhi ya watakaoanza kuchangia tutakapokutana alasiri; Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, wengine wataendelea kutangazwa kwa kadri uchangiaji utakavyokuwa ukiendelea.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji,Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji. Wakati tunahitimisha Bunge, tulimtaja Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, na wakati huo Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos na Mheshimiwa Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela wanajiandaa.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kuifanya katika Taifa letu. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kazi na namna ambavyo wanamsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo matatu ya kuzungumza kwenye Wizara hii. Jambo la kwanza ni namna ambavyo bado tunaendelea kuagiza bidhaa mbalimbali kutoka nje ya nchi ambazo tuna uwezo wa kuzizalisha ndani ya nchi yetu. Hili nimekuwa nikilisema sana. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wakati anaeleza hapa asubuhi amejaribu pia kuelezea jinsi ambavyo bado tunaagiza mafuta ya kula, bado tunaagiza ngano, tunaagiza vitunguu, na tunaagiza vitu vingi sana kutoka nje ya nchi, ambapo vitu hivi tuna uwezo wa kuvizalisha wenyewe ndani ya nchi yetu kupitia mashamba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikishauri sana, yako mashamba makubwa ambayo walipewa wawekezaji miaka ya nyuma wayaendeleze. Wawekezaji hawa wameyatelekeza mashamba haya. Unakuta mtu amepewa shamba ekari 40,000, ekari 30,000, lakini kwenye ekari 40,000 huko anatakiwa alime ngano kwa asilimia 100, halimi hiyo ngano. Ekari 40,000, anaishia kulima ekari 3,000 au 2,000. Ekari 38,000 anatelekeza, ameacha. Unakuta kwenye shamba hilo la ekari 40,000 yeye mwenyewe anakodisha wananchi wanaozunguka maeneo hayo ekari 5,000, shamba linalobaki lote ameliacha. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, nenda kwenye mikoa mikubwa kama Morogoro, Tabora na Mwanza, mashamba yametelekezwa. Kule Misungwi kuna shamba la vitunguu, *scheme* ya umwagiliaji nzuri kabisa ambayo Mwisraeli alitutengenezea vizuri, sasa imetelekezwa, hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, haya mashamba Watanzania wako tayari kuyaendeleza, na hata kama sio Watanzania, wako wawekezaji wenye uwezo na *vision* ya kuendeleza haya mashamba, na wana nguvu, wana mtaji wanaweza kuwekeza. Hao wawekezaji ambao hawawezi kuwekeza hayo mashamba, watupishe tuweke watu wengine. Sasa hili limekuwa kama wimbo, tumekuwa tukilisema sana, lakini hatuoni Serikali ikizichukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Kanda ya Ziwa na Mwanza kwa ujumla tunahangaishwa sana na kitu kinachoitwa mfumuko wa bei. Bidhaa za Viwandani zimekuwa zikipandishwa bei na wafanyabiashara na zinawaumiza watumiaji wadogo wadogo kule vijijini. Unakuta kitu kama nondo, milimita kumi sasa hivi ni shilingi 18,000 mpaka 20,000, mwingine anauza shilingi

21,000 au shilingi 22,000, lakini ni kuanzia shilingi 18,000 mpaka shilingi 22,000. Nani anayedhibiti hii bei ya nondo kule kwa mtumiaji Busongo, Nunduli, Serengeja mpaka Mwaulile? Kwa sababu mtu anajiamulia kutengeneza bei yake anayoitaka mwenyewe, anakwenda kuuza sokoni, na anayeumia ni mwananchi wa mwisho kabisa kule kijijini ambaye bei hi inamuathiri moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi tulikuwa tunazungumza hapa habari ya *Tanga Cement*. Sisi kanda ya ziwa hatuna kiwanda cha cement. Tunategemea sana *Tanga Cement* ambao ndiyo majirani wetu wa karibu kutuletea kule *cement* kule Tanga. Nimejitahidi kuangalia kwa nini hii kelele imetokea pale asubuhi? Nilichojifunza ni mambo matatu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga katika hali hiyo inayoendelea sasa hivi, ile *deposit* ya Tanga ambayo inachimbwa sasa hivi, inakwenda kuwa machimbo, kwa sababu watu watachimba ule mzigo, watapeleka Dar es Salaam kwa ajili ya cement. Kwa kuwa mahitaji ya Dar es Salaam ni makubwa sana, maana yake huyu mwekezaji anayetaka kununua kile kiwanda atawekeza kule nguvu zaidi ya kwenda kuchimba *material* na kupeleka Dar es Salaam kwa ajili ya *production*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo naliona hapo, kwa nini tunashindwa kuweka wazi jambo hili? Kwa sababu viwanda hivi ni miongoni mwa viwanda ambavyo vilikuwa ni vya Serikali. Kule Tanga kuna viwanda viwili vya chuma ambavyo wawekezaji wameshindwa kuviendeleza na Serikali imevichukua. Ukienda kule Moshi kuna viwanda vya mbao na miti, wawekezaji wameshindwa kuviendeleza, Serikali imevichukua. Halikadharika Mwanza, halikadharika Arusha. Sasa najiuliza swali dogo tu, kwa

nini hiki kiwanda, kwa masharti hayo hayo ambayo walipewa mwaka 1997, kwa nini hiki kiwanda kisirudi Serikalini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hawa wawekezaji ambao tuliwapa kwa nia njema wameshindwa kukiendesha kiwanda na kukiendeleza, wamefilisika, kama mlivyofanya Wizara ya Uwekezaji kuchukua vile viwanda vya wengine kupitia Msajili wa Hazina, kwa nini msifanye hivyo hivyo kwenye kiwanda hiki, mkarudisha Serikalini, halafu Serikali ikamlipa huyo mwekezaji aliyeshindwa kuendeleza, halafu ikatafuta mwekezaji mwingine ili kupunguza hizi kelele ambazo zimekuwa zikiendelea katika Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu nililoliona, tutakaporuhusu kiwanda hiki kimilikiwe na mtu huyo huyo mmoja, kwa sababu tunafahamu viwanda vikubwa katika nchi hii viko vitatu. Kiwanda hiki cha Tanga, Twiga pamoja na Dangote, washindani wakubwa wawili sasa ukishajumlisha hicho kiwanda kikawa kitu kimoja, tafsiri yake ni kwamba, ushindani hautakuwepo, kwa sababu huyu mtu atakuwa anajipangia bei anavyotaka yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei anayoiamua yeye; leo tunanunua cement kule Mwanza shilingi 24,000 mpaka shilingi 25,000. Tutakapompa dhamana ya kumiliki na kiwanda kingine kiwe kimoja, tafsiri yake ni kwamba, akiamka akasema bei ni shilingi 40,000, hakuna wa kushindana naye kwa sababu ndiye mwenye viwanda vikubwa kwenye nchi yetu. Sasa huu ushindani tutaufanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba jambo hili Wizara iingilie kati, ione namna ambavyo inaweza ku-*rescue situation* hii ili sisi watumiaji wa mwisho kule chini kwa wananchi, tuweze kutumia gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ajitahidi sana yeye na Wizara yake kulinda wawekezaji wa ndani. Kumekuwa na changamoto nyingi sana. Wawekezaji hawa wa ndani wanapata misukosuko midogo midogo huko kwenye zile taasisi za Serikali. Shida ni kwamba, Mwafrika ukipata hela, unaulizwa maswali milioni moja kuliko angepata hela mtu mwingine ambaye sio Mwafrika. Yaani ni kwamba, kuna watu, kikundi kidogo kimejimilikisha fedha nchi hii, kiasi kwamba akija mtu mwenye hela mpya, maswali atakayoulizwa ni mengi kuliko uwekezaji alioufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mtu aliingiziwa fedha, shilingi milioni 500 kutoka kwenye akaunti ya Mheshimiwa Kingu, maswali atakayopigiwa na Benki Kuu, ni afadhali akaingiziwe hiyo milioni mia tano akiwa Uganda. Utaulizwa fedha inatoka wapi? Yaani hata wao hawajui fedha inatoka wapi. Fedha huwa inatoka benki, kwenda benki. Ukinikuta na fedha nyumbani kwangu, hapo chukua hatua, lakini kama Mheshimiwa Kingu ameingiza fedha kutoka benki kwenda benki, unauliza maswali gani, kwamba fedha inatoka wapi? Fedha huwa inatoka benki inakwenda benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana, wawekezaji wa ndani, watu wanajitahidi sana kuwekeza ndani ya nchi yao, lakini vikwazo na ukiritimba umekuwa ni mwingi sana, kana kwamba hawana uwezo wa kuwekeza kwenye Taifa lao. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri hilo nalo ulitazame kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, baadaye atafuatia Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sisi wote Afya njema tuko hapa kwa kuisaidia Serikali yetu chini ya Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, mwana mama shupavu ambaye ana nia nzuri ya kuhakikisha uchumi wa nchi yetu unakimbia. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nina hoja yangu ya viwanda vilivyobinafsishwa. Mwalimu Nyerere alivitengeneza viwanda hivi kwa kanda maalum, na alihakikisha kila kanda uchumi wa kikanda unakwenda vizuri. Mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani tulikuwa na viwanda vya korosho 13. Viwanda vyote vimebinafsishwa na waliobinafsishiwa wamekaa navyo kwapani, hakuna wa kuwauliza wala wa kuwahoji. Wananchi wa Mikoa hii hawana ajira, na matokeo yake sasa hivi akina mama na vijana wameamua kutafuta vijimtaji vidogo vidogo, ndiyo vinaitwa viwanda vidogo vidogo, wanabangua korosho. Hii imetokana na bei ya korosho kuwalalia vile vile wale ambao wamechukua viwanda vile, ndio wanaonunua korosho kupeleka nje. Maana yake ni kuwa, uchumi wa Tanzania unachezewa na wafanyabiashara wakubwa wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na viwanda Mkoa wa Tanga; Viwanda vya Gossage, viwanda vya chuma, viwanda vingi vya kutengeneza mpaka *biscuit* Tanga, leo *biscuit* tunaagiza kutoka nje, pipi tunaagiza kutoka nje. Halafu mnasema Tanzania

tunataka tuondoke na kuendelea katika uchumi wa kimaendeleo wa viwanda, ni pagumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi inaangamia sasa hivi kwa kuletewa vyakula vibovu. Tunaona katika mitandao, *chocolate* inafunguliwa imewekwa dawa ndani. Hizi dawa ni za kuwaangamiza vijana wapate *hormones* mbaya na zile *hormones* zitawafanya kuwa mashoga, na wakiwa mashoga watakuwa hawawezi kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pipi, *biscuit, juice* mpaka maji na mafuta ya kula, lakini leo unashangaa kibali kinapita cha kuingiza mafuta *tones of tones,* lakini viwanda vyetu vyote vimefungwa. Nenda Shinyanga, tulikuwa tunakula mafuta mazuri ya *Okay*. Tulikuwa tunakula *Super Ghee* Tanzania, tulikuwa tunakula *Tan Bond* na tumepeleka mpaka nchi za Jirani. Ziko wapi *Tan Bond*? Iko wapi *Super Ghee*? Iko wapi *Okay*? Matokeo yake tunaagiza mafuta kutoka nje, haiingia akilini kwa Watanzania kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanakosa ajira ya viwanda vyao, tunawaachia wafanyabiashara ambao wanasema wamewekeza, halafu vitu vyote, leo *material* zinapelekwa nje, wanatuletea mafuta machafu ambayo yanabadilisha afya za Watanzania. Hii haikubaliki. Kwa kweli inabidi tusage meno na tutafute mazingira magumu ya kuikwamua nchi. Pipi inatoka India, *chocolate* inatoka China, *juice* zilizoharibika viwandani, zilizo-*expire* wanazibadilisha *dating* wanazileta Tanzania. Jamani tunawahurumia watoto hawa? Tunaiuhurumia nchi? Mimi leo lazima niseme ukweli maana yake napita kujiuliza kwa miaka yote 20 tunazungumza neno hili hili, lazima lifike mwisho. Hili neno la kuagiza kila kitu kutoka nje,

mpaka *tooth pick* inatoka nje, lazima ifike mwisho. Jamani, *enough is enough.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile viwanda vilivyofungwa, Wabunge ninyi nyote tuungane kwa pamoja tumsaidie Mheshimiwa Rais. Rais anafanya kazi, sisi tunafanya nini humu ndani? Kazi tuliyokuwanayo ni moja, tumuunge mkono kwa kuhakikisha tunaazimia kwa pamoja, tuiombe Serikali walete taarifa katika Kamati ya Viwanda na Biashara, wawekezaji wote ambao wamewekeza sugu na viwanda havifanyi kazi na wamekaa navyo na baadaye havifanyi kazi na kuhakikisha ajira hamna, kuwa tunawaonea aibu, aibu gani wakati wote ni matajiri. Tunashindwa kutoa ajira! Nenda Mkoa wa Lindi, aibu tupu! Hatuna kiwanda hata kimoja. Tunategemea kiwanda cha korosho, nacho kimefungwa. Aliyefunga nani? Mimi na wewe hatujui. Kwa nini tufikie hapo? Kwa nini tumwache mwananchi wa Nangaro hana kazi? Kwa nini tuwafanye akina mama na vijana hawana kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna vijana ndekejo ambao wanahangaika hapa wamemaliza vyuo vikuu hawana kazi, viwanda vimefungwa; na mtu aliyevifunga anakuwa na ubavu wa kusema hakuna wa kuniambia nifungue kiwanda hiki. Kweli nchi hii ya kweli ilimkomboa Mwafrika na Mtanzania kweli! Ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, azimio langu, au ushauri wangu, Serikali sikivu itumie *TR* kuhakikisha anapeleka katika Kamati taarifa yote ya viwanda vyote vilivyofungwa ili wajulikane kwa nini wanaleta kiburi hiki? Pia alipe faini, maana yake haiwezi kuacha kwa kumhoji tu, amekaa miaka mingi, miaka nenda miaka rudi hakifanyi kazi, na ametumia nafasi hiyo kuchukua mikopo benki, lakini wanachi hawana ajira. Hivi vitu lazima

tukubali kwa pamoja. Tuungane Wabunge wote kwa pamoja tuwe na azimio moja la kuhakikisha viwanda vinafunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Pwani tunatengeneza chumvi, tuna viwanda vya chumvi. Lindi chumvi, Mtwara chumvi, Tanga Chumvi, na Pwani chumvi. Amekuja mwekezaji, anawekeza kiwanda cha chumvi, analeta chumvi kutoka India. Mheshimiwa Rais mpendwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan alikuja Lindi, akasema, ninajua kero ya Lindi ni chumvi. Naomba ufumbuzi upatikane. Mpaka leo, chumvi inaletwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watu wa Lindi wamekaa na chumvi, watu wa Mtwara wamekaa na Chumvi. Uchumi wa Pwani ni chumvi. Leo chumvi inatoka India mpaka inafika Tanzania, inaachwa chumvi kutoka Kilwa *tones of tones,* watu wamechukua mikopo mpaka wame-*paralyze,* wanauziwa majumba yao, lakini chumvi zimewajalia majumbani, hakuna mahali pa kupeleka, eti kisa, mwekezaji ametafuta soko la Tanzania na kuhakikisha anatumia soko la Tanzania kupeleka chumvi Burundi, kupeleka chumvi Rwanda, kupeleka chumvi Zambia, kupeleka chumvi Uganda. Sisi wetu Watanzania masikini, watu wa chini wanahangaika na chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na Mkutano wa Madini, nikaenda pale, wananchi wanasema je, mikopo hii mtaifanyaje? Tumechukua mamilioni ya mikopo benki. Benki, wao wanaweka riba tu, na riba ikifizidi wanauza nyumba yako. Chumvi iko ndani. Hili siyo la kuliachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Mwanza analia, Mbunge wa Tanga analia, Mbunge wa Kagera analia, sasa

tunakwenda wapi? Hatuna maamuzi. Bunge hili liwe *strong,* Bunge la kufanya kazi lililotuleta hapa, tumkomboe mwananchi. Mwananchi huyu ndiye aliyetufanya sisi hapa tukaitwa Wabunge. Kama tutakuja hapa hatujawasaidia wananchi wale, kwa kweli tumehangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la mwisho. Mimi natoka Lindi, nataka nipate majibu, Kiwanda cha Korosho cha Lindi, maana yake kwanza ndiyo eneo la kujidai, kinafunguliwa Lini? Kiwanda cha Tandahimba kinafunguliwa lini? Majibu hayo yawe na muda, siyo nikae hapa mpaka mwaka mzima, kesho tena nianze na biashara hii, siwezi nikakubali. Kwa kweli inanikirihisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dharau tunavyodharaulika watu wa kusini kuonekana masikini, hatuna viwanda. Viwanda vile vilikuwa vinaajiri watu 3,000, leo hakuna hata mtu mmoja, vimefungwa, mashine zote zimetolewa. Kama mnabisha hapa, tuondoke twende Lindi tukafungue viwanda mwone kama mtakuta mashine ndani ya vile viwanda. Wame vinyofoa na hakuna wakumwuliza chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Riziki Said Lulida ahsante sana kwa mchango wako. Tayari nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, wakati huo Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, anajiandaa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipatia nafasi niweze kusema yale yanayojiri kwenye Wizara hii. Kati ya Wizara ambayo tuliitegemea

na Watanzania wameendelea kuitegemea kwa ajili ya kuongeza ajira; na pili, kwa ajili ya kuongeza uchumi wa Watanzania na uchumi wa Taifa letu ni Wizara hii ya Uwekezaji, Viwanda pamoja na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala zima la viwanda na ambalo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema. Mwaka 2022 Serikali ilihamasisha Watanzania wa Mikoa mitatu; Dodoma, Singida na Simiyu, kwenda kuwa Mikoa ya Kimkakati ya kulima zao la alizeti ili tuweze kuondokana na wimbi kubwa la uingizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walihamasika na wakaomba ili waweze kutekeleza mkakati huo wapatiwe mbegu na vitu vingine. Pamoja na changamoto zote zilizokuwepo kwenye upatikanaji wa mbegu na pembejeo, wananchi hawa walifanya. Vile vile wakati tunapitisha bajeti, tuliondoa kodi kwenye mafuta kutoka nje ya nchi. Wananchi wetu wakalima alizeti, watu wa viwanda vya kuchakata mafuta, wameamua kupunguza bei ya mazao ya kuchakata mafuta hususan zao la alizeti. Baada ya kupunguza bei, wananchi wanaona hakuna sababu yoyote ya kuendela kulima zao la alizeti ambapo wanatumia gharama kubwa kwenye uzalishaji, likija suala zima la mapato, hawapati kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kisingizio wanachokileta leo na Mheshimiwa Waziri amekisema eti kwamba watu hawa wamefunga viwanda kwa sababu ya ukosefu wa malighafi za viwanda vyao. Hivi leo nani anaeweza kwenda kulima atumie laki tano kwenye heka moja aje avune magunia 20 aende akauze kwa elfu Sitini? Ni nani huyo anaeweza kufanya kitu cha namna hii? Kwa hiyo, kosa ni la Serikali ambao ninyi wenyewe mnaleta

hapa mnatushawishi Wabunge tupunguze kodi kwenye mafuta halafu mnaendelea kutoa vibali vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, leo wafanyabiashara wote wa Sekta ya mafuta ya kula wameamua kuagiza mafuta nje kwa sababu kodi yake ni ndogo na faida yao ni kubwa, mazao ya alizeti yanateseka mtaani yako kule wananchi hawana mahali pa kupeleka. Sasa, kwa nini tunafikia kwenye hatua hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kuanagalia kwenye viwanda vyenyewe bado hatuna viwanda vya kutosha ndani ya taifa letu. Leo ninapozungumza hapa Serikali yetu ama nchi hii hatuna viwanda vya kutengenezea hata vifungashio. Leo vifungashio vya kila zao tunatoa Kenya, vifungashio hivyo zao la Parachichi leo *box* tunachukua Kenya na wananadika *Product from* Kenya wakati parachichi inatoka Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchele leo wa Kyela Kifungashio kinatoka Kenya unaandikwa ni mchele wa Kutoka Kenya wakati ni mchele wa kutoka Tanzania Kyela. Hivi hata vifungashio? Viwanda leo tuna mashamba ya miti yako pale Iringa ya kutengeneza makaratasi ndio tunaagiza vifungashio kutoka Kenya? Waziri, tunakuomba tafadhari kama kuna sehemu ambayo unatakiwa uwekee mkazo ni kukuza na kutangaza bidhaa zetu. Anza na viwanda vya vifungashio, tangaza nchi yako, tangaza bidhaa yetu ili tuweze kuondokana na huu urasimu ambao tunafanyiwa na nchi za wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la leseni. Imekuwa ni muda sasa na ni changamoto kubwa kwa wananchi na wafanyabiashara wetu wadogo wadogo kule chini. Leseni unakata lakini unatakiwa kuihuisha kila mwaka kitu ambacho kinakuwa ni kero kwa wafanyabiashara wetu. Hata

hivyo, kila ninapouliza naambiwa suala la kuhuisha leseni ili kuwatambua wafanyabiashara waliopo kwenye eneo husika ama tulionao nchini. Nikawa najiuliza hivi ni kwa nini Vitambulisho vya Taifa hatuhuishi kila mwaka ili tujue nani kafa, nani yupo, nani kahama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama suala ni kutambua na kujua kwa nini vya taifa hatuhuishi kila mwaka? Leseni ambayo watu hawa wanajenga uchumi wa Taifa lao, wanalipa kodi kwa Taifa lao, leseni wanalipia lakini leseni hiyo kila mwaka umsumbue mwananchi huyu Kwenda kupanga foleni Manispaa kutafuta leseni. Hata hivyo, kwenye suala la leseni hilo hilo, tulisema hapa mfanyabiashara anaeanza biashara asikadiliwe kodi mpaka kipindi cha miezi sita afanye kwanza biashara. Kinachofanyika kwa uhalisia ulioko huko chini sio kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili upate *TIN* ni lazima uwe na leseni ambayo umetoka nayo Manispaa. Ukiwa na leseni ukienda kupata *TIN* ni lazima ukadiliwe. Vilevile, wanakukadilia kwa miezi hiyo ya huko nyuma. Kwa hiyo, ukishakadiliwa ni lazima ulipe hakuna namna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mfanyabiashara akishindwa kulipa anaandikiwa deni. Hilo deni linakwenda mwisho wa siku mnakwenda kufunga biashara za wafanyabiashara na mara mnapeleka kesi Mahakamani, kuzimaliza hamzimalizi, watu wanaendelea kufirisika ndani ya Taifa hili, halafu tunasema tunataka kutengeneza mabilionea wa Tanzania. kwa mfumo tulio nao hakuna mabilionea ni masikini wa Tanzania watanendelea kutngenezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe kwenye suala la Leseni Mheshimiwa Waziri, wasaidieni watanzania kupata leseni

iwe ni mara moja. Kama kuna michnago, kwanza michango kwenye biashara ziko lukuki, msimsumbue tena kaleseni kila mwezi, kila mwaka anaenda kuhangaika nako. Wekeni mfumo ambao utamsababisha huyu mwananchi akate leseni hata ndani ya miaka mitano afanye biashara akiwa na uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukadiliaji wa mapato *TRA*. Suala la ukadiliaji wa mapato pia nalo ni changamoto. Mtaji wangu ni kidogo, ukifika *TRA* kwanza unaulizwa eneo lako la biashara ni la kwako binafsi ama umekodi? Kama umekodi unaulizwa kiasi gani? Mtaji wako unaoanza nao biashara ni kiasi fulani. Nimefanya biashara nikifika wakati wa makadilio ya biashara ninakadiliwa kuanzia mtaji wangu mpaka na faida. Hii sio haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unachukuaje? Mitaji yenyewe tumekopa benki. Wajasariamali wetu hawa, wafanyabiashara wetu wanaenda kukopa benki. Kwa hiyo, unapomkadilia mpaka mtaji wake humtendei haki. Tumekuwa tukisema hapa biashara siku zote ili niweze hata kulipa mkopo wangu benki na kufanya mambo mengine tunatumia faida sio mtaji. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na Wizara ya Fedha suala la kulipa kodi kwa wafanyabiashara tu-*charge* kutokana na faida sio kujumlisha na mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa Kituo Jumuishi *(One stop Center)*. Tumekuwa tukisema pia hili jambo kila wakati, iwe ni wawekezaji wetu lakini hata wafanyabiashara wetu wadogo wadogo. kumekuwa na changamoto sana. Wizara ya Madini wameweza, Mheshimiwa Dada yangu Ashatu, wewe unashindwa nini mama? Tusaidieni, wasaidieni wafanyabiashara wekeni kuwe na eneo moja dirisha moja. Watu hawa wakifika lile eneo aingie dirisha la kwanza atoke, aingie la pili atoke, aingie la tatu atoke badala ya changamoto leo anazozitumia

mfanyabiashara. Anatakiwa kwenda *TRA,* manispaa, benki, *OSHA,* aende sijui nani… vurugu anatumia siku tatu, wiki, miezi hajakamilisha hiyo michakato. Kwa hiyo, tunaomba pia wewe kama walivyofanya Wizara ya Madini, halikadhalika Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara tusaidieni hilo jambo ili tuweze kuwasaidia hawa wafanyabiashara wa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshaji wa Vibali vya wawekezaji. Wawekezaji wetu wengi wamekuwa wakija nchini lakini kumekuwa na urasimu sana. Tuombe angalieni Kanuni zetu, Sheria zenu. Tunatambua mnataka kupata wawekezaji wenye uhakika ndani ya Taifa letu. Punguzeni huo mlolongo, punguzeni kuvuta vuta miguu. Twendeni tufanye kazi tukimbizane na *speed* ya Mheshimiwa Rais, anayoifanya ili tuweze kupata wawekezaji wa kutosha watakaoleta tija ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba nizungumzie na mimi suala la Sakata la Twiga pamoja na Tanga. Mheshimiwa Waziri, utanisaidia tu, nilikuwa najiuliza hivi kama Tanga amefirisika na anaona hawezi tena kuendelea na hii biashara, kwa nini achague mtu wa kumuuzia hiyo biashara yake? Kwa nini? Pia ninataka nijue hivi anachagua yeye ama Serikali ninyi ndio mnamchagulia mtu wa kununua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Kunti nimefirisika kwenye biashara yangu sioni dalili huko mbele za kuendelea na hii biashara si natangaza? Kwamba biahara hii siwezi kuendela nayo natangaza nauza hii biashara ili nipate watu wengine mbadala tofauti, waje hapa kama ni mnada nipige mnada nipate kile ambacho ninakihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini leo tunasimama na msimamo wa kwamba Twiga ndio aende akanunue Tanga?

Ninapata shida ukija hapa uniambie. Kwa nini mnalazimisha Twiga amnunue *Tanga Cement*? Nataka hayo majibu yenye kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa wakati wako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti Majala, kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, wakati huo wafuatao wajiandae. Wa kwanza ni Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa, wa pili ni Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, wakifuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru lakini nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa uhai. Pia, niishukuru familia yangu kwa kunivumilia kuwa peke yao na mimi nikichapika na kazi huku za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote humu ndani ni viongozi. Familia zinatutegemea, taifa linatutegemea lakini vizazi vijavyo vinatutegemea sana. Kwa kadri tutakavyofanya vizuri sasa hivi, ndivyo tutakavyoweka mazingira mazuri ya vizazi vinavyokuja. Inashangaza katika *level* hii ya uongozi, sisi kwa maana ya Wabunge kufikiria katika *level* ya kifamilia kwa kweli tutakuwa hatuitendei haki nchi hii. Tunatakiwa kufikiria katika *level* ya kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kuiwezesha nchi hii kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia na mimi hili jambo lilozungumziwa na wabunge wengi hapa la uuzwaji wa Tanga *Cement*. Kwa sababu gani? Lina masilahi ya nchi. Tunatamani kabisa kwamba Wabunge wote tukae hapa tukiwa na mtizamo huo kwamba hili jambo tukiliendea Kimasihala

tutapata doa kubwa sana kwa kizazi kinachokuja kwa kuliingiza taifa hili katika janga. Tunayo kila sababu ya kufanya a*nalysis* ya kutosha kabisa na kufanya maamuzi ya kufanya jambo hili lakini pia Sheria zinatakiwa zifuatwe lakini pia wataalam waachwe huru wafanye kazi zao kitaalamu ili kusudi tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dhana miongoni mwetu kusema kwamba linalofanyika sasa hivi la kuuzwa kwa Tanga *cement* kwamba ni jambo baya. Hata hivyo, nataka nikwambie kwamba ubaya au uzuri wa jambo hili tunaweza tukauangalia au tukaliona katika muktadha wa misukumo isiyopungua minne. Jambo hili liko katika misukumo minne kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, msukumo wa kwanza, nii msukumo wa muuzaji. Muuzaji amekuwa na changamoto ya uendeshaji wa Kampuni hii kwa takribani miaka minne au mitano tangu Mwaka 2016. Hivi sasa amekuwa akipata hasara hali ambayo iliyofikia mpaka sasa hivi tunavyokwambieni ni takribani miezi minne watu hawajalipwa mishahara yao. Jambo hili kwa namna yoyote ile hakuna mfanyabiashara ambae anaweza kulivumilia. Kwa sababu athari zake ni kubwa. Athari zake ni kwamba:-

(i) Serikali inakosa kupata kodi yake kwa maana ya *corporate tax;*

(ii) Kuna watu wamewekeza pale ambao walikuwa na matumaini ya kupata faida kwa maana ya *dividends,* hawapati kampuni inashindwa kuwalipa.

(iii) Pia huyu anahusiana na watu wengine kwa maana wanunuzi kwake lakini kwa anaowauzia (*suppliers* na *customers)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali kama hiyo lazima kuna mazingira ambayo yanapelekea mahusiano yale yakawa sio mazuri. Tunasema kuna *jeopardize* uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kuna msukumo mwingine, huu ni msukumo wa mnunuzi. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana la kasi sana la bidhaa hii ya *cement*. Tanzania imezalisha kiasi kikubwa sana cha *cement* mpaka kufikia mwaka 2022, kulikuwa na uzalishaji wa takribani tani zipatazo milioni 7.5. Pia, kumetokea ongezeko la soko la nje ambalo Tanzania kupitia viwanda vyake hivi vimelipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na ongezeko kubwa kiasi cha kwamba mpaka kufikia mwaka 2022, Tanzania iliweza kuuza nje kiasi cha dola milioni 147.6. Hata hivyo, pamoja kuuza nje hivyo, pia tuliweza kununua kutoka nchi za nje *cement* hiyo hiyo kwa thamani ya dola milioni 137.2. Sasa ukiangalia hapo kwa mtazamo huo unaweza ukakuta kabisa kwa mfanyabiashara yeyote yule mwenye jicho hawezi kuiachia hiyo fursa. Huo ni msukumo ambao mfanyabiashara unamsukuma aamue kuinunua hiyo kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kuna msukumo wa Serikali. Serikali inatarajia kupata pesa kwa mtindo wa kodi kama nilivyowahi kusema hapo. Serikali inatagemea sana kuimarika kwa bidhaa hii ya *Cement* kwa ajili ya kuweza kukidhi haja ya mahitaji ya miradi yake ya kimkakati kama vile Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini na mabwawa mengine ya umwagiliaji, Mradi wa *Fly over,* Mradi wa Reli na miradi mingine ambayo inatarajia kabisa kwamba kama atanunua kupitia soko hili la ndani kwa vyovyote vile watakuwa wamenunua kwa bei ya chini kabisa na hivyo kufanya miradi hii kuwa *viable* na kuleta tija mwishoni mwa safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtazamo mwingine tena, huu ni mtazamo wa walaji. Walaji wanategemea kabisa kwamba bidhaa hii iwe ni ya bei ya chini lakini iwe ni bidhaa ya uhakika, kusiwe na bei za kubadilika badilika. Katika mazingira hayo kama nilivyojaribu kusema huko mwanzo unaona kabisa kwamba mazingira haya yote unapelekea uuzwaji wa Tanga *cement* kuwa hakuna njia lazima *Tanga Cement* iuzwe. Hii ina-*justify* kwamba Tanga *cement* iko katika mazingira ya kwamba lazima iuzwe kwa ajili ya masilahi mapana ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kinachotokea sasa hivi kumekuwa na madai ya hapa na pale kama nilivyosema watu wamekuwa wakidai kwamba jambo hili si zuri, ni masuala ya kufirika tu. Unavyozungumzia *cartel* kwamba *Twiga Cement* Ikinunua Tanga *cement* itasababisha *cartel* hilo ni jambo la kufikirika. Kwa sababu hakuna mazingira yoyote yale ya kibiashara kwamba yanaonesha *cartel* inaweza ikajitokeza. Kwa sababu gani? Kwa sababu *cartel* inakuja baada ya kuwa na *stiff competition* yaani ushindani uliokuwa mkubwa sana miongoni mwa makampuni yaliyoko kwenye *participation* ya biashara hiyo. Kiasi cha kutishiwa kuona kwamba kuendelea kuvutana inasababisha wao kuwa na *cost* ya *production* kuwa kubwa. Sasa kwa namna moja wanalazimika kwamba basi wapange bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira hayo hayapo hapa kwetu kwa sababu gani? Hapa kwetu sio tu bidhaa ya *cement* lakini bidhaa yoyote ile hakuna bidhaa ambayo ina *meet competitive market*. Masoko yetu yaliyoko hapa hapa nchini yana viashiria tu vya kuonesha kwamba kuna *competition* lakini *is not competitive market* na hivyo suala zima la kusema kwamba kuna *cartel* hili ni suala la kufikirika na tusiingie katika mtego huu. Tuiache Twiga *cement* ainunue *Tanga Cement* kwa sababu

kutakuwa na tija kubwa, *production* itakuwa kubwa lakini pia atakuwa na ushindani na makampuni mengine ya nje.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:**…kutakuwa na uwezo wa kuwa na *creativity* katika kampuni lakini pia …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela, kiti kikizungumza inabidi usubiri. Naomba upokee taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, sidhani kama kuna mtu ana shida ya nani kumnunua nani. Nataka nimpe tu taarifa kwamba kwenye kuangalia hili hatuangalii *stiff competition* peke yake, namna ya ku-*measure* iko nyingi. Hali ya soko*, share markets, capacity* ya viwanda kuzalisha na sababu nyingine. Ukisoma *Major analysis and report* ya *FCC* ukurasa wa 34, wenyewe wanakili kwamba hawa waki-*major* wakafika asilimia 42 na *point* ya *share* ya *market*, hiyo ndio changamoto iliyopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, unapokea taarifa?

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa kwa muktadha kwamba *market share* sio inayosababisha *cartel* kwa kadili nilivyojaribu kuzungumza hapa. Kwa sababu sikuwa na muda tu, kama ningekuwa na muda ningeweza kumpa *fact* zote zinazosababisha *cartel* na miongoni

mwake ni *competition* ya *market* na sio kuwa na wingi wa *share*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi Dangote ana share takribani kwa mfano *20 percent* lakini anaweza aka-*inject capital* kubwa pale kiasi cha yeye akawa na uwezo sasa wa kuwa na *share* asilimia 60 utamfukuza sokoni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante sana Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, na muda wako umekwisha, hitimisha hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru kwamba ninachotaka kuhitimisha ni kwamba tuynatakiwa tuwe makini kwamba Serikali yenyewe iwe makini katika utendaji wake kwa sababu shida iliyoko hapa siyo wafanyabiashara walioko sokoni shida inaweza ikapatikana kwa watendaji wa Serikali katika kutimiza majukumu yake; na kutokutimiza majukumu kwa Serikali isitupiwe kwamba hawa wafanyabiashara wanafanya kosa la jinai ambalo sisi nafikiri tunaweza pia tukaliona kwamba siyo kosa isipokuwa huu ni udhaifu wa upande mwingine. Mimi ninaomba tuwe *serious* biashara tunahitaji biashara kubwa wafanyabiashara wakubwa wakubwa ambao wataiondoa nchi hii hapa tulipo na kuwa katika viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Issa Ally Mchungahela kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ambaye angefuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa lakini hata hivyo atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Gallos.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi pia na mimi ya kuchangia, na nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa. Lakini kwa kwenda haraka nipongeze pia juhudi kubwa ambazo zimekuwa zinafanyika hasa kwenye kukuza diplomasia ya uchumi kwa sababu kazi kubwa imefanyika, nyote ni mashahidi; Mheshimiwa Rais amezunguka huku na huku akijaribu kuvutia wawekezaji. Kwa hiyo pongezi kubwa ziende kwako Mheshimiwa Waziri kwa sababu iko chini ya wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi unahitimisha nilitaka kujua pia, miongoni mwa vitu ambavyo nilitaka nijue nisije, nikakushikia shilingi shemeji yangu. Tumeona mkisafiri huku na huku tuna *register* wakandarasi zinafanyiwa *memorandum* nyingi sana. Tunataka kujua, katika zile *memorandum of understanding* ambazo zimesainiwa ni kampuni ngapi zimesharipoti hapa na zimeshaanza kufanya biashara au zimeajiri Watanzania; muweze kutusaidia ili zile fedha ambazo mnakuwa mnazitamka kule *at least* tuone kwamba zimeshaanza kuingia nchini na zinafanya kazi, hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili sehemu yetu kubwa ambayo ni Wizara ya Madini halijaribiwi kuongelewa kwa kirefu kabisa ni *issue* ya Liganga na Mchuchuma. Hili jambo tumeliongea kwa muda mrefu sana kama Kamati. Lakini nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri lakini pia Mheshimiwa Rais, kwa sababu kwa taarifa ambazo tunazo na hotuba ambayo imetolewa ulituahidi mwezi wa nne fedha itakuwa imetoka lakini huu ni mwezi wa tano; na kwenye hotuba yako uliyotoa ni kwamba tayari pesa ile bilioni 15.4 iko kwenye *process* nzuri, kwa hiyo wale wananchi wa Ludewa wanaenda

kulipwa pesa yao na haitimaya matatizo haya ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu tunahakika yatamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema tunauhakika yatamalizika, Serikali haikuwa imefanya *commitment* yote ile pale ndiyo maana Kamati tulikuwa tunapiga kelele. Kwamba tunataka tuone mkono wa Serikali pia. Kwa sababu tunavyosema mkandarasi alikuja tukakubaliana hivi ilhali Serikali haijawekeza hata shilingi ilikuwa inakuwa ngumu kwetu. Ndiyo maana tukaomba kwamba basi hata fidia tulipe sisi kama Serikali, na baada ya hapo ndipo turudi nyuma tuanze kutafakari ni wapi tunaenda au ni nini tunafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kulipa fidia kwa sababu tuna uhakikia ni bilioni 15.9 za walipa kodi wa Tanzania zitakuwa zimewekwa pale sidhani kama kutakuwa na kurudi nyuma. Ni lazima tuone majibu na tuone mradi huu mkubwa wa liganga na mchuchuma ukinyanyuka na hatimaye uweze kutupa matokeo yale ambayo tunayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea mara nyingi na nimekuwa najiuliza huyu bwana ambaye tulikuwa tumeingia naye mkataba nadhani niliwahi kutoa taarifa kwenye Kamati hawa watu kiongozi wao ambaye alikuwa ni mwenyekiti wa *group* yao alinyongwa tarehe 09 Februari kwenye nchi yao, kwa makosa ya rushwa na kujihusisha na vikosi vya mafia na vurugu nyingine ambazo zilikuwa zinaendelea huko. *Since then,* kumekuwa na hali ya sintofahamu. Kwa sabau kula wakati tukiuliza Mheshimiwa Waziri tunambana sana na kweli *sometimes* alikuwa anatoa majibu lakini unaona alikuwa anafikia hatua unaona anajibu lakini inafikia *stage* hawezi kuendelea tena

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kipo ni kimoja; mimi niombe tena, hata kama tunarudi kwenye meza ya majadiliano, maana kunakuwa na tetesi kwamba huyo mtu kuna Serikali inataka imchukue halafu yenyewe irudi kwenye meza badala yake. Lakini ukijaribu kuangalia huyu mtu kwenye makubaliano yetu alikuwa anakuja na Dola za Kimarekani milioni 600 halafu tunaunda kampuni ya ubia. Tukiunda kampuni ya ubia huyu mtu anaenda kukopa bilioni 2.4 dola kwa kutumia mtaji wa eneo lile ambalo tumempa na hati zetu. Na huyu mtu amekwamisha mradi huu kwa muda mrefu kwa sababu anadai vivutio vya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unajiuliza fedha yenyewe ni dola milioni 600 hujaja nayo, bado tunaunda kampuni ya ubia ya kukusaidia kukopa hutaki kwenda, pili unataka vivutio vya ziada ilhali hata shilingi hujaweka. Sasa mimi nimekuwa na wasiwasi sana; lakini Mheshimiwa Waziri nikawa najiuliza, maana kuna tetesi nyingine zipo, kwamba *CEO* wa hii kampuni ni mtanzania mwenzetu, hivyo ninaomba wakati una *wind up* utujibu. Huenda hii kampuni inasemekana ipo china kumbe ipo hapahapa, tunazungushana na wenzetu. Kwa hiyo nilikuwa naomba hili pia tupate majibu ili tuweze kuondoka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo jingine ambalo limeongelewa na watu wengi sana hapa, na mimi sitaki kuwa mbali ya hili, ningependa niligusie pia. *Issue* ya utoaji wa Kampuni ya *Tanga Cement* ikichukuliwa na *Twiga Cement*. Mimi sina shida sana na *issue* ya *take over* lakini kwa sababu jambo hili limeleta taharuki, jambo hili limelalamikiwa na watu wengi sana; Mheshimiwa Waziri nikuombe, kwa busara. Jana Mheshimiwa Ulega hapa wakati anamaliza alisema jambo moja kwamba Mheshimiwa Rais asingependa aone manung'uniko na vurugu zile. Ndugu zangu wa Kigoma waliokuwa pale wakashangilia,

Mbunge mwenzangu wa Kigoma aliyekuwa hapa mbele yangu akaanza kupiga simu jimboni kwamba mambo yamemalizika nikasikia na wananchi wanashangilia kwenye TV. Maana yake ni kwamba jambo hili lilikuwa na shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusingependa twende na mambo ambayo yanatuletea shida. Mimi kwangu ukiniambia mtu anamiliki *share hundred percent,* kama antulipa kodi na ameajiri Watanzania *its fine,* acha amiliki. Kwa sababu *at the end of the day* hatutegemei kwamba kiwanda hiki cha Twiga kitashindwa ku-*expand* au Kiwanda cha Tanga kitashindwa ku-*expand* kwa sababu tu kina *limit.* Lakini tunachokisema, sheria yenu mliyojiwekea wenyewe ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Bunge hatuwezi kutunga sheria halafu tukakanyaga sheria sisi wenyewe, hapo ndipo utata unapokuja. Ndiyo maana tunaomba, kama kweli sheria ilitungwa na iko hivyo tuheshimu sheria tulizojitungia wenyewe, maana kama hatutazijali hizi sheria kesho zitatuletea shida hapa hilo ndilo tunaloliomba. Maana kweli *FCC* ipo chini ya Wizara, hii *FCT* ipo chini ya Wizara hii. Haiwezekani tukawa na taasisi mbili chini ya wizara moja zinasimamiwa na Waziri mmoja; huyu anasema hivi na huyu anasema hivi halafu sisi tukaamua ku-*side* na taasisi moja wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubali turudi nyuma kama kuna *irregularities* zilizofanyika wakati wa *take over* hii tuzifute tutangaze upya. Kukiwa *open* kila mmoja akaona tutaweza kwenda mbele. Maana ilisomwa habari hapa, kuna kampuni gani ambayo sijui imefutiwa usajiri, walisema ni Chalinze au *whatever,* nimesikia, kwamba ilifutiwa usajiri. Lakini kama ilikuwa na usajiri mpaka mwaka jana inafungua kesi mtawafikia *BRELLA* huko; lakini yenyewe bado ni sehemu ya ile kesi kwa

sababu tayari walishakuwa na usajiri kipindi jambo linaanza na kama halipi, hakuna anaye mtetea asilipe. Na kama ana fedha huyu mtu mnasema kampuni ya mfukoni…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** … na kama ni kampuni ya mfukoni tayari mnasema ana fedha, hii fedha anaitoa wapi na ni kampuni ya mfukoni? Kwa hiyo ningependa tusiende sana kujiuliza huko kutaja kampuni au kufanya nini; tunachotaka tuone *procedure* yetu iko sawa ili tuweze….

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra naomba upokee taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Msukuma.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru napenda kumpa taarifa mzungumzaji. Nilivyochangia mchana nilisema kampuni hii ni kampuni ya *briefcase* ambayo haijukani inakotokea. Sikutaka kwenda mbali kwa sababu muda wangu wa kuchangia ulikuwa mchache; lakini tunao ushahidi na uthibitisho ambao unaonesha kuwa kampuni hii ni hewa haijulikani ilikotoka *address fake*, kiwanda kiko kwenye *plot* Kinondoni na wenye kiwanda ninazo picha zao hapa ukitaka tukabidhi tukabidhi. Tuachana na hizo biashara ya matapeli Bungeni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ezra Chiwelesa unapokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Msukuma?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa, maana kama kampuni ilisajiliwa na swerikali

halafu tunaita ni kampuni *fake*, kwamba ni za kwenye *briefcase means* kampuni nyingi ziko hapa mnatuambia tuna makampuni yamesajiliwa kumbe hayapo basi Serikali irudi nyuma ikayaangalie kama yapo mengine yafutwe sawa na hiyo Kamapuni ya Chalinze ilivyofutwa. Napokea taarifa ya kaka yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kumalizia, nime-*experience* kidogo na haya mambo, naomba ni *share experience* yangu. Nimefanya kazi Air Tanzania mwaka 2020, *that time* nilikuwa najihusisha kama *cabbing crew*. Kilichokuwa kinafanyika; hizi *take over* ni nzuri *sometimes take over* ni mbaya. Unakatiwa tiketi *Air Tanzania* ndani inasema Air Tanzania *cover* juu limeandikwa *South African Airways*. Kilichokuwa kinatokea ukishasoma kesho una haja ya kwenda *Air* Tanzania, si utakata moja kwa moja kwa msafirishaji mwenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *sometimes take over* ni nzuri lakini *intention* ya yule anaye-*take over* unaijua? Huyu bwana Tanga anazalisha *clinker* kwa sehemu kubwa, *Twiga Cement* akishakaa na *Tanga Cement* wakaanza kushirikiana na *shareholder* ni mmoja huyu anahitaji *material* kutoka kwa mwenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, achana na mambo ya sukari ile ni miwa, huwezi kutoa muwa Kagera ukaupeleka Bukoba kwenda kuzalisha ukaupeleka Morogoro kwenda kuzalisha, hautakulipa. Huyu bwana akichukua *clinker* Tanga kwa bei ambayo wanajuana wao akaongeza tu bei ya *transport,* kwamba *transportation cost* yangu mimi kutoka Tanga kwenda Dar es salaam ni kadhaa maana yake *production cost* yake itakuwa kubwa, twiga pale. *Production cost* ikiwa kubwa ata-*declare low profit* aki-*declare low profit* maana yake kodi tutapata ndogo.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi tukipata ndogo huku Tanga akapunguza *production* ya *clinker* maana yake huyu anaweza akafanya biashara tukapata kiwanda kipya kinazalisha lakini hatupati faida na kodi kwa Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra…

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ungeacha nimalizie tu

**MWENYEKITI:…**naomba upokee taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mhagama

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuongezee taarifa Mheshimiwa *Engineer* Ezra kwamba Teknolojia ya Twiga ni ya viwango vya juu sana ukilinganisha na teknolojia ya *Tanga Cement* maana yake nini? Maana yake uwezekano wa Tanga Cement na *asset* zilizopo pale *Tanga Cement* pamoja na *resources* zilizopo pale zikawa zinatumika kusafirishwa zaidi kwenda kuzalisha Dar es salaam kuliko kuendeleza kiwanda cha Tanga

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiwelesa unaipokea taarifa?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipokea na unilindie muda kidogo kuna jambo nilikuwa namalizia. Kwa hiyo ninachosema ni kwamba, tunaweza tukaendelea na *production ya cement* Tanga, *its fine,* itaendelea kuwepo pale, lakini wakazalisha kwa kiwango kidogo halafu Dar es salaam

wakaongeza huku waki-*declare* kwamba *cost of production* kwa Dar es salaam ni kubwa kwa sababu watakuwa wanaunua *raw material* pale. Kiwanda kile kitazalisha *less* tutakiua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge wa Kanda ya Ziwa *cement* tunayotumia kwa sehemu kubwa ni *cement* ya Simba. Leo hata mkisema kwamba *cement* inazunguka nchi nzima leo tunaona mfuko 24,000, *cement* ukiitoa Mtwara ukaifikisha Biharamulo utauza mfuko kwa shilingi ngapi? *Cost of production* ni ileile *transportation cost* itakuwa kubwa; ndiyo maana kama hilio jambo tunalisema hapa Serikali itusikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo hata ya Liganga na mambo mengine Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kusema, sasa msiposikiliza tuangalie mbele siyo leo *take over* ya leo ni nzuri kwa sababu amekaa na fulani ameongea lakini baada ya miaka mitano miaka kumi miaka 20 tunaoongea sisi hatutakuwepo, hata Wabunge tunaoongea humu ndani ya bunge labda watakuwa wamebaki asilimia 30 au 20, sasa *where are we going* baadaye? Turudi hapa tena kubadilisha sheria? Turudi hapa kulaumiana? Ni bora tunapowashauri leo msikilize kuliko kusubiri mambo yaharibike baada ya miaka 10 miaka 20 warudi hapa watu kuja kubadilisha sheria

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo nashukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa. Nilimwita Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos aweze kuchangia; wakati huo Mheshimiwa Kwagilwa Mheshimiwa Shigongo, wanajiandaa.

**MHE. TAUHIDA C. GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia. Kwanza kabisa nimpongeze Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuipeleka Tanzania mbele na kuifanya Tanzania isonge mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo machache tu, nina mambo matatu ambayo kwa leo ningependa kuyazungumza. Kwanza kabisa nianze na suala la Kiwanda cha Viuadudu kilichokuwepo Mkoa wa Pwani

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa zaidi nikushauri Mheshimiwa Waziri kwenye kiwanda hiki. Jambo la kwanza, kwa namna ambavyo tumeenda kukitembelea kama Kamati, tungetamani sana kuona unapata muda na kukutana na mawaziri wenzio, aidha Waziri wa Afya au Waziri wa *TAMISEMI*. Kile kiwanda ili kiweze kufanya vizuri, ili kiwanda kiweze Kwenda kwanza tuanze na soko letu wenyewe la ndani. Kwenye suala hili la Kiwanda cha Viuadudu tungeanza kupata kwanza soko tungetengeneza sisi wenyewe tukaacha kununua dawa kutoka kwa wafanyabiashara wa kawaida ambao wanatuletea. Tafsiri yake Mheshimiwa Waziri si nzuri; na kwa nini si nzuri, kile kiwanda ni cha kwetu. Tunanunua dawa kutoka kwa watu wengine wa nje. Imani tunayoijenga tunawaza kwamba hasa kinachotusumbua pale ni *ten percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanze na masoko yetu ya ndani. Kama mtakaa na Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu mkaweka mikakati dawa zile mtazitoa vipi ile fedha itazunguka ndani na itatupa faida. Kiwanda kitaleta faida dawa zitakuwa zinafanyiwa kazi ndani ya Tanzania, lakini isitoshe pia itakuwa inafanya kukuza kiwanda chetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninataka kushauri, Mheshimiwa Waziri na hili leo ndilo limenifanya nisisimame kwenye Wizara hii. Wakati tuko kwenye ziara ya Kamati tulipita *TIRDO,* kama sikosei pale panaitwa *TIRDO,* Dar es salaam; tuliwakuta vijana ambao wanafanya kazi moja nzuri sana. Hao leo ndio wamenihamasisha kusimama hapa kuchangia. Mpaka ukafika wakati najiuliza, hawa vijana ni Watanzania? Wako hapa hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri hajawahi kuwaona au hajawahi kubahatika kwenda kuwaona namshawishi aende akawaone. Hivi leo kijana wa Mtanzania ana uwezo wa kufanya vitu vikubwa, anau wezo wa kufanya mambo makubwa lakini anakosa nguvu ya kifedha. Kuna muda lazima tuoneshe njia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika pale kijana wa Kitanzania anatengeneza kifaa cha umeme, ananiambia leo mimi kama niko Dodoma nyumbani kwangu taa watoto wameziwasha mpaka saa tatu asubuhi nina uwezo wa kuiambia kupitia simu naomba taa uzime na taa zikazima. Hawa vijana wako Tanzania Mheshimiwa Waziri hatuoni thamani yake? hatuoni wanacho kifanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwenye hili dada yangu ataniwia radhi kidogo niseme. Hebu tuangalie kwa namna ya kipekee; tunamuuliza kijana wa Kitanzania umeshindwa wapi umekwama wapi anasema fedha, lakini vifaa vile vile ambavyo tumeoneshwa pale anasema kwamba kama atapata mtaji mzuri hata upatikanaji wake bei yake itakuwa chini. Ana uwezo wa ku-*control* umeme wa ndani ya nyumba, kifaa hicho kijana wa Kitanzania anaweza kutengeneza. Mheshimiwa Waziri tuondoshe

wenzio tulipo kila kitu tunategemea kutoka nje kila kitu tunategemea kutoka kwa nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuondoshwe kwenye akili ya kutawaliwa, Watanzania tuhamishwe kwenye akili za kutawaliwa, tuwape vipaumbele vijana. Ni mara nyingi nikisimama namuongelea kijana kwa sababu nukiongelea kijana nimemuongelea mwanamke; mwanamke ndiye mwenye mzigo wa kukaa na kijana wake, asipokuwa na ajira mama ana huzuni, asipokuwa na ajira na hajui mtoto wake anapokwenda mama anahuzuni. ndio maana muda mwingi namuongelea kijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hapa kwako juu hakuna shida hebu angalia hapa chini kwako kuna nini? Chungulia; unafanya kazi kubwa na kazi unazozifanya zinaitwa kazi, ni zile kazi kubwa chungulia chiniyako kuna nini? Kunaendelea nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimi muda mfupi niliokuwepo kwenye Kamati hii ya viwanda dada yangu niseme kuna vitu haviniridhishi na kuna vitu naweza kuongea hapa lakini kuna vitu ninaweza nikakushauri kama Waziri tutakapokutana. Mheshimiwa Waziri angalia kuna kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani jambo kubwa sasa Tanzania tunalotaka kuona tunataka kuona milango ya ajira za vijana ikifunguka; Wizara yako imebeba Wizara ya Uvuvi Wizara yako imebeba Wizara ya Kilimo leo tunahamasisha watu walime kama wewe viwanda hukuvifungua watapeleka wapi? Watauza vingine vitabaki vitaoza. Naomba tuwe na mikakati ya sasa na ya baadaye. Mikakati ya baadaye tutauza nje, ya sasa tutatengeneza bidhaa za ndani kwa kuona wakulima wanapata

nguvu. Mheshimiwa Waziri umebeba Wizara nyingine nyuma yako, wizara ulizozibeba tunaomba tuone mabadiliko. Pambana, mwanamke hajui kushindwa, mwanamke anajua kupambana, mwanamke siku zote anaonesha dira, anaonesha njia, analeta mabadiliko, hiyo ndio kazi ya mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ataniwia radhi, sijasema nimejisikia tofauti kwenye hili suala la *Tanga Cement*. Nimetafakari toka asubuhi linavyochangiwa, sijui lakini ni dhahiri kwamba sioni kama limetendewa haki na Bunge hili, kwa sababu Mheshimiwa Waziri leo ukienda kwenye Kamati ya Sheria hawaujui huu mgogoro ukoje, Kamati yetu ambayo Waziri yupo, hatulijui hili jambo likoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala sasa kwa namna nilivyolisikia linavyochangiwa, maana yake nimekuja kulipima, nimekuja kulikuta, Wabunge wanaotoka Tanga kwa namna wanavyotetea wana haki yao na sioni walipokosea, lakini nikamsikiliza kaka yangu Musukuma alipozungumza nikasema, hee! Ndio yaliyopo haya. Hebu hili suala Mheshimiwa Waziri aliweke kinaga ubaga tulifahamu likoje, kwa sababu linaleta dhana mbaya ndani ya Bunge, linaleta sintofahamu ndani ya Bunge, watu watakuja kutafsiriana sivyo ilivyo, lakini kila mmoja ukimsikiliza ana haki yake ya kusema hayo anayoyasema. Katika suala hili nadhani Wizara ina Mwanasheria, nafikiri zaidi lipelekwe kwenye sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yetu kwenye hili sio Tanga kanunua nani, *cement* kanunua nani, hofu yetu tuko salama? Hofu yetu Watanzania kwenye haya wako salama? Ndio maana watu wanalichangia. Ukikaa ukisikiliza hoja kwa makini hutokuwa na maswali ya kujiuliza na kila mtu utampa haki yake. Asubuhi nimemsikiliza Mheshimiwa Mnzava, kaka yangu hapa

nimemsikiliza, kwa hiyo nilichoona mimi kwa tafsiri yangu wanatetea Tanga yao, wanatetea vijana wao, ndicho nilichokitafsiri, lakini mbele hakuko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Musukuma Kaka yangu kasema, kunakuwaje na kampuni ya mfukoni. Nimwambie Mheshimiwa Waziri, nikitaka nilichambue sana kwa upana, nahisi sintoitendea haki Serikali yangu, kwa sababu kunakuwaje na kampuni ya mfukoni? Nikushauri Dada yangu Mheshimiwa Waziri kwa upendo, hili jambo waliangalie, kama mchakato umefika sehemu haujakaa vizuri warudi hatua tatu nyuma. Kurudi nyuma tukatoa maamuzi sahihi sio kitu kibaya na haifanyi kuwa amefanya vibaya, amekuwa mtu wa busara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sakata hili au tatizo hili tunakosa mchango mzuri kwa sababu halileti tafsiri nzuri kwa umma, halileti tafsiri nzuri kwa Bunge na nafikiria hata Spika wetu kwa sasa linamuumiza kichwa. Mheshimiwa Waziri aliweke wazi, kuna shida gani, kuna siri gani zimejificha ambazo wengine hatuzifahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo liende kisheria, lipelekwe kisheria kama mchakato kuna sehemu umeharibika urudiwe upya, kila mwananchi na kila Mtanzania hususan Wabunge wanaowakilisha Tanzania waelewe kuna nini, ili tutakapokuja kulichangia tena kabla ya kutoa maamuzi lipi liwe lipi tunaomba hili jambo tushirikishwe, tuisaidie Tanzania kama Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo aweze kuchangia.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili nichangie Wizara yetu hii ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Mimi ni mmoja wa Wabunge wanaotokea Mkoa Tanga, kwenye hili suala la Kiwanda cha *Tanga Cement* nafikiri Mheshimiwa Tauhida ameliweka vizuri sana. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Tauhida kwamba Serikali inao wajibu ya kutoa ufafanuzi kwa wananchi wapate kulielewa, lakini zaidi taratibu za kisheria ni za muhimu kufuatwa kwa sababu ndio misingi tuliowekeana kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichangie kwamba, Wizara yetu hii kwenye suala zima la uwekezaji. Tunao Watanzania ambao ni wawekezaji ndani ya nchi yetu, lakini vile vile tunao wawekezaji ambao sio Watanzania ambao wamekuja kuwekeza ndani ya Tanzania. Sasa nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha pana mapitio mengi ya kisera yanafanyika na pana mapitio mengi pia ya kisheria yanafanyika ili kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili la uwekezaji ni bahati mbaya sana kama nchi tumekuwa na mtazamo wa *outward looking*, yaani kila sheria na kila sera tunapojaribu kuileta ya uwekezaji inamwangalia na kumlinda zaidi mwekezaji kutoka nje na inamwangalia kidogo sana mwekezaji ambaye ni Mtanzania. Mwaka jana hapa, nitatolea mfano, tumepitisha Sheria mpya ya Uwekezaji, fikiria ni sheria mpya hii, hata miezi sita haijamaliza, lakini sheria ile ilitoa fursa kwamba ili mwekezaji aweze kupata *incentives,* aweze kupata vitu vyote vya misamaha ya kikodi na vivutio vya kiuwekezaji akiwa ni

Mtanzania, lazima awe na mtaji wa dola laki moja. Akiwa ni mtu kutoka nje anatakiwa awe na dola laki tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaposema dola laki moja kwa Mtanzania ndio aweze kupata *incentives,* vivutio vya kuwekeza, unaongelea zaidi ya milioni 200 na kitu za Tanzania. Sasa unawaweka wapi Watanzania ambao wana mitaji ya milioni 150, 170, 180. Ndio kusema kwamba sheria hii wao haiwapi fursa ya kuitwa wawekezaji ndani ya nchi yao, wala ya kupata upendeleo na vivutio kama ambavyo mtu kutoka nje anapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wenzetu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji lazima sera hizo wanazozifanyia mapitio zije zikimtazama Mtanzania, mwekezaji wa ndani, mzawa, ili aweze kunufaika na uwekezaji ndani ya nchi yake. Nasema hivyo kwa sababu hata Bunge hili ambalo tumekaa hapa kesho kutwa bajeti ikija kusomwa, maeneo mengi ambayo tutakuwa tumetaja yameongeza kodi ni yale yanayoenda kuwaathiri Watanzania wawekezaji ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepambana sana hapa Bungeni kubadilisha sheria pale *TIC* ili kwamba mwekezaji akitoka nje akiingia ndani ya jengo mmoja apate vitu vyote ndani ya jengo hilo. Kuanzia usajili, kila kitu mpaka anatoka pale na leseni yake ya biashara, anakwenda kufanya biashara, lakini wafanyabiashara wetu wa ndani ambao ndio Watanzania, wawekezaji wa ndani, hatujawapa jicho hilo. Yeye akitaka kuanza kufanya biashara anazunguka, anazunguka mitaa yote mpaka viatu vinakwenda upande hajasajili biashara na hao ndio walio wengi na ndio Watanzania wenye nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hizi sera wanazosema wanazifanyia mapitio ambazo wamezitaja kwenye hotuba yao,

ni vyema zikaja na jicho la kumwangalia Mtanzania mwekezaji wa ndani. Mwekezaji wa nje akiingia na huu mtaji wake wa laki tano kwanza kuna wakati anapewa likizo ya kodi, hata miaka mitatu wanaita *grace period*, lakini hata vifaa anavyonunua vinasamehewa kodi. Nitatolea mfano wa wachimbaji wadogo, mchimbaji wetu mdogo kwa mfano akisema anaagiza *grader* leo hapa, lazima wataligonga *VAT,* lakini wale wachimbaji wakubwa waliopo hapa anaagiza yale ma-*grader* yanaingia bure, anaagiza mpaka magari yanaingia bure na anapewa na msamaha wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii haiwezi kuwa sawa. Hatuwezi kuwa na nchi ambayo hatuwajengi Watanzania wenyewe kuwa wawekezaji ndani ya nchi yao. Halafu mbaya zaidi mwekezaji huyu mkubwa wa nje ambaye tunamkimbilia na kuwaacha wa kwetu, sheria hii ambayo tuliitunga hapa inampa *free repatriation of profit* ambapo faida hii angepata mwekezaji Mtanzania ingebaki hapa hapa. Kwa hiyo ni ushauri wangu kwamba wawekezaji wazawa wa Tanzania ifike mahali kama tunavyotaka kuangalia kwa jicho la pili na kwa jicho la ukaribu wawekezaji wa nje ndio hivyo hivyo tunatakiwa tuwaangalie hawa wawekezaji waliopo ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, langu lilikuwa ni hilo, nashukuru sana kwa fursa hii, shukrani sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo. Nilimwita Mheshimiwa Eric James Shigongo wakati wafuatao wanajiandaa. Wa kwanza ni Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, akifuatiwa na Mheshimiwa Lucy John Sabu, wakati huo Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi anajiandaa.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kunipa nafasi ya kusimama tena ndani ya Bunge hili. Nikushukuru sana ingawa haupo kwenye kiti Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako wa Bunge letu hili Tukufu. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana sana, pia wananchi wangu wa Buchosa ambao nipo hapa Bungeni kuwawakilisha, nafanya kazi hii waliyonituma kwa uaminifu wote ili kero zao ziweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nianze kwa kusema, miezi 11 iliyopita nilisimama hapa Bungeni nikaeleza wasiwasi wangu. Ni kama nilikuwa na wasiwasi kwamba nchi yetu ingerejea ilikokuwa, kwa sababu tulikuwa tayari kwenye uchumi wa kati, pato la Mtanzania mmoja mmoja lilikuwa tayari limekwishafika dola 1,080, lakini kwa *corona* ilivyokuwepo, Ukraine vita na nini, nikahisi tungerudi tulikokuwa. Hata hivyo, kazi kubwa imefanyika na mtakumbuka niliwaomba hapa kwamba Watanzania tufanye kazi kubwa sana tumuunge mkono Rais wetu ili nchi yetu isirudi ilikokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo nina furaha sana moyoni mwangu kwa sababu taarifa nilizonazo ni kwamba nchi yetu imepenyeza na imezidi kwenda mbele pamoja na changamoto ilizokuwa nazo. *GDP* ya Taifa letu hivi sasa ni bilioni 85, wakati ule tunazungumza zilikuwa zinakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani bilioni 67. Leo ninapozungumza ni bilioni 85, tumekuwa na pato la Mtanzania hivi sasa kutoka 1,080 tumefika 1,232. Pamoja na yote yaliyotokea. Kwa hiyo naomba nisimame hapa kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sana tu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kuzungumza hapa, nirudie tena na nitazungumza kila ninaposimama kwamba *we*

*have the most intelligent in Africa and in the world*. Kuthibitisha hilo Tanzania *image* yake sasa hivi Kimataifa imebadilika kabisa. Sisi kukaa pamoja na dada zangu pale, kukaa pamoja, Rais amefanya *image* yetu imebadilika. Tanzania sasa hivi inajulikana kama *one of the democratic country in the world,* kwa sababu ya kuishi pamoja na ndugu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu hizi ziwaelekee Wabunge wote walioko hapa kwa namna wanavyotoa michango yao hapa Bungeni. Mimi hoja yangu ipo kwenye suala la umaskini wa Taifa letu. Najua wamezungumza juu ya viwanda, wamezungumzia Twiga, naomba nisiguse kabisa habari ya Kiwanda cha Twiga na Tanga *Cement*. Naungana na hoja ya dada yangu Tauhida pale alichokisema ndio ninachokisema mimi ya kwamba suala hili lina utata, limeleta kelele nyingi, turejee mezani tukaangalie tatizo liko wapi. Langu ni suala zima la umaskini wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maendeleo tuliyoyapiga nchi yetu ni tajiri lakini watu wake bado ni maskini. Bado ni maskini, watu wana shida nyingi sana huko mtaani, maisha ni magumu pamoja na pato letu kuongezeka mpaka dola bilioni 85, lakini watu bado wana shida nyingi sana, maisha ni magumu. Inavyoonekana ni kwamba hii bilioni 85 iko kwenye karatasi, lakini haipo mezani mwa Mtanzania wa kawaida. Hapo ndio nataka niongelee mimi hoja yangu ya leo kwamba, umaskini bado upo na ni lazima tutafute njia yoyote ile ya kuhakikisha hii 85 bilioni inaonekana kwenye maisha ya Mtanzania wa kawaida. Hoja yangu ipo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale wasomaji wa vitabu bila shaka wamewahi kusoma kitabu cha Marehemu Profesa Mtulya aliandika kitabu kinaitwa *Growth and Development*. Kwamba

kuna tofauti kubwa sana kati ya *growth* na *development*. Kukua ni ku-*increase in size*, tume-*increase in size* tuna pato kubwa la Taifa lakini *development in increase in activities*, kuongezeka kwa *activities* za Taifa. Kwamba ukuaji huu unaonekanaje kwenye maisha ya Shigongo, kwenye maisha ya Kingu, kwenye maisha ya mkulima wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado ukuaji huo haujaonekana kwenye maisha yetu. Ni kama jenereta liko nje, lakini ndani ya nyumba kuna giza na jenereta inawaka. Ina maana kinachokosekana hapa ni *cable* ya kutoa umeme nje kuingiza ndani, hakuna *connection* kubwa kati ya *GDP* na maisha ya Mtanzania wa kawaida. Sasa niliposimama hapa leo naongea na Wizara ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ni Wizara muhimu sana kwa Taifa letu. Wizara ya uratibu, Wizara hii ikisimama sawasawa kwenye uratibu itatuondolea umaskini wa nchi yetu. Nataka niseme mambo ambayo mimi naamini yakifanyika katika nchi yetu, umaskini wa Tanzania utaondoka au kupungua kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, naamini sana kwenye kilimo, naamini sana kwenye *agriculture*. Tulime na Serikali imeamua kulima kweli, Mheshimiwa Rais ameongeza fedha nyingi sana Wizara ya Kilimo ili tulime na kweli tunalima sana. Kilimo kitatutoa kwenye umaskini wetu, kimeajiri watu wengi katika nchi yetu, bahati mbaya sana kilimo chetu hiki, watu wengi wanatumia kilimo cha mkono, asilimia 70 ni jembe la mkono, asilimia 20 ni ng’ombe na asilimia 10 pekee yake ndio zimetumika zana za kilimo za kisasa kama trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme kitu kimoja kama Mheshimiwa Bashe analima, Mheshimiwa Ashatu ana mambo kadhaa ya kufanya. La kwanza, anatakiwa kuhakikisha mazao

yetu yanatangazwa na masoko yanatafutwa, hiyo *TanTrade* anayo yeye kwenye Wizara yake. La pili, anatakiwa kuhakikisha *mechanization* ya kilimo inafanyika, zana za kisasa anayo *TIRDO* ofisini kwake anayo *TIRDO* na anayo *TEMDO,* lakini lingine ana *CAMARTEC* katika zana za kilimo ambazo zinatumika huko mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utusaidie Wizara hii ipewe pesa za kutosha kwenye hayo maeneo niliyoyasema, tofauti na hapo tutalima kweli mazao lakini *post harvest loss* yetu itakuwa kubwa, mazao mengi yatakuwa yanaharibika na hakuna masoko, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo unatakiwa kulifanya ni *innovation*, utakumbuka nilishakuja hapa nikasema juu ya *innovation* ya kwamba ubunifu ni kitu cha muhimu sana kwenye Taifa letu. Tuna vijana wengi wamebuni vitu vingi sana, lakini hawana mitaji amezungumza dada yangu Tauhida hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshakuja hapa nikasema, narudia kusema tena na leo kwamba, kuna mtu mmoja kule Iringa aligundua umeme anasambaza kijiji kizima. Kuna kijana mmoja pale Mabibo alikuwa na redio yake anatangazia watu pale Mabibo lakini badala ya kusaidiwa katika nchi hii ukiwa mbunifu unajikuta unaingia kwenye matatizo. Hiyo sio jambo sahihi naomba tufanye kila kinachowezekana kuwasaidia wabunifu wa nchi yetu. Vijana wetu wanatoka vyuo vikuu na shahada wana ubunifu lakini hawana mitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishamshauri Mheshimiwa Waziri aanzishe *National Innovation Fund*. Aanzishe Mfuko wa Ubunifu wa Taifa na huu sio lazima akusanye pesa yeye, kuna *Global*

*Innovation Fund* huko ina pesa nyingi tu. Tunaandika mradi tunapewa mabilioni ya pesa, tena sio mkopo ni *grant*. Nilishamwambia, tulishaongea nikiwa Kamati ya Viwanda na Biashara nilisema sana. Nasema tena leo na leo nitakuwa mkali kidogo, nitataka nipate maelezo kwamba nini kinaendelea kuhusu *Global Innovation Fund*. Hatuwezi kuwa na vijana wenye akili kiasi hiki kwenye Taifa letu, hawana mitaji wana ubunifu wao ndani ya nyumba, lakini wanakufa bila kufanya chochote. Hatuwezi kukubali Waheshimiwa Wabunge, ni lazima *National Innovation Fund* ianzishwe. Kenya wanayo, South Africa wanayo, Ethiopia wanayo, kwa nini sisi hatuanzishi? Naomba sasa tuwathamini wabunifu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kuwawezesha Watanzania. Watanzania wanahitaji kuwezeshwa, China miaka 15 iliyopita iliamua kwa nia moja kwamba tunaenda kuweka watu wetu kwenye *list* ya makampuni 500 duniani haikuwepo hata kampuni moja ya Kichina. Leo ninapoongea hapa nusu ya ile *list* ni kampuni za Kichina. Kwa sababu nchi iliamua *we need a political will to change* mambo. Lazima tuamue kama Taifa ya kwamba ile *list* tuhakikishe tunafanya jambo wenyewe, watoto wetu waweze kuwa na pesa. Tuwape Watanzania uwezo wa kuwa na kipato waweze kushikilia uchumi wa nchi yao. Tumechoka kuwa watazamaji, wageni wanakuja hapa siku mbili, tatu wameshatajirika, wanaondoka hapa na mali zetu sisi tunaendelea kubaki maskini. Nataka majina mapya ya mabilionea kwenye nchi hii, majina mengi kwa muda mrefu ni yale yale tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru kwa mchango wako Mheshimiwa Eric James Shigongo. Nilimwita Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan aweze kuchangia.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu kuhusu Bajeti ya Wizara ya Biashara na Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna usemi wa Kiswahili unasema, "Ngoma ikipigwa Tanga, wanademka Pemba." Kwa *geographical location* baina ya Tanga na Pemba, asilimia 50 ya bidhaa tunazozitumia Pemba zinatoka Tanga. Kama hazikutoka Tanga, zitatoka Mombasa au Unguja Mjini. Kwa hiyo, bidhaa za chakula tunatoa kwa ndugu zetu wa Tanga, *the same* kwa bidhaa ya *cement* au saruji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saruji inapoadimika Pemba, aidha tunaipata kutoka Mombasa au inaagizwa nje ya nchi kwa Zanzibar. Kwa hiyo, nimesikiliza kwa makini sana mjadala wa hoja ya ku-*merge* Kampuni ya *Tanga Cement* na *Twiga Cement,* vizuri sana. Wasiwasi walionao ndugu zangu Wabunge wa Tanga, Mheshimiwa Mnzava na aliposimama kaka yangu Mheshimiwa Kitandula, ndiyo wasiwasi huo huo ukaniingia baadaye mimi Mbunge wa Pemba ambaye nawawakilisha wananchi wa Pemba, hasa wa Jimbo la Chake Chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, vile vile wanavyoogopa wao, nami ndiyo naogopa hivyo hivyo. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema mengi sana kuhusiana na jambo hili kwenye *how shares* zilivyokwenda, vipi sheria ilivyokuwa, lakini Mheshimiwa Mnzava amezungumza kwa upana na kwa usahihi zaidi, hakuna ambaye hakumwelewa. Hakuna ubishi kwamba yapo maamuzi ya

Mahakama kwenye jambo hili ya kuzuia na ku-*stop* ile *merge* isiendelee. Hiyo hakuna anayebisha kwamba yapo maamuzi ya Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnapataje nguvu na mabavu ya kwenda kutaka kuyapindua yale maamuzi ya Mahakama? Maamuzi ya Mahakama kisheria yanapingwa kwa vitu viwili tu; aidha uka-*appeal* Mahakama ya juu zaidi ya hiyo ikiwa maamuzi tofauti na yale yaliyotolewa na Mahakama ya chini, jambo ambalo baada ya maamuzi yale Serikali haikufanya; au uombe *review*. Mahakama yenyewe ikae, iyapitie maamuzi yake, halafu iseme kwamba aidha ilikosea au itoe maamuzi *otherwise*. Sasa hayo yote hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnataka kuendelea na mchakato, jambo ambalo Mahakama walishasema hili linavunja sheria kwa mujibu wa Sheria Na. 8 ya mwaka 2003 kifungu cha 11, kwamba *merging* ambayo itazidi asilimia hizo za *share market* hairuhusiwi. Sheria hizo tumezitunga wenyewe. Kuna mtu kwenye mjadala asubuhi anasema sheria mbovu. Hii ndiyo *international standards,* unaitaje sheria mbovu jambo ambalo ndiyo kimataifa linakubaliwa liwe hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji akija anayatazama yote hayo ili naye awe salama, asije akawa ameanzisha biashara, katikati ya *process* biashara yake inakwenda watu wanakuja ku-*merge,* wanali-*monopolize* soko, yeye anakufa, anaondoka. Kwa hiyo, vitu vyote hivi tunafanya kwa sababu hizi ndiyo *international standards.* Kwa hiyo, tunafuata sheria kwa sababu jumuiya hizi za Kimataifa ndizo zinataka sisi tuzifuate. Kwa hiyo, tumeweka utaratibu wetu wenyewe, sheria zinatakiwa zifuatwe. Hicho ndicho nilichotaka kusisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari za kwamba nani alikwenda Mahakamani, sijui *Chalinze Cement* akaenda Mahakamani; wakati *Chalinze Cement* anaenda Mahakamani alikuwa na *locus stand* ya kwenda Mahakamani na ndiyo maana akawa *part* ya kesi. Kama *Chalinze Cement* angekuwa hayupo, maana yake Mahakama inge-*determine* kwamba huyu jamaa siyo *part* ya kesi. Hiyo kesi imemalizika, *decision* imetolewa, mnatakiwa mtekeleze. Hii tabia ya kuwaachia Serikali maamuzi ya Mahakama wayazingatie, wayakanyage kanyage, wayapige mateke, tutawapa mamlaka ambayo baadaye tutakuja kuyajutia sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Bunge, tunatakiwa tusimamie kwa hali yoyote ile, Serikali waheshimu mhimili wa hizi *tribunal* zinapotoa maamuzi. Unaweza ukaiona ni *Quasi-Judicial Body* imetoa maamuzi, lakini anaye-*reside* pale ni Jaji wa Mahakama Kuu na ile ni *binding decision* yake. Unataka kuikwepaje sasa hivi? Kama kuna hoja mpya, nilikuwa nimesoma kwenye Gazeti la *Citizen,* hoja ya watu wa *FCC* ni kwamba maamuzi yalitoka 2022, sasa hivi 2023 mazingira ya soko yamebadilika. Kuna mazingira mapya, kila kitu kimebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, lakini mazingira yakibadilika hayabadilishi maamuzi ya Mahakama. Maamuzi ya Mahakama hayabatilishwi na mazingira mapya. Maamuzi ya Mahakama yanabatilishwa na sheria pia. Kwa hiyo, unatakiwa ufuatwe utaratibu wa kisheria kubatilisha yale maamuzi ya *tribunal.* Kwa sababu maamuzi yale yanasimama, Serikali chonde chonde, heshimuni sheria kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yale yalishatoka, mnachotakiwa ni kuyasimamia, na kama kuna jambo lingine linatakiwa kufanyika, mnatakiwa mliendee kwa busara zaidi.

Hakuna anayezuia *merge* isifanyike, lakini ikiwa utafuatwa utaratibu wa sheria na utaratibu tuliojiwekea wa kikanuni wetu wenyewe. Kwa hiyo, hicho ndiyo nilichokuwa nataka kusema juu ya wasiwasi wetu tulionao baada ya kusikia kilio cha Wabunge wenzetu majirani zetu ambao kuathirika kwao ni moja kwa moja kunaenda kutuathiri na sisi. Kwa hiyo, hicho ndiyo nilichotaka kuchangia, na ninaomba Serikali wasikilize kilio chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naomba nitangaze wageni walioko hapa jioni hii. Tuna wageni 350 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, Mbunge, ambao ni Taasisi ya Wanawake na Viwanda (WAUVI) kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Katibu wa WAUVI Mkoa wa Dodoma Ndugu Haruni Mchinjai. Hawa ni Taasisi ya Wanawake na Viwanda Dodoma. Karibuni sana na Ndugu Haruni Mchinjai yuko wapi, kiongozi wao? Haya tunashukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nawakumbusha mnaofuatilia mpira, ni kwamba Yanga ameshinda mbili bila, huko wanakoendelea kucheza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, nilimwita Mheshimiwa Lucy John Sabu, wakati huo Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, anajiandaa.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii, nami niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuletea wananchi maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais, katika kipindi hiki cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 miradi ya kimkakati na uwekezaji amezalisha ajira 101,353, na katika ajira hizo, ajira za vijana ni 81,082. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi nzuri anayoifanya lakini pia na watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia kuhusu Kiwanda cha Vifaatiba cha Simiyu. Tarehe 11 Novemba, 2016 Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima *(NHIF),* Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(WCF),* Bohari Kuu ya Dawa *(MSD),* Benki ya Uwekezaji wa Maendeleo *(TIB),* Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda *(TIRDO),* Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* na Mamlaka ya Dawa na *TMD* zilisaini randama ya makubaliano ya kuanzisha Kiwanda cha Vifaatiba zinazotokana na zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo mnafahamu, Mkoa wa Simiyu ni kinara katika uzalishaji wa zao la pamba na matarajio yetu katika mwaka huu tunategemea kuzalisha tani 300,000. Wananchi wamekuwa wakihamasika sana juu ya kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kwa sababu waliahidiwa kuanzishwa kwa Kiwanda cha Vifaatiba. Jambo hili Wabunge wa Mkoa wa Simiyu tumekuwa tukilisemea mara kwa mara, lakini utekelezaji wake bado unasuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la idhini ya uanzishwaji wa kiwanda hicho uliwasilishwa kwa Wizara ya Fedha na Mipango

tarehe 26 Juni, 2019, na gharama za utafiti pamoja na upembuzi yakinifu zilikuwa ni shilingi milioni 915 ambazo zilitumika katika utafiti na upembuzi yakinifu, lakini baadhi ya wataalamu walipelekwa hadi nje ya nchi kwenda kujifunza namna gani kiwanda hicho kitaanzishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya kuanzishwa kiwanda hicho cha vifaatiba yalikuwa mawili, ambayo yamo katika andiko la mradi. Lengo la kwanza ilikuwa ni kukabiliana na soko la pamba ghafi ambazo zinaenda nje; na pili kuipunguzia Serikali mzigo wa kuagiza bidhaa zinazotokana na zao la pamba hususan upande wa Wizara ya Afya. Kama ambavyo tunafahamu, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana katika uagizaji wa bidhaa hizi, ambapo ni zaidi ya shilingi bilioni 100 zimekuwa zikitumika katika uagizaji wa bidhaa hizi. Gharama ambazo zitatumika katika kuanzisha kiwanda hiki ni shilingi bilioni 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wazo hili, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye aliubeba mradi huu kipindi akiwa Makamu wa Rais na aliubeba kama mradi ambao ni mtoto wake. Sasa tunaomba Wizara itusaidie kwa sababu mradi huu umekuwa wa muda mrefu sana na wananchi walihamasika mpaka wakatoa eneo ambalo litasaidia kuanzishwa kiwanda hiki. Mradi huu tunategemea utasaidia kutoa ajira kwa vijana, na pia utasaidia wananchi wa Mkoa wa Simiyu kuweza kuhakikisha kwamba wanaongeza thamani ya pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza thamani ya pamba tutapunguza pia kuagiza vifaa ambavyo vinatokana na bidhaa zitakazotengenezwa na zao la pamba. Sasa tunamwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake,

aweze kutupa taarifa: Je, ni lini kiwanda hiki kitaanza rasmi? Kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Simiyu wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu juu ya uanzishwaji wa kiwanda hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Mama alithamini mradi huu na ndiyo maana alikuwa kama *champion* kwenye huu mradi kipindi akiwa Makamu wa Rais, hivyo basi, tuna imani kubwa kwamba kama mtaufufua mradi huu naye atafurahi sana, na wananchi wote wa Mkoa wa Simiyu, wamekuwa wakiusubiri mradi huu kwa hamu kubwa sana, na pia tunatambua kwamba unaenda kutatua changamoto mbalimbali zinazotokana na zao hili la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi ya kuzungumza, lakini nasisitiza juu ya jambo hili, juu ya uanzishwaji wa hiki kiwanda na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Simiyu tuna hamu kubwa sana ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy John Sabu kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, na wakati huo Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu na Mheshimiwa Festo Sanga wanajiandaa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwenye Bajeti hii ya mwaka 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda moja kwa moja kwenye hoja mahususi kabisa inayohusu Kiwanda cha *SONAMCO*, kiwanda ambacho ni cha usindikaji wa tumbaku. Kiwanda hiki kimesimama kwa muda mrefu sana, toka mwaka 2010 mpaka hivi sasa kiwanda hiki hakijawahi kufanya kazi na, kiwanda hiki kiko Mkoani Ruvuma katika Wilaya ya Songea katika Manispaa ya Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Desemba mwaka 2022 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliita wadau mbalimbali, wadau wa tumbaku na walikuja pale Songea na ukafanyika mkutano mkubwa sana ambao kimsingi mkutano huu umezaa matunda mazuri sana. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada hizi ambazo anazifanya hasa katika kuangalia ustawi wa Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkutano huo pamoja na mambo mengine, kulijadiliwa namna gani ya kuweza kufufua Kiwanda cha *SONAMCO* Kiwanda cha Usindikaji wa tumbaku ambacho kiwanda hiki endapo kitaanza kufanya kazi, maana yake kina uwezo wa kuajiri wananchi 3,000 ambao watakuwa wananufaika na kiwanda hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *Vodsen Tobacco Limited* ndiyo ambayo ilionesha nia ya kuwekeza na kuweza kufufua kile Kiwanda cha *SONAMCO* cha Songea Mjini. Kwa hiyo, sasa kupitia Bunge lako hili Tukufu, naomba nichukue nafasi hii sasa kumwomba Waziri wa Viwanda na Biashara ili aweze kuwapa uwezeshaji kampuni hii ili waweze kuja kuwekeza katika kiwanda hiki na kiwanda hiki kiweze kufanya kazi mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Hussein Bashe ambaye amekuwa akifanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba anainua Sekta ya Kilimo, pia Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku Tanzania, kaka yangu Stanley Mnozya ambaye amekuwa akifanya kazi nzuri, hata kufikia hatua hii ya kiwanda hiki sasa kuweza kuanza uwekezaji wa kuinua kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye suala la *Twiga* na *Tanga Cement*. Nimesikiliza toka asubuhi, Wabunge wengi humu ndani wamechangia, nami nikawa najiuliza tu, hata kama ninatoka Ruvuma ambapo tunahudumiwa kwa ukaribu sana na *cement* ambayo inatoka katika kiwanda cha Dangote, lakini nimesikia kilio cha Wanatanga wenzetu. Kwa kuwa wana Tanga ambao wamekuwa wakililia suala hili la *cement* kwa maana ya Kiwanda cha *Tanga Cement* kuendelea kuwepo hai, nikajaribu kujiuliza, ni nini ambacho kinasababisha? Nimegundua yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Twiga Cement* wanataka kununua Kiwanda cha *Tanga Cement,* lakini katika ununuzi wao maana yake, endapo watanunua hizo *shares,* tayari *Twiga Cement* watakuwa wanamiliki *share* zaidi ya 68% ambayo kimsingi sheria inakataza. Suala hili linakinzana na sheria ambayo tumeitunga wenyewe katika Bunge lako hili Tukufu. Sasa najiuliza, ni kwa nini Serikali inadhamiria kwa makusudi kuvunja sheria hii? Kwa nini Serikali isirudi nyuma na kukaa chini kuanza mchakato huu upya ili kupitia na kuhakikisha kwamba utaratibu huu unafanyika chini ya sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumwambia Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, zisikilize

kelele hizi za wengi. Sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Urudi tena upya kwa ajili ya mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nishauri Bunge lako Tukufu hili kwamba mchakato huu uanze upya hapa tayari mchakato haujakaa sawa sawa. Kwa sababu kama mchakato umeenda vizuri hakukuwa na sababu ya kelele nyingi ambazo zimekuwa zikipigwa humu ndani, mchakato urudi upya lakini pia sheria izingatiwe hakuna sababu ya kukanyaga sheria ambayo tuliitunga sisi wenyewe kuna sababu gani? Sioni kwanini sheria ivunjwe kwa makusudi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo jingine naomba niseme kwa kuwa jambo hili linasimamiwa chini ya Baraza la ushindani naomba baraza la ushindani liheshimiwe katika maamuzi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine la mwisho kwenye eneo hili marekebisho ya sheria kama sheria hii inakinzana na maamuzi ambayo yanataka kufanyika dhidi ya uwekezaji huu. Basi sheria hii irudi hapa tuirekebishe sheria kwanza badala ya kuikanyaga sheria na baada ya kurekebisha sheria ndiyo mchakato huu tuendelee nao. Aidha, kufanyike mapitio upya ambayo yatapelekea sasa mchakato huu kwenda vizuri na niseme tu kama kutakua kuna jambo lisiloeleweka zaidi basi nimuombe Mheshimiwa Spika aunde Tume kwa ajili kuchunguza jambo hili hatimaye jambo hili liweze kuleta majibu sahihi ambayo wananchi wa Tanzania wanamatumaini na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la Matrekta ya *URSUS,* haya matrekta yamekuwa yakilalamikiwa sana na matrekta haya yameletwa kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara. Hata hivyo mpaka sasa hivi wananchi ambao

walinunua haya matrekta wamekuwa wakilalamika, wamekuwa wakisumbuliwa na makampuni mbali mbali ambayo yanahusiana na madalali, Takukuru. Ingawaje Takukuru sasa hivi awafanyi hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme kwamba tunaomba sana mchakato huu wakufatilia jambo hili kama vile ambavyo Mheshimiwa Spika aliamua kulichukua na kulifanyia kazi kwa ukaribu nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Tulia Ackson Mwansansu kwa uamuzi wake aliyouchukua na kwamba sasa mchakato huo uende kwa haraka ili wananchi wawe na amani. Tumekuwa tukipigiwa simu, wengine wanakimbia majumba yao hawana amani kwenye maisha yao lakini bado wamefilisika na yale matrekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matrekta ni mabovu, unachukua tu trekta kitendo cha kuwa jipya kabisa unaliingiza shambani, unaambiwa na fundi limekatika mgongo mara limekatika sijui kifudifudi. Kwa hiyo, haya matrekta hayana nia njema kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, niombe Wizara pamoja na eneo ambalo Mheshimiwa Spika ameona wafanyie kazi jambo hili waharakishe huu mchakato hili wananchi waendelee kuwa na amani kwa sababu kinacho endelea huko mitaani inawezekana kabisa tukapata majibu ambayo siyo mazuri kwa wananchi yanayoendelea huko mtaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EPZ* naomba leo nizungumze na Waziri mwenye dhamana hii. Kwenye eneo hili la Viwanda na Uwekezaji *EPZ* walichukua maeneo ambayo yako kwenye Kata ya Mwenge Mshindo Wilaya ya Songea Mjini Manispaa ya Songea. Maeneo haya kimsingi yana miaka karibu kumi na tano wananchi hawajalipwa fidia ninaomba Waziri atakapokuja

aeleze Aidha, kama hawezi kulipa pesa zote shilingi bilioni tatu na milioni mia nane azikate pale katikati alipe kwa awamu mbili tofauti wananchi wale wanateseka wamekuwa wadumavu hawana maendeleo yeyote, hawawezi kuendeleza chochote kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana jambo hili uweze kulishughulikia na utakapo kuja hapa na niseme Mheshimiwa Waziri endapo kama jambo hili utotoa majibu yanayoeleweka ninakusudia kuondoka na shilingi yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, wakati huo Mheshimiwa Festo Sanga, anajindaa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa kabisa nitumie fursa hii kukushukuru wewe na kiti chako kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kwa ustawi wa Taifa langu na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba ni–*declare* Mwalimu Dkt. Ashatu ni mwalimu wangu alienifundisha Mzumbe *University* masomo nikiwa mwaka wa kwanza alinifundisha masomo ya uchumi. Kwa hiyo, ninachangia Bajeti ya Waziri ambaye ana sehemu ya kunifanya kuwa hivi nilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza kabisa ninakwenda kuchangia maeneo matatu la kwanza *Statistics* za Nchi zinaonyesha Kanda ya Mikoa zaidi ya kumi na nne inayojihusisha katika shughuli za kilimo cha pamba ambacho takwimu zinaonyesha ndani ya Taifa letu la Tanzania wakulima waliyojiajiri katika Sekta ya Kilimo ya Pamba wanakadiriwa kuwa takribani wakulima laki sita mpaka laki saba na wengi wanatoka kwenye Mikoa ya Mara, Geita , Mwanza, Simiyu, Tabora, Shinyanga, Singida na baadhi ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, chama kilichopo madarakani kwa mara ya kwanza ninaona dhamira ya Rais Samia kwenda kuandika *unique record* katika Taifa letu kwa sababu ya *initiative* hizi zilizofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza; nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Mwalimu wangu Hotuba ya Waziri inaonyesha Serikali imedhamiria kuhakikisha kwamba wawekezaji wote wanaofanya uwekezaji katika viwanda vya pamba mwaka huu pamba yote ya kulima niliyowataja kutoka Mikoa hiyo ambayo wanafanya jumla ya watu waliyojiajiri hizi ni ajira zaidi ya laki saba Rais wetu ameonyesha uzalendo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu toka nimekuwa Mbunge *term* yangu ya kwanza mwaka 2015 nimekuwa nikiwasemea wakulima wa pamba juu ya uhaba wa bei ndogo wanayoipata katika mazao yao ya pamba. Lakini kwa juhudi hizi za Rais tunaambiwa ya kwamba wakulima wote watakwenda kuuza pamba yao kwa viwanda vya ndani na nini kinakwenda kufanyika? Tunaona mikakati ya Serikali kuhakikisha

kwamba viwanda hivi vinakwenda kutengeneza vitambaa vitakavyo ongeza thamani ya pamba ya mkulima na kuongeza *export* nje hilo litakwenda kuleta nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *statistics* Waziri alizozisoma zinaonyesha *sales* yetu ya nje ime–*raise* kwa asilimia 64.4 na vitu vilivyochangia ku–*raise* kwa hiyo *sale* ya nje ambayo ni *dollar* kama milioni 4,000 bidhaa zinazo ongoza ni *gold, cotton, coal* na mengine kwa mpango huu Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie mwalimu wangu ninakupa *big up* sana, tunampa *big up* Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hichi anachokifanya anatafsiri kwa vitendo yale yote yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kumsadia mkulima wa zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuambie, nataka nilipe Bunge lako tukufu taarifa; wakulima wa pamba katika Taifa letu wanachukua idadi ya ajira ya watu wanaokadiriwa laki saba. Tukiweza kuwasaidia wakulima kuuza pamba ndani na bei yao ikapanda hiyo ni sawa na kusema ya kwamba *dollar* milioni 4,000 tulizozirekodi za *sale* kwa sababu tutakuwa tumeongeza thamani tutakwenda kuifanya Tanzania kupata fedha za kigeni na wakati huo tutakwenda kuinua pato moja moja la zaidi ya ajira laki saba nje ya ajira ambazo zitakuwa zimeguswa kutokana na *spiral over impact* ambayo itatokea katika uwekezaji huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mkija na mipango mizuri lazima tutawaunga mkono, lazima tutawasemea hongera sana Waziri, hongera sana Mwalimu wangu Dkt. Ashatu sisi tuna kuunga mkono katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo Rais Samia Suluhu Hassan anakwenda kuweka rekodi nyingine Taifa letu lilikuwa linakumbwa na uhaba mkubwa sana wa uzalishaji wa

sukari katika nchi. Nimesoma ripoti kutokana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri *statistics* zinaonyesha kwa juhudi za makusudi zilizofanywa na Serikali ya Rais Samia uwekezaji katika viwanda vya sukari umeongezeka na tume–*observe* ongezeko la tani 80,000 kwa mwaka peke yake wa 2022/2023 nani kama Mama Samia jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwenye hilo hatuna sababu ya kuacha kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwezesha mikakati hii na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha ya kwamba tunapanua uwekezaji wa zao hili la miwa pamoja na kuongeza uwekezaji katika uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa nimesoma ripoti viwanda vinaonyesha *TCDS* zao walizokuwa wameziweka mwanzo *expansion* itafanyika zaidi kuhakikisha ya kwamba sukari inakuwa ya kutosha katika taifa letu tuweze kutosheleza soko la ndani na kufanya *exportations* na kiusababishia Serikali yetu kupata faida zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu; nalotaka kulizungumzia nina mpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Tauhida inawezekana ameondoka. Mheshimiwa Tauhida amesema Mheshimiwa Waziri wewe ni msimamizi karibia wa Wizara zote katika masuala ya uwekezaji jambo ninalokushauri Mheshimiwa Waziri wangu na Mwalimu wangu Ashatu tunakuomba uweke jicho lako la karibu sana katika Taifa letu lazima tuwe na kitu kinaitwa *continuity* katika *investment* hili ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajitokeza wakati mwingine makampuni yamekuja yamewekeza, wamefanya uwekezaji mkubwa, wanapotaka ku–*renew* mikataba wanakuja na *plan*

kubwa za kuweka uwekezaji, sisi tunaona kwamba mtu akiwekeza eti miaka kumi, ishirini eti miaka mingi. Kuna mataifa mengine makampuni yanawekeza mpaka miaka mia mbili na rekodi zipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania makampuni yanakuja mtu anawekeza miaka ishirini, kwa mfano nilikuwa natolea mfano hawa watu wa Songas. Kampuni ya Songas imewekeza kwenye umeme na wamefanya juhudi kubwa kuzalisha umeme wa uhakika chini ya Wizara ya Kaka yangu Mheshimiwa January Makamba leo kwenye kusaini mkataba tunasikia eti wanabembeleza Serikali muwaongeze mkataba hivi jamani kwa umeme tuliokuwa tunauziwa senti sita na watu hawa na hawa ni mashirika ambayo wamekeza Serikali za Uingereza na Norway kweli watu hawa sasa hivi waanze kutuomba kuongeza mkataba na Taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito. Tujenge utamaduni wa kuwa na *continuity* ili tujenge *trust* kwa *investors* walioko nje wajue umuhimu wa kuweka Tanzania watapewa nafasi ya kutosha. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa kutoka wapi?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unilindie muda wangu hizi taarifa hizi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

## TAARIFA

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kumlindia muda nataka nimpe tu taarifa kwa sababu amewataja Songas, *TPDC* ambao ni wabia wakubwa wa Songas kwa miaka yote waliyokuwepo hapa nchini wameokoa zaidi ya trilioni kumi na sita kwa hiyo nadhani Mheshimiwa Kingu anahoja ya msingi namuongezea tu nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu, unapokea taarifa? Na muda wako umekwisha.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa hiyo ninapokea nimalizie, nimalizie na kama ametaja Shirika la Serikali mimi naunga mkono Mheshimiwa Waziri, tunakuomba Wizara yako inagusa Wizara zote katika mambo ya biashara, usiwekewe mipaka fuatilia uwekezaji katika Wizara zote tumsadie Rais na sisi tuna kuunga mkono mwalimu wangu, kiongozi wangu tuko pamoja na wewe kazi iendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu, kwa mchango wako. Nilimuita Mheshimiwa Festo Sanga, wakati huo Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya anajiandaa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyoko mezani ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Nina mambo matatu wakati Mheshimiwa Elibariki Kingu anachangia kuhusu mafanikio ya Mheshimiwa Rais kwenye Uwekezaji wa Sukari na hili waweze kutambua Watanzania ni kwa mara ya

kwanza wakati wote wa Ramadhan hatujaona sukari ikihadimika. Hili ni jambo kubwa sana ambalo Mheshimiwa Rais amelisimamia la Mfungo wa Ramadhan umeenda vizuri hakujakuwepo na kelele yeyote kuhusu sukari. Kwa hiyo, ninaunga sana haya maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Kingu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo matatu jambo la kwanza ni jambo la lumbesa Mheshimiwa Waziri ni muhanga mkubwa sana wa changamoto ya lumbesa na ninavyozungumza saa hizi Wananchi wa Makete na Mikoa mbali mbali nchini yawezekana wanaweza wakawa na nyota ya nuru na ya matumaini kwamba labda Serikali inaweza ikatoa mwanga kuhusu suala la lumbesa kwenye Taifa letu. Mheshimiwa Waziri mimi nitahitaji kushika shilingi kwa sababu gani? ukikaa na Mheshimiwa Bashe anakwambia suala la lumbesa ni suala la Wizara ya Viwanda na Biashara na unakuta ana asilimia mia moja ni sahihi kwa sababu nyie ndiyo watu wa vipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu la Tanzania ndiyo Taifa pekee ambalo tunapima mtu kwa kumkadiria kwamba gunia likifika kiwango hiki ndiyo limetimia gunia moja. Ukienda Kenya, ukienda *East Africa* zote nchi hakuna utaratibu wa kupima kwa kumkadiria mtu kwamba kwa kimo hiki ndiyo gunia la vitunguu limetosha pale Singida, kwa kimo hiki gunia la vitunguu limetosha pale Iringa na kwa kimo hiki viazi gunia limetosha. Mheshimiwa Waziri *it's a high time now* tuchukue nafasi ya ku–*introduce* vipimo kwenye upimaji wa mazao yote nchini kwa sababu gani? Suala la lumbesa *is a mindset* mtu anadhani gunia likiwa limefungwa kile kilemba cha juu ndiyo lumbesa kumbe hicho hicho kilemba ukienda kuweka kwenye mizani yawezekana hakijafika gunia la kilo mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *concept* ni hii kilo mia ndiyo sawa sawa na gunia moja hasa wakulima tuwatoe kwenye hili ombwe lakudhani kila kitu ni lumbesa tu–*introduce* vipimo Mheshimiwa Waziri una nafasi ya kukaa na Tamisemi kuna *selling points* maeneo tofauti tofauti kwenye Kata zetu, kwenye Vijiji vyetu wekeni mizani wakulima wasiibiwe na mfanyabiashara asiibiwe ili *concept* ya *mind set* ya suala la lumbesa iweze kufa kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana sana sisi Watu wa Makete navyo zungumza saa hizi wakulima kule, wafanyabiashara wanagombana na halmashauri ni lumbesa lumbesa sasa haieleweki yupi anaibiwa? yupi haibiwi? haieleweki kwa sababu gani? Hakuna mizani ya kupima *concept* yetu ni ile ile mbona sukari mnapima kwenye kilo? Mbona unga mnapima kwenye kilo? Mbona nyama mnapima kwenye kilo? Na hata parachichi nilisema limeanza na mguu mzuri linapimwa kwenye kilo. Ingekuwa parachichi haliuzwi kwenye kilo ingeleta matatizo makubwa kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Wizara kesho mnavyokuja kutusaidia kufunga hoja mtupe majibu suala la lumbesa kwenye taifa letu hili Wananchi wangu wa Matamba, Wananchi wangu wa Makete, Wananchi wangu wa Kinyika waweze kupata suluhisho la suala la changamoto la lumbesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili kwa Mheshimiwa Waziri wakati nazungumza hapa kuna suala la Kariakoo nimesoma nimepitia Hotuba yako yote swali langu moja tu nataka nijiulize Wafanyabiashara wa Kariakoo anae watetea ni nani kwenye nchi hii? kwa sababu nimepita kwenye Hotuba yako sijaona chochote kinacho zungumzwa Kariakoo *is our own* Dubai.

Kariakoo ndiyo Dubai ya Taifa letu na ndiyo iko chini ya Wizara yako, iko chini ya Wizara ya Fedha, iko chini ya Wizara nyingi tu ni Mpango gani Mkakati wa Serikali yetu kuhakikisha wanazidi kuinusuru Kariakoo? Kwa sababu kiuhalisia Mheshimiwa Waziri Kariakoo inazama hilo ndiyo ukweli ulioko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kaangalie floo ya wafanyabiashara wa kigeni Kariakoo imepungua kwa asilimia zaidi thelathini zaidi ya asilimia arobaini kwanini wamepungua? Mheshimiwa Waziri ni vyema mkaenda mkafanya vikao na wafanyabiashara Kariakoo mkakubaliana ni nini kifanyike ili Kariakoo kama Dubai yetu iweze kuinua, ili kama Kariakoo Dubai yetu isizame saa hizi Kariakoo *is moving to* Uganda Kampala, Kariakoo *now is moving to* Lusaka, Kariakoo *now is moving* to Lilongwe biashara sasa watanzania imegeukia kwenda kwenye mataifa ya Jirani. Tumefungua milango kwenye mataifa ya Jirani ndiyo tukafate bidhaa wakati sisi ndiyo tulikuwa tunalisha *East Africa* nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii bidhaa nyingi tunachukua kutoka kwenye mataifa ya *East Africa* wapi tumekwama kama Taifa? Kama Mawaziri ninawaomba sana jisikieni uchungu kuona Kariakoo inazama kama kuna changamoto za kikodi kama Mbunge nashauri kaeni na Wizara ya Fedha, kaeni na *TRA* mjue jinsi gani mnaweza mkainusuru Kariakoo na changamoto za kikodi Kariakoo ikatengama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unakaa na mfanyabiashara anasema naenda kufata shuka Uganda, naenda kufata mizigo Uganda *why* Uganda *and not* Kariakoo *there is a problem* tunaomba Mheshimiwa Waziri iangalie Karikoo kwa jicho la karibu kwa sababu utasema mbona unaizungumzia Karikoo tu kwanini uzungumzii Arusha? Kwanini uzungumzii Mbeya? Sisi Kariakoo kwa

maana Kariakoo ndiyo inalisha Arusha, ndiyo inayo Ilisha Mbeya lile ndiyo shamba kubwa linalolisha Taifa letu ni lazima na ninyi muichukue hii kama Dubai yetu mkaiangalia kwa mtazamo wa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wamepungua nenda *Msimbazi Post*, nenda *central* utakuta wafanyabiashara wa Kikongo, wafanyabiashara wa Nigeria wamekamatwa pale. Kama umekamata risiti ya mzigo iko hovyo *deal* na yule aliyetoa ile risiti ni nani usi-*deal* na wafanyabiashara wa kigeni. Ukimwi-*intimidate* huyu unazuia kesho kurudi, keshokutwa anatafuta njia nyingine ya kwenda. Tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri ucheki Kariakoo kwa jicho la karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ni kuhusu uwekezaji kwenye Mkoa wa Njombe. Mheshimiwa Waziri ninakuomba sana, suala la Liganga na Mchuchuma, na kwenye hotuba yako hapo ukipitia umezungumzia Liganga na Mchuchuma unasema hivi, matumizi ya chuma nchini yameongezeka kutoka tani 226,000 hadi tani 1,000,000; tangu nimezaliwa inazungumzwa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi ya *SGR,* tuna miradi ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, na uzuri *SGR* sio kwamba imekomea hapa, inaendelea. Hii miradi yote inayotumia chuma. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Liganga na Mchuchuma ianze kufanya kazi ili tuweze kunusuru Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilikufuata kwenye meza yako nikakuomba; sisi Makete tuna *wheather* ambayo inaweza kuzalisha mianzi kwa ajili yakutengeneza *toothpick* lakini leo hii *toothpick* zinatoka China. Ninaomba kwa fursa ambayo unayo usi-*concentrate* sana kwenye *coastal zone corridor* kwenye

uwekezaji. Kuna huku pembezoni mwa nchi kama Makete kuna sehemu nzuri ambazo unaweza ukawekeza na ukalisaidia Taifa letu kwenye maeneo ya kilimo na viwanda mbalimbali. Tunaomba sana utembelee kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi sina mambo mengi sana ni hayo mambo yangu matatu, Mheshimiwa Mungu akubariki na ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Sanga kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya lakini atachangia kesho. Kwa hiyo tunaendelea na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, wakati huo Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro pamoja na Abdul-Hafar Idrissa Juma.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mabula amenipa hapa Biblia zote mbili ya Agano la Kale na Agano Jipya; yote nitayatumia kwa nafasi yake. Agano la Kale Wizara ya Kilimo ndio wazalishaji wa mazao yote. Nimetoka Iringa nimeona alizeti nyingi, nimekuwa hapa Dodoma nimeona alizeti nyingi, nimekuwa Singida nimeona alizeti nyingi, Kigoma alizeti nyingi; inaonekana mikoa zaidi ya 20 sasa inalima alizeti. Kwa hiyo kwa sababu uzalishaji upo upande wa Wizara ya Kilimo ambalo ni Agano la Kale, jipya ni Wizara ya Viwanda na Biashara. Hapa ndipo tunataka tuzungumze vizuri. Unapotaka kulinda viwanda lazima udhibiti mianya yote ya magendo na u-*fix* kodi ambayo itasababisha bidhaa yote ya nje isinunuliwe ili kulinda viwanda vyako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka kuzungumza nini. Mikoa ambayo inalima alizeti, wakulima wamekopa benki, TADB imewapa fedha. Wasipouza mbegu yao kwa bei nzuri, TADB inafilisika, NMB inafilisika, CRDB inafilisika na mwananchi anafilisika. Viwanda wamekopa kwenye mabenki, wasipozalisha; kwa sababu taarifa wa Mheshimiwa Waziri imesema asilimia 25 ndivyo viwanda hivi vinazalisha maana yake miezi minne kwa mwaka, viwanda hivi vinakwenda tena kufilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tukiwa kama nchi tunafilisi viwanda kwa sababu ya kuachia *room* ya watu kuingiza bidhaa zao kutoka nje, hatuwasaidii Watanzania. Kwa hiyo Agano Jipya linapaswa litimilize Agano la Kale, kwamba wanazalisha lakini Agano Jipya linahakikisha kwamba watu wanauza. Kwa hiyo mwaka jana tuliweka kodi *equity duty* kwa sababu ya kuogopa mfumuko wa bei; sasa tumekwenda kuwauwa wakulima wetu. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara huko kwako ndiko wanakolima alizeti, kwa hiyo tunakwenda kuwafilisi wapigakura wako, lakini tunakwenda kuwafilisi wapigakura wa Mwigulu, hapo Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Mkalama wanalima alizeti nyingi. Kwa hiyo niombe hivi, mwaka huu tusiruhusu tukaondoa kodi ya mafuta ya nje, tukiruhusu tunakwenda kufilisi viwanda vyetu na wakulima wetu. Leo mkulima wa alizeti anauza shilingi 600 kwa kilo ambayo alikuwa anauza shilingi 900 mpaka 1000, hiyo huwezi kumlinda mkulima. Lakini mwenye mafuta anakwenda kuuza dumu 60,000 badala ya 70,000, maana yake huwezi kulinda viwanda. Kwa hiyo hatuwezi kulinda viwanda kama tunaruhusu magendo, tunaruhusu kuondoa kodi kwenye kwenye mafuta ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana na huu ndio ugonjwa ambao umeua viwanda vingi duniani. Hatuwezi kuendelea kukubaliana na jambo hili, lazima sasa Serikali ione namna ya kuweka kodi kwenye mafuta yanayotoka nje, kwa sababu mikoa yote 20 hii inalima alizeti. Na kwa hali hiyo ukiangalia Iramba na Singida yote, ukiangalia Dodoma hii wananchi maisha yao wamebadilisha kulingana na alizeti ambayo wanakamua ndani wanauza barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana, ili nchi iendelee lazima tuwe na wivu wa kuwaonea wivu wakulima wetu waendelee kuzalisha kuliko kuruhusu mataifa nje kuingiza mafuta. Niombe sana hili kwa mwaka huu Wabunge tusikubali kuondoa kodi kwenye mafuta ya nje, tutakuwa tunaua viwanda vyetu. Hili ni simu, ni kama vile Biblia inavyosema, kwamba asiyempenda wa nyumbani kwake ni mbaya kuliko asiyeamini. Kwa sababu sisi tunawapenda wa nje tunashindwa kuwapenda wa kwetu, tunaruhusu kuondoa kodi ili watu waingize mafuta wa kwetu wanabaki maskini, hapana. hii ni Hapana, lazima tukubaliane Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, lakini nimemsikiliza vizuri mchangiaji King, na mimi nilikuwa najiuliza, mikoa 17 inayolima pamba leo pamba yote tunaiuza nje; ni umaskini mtupu. Haiwezekani tukazalisha, tukaendelea kuuza *raw material* badala ya kuuza *production* iliyokamilika. Na hili nakwenda kuandika historia kwamba Rais mwananke ameamua kuhakikisha kwamba maghala yanatengenezwa hapa; na hii ni lazima Serikali i-*set* fedha kama ambavyo imependekeza. Hatuwezi kukubali kila mwaka kurudi pale pale. Nchi hii tuna miaka 60 ya uhuru hatuwezi kuwa tunauza *raw material* tunashindwa ku-*produce material* yetu hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili linakwenda kuweka rekodi, Waziri wa Viwanda na Biashara mwanamke wewe, na hili linakwenda kuweka rekodi, Spika wa Bunge mwanamke, Tulia huyu hapa. Kwa hiyo haya mambo hayatokei hivi hivi. Kwa hiyo niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi mzuri ambao sasa anakwenda kuuchukua kwa ajili ya pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua tukizalisha majora hapa, kwanza tukijenga tu kiwanda hiki ni zaidi ya bilioni 500, mfanyabiashara wa kawaida hawezi kupata fedha hizi. Hata ukienda kwenye benki wanakuona kama umechanganyikiwa hivi kwa sababu mitaji ile ni midogo na wanaogopa *risk* kuwekeza kwa mtu mmoja. Kwa hiyo Serikali lazima i-*set* fedha kwa sababu kama tunajenga madaraja, tunashindwaje kujenga kiwanda? Kwa hiyo hili ni jambo zuri. Na tukiweza hiki kiwanda, kwamba bidhaa ya pamba ina vitu vingi ambavyo Mheshimiwa Lucy alikuwa anazungumza hapa; kama vile vifaa vya hospitali na vifaa tiba, vinatokana na mabaki ya pamba inayotoka kwenye majora. Kwa hiyo tunakwenda ku-*save* hela nyingi ya kuagiza pamba nje; dola ya kigeni itakuja badala ya kuipeleka nje *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, kama watu watakuja hapa Afrika kununua, Afrika tukawa tunauza majora, hapa Tanzania, akija hapa Mkongo analala hoteli, anapanda taxi, anakunywa soda, anakunywa bia anapata na kamchepuko kidogo mambo yanaendelea. Kwa hiyo kuna vitu vingi ambavyo tutavifikia kuliko sasa. kwa hiyo mimi niombe Serikali iangalie wigo mpana, isiangalie tu kwamba tunakwenda kuzuia fedha za nje, tunazuia fedha kwenda nje, tunataka fedha za kigeni ziingie ndani ili zisaidie ukuaji wa kiuchumi hapa Tanzania. Na ndipo

tutawafanya wakulima walime wakiwa na uhakika bei wa soko zuri la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo soko la dunia hatuna uwezo nalo. Mwaka jana tumeuza pamba 1,560 mpaka 2,000 mwaka huu uki-*google* wewe unapata senti 0.71. Ukiondoa gharama zingine unapata senti 75. Kwa hiyo maana yake pamba inakwenda kununua kwa 1,060. Kwa hiyo tukiwekeza hiki kiwanda ndio mwarobaini na ndipo kukuza uchumi wa nchi hii. Halafu nikuombe; kwa sababu pamba inalimwa sana, mikoa 17, na tayari pale katikati Simiyu na Magu kuna eneo lipo basi muangalie namna ya kuleta maeneo hayo ili kuongeza uzalishaji wa zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kufanya *research* viwanda, vyetu hivi; kwa mfano viwanda vya miwa ambavyo vinatoa sukari, ni viwanda ambavyo wawekezaji wake wamejitahidi sana, na kwa kweli hata uzalishaji unaendelea. Nilipata kutembelea kiwanda cha Kagera *sugar* nikakuta wana mitambo matata ya kimarekani ambayo sijawahi kuona. Wanafyeka mapori kuongeza uzalishaji na bado wanahitaji. Sasa, yaandaliwe maeneo ambayo hayalimwi, yamebaki waongezewe kule Kagera *Sugar* ili waweze kulima na kuzalisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuwashauri pia wafanye *research* nzuri. unajua kwenye miwa si tu unaweza kutoa sukari na *molasses* pekee, Hapana; kwenye miwa unaweza uka-*produce* mpaka *diesel,* ipo kwenye miwa, kama tuta-*set* vizuri viwanda. Kwa hiyo lazima Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ifanye *research* ya kwamba zao hili linaweza ku-*produce* vitu gani ndani; huko ndiko kukuza mnyororo wa thamani. Hata

ukienda kwenye mkonge, mkonge sio umera pekee, lile zao la katikati ninyi watu wa Tanga lile likisindikwa linapandwa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunataka mfanye *research* kwa sababu tatizo tuna akili nyingi lakini maarifa hatuna, sasa hilo ndilo tatizo. Sasa tutumie maarifa kufanya *research* ili kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye viwanda ambavyo ni vya kisasa zaidi na ambavyo vinaweza kutoa vitu vingi kwenye mmea mmoja. Hili ndilo itakuwa ni suluhisho, kwa sababu hata ukienda Brazil kiwanda cha sukari kikikamua sukari kinatoa bidhaa nyingi mpaka kwenye mafuta lakini sisi bado tunabaki kwenye sukari, *molasses* na makapi mengine, tuondoke huko. Serikali iwasaidie wawekezaji wa sukari kufikia hatua hiyo ya uwekezaji wa kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, nilimwita Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro aweze kuchangia.

**MHE, NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye mchango wangu nami naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake mzuri, uongozi bora, uongozi unaonesha matumaini na dira dhabiti ambayo inaonekana kabisa kwamba nchi yetu inakwenda kuendelea na inaondoka kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji Waziri wa Wizara hii pamoja na Katibu wake Mkuu kwa kazi nzuri na uongozi mzuri walionao kwenye Wizara hii. Kwa kweli tunaona mambo yote ya uwekezaji, viwanda na biashara yako *consolidated* na yanachakatwa na kuratibiwa kwa pamoja katika namna ambayo kwa kweli tunaona kwamba Taifa letu linasogea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu asubuhi Waheshimiwa Wabunge wa Tanga, Pemba na wengine kutoka Kanda ya Ziwa wametoa michango yao kwenye sakata la uuzwaji wa Kampuni ya Tanga ambayo inataka kutwaliwa na Kampuni ya *Twiga Cement*. Yamkini watu wengi wamevurgwa na michango mbalimbali inayotolewa na pande mbili tofauti zenye mawazo tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tangumwaka jana wamekuwa wakifatilia jambo hili. Kwamba, mtu mwenye hisa zake, *Tanga Cement* anataka kuuza hisa zake kwa mtu ambaye amemchagua yeye kwa sababu anazozifahamu yeye. Mnunuaji anataka kununua zile hisa. *Fair Competition Commission (FCC)* wamefanya uchuunguzi na kuja na mapendekezo ya namna bora hili jambo linavyotakiwa kufanyika. Wapo wadau wengine Chama cha Walaji na chenyewe kikaenda mahakamani kushitaki kwamba zoezi lile libatilishwe; na mahakama yetu ambayo inafanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria ambazo tulizitunga sisi wenyewe hapa Bungeni na yenyewe imetoa hukumu kwamba zoezi lile lisiendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwaka huu mwezi wa pili tumeona *FCC* tena wametoa tangazo kwenye Gazeti la *Daily News* kwamba mchakato ule uendelee kama kawaida. Mimi sipingi kwamba mtu mwenye hisa asiziuze lakini tusi-*ignore*

mawazo ya Wabunge, wananchi na walaji ambao tangu asubuhi wamesimama hapa wakapaza sauti na kuonesha wasiwasi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Ngara sisi *cement* tunanunua shilingi 24,000 inayotokea Dar es Salaam, *cement* inayotokea Tanga huko ambako wanataka kuuza *share* tunanunua shilingi 22,000. *Cement* kuizalisha kwa siku moja, kiwanda kinaweza kikazalisha hata mifuko 5,000 lakini sisi wakulima ili tuweze kupata fedha tunalima mahindi, kuvuna mahindi ni miezi mitatu na siku nyingine zinaongezeka pale kutegemeana na mbegu uliyoipanda. Debe moja la mahindi nikiliuza ilitakiwa niweze kununua mifuko mitatu hata minne ya *cement.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi mwananchi wa nchini ili niweze kujenga nyumba nzuri na niweze kutumia saruji maana yake ni kwamba kilimo ninachokifanya, ninachokivuna hakitoshelezi kwa sababu bei ya bidhaa ziko juu ikiwemo saruji. Wasiwasi wetu tunaoupata ni kwamba kwenye mchakato huo wa mauziano inawezekana kabisa anayetaka kununua pengine ipo siku kwa kuwa yeye wameshatuambia *FCC* kwamba huyu akishanunua atakuwa ana *share* kubwa kwenye soko anaweza akafanya chochote. Akitaka kuua wadogo anaweza akashusha bei, akitaka kupata faida kubwa anaweza kupandisha bei, vile yeye anavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo hatuwezi kuliona. Vilevile anaweza akapunguza uzalishaji ili kuwe na *scarcity halafu* bei iweze kuongezeka. Hayo yote tunayoyazungumza ni vitu ambavyo tunavifikiria. Yamkini Serikali yetu kupitia kwa Dkt. Ashatu wameshaingia kwa undani kwa upana wake kwenye hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba kuishauri Serikali, hivi kuna shida gani hii wizara ikitupa semina Wabunge wakatukalisha pale Msekwa tukaelewa undani wa hili jambo, kuna shida gani? Kwanza sikumbuki kama amewahi kutupa semina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza ninaomba hii wizara watuletee taarifa ya kutosha, watueleweshe mchakato mzima ulivyo. Ninaogopa kwamba wananchi wangu wa Ngara na mimi nikiwemo tunanunua bidhaa kwa gharama kubwa sana. Nimeambiwa *Tanga Cement* wananunua shilingi 15,000 mfuko lakini sisi Ngara shilingi 24,000 wote ni watanzania ndani ya Taifa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba busara na hekima zitumike katika jambo hili ili kuhakikisha kwamba huko mbeleni, miaka minne, mitano inayokuja Watanzania wasianze kutuzodoa na kutukumbusha kwamba Waheshimiwa Wabunge walisema mle Bungeni kwamba hili jambo lingeweza kuleta athari kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana *FCC* ama taasisi yoyote ndani ya Serikali iweze kupewa mamlaka ya kufanya *regulation* ya bidhaa za ujenzi ikiwemo saruji na nondo. Kuna kipindi unashangaa nondo inauzwa shilingi 18,000, unakwenda dukani baada ya miezi miwili unashangaa nondo ya mita 12 inauzwa 22,000, bei zinakuwa zinabadilikabadilika. Sasa sijui *regulator* ni huyo huyo *FCC* ama sijui ni nani. Niombe Serikali itazame kwa upana wake namna ambavyo hizi bidhaa za ujenzi ikiwemo saruji na nondo ziweze kuwa *regulated* ili kuhakikisha kwamba Watanzania hawaumii kwenye kununua bidhaa ndani ya Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie mchango wangu kwenye enelo la Liganga na Mchuchuma. Uvumbuzi wa makaa ya mawe Mchuchuma ulifanyika mwaka 1860, ninazungumza miaka 163 iliyopita. Wajerumani walikuja wakagundua makaa ya mawe. Vivyo hivyo uvumbuzi wa chuma ulifanyika mwaka 1898 miaka 125 iliyopita. Wazungu wakavumbua wakaondoka, nchi yetu kupitia *NDC* wakatafuta mwekezaji, wakatangaza na zikajitokeza kampuni 48 ku-*bid*. Kati ya kampuni 48 ni kampuni moja tu ya Kichina ilionesha uwezo mkubwa, ilishinda tenda kwa kuomba kufanya miradi yote miwili, ya chuma na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba ule ukiusoma unakuta una changamoto, kwanza kwenye ule mkataba unakuta kuna *partner* ambaye hajulikani ni ile kampuni ile ya Kichina, Watanzania and *others* ambao *unknown* yaani hawa hawajulikani wako kwenye *question mark*. Hata hivyo, nchi yetu ikapata 20% kwenye ule mkataba mbali na hilo huyu Mchina akatakiwa kuleta dola 600,000,000 ili fedha hiyo sehemu yake itumike kwenda kutoa fidia kwa Watanzania wa kule Ludewa. Kwa bahati mbaya mambo mengi hayajafanyika, nampongeza Mama yetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutoa fedha ili fidia iende kutolewa kwa wale wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti ulifanyika kwenye lile eneo, leseni ikapatikana akapewa Mchina na leseni imepatikana baada ya mkataba kuwa umesainiwa. Sasa, hivi kweli hatuna uchungu mali ameigundua mzungu, mikataba tumewapa watu wa nje, hata leseni tumezichakata sisi wenyewe zote tumepeleka nje, Watanzania, hakuna Mtanzania hata mmoja amepewa leseni pale, mzigo wote leseni yote wanamiliki wale wachina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya ziko taarifa kwamba Kampuni ya kichina sasa imemilikiwa na Jimbo la *Sichuan.* Naomba kuishauri Serikali makaa ya mawe ni dili, ukiwa na mali huna sababu ya kuhangaika. Nimeambiwa Mchina amekuja sahivi wako hapa Tanzania lakini yule *original* mwenyewe hayupo, kuna wengine wamekuja pengine ni wale *others*, unaweza ukakuta na mimi nikikomaa kwenye wale *others* naweza nikawa ni mimi mwenyewe, maana wale hawajulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali wakati wa kuvuna na kuuza makaa ya mawe ni sasa, tufanye *negotiation*, tufanye *negotiation* ikamilike wakidengua dengua tumeshalipa fidia, leseni zikatwe pale, Watanzania wapewe, makaa ya mawe sio kitu cha kubembeleza bembeleza kama ilivyokuwa zamani, unachimba hapo hapo, mteja yuko hapo hapo, Serikali inauza hapo hapo, tunaingiza pesa hapo hapo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa unyeyekevu mkubwa, Serikali ichukue mawazo haya, tuanze kuchimba makaa ya mawe na chuma sasa, baada ya kumaliza *negotiation* na hata ikishindikana hiyo *negotiation* Serikali ichimbe, Watanzania wachimbe, tupate pesa ndani ya nchi yetu, Watanzania tutajirike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja Mwenyezi Mungu akubariki kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro. Nilimwita Mheshimiwa Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa aweze kuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii tuliyo nayo mezani. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali na Waziri mwenye dhamana, lakini kwa nafasi hiyo pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya kuhakikisha kuwa wawekezaji wanakuja Tanzania na matokeo ya uwekezaji yanatokea, tunaanza kuyaona. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuhakikisha anasimamia maono ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii tumeelezwa hapa na Waziri wakati anasoma bajeti yake kwamba mpaka sasa mpaka mwezi wa pili bajeti, fedha alizopokea kutoka Wizara ya Fedha hazijafika 60%, lakini Wizara hii ndio ambayo inaleta wawekezaji ambao ndio wanaolipa kodi na kulisaidia Taifa katika masuala mbalimbali. Nitumie nafasi hii basi kuiomba Wizara ya Fedha kwa sababu maziwa wanayoyakamua sehemu kubwa yanasababishwa na Wizara hii, basi Wizara hii waipe fedha kwa wakati hasa fedha za maendeleo ili waendelee kutoa yale ambayo yanategemewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza pia ipi dhamira ya uwekezaji katika Taifa letu. Michango mingi tumezungumza mambo mengi mazuri kwa ajili ya wananchi wetu, lakini naamini dhamira ya uwekezaji ni kuhakikisha tunakuza ajira katika Taifa letu, ni kuhakikisha tunaiongezea Serikali kipato kwa kodi, lakini ni kuhakikisha bidhaa zinapatikana bila usumbufu kwa wananchi wetu tena kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, bajeti ya Waziri imesema bidhaa ya *cement* au saruji tunazalisha kwa kiwango kikubwa kuliko mahitaji yaliyopo ndani ya nchi, hivyo tunauza nje ya nchi, lakini kwa nini bado bei ya *cement* kwa mujibu wa

taarifa ya Waziri ni Sh.17,600. Hii Sh.17,600 sio fedha ndogo kwa wananchi wetu wanyonge. Najiuliza kama *material* ya *cement* yanapatikana ndani ya nchi, wanafanya kila kitu ndani ya nchi, kwa nini bado bei yake haijafika kama bei ambazo tukinunua *cement* nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako baadhi ya marafiki zangu ni wafanyabiashara wa *cement,* wanaagiza bidhaa ya *cement* kutoka Iran. Bei ya bidhaa ya *cement* wanayonunua Iran mpaka wakija kuuza katika soko la Zanzibar, bado bei ni nafuu kuliko bei hii ya *cement* inayozalishwa ndani ya Tanzania na tunauza nje ya Tanzania. Sasa nini dhamira ya uwekezaji kwa wananchi maskini katika Taifa hili? Kama dhamira ya uwekezaji ni kuhakikisha wanapata bidhaa kwa bei nafuu, nataka Mheshimiwa Waziri aje aniambie, kwa nini pamoja na *cement* kuuzwa nje ya nchi kutokana na uzalishaji kuwa mkubwa, lakini bado bei yake ni kubwa kuliko *cement* ambayo inazalishwa kutoka nchi nyingine za na ikafika Tanzania na ikaweza kufanana bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini bei yake isiwe ndogo? Kwa nini bei ambayo mfanyabiashara ataenda kununua Iran asiwe ananunua ndani ya Taifa letu na huyu anasafirisha, analipa kodi na bado mambo mbalimbali yanaendelea kuyafanya. Kwa hiyo nataka kuona dhamira ya uwekezaji itoe matunda kwa wananchi maskini, sio tu peke yake kwa kutoa matunda katika ajira na Serikali kupata kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nizungumzie suala la ununuzi wa Tanga *Cement* kama ambavyo baadhi ya wenzangu wamezungumzia na ndio wajibu wetu kwa sababu tumechaguliwa tuje tuishauri Serikali na tusipoishauri tutakuwa hatujatenda wajibu wetu wa kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Mtoni na majimbo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu ya baadhi ya Wabunge ambao wameendelea kusimamia ama kuishauri Serikali iangalie mchakato wa *Twiga Cement* kuinunua Tanga *Cement* ni hofu ya kibiashara na ni hofu wazi kabisa. Hofu hiyo msingi wake ni sheria tuliyoitunga ndani ya Bunge hili, kama sheria tumeitunga ndani ya Bunge letu kwa dhamira ya kulinda hofu kama hiyo kitu gani kinatufanya Serikali ishindwe kusimamia sheria iliyotungwa na Bunge hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria imesema wazi katika masuala ya kuingia sokoni kama wakati wanafanya *merge* haitakiwi uzidi 35%. Mwenye mamlaka ya kusimamia hiyo sheria, watendaji kupitia Wizara hii *FCC* walikiri kwamba hili jambo likifanyika litazidi 35%, sasa leo kitu gani kilichotokea tena nyuma wakajisahaulisha yale waliyoyasema, tena hata wakajisahaulisha hukumu iliyotolewa na Mahakama ambayo haijatoa kwa kupenda, ni sisi wawakilishi wa wananchi ndio tulitunga sheria hii. Ni sisi wawakilishi wa wananchi ndio tulihakikisha panakuwepo na Mahakama, tulihakikisha panakuwepo na *FCC* kwa sababu tulijua yatatokea mambo ambayo tunataka kulinda maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sio dhambi mtu kuuza kitu chake, hata mimi naweza kuuza vitu vyangu, lakini katika Taifa hili kuna sheria, vipo vitu Mwenyezi Mungu amekutunuku wewe mwenyewe, ukivifanya katika Taifa letu ama ukivitumia katika Taifa letu ni makosa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo kuuza kitu chake mtu sio dhambi, lakini utaratibu wa sheria zetu ufuatwe. Utaratibu uko wazi, wanunuzi wapo, kama vipi itangazwe, mbona tumeona makampuni mengi yaliyo-*merge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kuanza kufuatilia masuala ya *merging* ya kampuni wakati *Millicom* anauza hisa zake

kuelekea iliponunuliwa sasa hivi na kampuni ya *Axian* na nilifuatilia sana kwa maslahi ya kampuni ambayo Serikali ya Zanzibar ina hisa Kampuni ya *Zantel*. Pale ndipo wakati nafuatilia nikalikuta suala hili pia, nikasema acha nilifuatilie kwa maslahi ya Taifa letu. Nikafuatilia tangu mchakato ulivyoanza, nikajua taarifa za watu na wadau mbalimbali waliokwenda Mahakamani, nikajua hukumu iliyotoka ambayo ilishauri kwamba suala hili lisifanyike kwa maslahi ya Watanzania. Ni Mtanzania gani mwingine huko nyuma ambaye ana maslahi tofauti na maslahi ya Watanzania ambaye anaruhusu suala hili lifanyike tena? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kampuni hii ikachukua ikamiliki soko zaidi ya 42%, wakiamua kuangusha bei ya saruji, wataua viwanda vingine vidogo vya Watanzania na watu wengine mbalimbali, hapo tutakuwa tunasaidia uwekezaji au tunaua uwekezaji? Je, jambo hili likifanyika bei ya saruji ikapanda zaidi kuliko ilivyo sasa hivi, tunawasaidia Watanzania au tumewaua Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inawezekana sheria hii kwa maono ya hawa imeshapitwa na wakati, lakini ndio iliyopo, tufuate sheria iliyopo. Pia niishauri Serikali kupitia Wizara hii na Serikali nzima, suala hili la *Tanga Cement* kuuza hisa zake na *interest* ya Twiga kununua tulitumie kama *visibility study* ama kama maono basi, pana sheria nyingi sana ambazo haziko sahihi kwa mujibu wa mwenendo wa masuala ya kibiashara katika Taifa letu. Kuna sheria za manunuzi nyingi haziko sahihi kwa wakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo hili tulitumie kama mfano kwamba Serikali ilete mabadiliko ya sheria mbalimbali ambazo wanadhani yanaweza yakasaidia masuala ya kibiashara. Katika hatua ya sasa, kile ambacho kipo kwa mujibu

wa sheria kiheshimiwe ili wafanyabiashara waendelee kuiheshimu Serikali, wawekezaji waiheshimu Serikali, lakini wananchi watambue yale tunayoyashauri na kupitisha katika Bunge ni kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tumefika mwisho wa *session* yetu ya jioni, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu kamili.

*(Saa 1.28 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 5 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*